الخِلافَةُ

مُنَاقَشَةٌ عِلْمِيَّةٌ فِيْ مَسْأَلَةِ الْخِلافَةِ الإسْلامِيَّةِ
الْجُزْءُ الأَوَّلُ

UKHALIFA

MJADALA WA KIELIMU

KUHUSU UKHALIFA WA KIISLAMU

JUZUU YA KWANZA

Juma Muhammad Rashid Al-Mazrui

YALIOMO

Maudhui Ukurasa
Utangulizi……
Tatizo la Riwaya katika dhehebu la Shia……
Mifano…….
Riwaya za kupotolewa Qur-ani……
Riwaya nyengine za kupotolewa Qur-ani……
Riwaya ya kwanza……
Riwaya ya pili……..
Mfano mwengine……..
Minhaj (Methodology) ya uandishi katika vitabu vya Kishia……
Tanbihi…….
SURA YA KWANZA: KUHUSU AYA 55 YA SURA 5…..
Maana ya neno Waliy (Walii)……
Kanuni juu ya neno lenye maana nyingi……..
Mfano…….
Tafsiri sahihi ya Aya hio……
Sibaq (Maneno yaliotangulia) ya Aya……..
Siyaq (Maneno yanayofatia) ya Aya……..
Kanuni za kiusuli……..
Illa (sababu) ilioletwa na herufi *"Inna"* baada ya amri……
Illa (sababu) ilioletwa na herufi *"inna"* baada ya katazo…...
Illa (sababu) ilioletwa na herufi *"Inna"* baada ya habari…..
Kanuni nyengine ya kiusuli……..
Kanuni za kilugha…….
Ushahidi wa shia…….
Tanbihi…….
Riwaya za kishia……..
Utangulizi…….
Riwaya……..
Kauli nyengine juu ya nani imemshukia aya hio……..
Mukhtasar……..
SURA YA PILI: KUHUSU AYA YA MAWADA……
Maana ya neno qur-baa……..

Maana za herufi *"fii,"* iliomo katika aya hio…….
Istithnaau (exception) hapa ina maana gani…….
Siyaq na sibaq ya aya hio…….
Kuwepo kwa herufi *laa* na herufi *illa*…….
Utafiti wa riwaya juu ya iliyemteremkia aya hio……..
Sanad……..
Hadithi ya pili……..
Sanad……..
Matn ya Hadithi……
Fiq-hi ya Aya…….
Riwaya nyengine juu ya sababu ya kuteremka Aya hio…...
Mukhtasari na nukta muhimu……..
SURA YA TATU KUHUSU AYA "NA WAONYE JAMAA ZAKO WA KARIBU"…….
Hadithi……..
Sanad ya Hadithi hii…….
Matn ya hadithi……...
Takhrij na maelezo…….
Maneno sahihi alioyatamka Mtume (s.a.w.) baada ya kuteremka Aya hio……
Sanad ya Hadithi……
Riwaya nyengine sahihi……..
Mukhtasari na nukta muhimu…….
SURA YA NNE KUHUSU MAJADILIANO…….
Utangulizi……
Jawabu kwa makala ya kwanza ya Sheikh X…….
Jawabu ya pili kwa makala ya kwanza ya Sheikh X……
Utangulizi…….
Maudhui…….
Jawabu kwa makala ya pili ya Sheikh X……..
Jawabu kwa makala ya tatu ya Sheikh X…….
Jawabu ya pili kwa makala ya tatu ya Sheikh X……
Jawabu kwa makala ya nne ya Sheikh X…….
Jawabu kwa makala ya tano ya Sheikh X……..
Nakala ya Hadithi al-Thaqalain…….
Matn ya Hadithi hio…….
Mukhtasari……

Khatima…….

بسم الله الرحمن الرحيم

الحمد لله رب العالمين، وأشهد ألا إله إلا الله وحده لا شريك لـه، القائـل ((وَقُلْ جَاءَ الْحَقُّ وَزَهَقَ الْبَاطِلُ إِنَّ الْبَاطِلَ كَانَ زَهُوْقًا)) وأشـهد أن محمدا رسول الله صلى الله عليـه وعلـى آلـه وصحبه وسلم, وبعد:

UTANGULIZI

Kitabu *Ukhalifa* ni utafiti wa baadhi za Aya[1] pamoja na Hadithi zake ambazo zimekuja kuzifasiri Aya hizo juu ya suala la ukhalifa. Asili ya kitabu hiki – sawa na vitabu vyangu vyengine vingi nilivyotangulia kuvichapisha – ni makala nilizokuwa nikiziandika katika ukumbi wa *Zanzinet* na ukumbi wa Jifunzeuislamu. Hakuna tafauti yoyote ile baina ya njia nilioitumia kuandika kitabu hiki na njia nilioitumia kuandika vitabu vyangu vyengine: vyote ni utafiti wa kuzirejesha Aya na Hadithi kwenye kanuni zake za kilugha na kiusuli.

Suala la ukhalifa ndio kikwazo kikubwa kilichojenga mtafaruku baina ya Shia na *Jumhur* (majority) ya Umma. Shia wanaona kuwa Allah – katika Qur-ani – na Mtume (s.a.w.) – katika Hadithi zake – walimchagua Ali na kizazi chake kuwa ndio Maimamu na Makhalifa baada ya Mtume (s.a.w.). Kwa mujibu wa Shia, hakuna tafauti baina ya utume na uimamu isipokuwa wahyi![2] Bali kwa mujibu wao, Maimamu wao wana ujuzi na fahamu sawa na Mtume wetu Muhammad (s.a.w.)[3] na hawakosei na ni bora zaidi kuliko Malaika na Mitume wengine waliotangulia![4] Kwa mantiki hii, Shia

---

[1] - Kitabu hiki kinajadili Aya tatu tu.

[2] - Yaani wote – Mtume na Maimamu – huchaguliwa na Allah; na wote ni *ma'asumun* (Hawakosei wala hawatendi dhambi); na wote matendo yao na maneno yao ni Hadithi! Hata hivyo, mmoja wa madokta wa Kimisri walioingia Shia, nilimsikia katika T.V ya *Al-Thaqalain* akisema kuwa Maimamu wa Ahlul-Bait wanapata wahyi! Natarajia hii ni kauli yake binafsi: si kauli ya Shia kama ni madhehebu.

[3] - Inasema riwaya yao: "Ali na Maimamu, Allah kawapa elimu sawa na ya Mtume Muhammad (s.a.w.) na kawapa fahamu kama ya Mtume Muhammad (s.a.w.)". Tazama Ibn Babawaih Al-Qummi *Al-Imamah Wa Al-Tabsirah* uk. 170, Hadithi na. 22-23-24.

[4] - Na hivi ndivyo alivyosema Al-Khomeni kwamba kuitakidi kuwa Maimamu wao ni bora kuliko Malaika na Mitume ni jambo la lazima katika madhehebu yao. Katika kitabu changu *Mezani Ya Haki*, niliyanukuu maneno hayo ya Al-Khomeni kutoka katika kitabu

wanaona kwamba kuukataa uimamu wa Maimamu wao basi kunaifanya dini yako yote iwe batili,[5] bali kunaifanya tawhidi yako iwe haikutimia hadi hapo utapowakubali Maimamu wao kumi na mbili,[6] kuanzia Sayyidna Ali hadi kufikia kwa yule aliyekimbilia mapangoni si chini ya miaka 1000 iliopita na ambaye wanamngoja ili aje kuukomboa ulimwengu kutokana na dhulma![7]

Kwa hali yoyote ile, suala la ukhalifa halikuwa suala la khilafu za kiitikadi na kifiq-hi tu, bali imekuwa ni sababu kubwa ya mvutano uliopelekea wakati mwengine hata kumwagika damu za Waislamu kama munavyoona hali ya sasa huko Iraki.[8] Kwa kwetu, suala hili labda wakilijua watu

---

cha Dr. Al-Buttiy *Al-Salafiyya* uk. 112, naye akatoa marejeo Ayatullah Al-Khomeni *Al-Hukuma Al-Islamiyya* uk. 52. Lakini hatimae nimekipata kitabu hicho cha Al-Khomeni na katika kopi yangu ni uk. 93.

[5] - Na hivi ndivyo alivyotoa fat-wa Al-Sistani hivi karibuni, alipoulizwa kuhusu Madhehebu ya Kiibadhi, akajibu: "Kila ambaye hafuati Maimamu kumi na mbili, basi huyu yuko katika batili". Fat-wa hio ilikuwa kwenye mtandao wake Al-Sistani na ikatangazwa na T.V. ya Mustaqillah. Na hivi karibuni nilikuwa nasikiliza tafsiri inayotolewa na mmoja wa Mashekhe wao, akasema kwamba hawa wote walioukataa Uimamu wa Ali basi amali zao ni bure! Siku nyengine – nilihadithiwa kwamba – alizifasiri Aya za motoni kuwa ni za wasioukubali utawala wa Ali na za peponi ni za wenye kuukubali utawala wa Ali (Mashia)!

[6] - Na kwa hivyo, Al-Jazairi anasema katika kitabu chake *Al-Anwaaru Al-Na'amaniyyah* j. 2, uk. 278, kwamba sisi tusiokuwa Shia na wao Mashia, basi Mungu wetu ni mwengine na wao ni Mwengine; Mtume wetu ni Mwengine na wao ni Mwengine! Na haya maneno yake nakunukulia:

> Sisi na wao hatukubaliani katika Mola, wala Nabii wala Imamu. Na sisi hatumkubali Mola huyu wala Mtume yule. Bali tunasema kwamba Mola ambaye Khalifa wa Mtume wake ni Abu Bakr basi huyo si Mola wetu wala Mtume huyo (ambaye Khalifa wake ni Abu Bakr) si Mtume wetu!

[7] - Cha kustaajabisha ni kuwa Imamu huyo wa kumi na mbili (Al-Mahdi Al-Muntadhar) kawakimbia Al-Abasiyyina wenye kupigana kwa panga; vipi atapambana na Mmarekani na dola nyengine za Magharibi zenye nyuklia?! Baadhi ya nadharia za kutoweka kwa Imamu huyo zinaeleza kwamba sababu ya kukimbia na kujificha ni kuwa hakuwa na Ansar (wakumnusuru), yaani wa-kumsaidia. Lakini tukitazama leo tunaona Iran ni dola moja tishio yenye uwezo kamili wa kumsaidia Al-Mahdi, lakini bado Al-Mahdi anaendelea kujificha na hali ndio kama hii munavyoiona!

[8] - Kitabu hiki nilikiandika zamani: si chini ya miaka mitano nyuma tangu wakati Shia na Sunni wanauana huko Iraki kwa misingi ya kimadhehebu.

wasomi tu au mtu mmoja mmoja tu. Iran ilipogeuza fikra yake na kuanzisha harakati za kueneza itikadi zake duniani, juhudi kubwa zikaanza – ziliodhihiri katika ujenzi wa taasisi za kidini kama Bilal Muslim – si kwa lengo la kuwatoa makafiri na kuwaleta katika Uislamu, bali kwa lengo la kuwatoa Waislamu kutoka katika madhehebu zao na kuwapeleka katika madhehebu ya Shia. Kwa upande wangu, naona si vibaya mtu kuhajiri madhehebu moja kwenda nyengine ikiwa kafanya hivyo kwa kukujua vyema atokako na kukujua vyema endako na akafanya hivyo kwa *ikhlasi*, kwa maana kwamba katika ufahamu wake – ikiwa ni mtu wa kuweza kupekuwa na kufahamu – kaona kwamba huko alikokwenda ndiko kuliko sahihi zaidi: si kwa kufuata mali; lakini naona ni kosa kubwa kuwa tufanye kampeni maalumu na kujenga taasisi na kutafuta walinganiaji wa kulipwa ili kuwatoa watu katika madhehebu fulani kwenda nyengine! Bidii hii kama ingeelekezwa kule alikoielekeza Sh. Deedat na Sh. Ngariba, basi kheri kubwa ingelipatikana na fitna zisingelikuwepo.

Suala kubwa ambalo walinganiaji hao wa Afrika ya Mashariki na sehemu nyengine zote wanatulingania, ni:

1) Kuitakidi kuwa Allah na Mtume wake wamemchagua Ali kuwa ndiye khalifa baada ya Mtume (s.a.w.); kisha baada ya hapo ukhalifa ushikwe na watu maalumu katika kizazi cha Ali.
2) Makhalifa wengine ukhalifa wao ni batili, nao – pamoja na Masahaba wengine – wakati mwengine huitwa kuwa ni makafiri au wanafiki![9]

Hali hii ya mchafuko wa kiitikadi – ilioletwa na mambo mawili: pesa na uchache wa elimu – imechangia sana katika kujenga Afrika Masharika mpya iliojaa migogoro ya kimadhehebu, jambo ambalo halikupata kushuhudiwa au lilikuwa nadra katika zama zote za mababa na mababu zetu. Matatizo nilioyaona mimi na ambayo yamepelekea kupatikana kwa muitiko – japo kuwa ni mdogo – ni mawili kama nilivyoashiria kabla. Moja ni kuwa asilimia kubwa ya watu ama hatuna elimu kabisa au hatuna

[9] - Haya yako katika vitabu vingi sana, lakini kwa msomaji wa Kiswahili anaweza kurejea katika kitabu kiitwacho *Waulizeni Wanaofahamu* cha Tijani Al-Samawi. Hayo atayapata katika sehemu tafauti za kitabu hicho kama vile uk. 235, wa Sura inayozungumzia kuhusu Makhalifa watatu: Abu Bakr, Umar na Uthman.

uwezo wa kuchambua au tunao uwezo lakini hatuna vitabu vya kutosha vya madhehebu zote. Hilo ni mosi, nalo humpelekea mtu anapoambiwa kuwa hii Hadithi inasema, basi – kwa nia yake njema – huikubali tu, bila kujua je Hadithi hio ni ya-kweli au ni ya-kutunga au ni ya-kweli lakini ina maana gani. Halkadhalika wakiambiwa hii Aya inasema wanakubali, bila kujua vipi tutairejesha Aya katika tafsiri inayokubalika kielimu! Hili ni tatizo la watu kwa ujumla. Ama tatizo la pili, ni kuwa baadhi ya Mashekhe, dunia wameiweka mbele kiasi cha kwamba watu wanauza dini zao kwa njia mbalimbali. Madhehebu ni njia ya kufika kwa Allah: leo madhehebu imegeuka kuwa ni bidhaa ya biashara: inauzwa na kununuliwa: tunakubali kuuza imani zetu na kuwatukana watu bora baada ya Mitume: watu ambao kwa damu zao na mali zao ndio sisi tumeweza kujua kusali, tumeweza kufikiwa na Qur-an na mingineo – pesa itawaangamiza watu!

Mambo yanapofika katika hali hii, inakuwa ni wajibu wa kila mtu kutoa hoja yake. Mimi – kwa upande wangu – nimezipekuwa Aya ambazo Shia wanatolea ushahidi juu ya kuwepo kwa amri ya Allah juu ya ukhalifa wa Ali, lakini nikaona kuwa tafsiri walizotupa za Aya hizo hazikujengeka katika misingi sahihi inayokubalika katika elimu ya tafsiri. Pia nikazitazama riwaya wanazozitegemea katika kuzifasiri Aya hizo nikaona ni riwaya maudhui (za kutunga) tupu kwa mujibu wa *sanad* zake, bali na kwa mujibu wa *mutun* (texts) zake pia. Kwa hivyo, na mimi nimeamua kutoa mchango wangu wa ninachokijua juu ya suala hili la ukhalifa. Kitabu hiki ni juzuu ya kwanza; itafatiliwa na juzuu ya pili *In shaa Allah.* Huu ndio mchango wangu naomba munipokelee na muniombee dua.

TATIZO LA RIWAYA KATIKA MADHEHEBU YA SHIA

Mara nyengine Shia – bila ya kutujuilisha – hunukuu Hadithi kutoka katika vitabu vyao na kuuhubiri kwazo ulimwengu wa Waswahili. Baadhi ya watu wakiambiwa kuwa Hadithi hio imo katika kitabu *Al-Ihtijaj* – kwa mfano – cha Al-Tabrasi, mwanachuoni mkubwa aliyeishi karne ya sita, huwa wao hawajui Al-Tabrasi ni nani: hudhania kuwa ni msimulizi wa Kisunni tu, na hapo huiamini riwaya hio. Kwa hivyo, ni vyema wakati tunapotaja riwaya iliosimuliwa na Shia tuwaeleze watu, kwa vile aghlabu ya watu hawazikubali riwaya zilizosimuliwa na Shia.

Mimi kwa upande wangu, pia sizikubali riwaya za Kishia ila zikitimiza masharti matatu au moja ya matatu:

1) Ziwe zimepokewa kwa *sanad* sahihi katika mapokezi ya Kisunni au ya Kiibadhi.
2) Ziwe zinakubaliana na Qur-ani.
3) Ikiwa wengine hawakuzipokea riwaya hizo: zimepokewa na Shia tu, basi ziwe riwaya hizo haziungi mkono itikadi ya Kishia, kwani hapa itakuwa hakuna tuhuma.

Ama sababu yangu ya kuzikataa riwaya zao, si kwa sababu wao ni Shia, bali ni kwa sababu ya kuwepo katika vitabu vyao riwaya nyingi za kutunga kupita kiasi.[10] Na hili ndilo walilolisema wanavyuoni wakubwa miaka mingi sana. Na hata Al-Musawi – mwanachuoni wa Kishia – katika kitabu chake *Al-Tas-hihu* kakiri kwamba riwaya za kutunga ziko nyingi mno katika masimulizi ya Kishia. Na miongoni mwa walioandika kuhusu maudhui haya – kama tulivyosema katika *Mezani Ya Haki* – ni Dr. Mustafa Al-Sibai. Anasema Dr. huyo:

> Na vikundi vya kisiasa vilizama katika tope za uwongo – kwa wingi na kwa uchache – (kumzulia) Mtume (s.a.w.), basi Al-Rafidha (Shia) ndio waongo wao katika vikundi hivi.[11]

[10] - Riwaya za kutunga ndio balaa kubwa katika umma huu. Na riwaya za namna hio ziko katika madhehebu tafauti, lakini riwaya za namna hio zinapopindukia mipaka hata ikawa kitabu chenye maelfu ya riwaya hupati ila riwaya mia tu zilizo sahihi au chini ya mia, basi jambo hili linatia khofu kubwa na linatufanya tuzihadhari riwaya za watu wa namna hio.

[11] - Dr. Mustafa Al-Sibai *Al-Sunna Wa Makanatuha* uk 96.

Anasema Al-Imamu Malik kuhusu Shia: “usisimulie kutoka kwao hakika wao wanasema uwongo”.[12] Anasema Sharik Al-Qadhi naye ni Shia muadilifu: “chukua (riwaya) kwa yoyote utayemkuta isipokuwa *Al-Rafidha* (Shia) hakika yao wanatunga Hadithi na wanazifanya kuwa ni dini”.[13] Anasema Al-Imamu Al-Shafi: “sijapata kuona watu waliowazi zaidi kwa uwongo kuliko *Al-Rafidha* (Shia)”.[14] Anasema Yazid bin Harun: “watu wote wa bidaa, basi Hadithi zao zinaandikwa isipokuwa *Al-Rafidha* kwani wao wanasema uwongo”.[15] Anasema Dr. Mustafa Al-Sibai: “Na kama walivyotunga Hadithi za fadhila za Ahlu Al-Bait, (pia) wametunga Hadithi za kuwatia kasoro Masahaba hasa hasa Mashekhe wawili (Abu Bakr na Umar)”.[16] Na akasema: “Na namna hivi *Al-Rafidha* walivuuka mpaka katika kutunga Hadithi zenye kuwafikiana na matamanio yao na zikafikia – kwa wingi – mpaka wenye kutisha, kiasi cha kwamba Al-Khalili (si Mufti wa Oman) kasema katika (kitabu) *Al-Irshad* “Wametunga *Al-Rafidha* kuhusu fadhila za Ali na Ahlu Al-Bait kiasi cha Hadithi laki tatu!”[17]

Hayo ni baadhi ya yaliosemwa na baadhi ya wanavyuoni. Hivi karibuni, nimesoma kitabu kiitwacho *Lillahi Thumma Li-Taarikh* kilichoandikwa na mtu asiyejulikana.[18] Kuhusu masimulizi ya riwaya katika Shia, bwana huyo ana hiki cha kutueleza:

> Kasema Al-Sayyid Husain bin Al-Sayyid Haidar Al-Amili aliyekufa mwaka 1076 A.H. ‘Hakika ya kitabu cha Al-Kafi[19] kina vitabu 50 pamoja na *sanad* ndani yake kwa kila Hadithi yenye kutoka kwa Maimamu’.[20]

---

[12] - Ibn Hajar *Lisanu Al-Mizan* j. 1, uk. 10. Al-Dhahabi *Al-Mizan* j. 1, uk. 27, *tarjama* na. 73, *tarjama* ya Ibrahim bin Al-Hakam bin Dhuhair.

[13] - K.h.j.

[14] - K.h.j.

[15] - K.h.j..

[16] - K.h.j.uk. 97.

[17] - K.h.j. uk. 98

[18] - Kitabu hicho, kwa kweli ni utafiti mzuri, lakini mtunzi wake kauharibu utafiti wake katika baadhi ya sehemu, ambapo kama alivyoona yeye kuwa Shia wametunga riwaya naye pia kawazulia uwongo. *Wa Allahu Al-Musta’aan!*

[19] - Al-Kafi ndio kitabu sahihi chao cha Hadithi kwa Shia, lakini ukikisoma utastaajabu sana.

[20] - Tazama *Rawdhatu Al-Jannat* j. 6, uk. 114.

> Wakati Abu Ja'afar Al-Tusi aliyekufa mwaka 460 anasema: 'Hakika ya kitabu cha Al-Kafi kina vitabu 30'.[21]

Sasa suala ni kuwa vitabu ishirini vya ziada – na kila kitabu kina milango mingi – vimetoka wapi? Hii ina maana kwamba, katika kipindi hiki cha zaidi ya miaka mia sita baina ya muelezaji wa kwanza na muelezaji wa pili, vitabu 20 vimeundwa na kutumbukizwa katika riwaya za asili za Maimamu, hio ni 40% ya Hadithi za kitabu hicho muhimu kwa Shia.

Anaendelea mpekuzi huyo kwa kuzungumzia kuhusu kitabu *Tahdhibu Al-Ahkam* cha Al-Tusi. Anasema: "Wanavyuoni wetu[22] wanasema kuwa kitabu hicho kwa sasa kina jumla ya Hadithi 13590; wakati Al-Tusi mwenyewe mtunzi wa kitabu hicho – kama ilivyo katika vitabu vingi vya asili – anasema kwamba *Tahdhibu Al-Ahkam* ni zaidi ya Hadithi 5000 yaani hazizidi kwa hali yoyote ile Hadithi 6000. Suala ni kuwa idadi yote hii ya 13590 imetoka wapi kama si kuwazulia Maimamu mambo mengi ambayo hawakupata kuyatamka.[23]

Ama katika ukumbi wa Zanzinet, mmoja wa wafuasi wasomi wa Madhehebu hio, alitwambia kwamba mmoja wa wanavyuoni wakubwa wa Hadithi wa Kishia naye ni Al-Majlisi anasema kwamba katika jumla ya riwaya 17,000 za Al-Kuleini ni riwaya 6000 tu ambazo ni sahihi. Na bila shaka hii ni idadi kubwa sana ya Hadithi dhaifu na za kutunga katika kitabu kimoja tu ambacho Shia wanakizingatia kuwa ndio kitabu sahihi kuliko vyote. Sasa jiulize wewe kwamba ikiwa kitabu bora chao kwa mujibu wa mtazamo wa Shia kina karibu ya *thuluthi* mbili *(two thirds)* ya Hadithi dhaifu na za kutunga, vitabu vyengine vikoje?!

Ama Al-Musawi, mwanachuoni wa Kishia,[24] yeye maneno yake tumeyanukuu pia katika kitabu *Mezani Ya Haki* na si vibaya hapa tukayakumbusha tena. Anasema:

---

[21] - Tazama *Al-Fahrasat* 161.

[22] - Bwana huyu anajifanya kuwa ni Shia lakini inavyoonesha si kweli: lakini kilichomuhimu kwetu si yeye ni nani, bali ni yeye anasema nini.

[23] - Mwisho wa kunukuu pamoja na kuusherehesha kidogo.

[24] - Nilipojadiliana na baadhi ya wanafunzi wenzangu kule Msikiti wa Shia ulioko Amani, waliniambia kuwa Al-Musawi si Shia wala hajulikani kamwe; sijui kwamba hivyo

> Pamoja na kwamba sisi tunaitakidi kwamba asilimia kubwa ya riwaya za kutunga kutoka kwa Maimamu (wa Kishia) zimetungwa baada ya Ghaiba Kuu (kujificha moja kwa moja kwa Al-Mahdi Al-Muntadhar)….lakini mfuatiliaji muadilifu hana budi kusema kwamba (hata) katika zama za Maimamu wa Kishia vile vile zimetungwa riwaya kutoka kwao (Maimamu wa Kishia) kama zilivyotungwa kutoka kwa Mtume Mtukufu (s.a.w.).[25]

Anaendelea Al-Musawi:

> Hakika ya mfuatiliaji wa riwaya ambazo wamezileta wasimulizi wa Kishia katika vitabu vyao walivyovitunga baina ya karne ya nne na ya tano A.H., basi anafikia natija ya kuhuzunisha sana, nayo ni kuwa juhudi iliofanywa na baadhi ya wasimulizi wa Kishia katika kuuharibu Uislamu ni juhudi iliosawa na mbingu na ardhi kwa uzito wake (yaani ni juhudi kubwa sana). Na nafikiria kwamba (wasimulizi) hao hawakukusudia kuizamisha itikadi ya Kishia katika nyoyo bali walikusudia kuuharibu Uislamu na kila chenye kuhusiana nao.[26]

Na – bila shaka – mchunguliaji katika vitabu vya Kishia, mbali na kuona Hadithi nyingi zenye kugongana na Qur-ani, basi pia anaona Hadithi nyingi zenye kugongana zenyewe kwa zenyewe. Na kwa hivyo Al-Tusi – mmoja wa wasimulizi wakuu wa riwaya za Kishia – analalamika kwa kusema:

---

ndivyo walivyoambiwa na Mashekhe wao au ilikuwa ni *taqiyya.* Sasa nawaomba warejee kitabu kilichoandikwa na Dr. ‘Alaa Al-Din bin Al-Sayyid Amir Muhammad Al-Qazwini, mtaalamu wa Kishia, ambacho ni jawabu yake kwa Dr. Musa Al-Musawi alichokiita *Ma’a Al-Dukturi Al-Musawi* wataona kuwa Al-Musawi anatokana na ukoo mashuhuri na wenye heshima kubwa katika ulimwengu wa Kishia. Na babu yake ni Al-Sayyid Abu Al-Hasan, mwanachuoni wa Kishia, ambaye moja ya vitabu vyake anakinukuu Dr ‘Alaa huyo. Na Al-Musawi alikuwa pamoja na Al-Khomeni. Yote hayo utayapata katika kitabu *Ma’a Al-Dukturi Al-Musawi* cha Dr. ‘Alaa.

[25] - Yaani zimetungwa riwaya hizo kisha zikanasibishwa na Maimamu wa Kishia na nyengine zikanasibishwa na Mtume (s.a.w.) ilhali wao hawajazitamka kamwe. Tazama Al-Musawi *Al-Tas-hihu* uk. 135.

[26] - K.h.j 15.

> Amenikumbusha mmoja wa marafiki..kuhusu Hadithi za Sahibu zetu (Shia)…na kile kilichomo ndani yake miongoni mwa tafauti, kutokukubaliana (Hadithi hizo), migongano na kupingana, mpaka ikawa hakuna maafikiano ya riwaya moja ila utaikuta nyengine iko kinyume yake; wala haikusalimika Hadithi ila utaikuta nyengine inagongana nayo…….[27]

Hayo, ni baadhi ya maoni ya wataalamu, na kwa sababu hio ndio maana nimesema kwamba kwa uoni wangu ninahisi kwamba hatuwezi kutoa hoja kwa riwaya za Kishia ila zikiwa zimetimiza masharti matatu tulioyataja kabla.

MIFANO

Hatuwezi kumaliza riwaya za kutunga zilizomo katika vitabu vya Kishia, kwani hili litatulazimu tuandike kitabu chenye juzuu si chini ya mia ambacho kinakusanya riwaya hizo tu. Lakini na-tutowe mifano miwili mitatu tu kuhusu Hadithi hizo. Cha kufahamu ni kuwa Hadithi zote *taqriban* zilizotungwa katika vitabu vya Kishia, ni zile za kuhusu ukhalifa, uimamu na fadhila za Ahlu Al-Bait: Hadithi nyengine hazikuwa muhimu kwao. Mfano wa Hadithi hizo, ni zile tulizozinukuu katika *Mizani Ya Haki*[28] ambapo Sayyidna Ali (k.w.) ananukuliwa akisema:

1) Wallahi nilikuwa pamoja na Ibrahim (alipotupwa) kwenye moto, na mimi ndiye niliyeufanya (moto huo) uwe baridi na salama (kwa Ibrahim). Na nilikuwa pamoja na Nuh katika Safina, na nikamuokoa kutokana na gharka. Na nilikuwa pamoja na Musa nikamfunza Taurati. Na nikamfanya Issa atamke katika godoro (la uchanga yaani katika utoto) na nikamfunza Injil. Na nilikuwa pamoja na Yusuf katika shimo la kisima nikamuokoa kutokana na hila za ndugu zake. Na nilikuwa katika busati pamoja na Sulaiman nikamdhalilishia upepo![29]

[27] - Al-Tusi *Tahdhibu Al-Ahkam* j. 1, uk. 2, katika utangulizi wa Sheikh Al-Tusi mwenyewe.
[28] - Uk. 136-140.
[29] - Tazama *Al-Anwaar Al-Na'amaniyya* j. 1, uk. 31.

2) Mimi ndiye niliyekuwa juu na nikashinda; mimi ndiye ***ninayehuisha*** na ***kufisha***; mimi ndiye wa mwanzo na wa mwisho, mimi ndiye (mjuzi wa) yalio dhahiri na ni mjuzi wa yaliojificha.[30]
3) Ali ni kama Qur-ani: hakosei wala haimjii batili mbele yake wala nyuma yake.[31]

RIWAYA ZA KUIPOTOWA QUR-AN NA

KUMUONGEZA ALI NA AHLU AL-BAIT

WENGINE KATIKA AYA ZAKE

1) "Kutoka kwa Jabir kutoka kwa Abi Ja'afar juu yake iwe amani kasema: 'Kateremka Jibril kwa Mtume (s.a.w.) na Aya hii: 'Na mukiwa muna shaka katika yale tuliomteremshia Mja wetu ***kuhusu Ali*** basi leteni sura iliomfano wake'. Hii ni Aya ya 23 ya Sura ya 2. Maneno: ***"Kuhusu Ali"*** ni nyongeza: si maneno ya Allah.[32]
2) "Basi wakabadilisha wale ***waliowadhulumu watu wa Muhammad*** kauli kinyume na ile walioambiwa, basi tukateremsha juu ya wale ***waliowadhulumu watu wa Muhammad*** adhabu kutoka mbinguni kwa sababu ya ufasiki waliokuwa wakiufanya". Hii ni Aya ya 59 ya Sura ya 2, maneno ***waliowadhulumu watu wa Muhammad*** hayamo katika Qur-ani: hapa yameongezwa katika jaribio la kuhalalisha ukhalifa wa Al-Imamu Ali (k.w.). Aya hio katika usahihi wake inasomeka hivi:

> **Basi wakabadilisha wale *waliodhulumu* kauli kinyume na ile walioambiwa, basi tukateremsha juu ya wale *waliodhulumu* adhabu kutoka mbinguni kwa sababu ya ufasiki waliokuwa wakiufanya.[33]**

[30] - Sheikh Al-Mufid *Al-Ikhtisas* uk. 157. Tazama! Sifa zote za Allah kapewa Ali!
[31] - Muhammad Jawwad *Imamat Ali Baina Al-'Aqli Wa Al-Qur-ani* uk. 110-111.
[32] - Tazama nakala hio katika *Al-Kafi* j. 2, uk. 381.
[33] - Tazama upotoshaji wa Aya hio katika *Al-Kaafi* j. 2. uk. 394. *Tafsir Al-Qummi* j. 1, uk. 48. *Faslu Al-Khitaab* uk. 204.

3) “Kutoka kwa Jabir kutoka kwa Abi Ja’afar juu yake iwe amani kasema: ‘Kateremka Jibril kwa Mtume (s.a.w.) na Aya namna hii: ‘Ni kiovu kilioje kile walichokiuzia nafsi yao kwacho, ya kwamba wameyakufuru yale alioyateremsha Allah ***kuhusu Alii*** kwa sababu ya uadui”. [34] Hii ni sura ya 2 Aya ya 90. Maneno **“Kuhusu Ali”** ni nyongeza katika jaribio la kuhalalisha ukhalifa wake baada ya Mtume (s.a.w.).
4) “Kutoka kwa Jabir kutoka kwa Abi Ja’afar juu yake iwe amani: ‘Basi hawatoamini mpaka wakufanye wewe kuwa ndio muamuzi katika ugomvi baina yao, kisha wasione uzito katika nafsi zao kutokana na ile (hukumu) atayoihukumu Muhammad ***na watu wa Muhammad*** na wasalim amri kusalim (kwa kweli kweli)”. [35] Hii ni Aya ya 65 ya Sura ya 4: maneno: ***“Na watu wa Muhammad”*** ni nyongeza yenye lengo la kutaka kuupa nguvu upande wa Ali na kizazi chake.

Hizo ni baadhi ya nukulu ambazo tulizinukuu katika kitabu chetu *Mezani Ya Haki*.[36] Sasa endelea kujiongezea nukulu nyengine mbili:

5) Kutoka kwa Abi Abdillahi (a.s.) kasema: “Na hakika ya utawala wa Ali ni uteremsho kutoka kwa Bwana wa ulimwengu wote”.…”..Hakika ya utawala wa Ali ni kikumbusho kwa wachaji wenye ujuzi*Na Sisi tunajua kwamba katika nyinyi wako wenye kukadhibisha*Na Ali ni masikitiko (majuto) juu ya makafiri**Na kwa hakika utawala wake ni haki ya yakini**Basi litukuze Jina La Mola wako Aliye Mkuu”. Hizi ni Aya za mwisho za Sura 69 Aya 43 halafu 48-52. Hapa utawala wa Ali umechomekwa katika kila Aya *taqriban*![37]

6) Kutoka kwa Abi Abdillahi (a.s.) kasema kuhusu kauli yake Allah Mtukufu: “Muulizaji aliuliza kuhusu adhabu yenye kutokea**Kwa wenye kuukufuru utawala wa Ali haina cha kuizuia (adhabu hio)”. Kisha akasema (Abu Abdillah, Ja’afar Al-Saadiq): “Jibrilu

[34] - Tazama *Faslul-Khitab* uk.205, na *Al-Kafi* j. 2, uk. 380.
[35] - Tazama nyongeza hio katika *Faslul-Khtab* uk. 225.
[36] - Nakala nyengine hatukuzinukuu hapa kwa kuepuka kukariri. Tazama *Mezani Ya Haki* uk. 136-140.
[37] - Tazama *Faslu Al-Khitab* uk. 284.

kamteremshia (Aya hizo) Mtume (s.a.w.), na katika riwaya ya pili: "Namna hivi ndivyo ilivyo katika Msahafu wa Fatima". Hizo ni Aya 1-2 za Sura 70. Hapa pia utawala wa Ali pia umepachikwa.[38]

Hii ni baadhi tu ya mifano[39] – iko zaidi ya mia mbili na wengine wanasema kwamba iko zaidi ya elfu mbili – ya namna gani watetezi wa Al-Imamu Ali na kizazi chake, bali maadui wa Ali na kizazi chake, walivyotunga riwaya za uwongo mpaka wakafikia kuipotosha Qur-ani kama mulivyoona.

RIWAYA NYENGINE ZA KUIPOTOA QUR-ANI NA KUWEPO KWA MSAHAFU WA FATIMA NA VITABU VYENGINE

RIWAYA YA KWANZA

> Kutoka kwa Abi Basir kasema: "Niliingia kwa Abi Abdillah (Ja'afar Al-Saadiq), nikamwambia: 'Mimi ni muhanga kwako, hakika ya mimi nakuuliza suali: 'Je kuna anayesikia maneno yangu hapa? Kasema, basi Abu Abdi-llahi akaondosha pazia baina yake na nyumba nyengine, akachungulia ndani yake[40] kisha akasema: 'Ewe Aba Muhammad uliza yale yaliokudhihirikia (unayotaka kuuliza). Akasema: 'Nikamwambia: 'Mimi ni fidia kwako, hakika ya Mashia wako wanazungumza kwamba Mtume (s.a.w.) kamfundisha Ali mlango ambao hufunguliwa yeye (tu) kutoka katika mlango huo milango elfu moja (mingine). Akasema: 'E Abu Muhammad! Mtume (s.a.w.) kamfundisha Ali milango elfu moja;

---

[38] - Enyi wenye akili! Basi nyinyi bado munazikubali tu riwaya za watu hawa ambao hawakuona tabu kumzulia Mwenyezi Mungu uwongo wakazidisha mambo wayatakayo katika Kitabu chake?! Kipi basi kitachowazuia wao wasitunge riwaya za kumzulia Mtume wake au wasizifasiri Aya kwa mujibu wa matamanio ya nafsi zao ikiwa jambo la kuipotoa Qur-an halikuwa zito kwao?!

[39] - Mimi – kama nilivyotangulia kusema – kwamba nukulu hizi nazinukuu kutoka kitabu *Al-Shi'a Wa Tahrifu Al-Qur-an* cha Sh. Muhammad Mala-Llah. Sikukipata kitabu *Faslu Al-Khitab* kwani nilivyofahamu ni kuwa kitabu hicho kilitoka mara moja tu baadae wakalaumiana kwa kuitoa siri hii, na hakikuchapishwa tena. Lakini hata hivyo, nimeona katika baadhi ya vitabu vyao vyengine vya kutegemewa wakinena kinaga ubaga kwamba Qur-ani hii imepotoshwa, kiasi cha kwamba Al-Jazaairi yeye kasema kuwa hayo ni makubaliano ya Shia. Hata hivyo, tunakuta wako Shia wasiolikubali jambo hilo: sijui kama kutokukubali huko ni kweli au *taqiyya* iko kazini!

[40] - Lo! Jamaa Imamu achungulia nyumbaningwa! (Ni nyumbani kwa watu kwa Kipemba) na kwa lugha ya vijana Imamu apiga bodi!

kutoka katika (kila) mlango mmoja katika hio, hufunguliwa milango elfu moja (mingine)…….Kisha akasema (Al-Imamu Ja'afar Al-Saadiq): 'E Aba Muhammad! Na sisi tuna (kitabu kiitwacho) Al-Jaami'a, na nini kinakujuilisha wewe nini hio Al-Jaami'a?!...Akasema (Al-Imamu Ja'afar Al-Saadiq): 'Ni kitabu ambacho urefu wake ni dhiraa sabiini kwa dhiraa za Mtume (s.a.w.) na kakitolea imla kutoka katika kinywa chake (Mwenyewe Mtume s.a.w.), na Ali (akawa) anaandika kwa mkono wake wa kuume!.....na sisi tuna Jafr! Na nini kinakujuilisha wewe nini hio Jafr?!...Akasema (Al-Imamu Ja'afar Al-Saadiq): 'Ni chombo cha ngozi ndani yake kuna elimu yote ya Mitume na Mawasii (Maimamu wanaochaguliwa baada ya Mitume) na elimu ya Maulamaa waliopita katika Banii Israail!.....Na sisi tuna Msahafu wa Fatima na nini kinakujuilisha wewe nini huo Msahafu wa Fatima?!...Akasema (Al-Imamu Ja'afar Al-Saadiq): 'Ni Msahafu ndani yake kuna mfano wa Qur-ani yenu hii mara tatu, Wallahi haimo (humo) hata herufi moja ya Qur-ani yenu hii……Na sisi tuna elimu ya yaliokuwa na yatayokuwa mpaka siku ya Kiama.[41]

Msahafu huu wa Fatima alipewa na Jibril baada ya kufa Mtume (s.a.w.) na akawa Ali ndiye muandikaji wa Msahafu huo![42]

Kizazi cha Hasan kilifaya Hasad kwa sababu ya kupewa akina Al-Imamu Ja'afar Al-Saadiq (anayetokana na kizazi cha Husain) Al-Jafr (Chombo cha ngozi ndani yake kuna elimu yote ya Mitume na Mawasii yaani Maimamu wanaochaguliwa baada ya Mtume na elimu ya Maulamaa waliopita katika Banii Israail).[43]

RIWAYA YA PILI

Na katika riwaya ya Abi Dhar, (kasema) kwamba Mtume (s.a.w.) alipokufa, Ali aliikusanya Qur-ani na akaja nayo kwa Muhajirina na Ansar na akawaonesha yale Mtume (s.a.w.) aliomuusia kwayo. Basi Abu Bakr aliifungua. Katika ukurasa wa kwanza alioufungua zikatoka fedheha

[41] - Tazama Al-Kuleini *Al-Kafi* j. 1, uk. 294-296, mlango wa 97: Babu dhikri Al-Sahifa wal-Jafri wal-Jami'a wa Mus-hafi Faatima. Anasema aliyetia maelezo kitabu hicho kwamba hii ni: "Hadithi sahihi"!

[42] - Tazama Al-Kuleini *Al-Kafi* j. 1, uk. 296, riwaya na. 2.

[43] - Tazama Al-Kuleini *Al-Kafi* j. 1, uk. 296, riwaya na. 3. Soma pia mlango huo wenye jumla ya riwaya nane kuhusu vitabu hivyo walivyopewa Shia na Jibril na Mtume (s.a.w.)!

za jamaa (Muhajirina na Ansar). Basi Umar akaruka na kusema: ‘E Ali irejeshe (hio Qur-ani yako) sisi hatuna haja nayo!’ Basi akaichukua (Ali) kisha akaondoka. Kisha wakamleta Zaid bin Thabit – na alikuwa katika Wasomaji wa Qur-ani -, Umar akamwambia: ‘Hakika Ali kaja na Qur-ani ndani yake kuna fedheha za Muhajirina na Ansar, na (kwa hivyo) tumeona tuandike Qur-ani tuzitoe kutoka katika (Qur-ani hio, Aya zote) ambazo ndani yake kuna fedheha za Muhajirina na Ansar. Zaid akamkubalia, kisha akasema: ‘Je nikimaliza (kuandika) Qur-ani munayoiomba (kuandikiwa), kisha Ali akaja akaidhihirisha Qur-ani alioiandika, je si itakuwa kazi yenu yote ni bure? Umar akasema: ‘Sasa hila ni nini?’ Zaid akasema: “Nyinyi ni wajuzi zaidi wa hila”. Umar akasema: “Hakuna hila ila tumuue (Ali) ili tupumzike naye”. Basi akafanya njama za kumuua kwa kumtumia Khalid bin Walid, lakini akashindwa”.[44]

Basi Umar alipokuwa Khalifa akamuomba Ali ampe ile Qur-ani ili waipotoe, akasema (Umar kumwambia Ali): “Ewe Aba Al-Hasan: ‘Lete ile Qur-ani ambayo ulimjia nayo Abu Bakr ili tukubaliane juu ya hio”. Akasema (Ali): “A wapi tena! Hakuna njia ya kuifikia hio tena, mimi nilikuja nayo kwa Abu Bakr ili kukusimamishieni hoja tu, ili musijemukasema Siku ya Kiyama kwamba sisi tulikuwa tumeghafilika (na Qur-ani) hii, au mukasema kwamba hukutuletea. Hakika ya Qur-ani niliokujieni nayo haiguswi ila na waliotakasika na Mawasii (Maimamu) katika kizazi changu![45] Umar akauliza: “Je kuna wakati maalumu wa kuidhihirisha?! (Ali) akasema: “Ndio: ataposimama msimamizi (Al-Mahdi Al-Muntadhar au kwa Kiswahili ni Muhudi), ataidhihirisha na kuwafanya watu waifate hio”![46]

MFANO MWENGINE

[44] - Maneno ya riwaya hii ikiwa mtu ana akili ya kufikiri na kuchambua, basi yanatoa ushahidi wa wazi kwamba chuki za Shia dhidi ya Umar (r.a.) ni chuki zilizoundwa kwa njia kama hizi.

[45] - Tazama akili za watu hawa! Sasa huku si kumtia aibu Ali kwamba hakufikisha ujumbe? Ni kitabu gani cha Allah ambacho kinafichwa watu wasikione ila watu maalumu. Tena musijemukadhania kwamba haya ni maneno yanayosemwa tu na Shia: hizi ni itikadi thabiti kwao. Na wanaamini kabisa kwamba vitabu hivyo tulivyovitaja hapa vitadhihiri atapokuja Al-Mahdi Al-Muntadhar. Lakini usijitaabishe bure ukamuuliza Shia: atakupiga *taqiyya* moja tu uanguke huko!

[46] - Tazama vituko hivi katika Abu Mansur Al-Tabrasi *Al-Ihtijaj* j. 1, uk. 156.

Mfano mwengine niliupata nilipotembelea katika maktaba ya Iran katika maonesho ya vitabu yaliofanyika Oman mwaka huu (2007).[47] Nilipotembelea hapo nilijinunulia Msahafu. Msahafu huo ni Qur-ani hii hii ya kawaida: si ile ya Fatima ilio mara tatu ya hii; lakini pembeni mwa kila Aya *taqriban* wameitilia riwaya zilizopokewa kuhusu fadhila za Ahlu Al-Bait. Ukizisoma Hadithi hizo unaweza kuona kizunguzungu! Basi *Wallahi* mpaka Aya isemayo: **"وَلِلَّهِ الأَسْمَاءُ الْحُسْنَى فَادْعُوْهُ بِهَا (Na Allah ana majina mazuri (matukufu) muombeni (au muabuduni) kwa hayo**",[48] pembeni wametuekea riwaya itokayo kwa Abu Abdillah (Ja'afar Al-Saadiq) akisema:

> Sisi (Maimamu wa Ahlul-Bait) *Wallahi* ndio majina matukufu (yenyewe) ambayo Allah haikubali kutoka kwa waja amali yoyote ila kwa kutujua (kututambua) sisi!

Halafu, baada ya hayo, chini wakatutilia marejeo ya riwaya hio kuwa imo katika kitabu *Al-Kafi* cha Al-Kuleini.[49] Nayo – bila shaka – ni Hadithi sahihi kwao, kwani mtiaji maelezo wa kitabu hicho *Al-Kafi*, kila anapoipitia Hadithi dhaifu basi chini husema kuwa hii ni Hadithi dhaifu; ama Hadithi hii ni miongoni mwa alizozitia maelezo kidogo bila ya kusema kuwa ni dhaifu. Pia kuchapishwa Hadithi hio pembeni mwa Qur-ani Tukufu, haiwezekani ila kwa kupatikana ruhusa kutoka kwa *Maayatollah* na *Maruhullah*, na hii inaonesha kuwa kwao ni Hadithi sahihi.

Sasa nini tena kilichobakia; nini kitatufanya sisi tuwe na imani na riwaya za Kishia – hasa hasa za kuhusu uimamu na ukhalifa – baada ya kuwa kuna maelfu ya riwaya za namna hii. Kwa ufupi, ni kuwa katika Msahafu huo niliounununua, kila Aya nzuri *taqriban* basi imeekewa Hadithi kwamba ima

---

[47] - Nilipoandika kitabu hiki.

[48] - Sura 7 Aya 180.

[49] - Naam! Nimekirejea kitabu hicho nikaikuta kweli riwaya hio imo katika kitabu hicho sahihi chao cha Shia katika j. 1, uk. 192, Hadithi na. 4, kitabu *Al-Tawhid*, mlango wa 45: *babu Al-nawadir.*

Aya hio ni ya Ali au Maimamu wengine wa Kishia pamoja na wafuasi wao![50] Kwa hivyo, hali hii, inatufanya sisi tuzihadhari sana riwaya hizo.

MINHAJ (METHEDOLOGY) YA UWANDISHI KATIKA VITABU VYA KISHIA

Jambo jengine muhimu ambalo mimi nahisi linahitaji kurekebishwa ni njia inayotumiwa na ndugu zetu katika uandishi. Katika njia zao za uandishi kuna baadhi ya kasoro ambazo ni vyema wakazirekebisha ili vitabu vyao tupate kuwa na imani navyo. Kasoro hizo:

1) Ni kuwa wao hunukuu Hadithi, kisha wakataja marejeo. Mara nyengine hutumia neno *"Masadir" (Sources).* Kisha wakataja Masadir iliopokewa Hadithi hio. Na hapa hufanywa kitu ambacho si sahihi:
   a) Kuchanganya baina ya *Masadir* na *Maraji'u*. *Masadir (Sources)* ni vile vitabu vya walioipokea Hadithi, kama Al-Bukhari na Muslim. Ama *Marajiu (references* au marejeo) ni jumla jamala: yanaingiza vitabu vya wapokezi wa Hadithi na wasioipokea Hadithi hio bali wameitaja tu katika vitabu vyao vya uchambuzi kama vile Ibn Hajar na wengine. Sasa asiyejua ataona kwamba Hadithi hio imepokewa na kundi kubwa la wapokezi, kumbe wapokezi ni wawili au watatu. Jambo hili limo katika vitabu vingi vya ndugu zetu, hasa hasa kitabu *Al-Ghadir* cha Al-Amin na *Al-Murajaat*[51] cha Sharafu Al-Din Al-Musawi.

---

[50] - Hata Mtume (s.a.w.) huwa hatajwi sana ukilinganisha na Ali na Maimamu wa Ahlu Al-Bait.

[51] - Yaani katika maelezo yaliotiwa chini na Husain Al-Radhi. Kwa mfano maelezo alioyatia katika Aya ya 23 ya Sura 42 katika *Al-Muraja'at* uk. 124-126. Utaona hapo kataja sababu ya kuteremka Aya hio halafu akataja marejeo mengi mpaka akamtaja Al-Shaukani ambaye ni mwanachuoni wa kiasi cha miaka 200 tu iliopita. Na sisi tunapotaja sababu ya kuteremka Aya, huwa tunahitaji riwaya sahihi tu, na hii ina maana kwamba tunukuu riwaya kutoka kwa wapokezi wa Hadithi tu. Lakini ile yote ni katika mbinu za kutaka kuwafanya watu waone kwamba riwaya hio imepokewa na idadi kubwa ya wapokezi.

b) Kutosheka na kunukuu riwaya tu hata kama ni dhaifu kiasi gani, bila ya kubainisha chochote kuhusu *sanad*[52] na *matn*[53] ya riwaya hio. Bali mara nyingi hukwambia kuwa ni Hadithi sahihi. Na hili halikubaliki katika uwanja wa elimu, hasa hasa katika vitabu vya kujadili tafauti za kimadhehebu.

2) Kusema fulani kaipokea Hadithi wala hajaipokea. Bali kaitaja tu: na kuna tafauti baina ya kupokea Hadithi na kuitaja. Na haya yamo katika vitabu vingi; mfano mmoja ni yale aliyoyasema Dr. Alaa Al-Din bin Al-Sayyid Amir Muhammad Al-Qazwini katika kitabu chake *Maa Dr. Musa Al-Musawi*,[54] ambapo alidai kwamba Hadithi isemayo kwamba Mtume (s.a.w.) alisema:

> Nani atanibaii (kuekeana ahadi na mimi ya kunitii) ili awe roho yangu naye ni wasii wangu na msimamizi wa jambo hili baada yangu….Ali akambaii**,**

Alisema Dr. huyo kwamba Hadithi hio imepokelewa na Al-Shahrastani! Lakini ukikirejea kitabu hicho cha Al-Shahrastani,[55] utaona kwamba yeye hakuipokea Hadithi hio, bali anatoa hoja za Shia na nini wametegemea juu ya itikadi yao tu. Na kwa hivyo, yeye hutumia lugha kama: "wakasema..wakasema..wakasema".

3) Jambo la tatu lililomo katika makala zao na vitabu vyao, ni kuwa Sheikh wa Kisunni – kwa mfano – hujadili maudhui, akataja kauli za kila kundi na hoja zao. Basi hapo hapo kitabu chake hicho hufanywa kuwa ni marejeo, na kwa hivyo msomaji hudhani kuwa Sheikh huyo ni katika jumla ya waliozisema kauli hizo kwa kuzikubali, kumbe yeye kazitaja kauli hizo kwa ajili ya kuzijadili kauli tafauti tu: si kwamba kazitaja kwa kuzikubali. Hili

---

[52] - *Sanad* maana yake ni "Msururu wa wapokezi wa Hadithi". Kwa mfano Hadithi inayosema: kutoka kwa Abi Ubaida, kutoka kwa Jabir bin Zaid, kutoka kwa Ibn Abas, kutoka kwa Mtume (s.a.w.) kwamba amesema: "Mmoja wenu akishika kiume chake na-atie udhu (tena)," basi msururu huu wa wapokezi wa Hadithi, yaani "Abi Ubaida, kutoka kwa Jabir bin Zaid kutoka kwa Ibn Abas," ndio huitwa *sanad.*

[53] - *Matn* ni yale maneno yenyewe yaliyopokewa kutoka kwa Mtume (s.a.w.), kama: "Mmoja wenu akishika kiume chake na-atie udhu (tena)". Hii ndio huitwa *matn* ya Hadithi.

[54] - Uk. 60.

[55] - Al-Shahrastani *Al-Milal Wa Al-Nihal* j. 1, uk 180.

tumelishuhudia hata katika ukumbi wa *Zanzinet* vile vile tulipokuwa tukiijadili Hadithi ya Ibn Umar ya kujuzu kuingilia kwa njia isio ya kawaida.[56] Bali – kwa tabia hii – utakuta wakati mwengine hunasibishiwa watu fulani kitu ambacho hawakiamini kabisa bali labda huwa wanakitaja tu katika vitabu vyao kama ni moja ya kauli za Waislamu. Mfano mmoja – mifano iko mingi lakini ninafupisha – ni kile kilichoandikwa na Sheikh Mahdi Hamad Al-Fatlawi kwamba miongoni mwa mambo waliokubaliana Suni na Shia ni kuwa Al-Imamu Al-Mahdi Al-Muntadhar ni wa mwisho katika Makhalifa kumi na mbili….na kwamba (dola yake) ni ahadi ya Allah iliotajwa katika Qur-an![57] Sasa sijui makubaliano haya yako katika vitabu gani vya Kisunni!

4) Tafsiri za Aya wanazodai kuwa zinawahusu Ahlul-Bait, ni tafsiri zisizokubaliana na *minhaj (Methodology)* au njia sahihi ya tafsiri iliokubalika katika Umma, ya kuijenga tafsiri katika lugha ya Kiarabu na Usuli Al-fiqhi na mingineo katika fani za tafsiri. Hili tumeliashiria katika *Mezani Ya Haki.*

TANBIHI YA KWANZA

Tumeeleza katika utangulizi huu tatizo la kuwepo kwa uwongo mkubwa uliosimuliwa na Shia, kwa ushahidi tulioutoa. Jambo la kusikitisha ni kuwa hadi leo hii kuna ambao bado wanaendelea kuwadanganya watu! Mutakumbuka kwamba huko nyuma – kwa uwezo wa Allah na tawfiki yake – tuliandika kitabu *Mezani Ya Haki* kinachoijadili Hadithi Al-Thaqalain. Kwa habari niliopewa ni kuwa Sheikh Abdillahi Nasir akasema

[56] - Na mifano juu ya hili pia ni mingi sana hatuwezi kuisha. Natutoe mfano mmoja tu. Wanapoizungumzia sababu ya kuteremka Aya isemayo: **"Hakika Walii wenu ni Allah na Mtume wake na Wale walioamini…"** Sura 5, Aya 55, hutaja marejeo ya Kisunni mengi yenye kusema kuwa Aya hii imemterekia Ali wakati alipotoa sadaka ya pete naye yumo kwenye Sala. Sharafu Al-Din Al-Musawi katika *Al-Murajaat* uk. 137, Muraja'a na. 12, kafikia kusema kuwa Al-Mufassirina wamekubaliana kuwa Aya hii imemterekia Ali! Ilhali Masunni wao wameinukuu tu riwaya hii kama ni moja ya riwaya zilizosimuliwa kuhusu sababu ya kuteremka Aya hio, halafu wakasema kuwa hii ni riwaya ya kutunga, kama utavyoona maelezo yetu katika kitabu.

[57] - Tazama Mahdi Hamad Al-Fatlawi *Maa Al-Mahdi Al-Muntadhar* uk. 29.

atakijibu “apawe wiki mbili”. Yaani wakati huo ilikuwa bado kutoka kitabu rasmi: ni makaratasi tu. Ninasimuliwa kuwa walijifungia ndani Kiponda yeye na wenzake wawili (majina hatuyataji),[58] lakini wiki mbili zikakatika na hawakutoka na jawabu. Na huu sasa ni mwaka wa saba. Kwa hali yoyote ile si muhimu kujibu na kutojibu, muhimu ni:

a) Kuikubali haki.
b) Kusema ukweli.

Katika siku ya Al-Khamisi ya tarehe 6 *Jumada al-ula* 1433 H. (29/3/2012), nilitembelewa na kijana mmoja kutoka Mwanza Tanzania anayeitwa Sh. Othmn Idi. Ni kijana ninayemfahamu zamani, kasoma hapa hapa Oman; ni mtu wa dini wala sijasikiapo kutoka kwa mtu yoyote akimtuhumu kwa ubaya wa aina yoyote ule katika kipindi chote cha miaka saba aliokaa hapa wala baada ya kurudi huko nyumbani. Cha muhimu ni kuwa kaniambia kuwa Abdillahi Nasir alikuja Mwanza akatoa muhadhara wake. Akaulizwa kuhusu kitabu *Mezani Ya Haki* cha Juma Al-Mazrui. Akasema:

> hiki kitabu nimeshakijibu, na huyu muandishi mimi nimekutana naye lakini nikamuona kuwa si mtu mwenye *thaqafa* kubwa!

Hayo ni maneno ya Abdillahi Nasir kwa mujibu wa nukulu hio ya Sheikh huyo wa Mwanza. Sasa ninachotaka kuwahakikishia wasomaji ni kuwa mimi nikipita mbele ya macho ya Abdillahi basi hanijui labda anijue katika Dvd zangu. Abdillahi Nasir na mimi tulionana mara moja katika uhai wetu tangu mimi niko mdogo labda nina miaka 20 au na mbili mpaka na tano. Alitutolea muhadhara Kiponda na akasema kuwa katika Shia hakuna kauli ya kujuzisha kuingilia mke kwa njia ya nyuma na kama yuko mwenye ushahidi huo kutoka katika vitabu vya Kishia na-aulete. Na mimi wakati huo nilikuwa ninao ushahidi huo: nimeihifadhi kauli hio imo katika kitabu *Al-Intisaar* cha mwanachuoni mkubwa wa Kishia aitwae Sh. Abu Al-Qasim Ali bin Hussain Al-Musawi maarufu kwa jina la Al-Sharif Al-Murtadha.[59] Nikataka kunyanyuka nimwambie, mwenzangu akanambia “aa wacha haina maana”, nikamsikiliza, lakini kwa leo naona inayo maana

[58] - Kwani wao hatujasikia kuwa wamesema uwongo.

[59] - Al-Sharif Al-Murtadha *Al-Intisar* uk.125-126. Na kwa sasa hivi nimeiona kauli hio katika vitabu vyengine pia.

na bora ningalimwambia “aa tulia, inayo maana”. Maana ni kuidhihirisha haki na kuiondoa batili na hii ni maana kubwa bali ni wajibu.

Kwa hali yoyote ile ninachotaka kukisema hapa ni kuwa, mimi na Abdillahi Nasir hatujakutanapo hata siku moja, maneno yake hayo hayana ukweli hata chembe moja.

Pili ni kuwa hata nikawa na *thaqafa* kubwa au ndogo au sina kabisa; hilo si muhimu: muhimu ni kuwa je nilichokiandika ni haki au ni batili? Kama ni haki akifuate na awaamrishe watu wakifuate; kama ni batili abainishe ubatili wake nami niko tayari kuifuata haki.

TANBIHI YA PILI

Mmoja wa maustadhi aliwahi kuniambia: “wewe mara unatoa kitabu cha kuwajibu Mashia, Mawahabi wanafurahi; na mara unawajibu Mawahabi, Mashia wanafurahi”. Mimi nikamwambia: “mimi siandiki chochote kwa ajili ya kumkera Shia wala kwa ajili ya kumfurahisha; kwa ajili ya kumkera Wahabi wala kwa ajili ya kumfurahisha: mimi ninaifikisha haki kwa watu”.

Kwa hivyo, ningependa kutoa *tanbih*i kuwa mtu asije akaona kwamba mimi kuandika makala na vitabu hivi juu ya itikadi za Kishia kwamba mimi naipiga vita au naichukia Shia, *laa*, si hivyo, Shia wamekuwepo Afrika Mashariki kwa karne nyingi wala hakuna aliyekuwa akiwasema, lakini Shia sasa wamejihusisha na tafauti za kimadhehebu na wamekuwa wakitulingania kwamba tuache madhehebu zetu na twende katika madhehebu yao,[60] bali na pia wamekuwa wakifanya kazi ya kuwatoa

[60] - Na jambo hili linasababisha fitna kubwa baina ya Waislamu. Mtandao wa intaneti wa Al-Jazira umemnukuu Mwanachuoni Dr. Yusuf Al-Qaradhawi katika mkutano uliofanyika Qatar uliowajumuisha Sunni na Shia:

> Na Al-Qaradhawi akapinga kwa nguvu katika Mkutano wa Doha …majaribio ya Irani ya kuingiza Ushia katika miji ya Kiarabu ya Kisunni kiukamilifu, akizingatia kuwa hilo linapelekea katika fitna baina ya makundi mawili hayo, na akatangaza katika Mkutano wa Doha kupeleka kuwatuma ujumbe wa umoja wa

wasiokuwa na elimu kutoka katika madhehebu zao. Jambo hili hatuwezi kulifasiri isipokuwa kwamba wao wanatuona sisi kuwa si Waislamu kama walivyosema wanachuoni wao, Ni'matul-Lahi Al-Jazaairi na Al-Sistani na wengine, ndio maana juhudi zikafanyika kutuleta katika Uislamu! Jambo hilo linafanyika kwa njia mbali mbali kama vile mihadhara, makala na vitabu vya Kiswahili, ambavyo ndani yake kuna kuwaponda Masahaba wa Mtume (s.a.w.), wake zake na kututaka sisi tufuate madhehebu inayoitwa ya Ahlu Al-Bait! Kwa hivyo, natarajia kwamba na sisi ni haki yetu ikiwa hatukuukubali wito huo – baada ya kuwa umetolewa katika njia hizo mbali mbali – kwamba na sisi tutoe sababu zetu za kwanini tumeukataa wito huo. Kwa hivyo, ufupisho ni kuwa Shia wanaona kuwa itikadi zetu si sahihi; na sisi tunaona kuwa itikadi zao si sahihi; Shia wanaandika kutuonesha wapi tumekosea, kwa hivyo, na sisi watupe fursa tuwaoneshe wapi wamekosea. Katika kufanya hivi, watu wataweza kutanua maarifa yao zaidi na labda iko siku tutaweza kufikia muafaka wa pamoja.

Kwa hivyo, atayekisoma kitabu changu hiki akiwa ni Shia, Sunni au Ibadhi, naomba aweke kasumba za kimadhehebu pembeni, aifanye fikra yake kama ni fikra tupu: fikra ya mtu anayetafuta ukweli kwa mara ya kwanza kana kwamba hana itikadi hii wala ile. Natarajia – akifanya hivyo – ataweza kuufikia ukweli.

Ahsante:
Juma Muhammad Rashid Al-Mazrui.

Maulamaa wa Kiislamu kwenda Iran ili kuzungumza na maafisa wa serikali huko kuhusiana na masuala hayo.

Na akasema Al-Qaradhawi akielezea kitachozungumzwa katika mazungumzo ya T.v. yatayofanyika (kwa sasa yameshafanyika) baina yake na Ayatullah Ali Akbar Hashim Rafsanjani aliyekuwa Raisi wa Iran: "Tutazungumzia mambo ambayo yanachochea pande mbili (Sunni na Shia) kama vile kuwatukana Masahaba na jaribio la kuwatia Sunni katika Ushia na kuwatia Shia katika Usunni".

SURA YA KWANZA

KUHUSU AYA "HAKIKA WALII WENU NI ALLAH NA MTUME WAKE NA WALE WALIOAMINI"

بسم الله الرحمن الرحيم

الحمد لله رب العالمين، والصلاة والسلام على خير المرسلين، سيدنا ونبينا محمد وعلى آله وصحابته أجمعين، وعلى أتباعه وحزبه إلى يوم الدين.

وبعد:

Mwenyezi Mungu (S.W.) anasema:

إِنَّمَا وَلِيُّكُمُ اللَّهُ وَرَسُولُهُ وَالَّذِينَ آمَنُوا الَّذِينَ يُقِيمُونَ الصَّلاةَ وَيُؤْتُونَ الزَّكَاةَ وَهُمْ رَاكِعُونَ

> **Hakika *Walii* wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini tu: wale ambao wanasimamisha sala na wanatoa zaka nao ni wenye kurukuu.[61]**

Aya hii ni katika Aya tegemezi ambazo Shia wamezichukua katika kuthibitisha dai kwamba suala la ukhalifa baada ya Mtume (s.a.w.) si suala la shura (mashauriano), bali ni suala ambalo limetokana na amri tukufu ya Mwenyezi Mungu Mwenyewe. Na hii ni kwamba wao wanalifasiri neno ***Waliyyu (Walii)*** – lililotajwa katika Aya hio – kuwa maana yake ni msimamizi wa mambo, yaani mtawala. Na kwa hivyo, maana ya Aya hio – kwa mujibu wao – ni:

> **Hakika *msimamizi* wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na wale walioamini tu: wale ambao wanasimamisha sala na wanatoa zaka nao ni wenye kurukuu.**

Kisha wakapokea riwaya zenye kusema kwamba makusudio ya maneno: **"Na wale walioamini tu: wale ambao wanasimamisha sala na wanatoa zaka nao ni wenye kurukuu"** ni Al-Imamu Ali (k.w.), na kwamba yeye

[61] - Sura 5 Aya 55.

ndiye aliyekusudiwa katika sehemu hio ya Aya. Na kwa hivyo tafsiri ya Aya hio itakuwa hivi: "Hakika *msimamizi* wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na Ali". Hii ndio tafsiri ya Shia ya Aya hio, wakitegemea riwaya zilizopokewa juu ya maana hio.

Dr. 'Alaa Al-Din bin Al-Sayyid Amir Muhammad Al-Qazwini – katika jawabu yake kwa Dr. Musa Al-Musawi alioiita *Ma'a Al-Dukturi Al-Musawi* – baada ya kuinukuu Aya hio, alisema:

> Miongoni mwa maandiko ya wazi juu ya kuwepo andiko juu ya ukhalifa wa Al-Imamu Ali (a.s.) ni kauli Yake (Allah) Mtukufu (isemayo): ((Hakika Walii wenu…..Aya (hio tulioinukuu)).[62]

Kisha baada ya hapo, Dr. akatoa maelezo yake; pamoja na maelezo na riwaya kutoka katika vitabu vya wanavyuoni wa tafsiri, lakini kwa masikitiko kafanya hivyo bila ya kubainisha riwaya sahihi na dhaifu bali na bila ya kwenda kwa mujibu wa elimu ya tafsiri! Na Al-Tabatabai naye katika tafsiri yake *Al-Mizan*,[63] ana maelezo marefu, yote ni yakujikalifisha tu na kwenda kinyume na misingi ya tafsiri ilimradi atetee itikadi yake.

Kwa ufupi ni kuwa Shia wanaona kuwa Aya hio, ni andiko la wazi kwamba ukhalifa ni amri ya Mwenyezi Mungu, na kwamba – kwa mujibu wa Aya hio, ukiifungamanisha na Hadithi zilizopokewa juu ya tafsiri yake basi – tunapata kwamba Allah kamfanya Ali kuwa ndiye msimamizi wa mambo ya Waislamu (yaani Khalifa) baada ya Mtume (s.aw.). Nao – kama tulivyosema – wanategemea riwaya zilizopokewa kwamba Aya hio imemteremkia Ali (k.w.). Kwa hivyo, ikiwa Aya hii imemteremkia Ali (k.w.) na Aya inasema:

إِنَّمَا وَلِيُّكُمْ اللَّهُ وَرَسُولُهُ وَالَّذِينَ آمَنُوا الَّذِينَ يُقِيمُونَ الصَّلاَةَ وَيُؤْتُونَ الزَّكَاةَ وَهُمْ رَاكِعُونَ

[62] - Dr. 'Alaa Al-Din bin Al-Sayyid Amir Muhammad Al-Qazwini *Ma'a Al-Dukturi Al-Musawi* uk. 62

[63] - J.6, uk. 5-25

Hakika *Walii* wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini tu: wale ambao wanasimamisha sala na wanatoa zaka nao ni wenye kurukuu,

hii ina maana kwamba Walii wetu ni Allah (S.W), Mtume (s.a.w.) na Ali (k.w.)!

Sasa wakati tumo katika kulitafiti suala hili, basi hatua ya kwanza ni kujua nini maana ya neno *Waliyyu "Walii"* lililotajwa katika Aya hio. Ikiwa neno hilo lina maana moja, basi maana itakuwa ni hio: na kama lina maana nyingi, basi hatua ya pili ni kutazama tena je katika maana nyingi hizo, ni ipi iliokusudiwa hapo katika Aya hio. Halafu hatuwa ya tatu ni kuzitazama riwaya zote zilizosimuliwa kuhusiana na Aya hio.

MAANA YA NENO *WALIYY* (WALII)

Neno *"Waliyyu (Walii)"* linatokana na neno la Kiarabu: *waliya* (Kitendo kilichopita) *yaliy* (Kitendo kilichopo na kijacho) *walayatan* na *wilayatan* (Jina yaani noun). Na wingi wake (plural yake) ni *Awliyaau.* Ama ukiitazama maana ya neno hilo, utakuta kwamba ni neno lenye maana nyingi; nyengine ni tafauti; na nyengine zinakurubiana. Maana hizo ni:

Mosi:

Mlinzi na msaidizi. Maana hii imo katika Aya isemayo:

أَفَحَسِبَ الَّذِينَ كَفَرُوا أَنْ يَتَّخِذُوا عِبَادِي مِنْ دُونِي أَوْلِيَاءَ إِنَّا أَعْتَدْنَا جَهَنَّمَ لِلْكَافِرِينَ نُزُلاً

Basi je wanadhani wale waliokufuru kwamba vile kuwafanya waja wangu kuwa ndio *walinzi* badala yangu….[64]

Neno lililotumika katika Aya hii kumaanisha walinzi ni neno *Awliyaau* ambalo ni wingi wa neno *Waliyy* (Walii). Na Aya kama hizi ziko nyingi.

Pili:

[64] - Sura 18 Aya102.

Rafiki na kipenzi. Maana hii imo katika Aya isemayo:

أَلا إِنَّ أَوْلِيَاءَ اللَّهِ لا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلا هُمْ يَحْزَنُونَ

E sikilizeni! Hakika *vipenzi* vya Allah hakuna hofu juu yao wala wao hawahuzuniki.[65]

Neno lililotumika katika Aya hii kumaanisha vipenzi ni neno *Awliyaa* ambalo ni wingi wa neno *Waliyy* (Walii). Na Aya kama hizi pia ziko nyingi.

Tatu:

Msimamizi wa mambo. Maana hii imo katika Aya isemayo:

فَإِنْ كَانَ الَّذِي عَلَيْهِ الْحَقُّ سَفِيهاً أَوْ ضَعِيفاً أَوْ لا يَسْتَطِيعُ أَنْ يُمِلَّ هُوَ فَلْيُمْلِلْ وَلِيُّهُ

Na kama yule ambaye juu yake iko haki (mkopaji) ni mjinga au dhaifu au hawezi kuandikisha mwenyewe, basi na-aandikishe *msimamizi* wake…[66]

Neno lililotumika katika Aya hii kumaanisha msimamizi ni *Waliyy* (Walii).

Nne:

Mrithi. Maana hii imo katika Aya isemayo:

فَهَبْ لِي مِنْ لَدُنْكَ وَلِيّاً

Nipe *mrithi* kutoka kwako...[67]

---

[65] - Sura 10 Aya 62 . Pia tazama Sura 8 Aya 72-73.
[66] - Sura 2 Aya 282.
[67] - Sura 19 Aya 5.

Neno lililotumika katika Aya hii kumaanisha mrithi ni *Waliyy* (Walii).[68]

KANUNI (LAW)

Baada ya kuona kwamba neno hilo *"Waliyyu (Walii)"* lina maana tafauti, ni vyema kuzungumzia kidogo juu ya msimamo wa wanavyuoni kuhusu neno la namna hii. Wanavyuoni wametafautiana juu ya neno lenye maana nyingi ***(mushtarak)*** likitumika katika Aya au Hadithi je huwa maana zote hizo zimekusudiwa? Wengine wakajuzisha kuwa maana zote zizingatiwe; na wengine wanaona kwamba ikiwa kuna *qarina (context)* itayobainisha maana moja iliokusudiwa basi itazingatiwa na kama hakuna basi itabidi neno hilo liachwe mpaka tupate ushahidi juu ya maana iliokusudiwa. Na kauli kwamba neno lenye maana nyingi *(mushtarak)* linaachwa kama lilivyo hadi kuwe na ushahidi juu ya maana iliothibiti, ndio kauli ya *jumhur* (majority) ya Umma kwa mujibu wa alivyosema Sheikh Muhammad Al-Khudhari. Anasema:

> Na makusudio ya ujumla wa *mushtarak* (neno lenye maana nyingi) ni (kuwa) litumike bila ya kufungamanishwa (na kitu) na zikusudiwe maana zake zote. Na hili *Jumhur* wamelikataa.[69]

Pia katika kitabu *Matnu Al-Tanqih* kilicho pamoja na sherehe yake *Sharhu Al-Talwih* na kikaambatanishwa pia na kitabu *Al-Tanqih Maa Al-Tawdhih* yamekuja maneno yafuatayo: "…Hukumu ya *Mushtarak* (neno lenye maana nyingi) ni kulitazama hadi ipate uzito moja ya maana zake".[70] Kisha mshereheshaji mmoja – katika sheherehe mbili hizo – akasema:

> Na kutoka kwa (Al-Imamu) Al-Shafi Allah amrehemu (ni) kwamba *(Al-mushtarak)* inapewa maana zote mbili ikiwa hakuna qarina (context): wala haipewi maana moja maalumu ila kwa (kuwepo kwa) qarina (inayoonesha maana hio).[71]

---

[68] - Kwa kujua zaidi maana ya neno *Waliyy* (Walii), unaweza kutazama kamusi mashuhuri la Kiarabu *Lisanu Al-Arab J.* 15, uk. 400-407, mada (Waliy).

[69] - Sheikh Muhammad Al-Khudhari *Usulu Al-Fiqhi* uk.177.

[70] - J. 1, uk. 163.

[71] - Marejeo iliotangulia uk. 164.

Anasema Al-Imamu Al-Salimi (Ibadhi): “Na kauli ya kutokulitumia neno *mushtarak* (neno lenye maana nyingi) wakati mmoja katika maana zake zote ndio (kauli) sahihi kwetu”.[72]

Ama Al-‘Allamah Muhammad Ridhaa Al-Mudhaffar (Shia) – baada ya maelezo – anaishia kwa kusema: “Na kilicho haki kwetu ni kutojuzu matumizi kama haya (yaani kutojuzu kulitumia neno *mushtarak* katika maana zake zote)”.[73]

Anasema Al-Qurtubi:

> Kwa sababu lafdhi ikiwa inaingia katika maana mbili sawa sawa, basi kilichowajibu ni kutokuiendea maana moja (katika maana mbili hizo) ila kwa (kuwepo kwa) ushahidi (wenye kuonesha kwamba maana moja hio ndio iliokusudiwa).[74]

Baada ya nukulu hizi mbili tatu za wanavyuoni wakubwa, ni vyema ukaelewa kwamba wao hawatafautiani kujuzu kutumika ***mushtarak*** (neno lenye maana nyingi) wakati mmoja na ikawa maana iliokusudiwa ni moja ikiwa kuna *qarina*[75] yenye kuonesha kwamba maana kadha ndio iliokusudiwa. Katika hali hii hakuna khilafu madamu uko ushahidi wa kuwa iliokusudiwa katika maana nyingi hizo ni maana kadha, lakini khilafu ni pale pasipo na ushahidi juu ya maana moja maalumu.[76] Anasema Al-Imamu Al-Salimi:

---

[72] - Al-Salimi *Sharhu Tal-A’ti Al-Shams* j. 1, uk 138.

[73] - Muhammad Ridhaa Al-Mudhaffar *Usulu Al-Fiqhi* j. 1, uk. 32 .

[74] - Al-Qurtubi Al-Hafid *Bidayatu Al-Mujtahid* j. 1, uk. 39.

[75] - *Qarina* ni *context* au vifuatanishi vya maneno yaani kitu kilichomo katika msururu wa maneno. Na pia ushahidi mwengine ulio nje ya maneno hayo, pia huitwa *qarina*, lakini ushahidi ulio nje ya maneno kwa Kiingereza hauitwi *context*. Kwa hivyo, neno la Kiarabu *Qarina* lina maana pana zaidi kuliko neno la Kiingereza c*ontext*.

[76] - Maelezo juu ya maudhui hii ni marefu kidogo, lakini tunazungumzia sehemu inayohitajika tu katika maudhui yetu.

> Na faida ya khilafu iliotangulia katika hukumu ya *Al-Mushtarak* (neno lenye maana nyingi) ni pale wakati pasipo na *qarina (context)* yenye kuonesha kukusudiwa kwa moja ya maana zake….[77]

Anasema Al-‘Allamah Muhammad Ridhaa Al-Mudhaffar:

> Hakuna shaka kwamba inajuzu kuitumia *Al-Mushtarak* (neno lenye maana nyingi) katika maana yake moja ikiwa kuna *qarina (context)* yenye kuainisha (maana moja hio).[78]

Na hili ndilo alililolisema Al-Imamu Al-Shafi katika nukulu hio tulioinukuu kabla, akasema: “….Wala haipewi maana moja maalumu ila kwa (kuwepo) qarina (inayoonesha maana hio)”.

MFANO

Pamoja na kuwa mifano tumeitoa katika vitabu tafauti lakini huenda ikawa msomaji wa kitabu hiki hakuwahi kuvisoma vitabu hivyo. Mfano mzuri wa kukufahamisha hili ni neno **”عَيْنٌ“** “Ain”. Neno hili katika lugha ya kiarabu lina maana nyingi. Kati ya hizo ni:

1) Jicho.
2) Dhahabu.
3) Chemchem.
4) Dhati.
5) Jasusi.

Lakini ikiwa nitasema nimekunywa maji katika **عَيْنٌ** *Ain* ile pale, basi utafahamu kuwa ninachokikusudia ni chemchem, kwa sababu kifuatanishi *(qarina au context)* hapa ni kule kutajwa kwa maneno “kunywa maji” ndiko kulikobainisha makusudio yangu. Sasa tazama tofauti ya hayo na nitakaposema kuwa Marekani katuma **عَيْنٌ** “Ain” wake kupeleleza pahala fulani, hapa hutosema tena kuwa katuma chemchem, bali utasema katuma jasusi. Na halkadhalika katika lugha ya Kiswahili, iwapo nitasema nipe mto nilalie, bila shaka utafahamu tofauti na nitakaposema kwamba mto huu una samaki wengi, pamoja na kuwa neno ni lile lile. Lakini kama nitasema nimeona mto, bila ya kuainisha mto gani wala kutaja vifuatanishi vya maneno *(qarain au contexts)* vyenye kubainisha makusudio yangu ya

[77] - Al-Salimi *Sharhu Tala’ti Al-Shams* j. 1, uk 137.
[78] - Muhammad Ridhaa Al-Mudhaffar *Usulu Al-Fiqhi* j. 1, uk. 32.

neno *mto* basi hapa ndipo pale wanapotafautiana wanavyuoni juu ya kujuzu au kutokujuzu kuzikubali maana zote za neno hilo.

Kwa hali yoyote ile, msingi tunaokusudia kuuzungumzia katika Aya yetu hio isemayo: **“Hakika *Walii* wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini tu”.,** hauna khilafu (kwa kadiri ninavyojua); isipokuwa matawi yake ndio yenye khilafu. Msingi huo ambao wanavyuoni hawatafautiani ndani yake ni yale maneno tuliotangulia kuyanukuu kutoka kwa Al-Imamu Al-Salimi, Al-allamah Al-Mudhaffar na Al-Imamu Al-Shafi kwamba:

> Hakuna shaka kwamba inajuzu kuitumia *Al-mushtarak* (neno lenye maana nyingi) katika maana yake moja ikiwa kuna qarina (context au vifuatanishi vya maneno) yenye kuainisha (maana moja hio).

Katika hili – kama alivyosema – mwanachuoni huyu hakuna shaka kabisa. Kwa hivyo, kazi yetu iliobaki ni kuvitazama vifuatanishi vya maneno vilivyomo katika Aya hio: je vinaonesha maana gani kuwa ndio iliokusudiwa?

TAFSIRI SAHIHI YA AYA HIO

Katika kitabu chetu *Mezani Ya Haki* tumebainisha baadhi ya njia (methodologies) sahihi zinazotumika kwa wanavyuoni wa Umma ili kuweza kufikia maana sahihi ya Aya na Hadithi. Sasa kabla ya kuendelea kuielezea tafsiri sahihi ya Aya hio, ningependa kunukuu baadhi ya nilioyasema huko ili tuweze kufahamiana vizuri. Nilisema:

> Miongoni mwa mambo ambayo wanavyuoni wa tafsiri wanayazingatia katika kuifasiri Qur-ani ni:
>
> *1) SIBAQ* (Maneno yaliotangulia).
> *2) SIYAQ* (Maneno yanayofatia).
> *3) KANUNI ZA KIUSULI* (fundamentals of Islamic Jurisprudence) yaani misingi ya elimu ya Sharia ambayo ni katika fani zinazotumika katika kufasiria maandiko na kwa hivyo kuifikia tafsiri sahihi ya Qur-ani na Hadithi.

4) KANUNI ZA KILUGHA.

Ni lazima turudi katika misingi hii ili tusije tukawa kama wale wenye kuchukua juu juu tu na ilhali sisi tunawacheka wao kwa kosa hilo hilo. Sasa ili tuifahamu Aya hii ni lazima tuiweke katika kila kanuni katika kanuni zinazotumika katika kuifasiri Qur-ani. Natuanze kuitazama *Sibaq* ya Aya.

Sibaq ni msingi mmoja ambao unatumika katika kuyafahamu makusudio ya Aya na Hadithi. Nao si msingi wa Kisunni na Kiibadhi tu, bali ni msingi unaotumika kwa Umma mzima, kwani ni msingi uliojengeka katika lugha ya Kiarabu.[79] Na kwa hivyo, hata katika vitabu vya Kishia utaukuta ukitumiwa. Kwa mfano katika kitabu cha Al-Sayyid Saeed Akhtar Rizvi *Tangazo La Ghadir* kilichofasiriwa na Sheikh Musabbah Sha'aban Mapinda na kuchapishwa na *Bilal Muslim* utaona katika ukurasa wa 21 wa kitabu hicho, wakati Al-Sayyid yumo katika kuthibitisha kwamba neno *Mawla*[80] lililomo katika Hadithi hio ya *Ghadir Khummi* maana yake ni: "Mwenye mamlaka". Katika kichwa cha habari alisema hivi: "Maana ya neno *Mawla* kwa mujibu wa fuo lake (kwa mujibu wa maneno yatanguliavyo na yafuatavyo)".[81] Halafu akaanza maudhui yake kwa kuelezea kanuni hii ya *Sibaq* na *Siyaq.* Na maneno yenye maana kama hio pia yamo katika kitabu *Al-Wasiy*[82] cha Ayatu-Llah, Sayyid Ali Al-Haydari.

[79] - Bali huu ni msingi uliomo katika lugha zote; na kwa hivyo ni jambo la kimaumbile ambalo binaadamu hawatafautiani.

[80] - Ukweli ni kuwa neno "Mawla" katika Hadithi hio ya Ghadir halina maana hio ya mtawala, kama utavyoona kwa ufupi humu katika sura ya nne inayohusu mjadala wetu katika intaneti.

[81] - Maneno yaliomo ndani ya breketi: "Kwa mujibu wa maneno yatanguliavyo na yafuatavyo" si maneno yangu: ni tafsiri ya Sheikh Mapinda.

[82] - Uk. 100.

SIBAQ (MANENO YALIOTANGULIA)

Sasa baada ya hayo na-tuitazame *Sibaq* ya Aya hio tunayoijadili hapa. Tukirudi katika Aya yetu hio tunayoijadili hapa inayosema:

إِنَّمَا وَلِيُّكُمُ اللَّهُ وَرَسُولُهُ وَالَّذِينَ آمَنُوا الَّذِينَ يُقِيمُونَ الصَّلاةَ وَيُؤْتُونَ الزَّكَاةَ وَهُمْ رَاكِعُونَ

Hakika *Walii* wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini tu: wale ambao wanasimamisha sala na wanatoa zaka nao ni wenye kurukuu"[83]

tunakuta kwamba Aya hio imetanguliwa na Aya hizi:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لا تَتَّخِذُوا الْيَهُودَ وَالنَّصَارَى أَوْلِيَاءَ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ وَمَنْ يَتَوَلَّهُمْ مِنْكُمْ فَإِنَّهُ مِنْهُمْ إِنَّ اللَّهَ لا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ

Enyi mulioamini musiwafanye Mayahudi na Manasara (Wakiristo) kuwa (ndio) rafiki zenu: wao wenyewe kwa wenyewe ni marafiki: na atayewafanya marafiki miongoni mwenu basi hakika yeye ni katika wao, hakika Allah hawaongozi watu madhalimu.[84]

فَتَرَى الَّذِينَ فِي قُلُوبِهِمْ مَرَضٌ يُسَارِعُونَ فِيهِم يَقُولُونَ نَخْشَى أَنْ تُصِيبَنَا دَائِرَةٌ فَعَسَى اللَّهُ أَنْ يَأْتِيَ بِالْفَتْحِ أَوْ أَمْرٍ مِنْ عِنْدِهِ فَيُصْبِحُوا عَلَى مَا أَسَرُّوا فِي أَنفُسِهِمْ نَادِمِينَ

Basi utawaona wale ambao katika mioyo yao kuna maradhi, wanawakimbilia wao: wanasema tunaogopa (na sisi) kutupata mzunguko (mambo yasije yakatugeukia); Basi huenda Allah akaleta ushindi au jambo (jengine) litokalo kwake, (na hapo) wawe ni wenye kujuta kwa yale walioyaficha katika nafsi zao.[85]

---

[83] - Sura 5 Aya 55.
[84] - Sura 5 Aya 51.
[85] - Sura 5 Aya 52.

وَيَقُولُ الَّذِينَ آمَنُوا أَهَؤُلَاءِ الَّذِينَ أَقْسَمُوا بِاللَّهِ جَهْدَ أَيْمَانِهِمْ إِنَّهُمْ لَمَعَكُمْ حَبِطَتْ أَعْمَالُهُمْ فَأَصْبَحُوا خَاسِرِينَ

Na walioamini watasema (wakati huo): 'Je hawa ndio walioapa kwa (jina la) Allah viapo vya nguvu kwamba wako pamoja na nyinyi? Vitendo vyao vimeporomoka na wamekuwa wenye kuhasirika.[86]

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا مَنْ يَرْتَدَّ مِنْكُمْ عَنْ دِينِهِ فَسَوْفَ يَأْتِي اللَّهُ بِقَوْمٍ يُحِبُّهُمْ وَيُحِبُّونَهُ أَذِلَّةٍ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ أَعِزَّةٍ عَلَى الْكَافِرِينَ يُجَاهِدُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَلَا يَخَافُونَ لَوْمَةَ لَائِمٍ ذَلِكَ فَضْلُ اللَّهِ يُؤْتِيهِ مَنْ يَشَاءُ وَاللَّهُ وَاسِعٌ عَلِيمٌ

Enyi mulioamini! Aliyeiacha miongoni mwenu dini yake, basi Allah ataleta watu anaowapenda nao wanampenda; ni wanyenyekevu kwa Waislamu (wenzao); wenye nguvu kwa makafiri; wanafanya jihadi katika njia ya Allah wala hawaogopi lawama za mwenye kulaumu, hio ni fadhila ya Allah anampa amtakaye na Allah ni Mwenye wasaa na ni Mjuzi (wa kila kitu).[87]

Baada ya Aya nne hizo, ndio ikaja Aya hio tunayoijadili ikasema:

إِنَّمَا وَلِيُّكُمُ اللَّهُ وَرَسُولُهُ وَالَّذِينَ آمَنُوا الَّذِينَ يُقِيمُونَ الصَّلَاةَ وَيُؤْتُونَ الزَّكَاةَ وَهُمْ رَاكِعُونَ

Hakika *Walii* wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini tu: wale ambao wanasimamisha sala na wanatoa zaka nao ni wenye kurukuu.[88]

Kwa hivyo, hapa kila mwenye akili – licha ya mwenye elimu – anaona kwamba neno ***Waliyyu (Walii)*** ambalo limo katika Aya hio, huwezi kulipa isipokuwa tafsiri ya kipenzi ambayo ni maana ya pili katika jumla ya maana tulizozitaja kabla. Na hii ni kwa sababu Aya za mwanzo

[86] - Sura 5 Aya 53.
[87] - Sura 5 Aya 54.
[88] - Sura 5 Aya 55.

zimetukataza kuwafanya makafiri kuwa ndio marafiki na vipenzi vyetu yaani zikatwambia kwamba vipenzi vyetu si Mayahudi na Wakiristo. Ikawa katika nafsi zetu – kama tutavyobainisha zaidi *In shaa Allah* – kuna suali: "sasa vipenzi vyetu ni nani", au suali: "kwanini tusiwafanye makafiri kuwa ni vipenzi?" Ndio ikaja Aya hii, kama ni jawabu ya suala hilo lililomo katika nafsi, ikasema: **"Hakika"**[89] yaani kwa sababu: ***"Walii* wenu"** yaani kipenzi chenu **"Ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini tu: wale ambao wanasimamisha sala na wanatoa zaka nao ni wenye kurukuu".**

Hivi ndivyo Aya zinavyofungamana: kwa kuzitazama Aya zilizotangulia, jawabu unaikuta iko wazi na kwamba dai la kuwa neno ***Waliyyu (Walii)*** hapa maana yake ni msimamizi wa mambo yaani mtawala, si makusudio ya Aya hii kamwe.

SIYAQ (MANENO YANAYOFATIA)

Baada ya kutazama ***Sibaq*** (Maneno yaliotangulia) ya Aya hio, sasa na-tutazame ***Siyaq*** (Maneno yanayofatia). Aya zinazofatia zinasema:

وَمَنْ يَتَوَلَّ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَالَّذِينَ آمَنُوا فَإِنَّ حِزْبَ اللَّهِ هُمُ الْغَالِبُونَ

Na atayemfanya Allah na Mtume wake na wale walioamini kuwa ndio vipenzi vyake, basi hakika kundi la Allah ndilo litaloshinda.[90]

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لا تَتَّخِذُوا الَّذِينَ اتَّخَذُوا دِينَكُمْ هُزُواً وَلَعِباً مِنْ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ مِنْ قَبْلِكُمْ وَالْكُفَّارَ أَوْلِيَاءَ …

Enyi mulioamini musiwafanye marafiki wale ambao wanaifanyia mzaha na mchezo dini yenu, miongoni mwa wale waliopewa Kitabu kabla yenu na makafiri…….[91]

---

[89] - Neno "Hakika" hapa ni tafsiri ya neno *"Inna"* nalo – kama tulivyobainisha – lina maana ya *Illa* (Sababu). Na kwa hivyo, maana ya Aya hio ni: **"Kwani"** au **"Kwa sababu kipenzi chenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini tu…"**

[90] - Sura 5 Aya 56.

وَإِذَا نَادَيْتُمْ إِلَى الصَّلاةِ اتَّخَذُوهَا هُزُواً وَلَعِباً ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ قَوْمٌ لا يَعْقِلُونَ

Na munapoita katika sala (munapoadhini) wanaifanyia mzaha na mchezo. Hayo ni kwa sababu wao ni watu wasiofahamu (kwa akili zao). [92]

Halafu baada ya Aya hizi, utaona zinafuata Aya nyengine nyingi za maudhui hio hio. Kwa hivyo, kudai kwamba Aya hii: **"Hakika *Walii* wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini tu…"..** imemshukia Ali na kwamba maana ya neno ***Waliyyu (Walii)*** hapa maana yake ni msimamizi wa mambo yaani mtawala, ni kuilazimisha tafsiri ambayo haifahamiki kwa mujibu wa ***Sibaq*** (Maneno yaliotangulia) wala kwa mujibu wa ***Siyaq*** (Maneno yanayofatia).

[91] - Sura 5 Aya 57.
[92] - Sura 5 Aya 58.

KANUNI ZA KIUSULI (fundamentals of Islamic Jurisprudence) ni misingi ya elimu ya Sharia ambayo ni katika fani zinazotumika katika kufasiria maandiko na kwa hivyo kuifikia tafsiri sahihi ya Qur-ani na Hadithi.[93]

Katika kuielezea kanuni hii, tulisema – katika *Mezani Ya Haki* – maneno haya yafuatayo – hapa nayapunguza kwa ajili ya mukhtasar – nimesema:

> Katika elimu ya *usulil-fiq-hi* kuna kitu kinaitwa **"عِلَّةٌ"** *"illa"* nayo ni sababu iliopelekea kuwepo kwa hukumu fulani au yenye kueleza kwanini pametolewa hukumu fulani au kwanini pamesemwa maneno fulani. Kielimu – kwa mtazamo wa baadhi ya wanavyuoni – kuna tofauti ndogo baina ya *"illa"* na "sababu" lakini kwa Kiswahili bali kwa kilugha huwa tunaifasiri *"illa"* kuwa ni "sababu". Kwa hivyo katika kitabu hiki tutalifasiri neno *"illa"* kuwa maana yake ni "sababu".
>
> Sasa *"illa"* (sababu) ziko za namna mbili kuu. Moja katika aina mbili hizo ni **"الْعِلَلُ الْمَنْصُوْصُ عَلَيْهَا"** (sababu zilizoelezwa kwa uwazi). Hizi kuna njia zake za kuzijua. Miongoni mwa njia hizo ni pale panapotajwa amri, au katazo au – wakati mwengine – habari kisha ikatiliwa mkazo kwa kuletwa herufi **إِنَّ الْمَكْسُوْرَةُ الْمُشَدَّدَةُ *"INNA*** ambayo *hamza* yake *(Alifu* yake) ina *Kasra* na *Nuni* yake ina *Shada*," basi hii huwa imeeleza *"Illa"* (sababu) ya amri hio au katazo hilo au habari hio iliotajwa kabla yake. Na hii ni pale ambapo kuna mfungamano wa maana baina ya maneno yaliotangulia kabla ya herufi **"إن" *"INNA"*** na maneno yanayofuatia baada yake. Na jambo hili liko wazi katika Qur-ani na limo katika

[93] - Ingawa huu si msingi mama wa kuifasiri Qur-ani: msingi mama wa tafsiri ya Qur-ani ni kuifasiri Qur-ani kwa Qur-ani yenyewe kisha Qur-ani kwa Hadithi sahihi za Mtume (s.a.w.), kwani mambo mawili hayo ni Wahyi, na Wahyi haugongani bali unajifasiri wenyewe kwa wenyewe. Pamoja na yote hayo, lugha ya Kiarabu ndio taa ya kuzifahamu Aya na Hadithi, kwani Qur-ani imeshuka kwa lugha ya Kiarabu, na kwa hivyo ni lazima tafsiri isigongane na lugha bali iwe kwa mujibu wa lugha, kwani Qur-ani haikwenda kinyume na lugha ya Kiarabu, bali ina Ibara ambazo kila aliyejaribu kutaka kuziiga ili aoneshe kuwa naye anaweza kuleta mfano wake, basi kageuka kuwa kichekesho cha kihistoria, kama vile Musailama Al-Kadhaab.

sehemu zake nyingi. Sasa soma mifano miwili mitatu ya Aya za Qur-ani ili izidi kukubainikia maudhi hii.

ILLA (SABABU) ILIOLETWA NA HERUFI *INNA* BAADA YA AMRI

Allah (S.W.) anasema:

"فَاقْضِ مَا أَنْتَ قَاضٍ* إِنَّمَا تَقْضِي هَذِهِ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا"**

"Hukumu unacho hukumu *_Hakika_ ya unachohukumu ni maisha haya ya kidunia tu". [94]

Sehemu ya kwanza ya Aya hii inatoa amri, nayo ni amri ya kudharau **(الأَمْرُ عَلَى التَّحْقِيْرِ).** Hapo – katika sehemu hio ya Aya – waliokuwa wachawi katika zama za Fir'auna wanatoa amri ya kumdharau Fir'auna kwa kusema: **"Hukumu unachohukumu"** kisha ndio wakaleta *"Illa"* (sababu) yao ya kusema maneno hayo, wakasema: **"Hakika unachokihukumu ni maisha haya ya dunia tu" –** *huna lako jambo: leo unahukumu; kesho unahukumiwa hali ya kuwa ni dhalili.* Katika utoaji huo wa *"Illa"* (sababu), herufi iliotumika ni ile ile **"إِنَّ" *"INNA".*** Na kwa hivyo kuna mshikamano baina ya maneno ya kwanza na maneno ya pili, kwani maneno ya pili ni *"Illa"* (sababu) ya maneno yaliotangulia.

ILLA (SABABU) ILIOLETWA NA HERUFI *INNA* BAADA YA KATAZO

Mwenyezi Mungu anasema:

وَلا تَقْرَبُوا الزِّنَى* إِنَّهُ كَانَ فَاحِشَةً وَسَاءَ سَبِيلاً**

Wala musiikurubie zina*Hakika yake ni (kitu) kiovu na ni njia mbaya ilioje.** [95]

Katika sehemu ya kwanza ya Aya hii kuna katazo: **"Wala musiikurubie Zina".** Ikawa katika nafsi kuna kujiuliza: "Kwanini tusiikurubie: kuna

[94] - Sura 20 Aya 72.
[95] - Sura ya 17, Aya 32.

nini ndani yake?” Ikaja sababu ya katazo hilo: Mwenyezi Mungu akatoa *“illa”* (sababu), na katika utoaji huo wa *“illa”* (sababu) herufi iliotumika ni ile ile **“إنَّ” *“INNA”*.** Akasema Mwenyezi Mungu: **“Hakika yake ni (kitu) kiovu na ni njia mbaya ilioje”.** Na kwa hivyo kuna mshikamano baina ya maneno ya kwanza na maneno ya pili, kwani maneno ya pili ni *“illa”* (sababu) yenye kueleza kwanini kumekuwa na katazo hilo.

ILLA (SABABU) ILIOLETWA NA HERUFI INNA BAADA YA HABARI

Mwenyezi Mungu anasema:

وَلَمَّا جَاءَتْ رُسُلُنَا إِبْرَاهِيمَ بِالْبُشْرَى قَالُوا إِنَّا مُهْلِكُو أَهْلِ هَذِهِ الْقَرْيَةِ، إِنَّ أَهْلَهَا كَانُوا ظَالِمِينَ

Na wakati wajumbe wetu walipomjia Ibrahim na habari njema, walisema hakika yetu sisi ni wenye kuwaangamiza watu wa mji huu, *hakika* ya watu wake wamekuwa madhalimu.[96]

Mwenyezi Mungu hapa anatoa habari ya matokeo yaliotokea katika zama za Nabii Ibrahim (a.s.) ya kuangamizwa kwa watu wa Nabii Lut (a.s.). Katika kusimulia habari za maangamizo hayo, Mwenyezi Mungu anatoa *“Illa”* (sababu) kwanini watu hao wameangamizwa. Katika utoaji huo wa *“Illa”* (sababu) herufi iliotumika kuonesha *“Illa”* (sababu) hio ni ile ile **“إنَّ” *“INNA”*.** Na kwa hivyo tafsiri ya Aya ni: **“Tuliwaangamiza watu hao kwa sababu ya udhalimu wao”:** udhalimu ndio *“Illa”* (sababu) ya kuangamizwa huko. Na kwa hivyo kuna mshikamano baina ya maneno ya kwanza na maneno ya pili, kwani maneno ya pili ni *“Illa”* (sababu) ya maneno yaliotangulia.[97]

Sasa baada ya haya, naturudi kuitazama Aya yetu hio isemayo:

إِنَّمَا وَلِيُّكُمُ اللهُ وَرَسُوْلُهُ وَالَّذِيْنَ آمَنُوْا الَّذِيْنَ يُقِيْمُوْنَ الصَّلاَةَ وَيُؤْتُوْنَ الزَّكاَةَ وَهُمْ رَاكِعُوْنَ

[96] - Sura 29, Aya 31.

[97] - Mwisho wa nilioyasema katika *Mezani Ya Haki* pamoja na kuondoa baadhi ya mambo kwa ajili ya kufupisha.

Hakika *Walii* wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini tu: wale ambao wanasimamisha sala na wanatoa zaka nao ni wenye kurukuu.[98]

Tukirudi katika Aya yetu hio, tutaona kwamba Aya hio imeanzia na herufi hio hio **إِنَّ الْمَكْسُوْرَةُ الْمُشَدَّدَةُ *"INNA*** ambayo *hamza* yake *(Alifu* yake) ina *Kasra* na *Nuni* yake ina *Shada*". Na kwa hivyo, Aya hii – kwa sababu ina mfungamano wa wazi na Aya zilizotangulia, basi ni wazi kwamba inaelezea sababu ya maneno yaliomo katika Aya hizo zilizotangulia. Sasa tazama sababu zote mbili, kisha tazama ipi inakubaliana na Aya zilizotangulia.

Moja: ni kuwa tulifasiri neno ***Waliyyu (Walii)*** hapa kuwa maana yake ni msimamizi yaani mtawala. Na kwa hivyo, ukichukua Aya zilizopita pamoja na *Illa (Sababu)* iliomo katika Aya hii isemayo: **"Hakika *Walii* wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini tu…",** maana itakuwa: "musiwafanye makafiri kuwa ni rafiki zenu, kwa sababu Allah, Mtume wake na Ali ndio watawala wenu!" Bila shaka hii ni tafsiri ya ajabu na yakujikalifisha. Ni wazi kwamba hakuna mshikamano wa maana katika tafsiri hii. Na hili haliwezekani katika maneno ya mtu mwenye hekima, basi vipi litawezekana katika maneno ya Muumba wa mtu na hekima yake?! Allah anakisifu kitabu chake kwa kusema kwamba Qur-ani hii ni:

قُرْآناً عَرَبِيّاً غَيْرَ ذِي عِوَجٍ لَعَلَّه….

Qur-ani ya Kiarabu isio na kombo (kasoro)…..[99]

Na anasema:

كِتَابٌ أُحْكِمَتْ آيَاتُهُ ثُمَّ فُصِّلَتْ مِنْ لَدُنْ حَكِيمٍ خَبِيرٍ

[98] - Sura 5 Aya 55.
[99] - Sura 39 Aya 28.

Kitabu (hiki) Aya zake zimetengenezwa vizuri (hiziingii kasoro) kisha zikafafanuliwa, kutoka kwa (Allah) Mwenye hekima, Mwenye ujuzi.[100]

Na akasema:

…وَإِنَّهُ لَكِتَابٌ عَزِيزٌ (41) لا يَأْتِيهِ الْبَاطِلُ مِنْ بَيْنِ يَدَيْهِ وَلا مِنْ خَلْفِهِ تَنْزِيلٌ مِنْ حَكِيمٍ حَمِيدٍ

…Na hakika yake ni Kitabu Kitakatifu*Hakijiwi na batili mbele yake wala nyuma yake, ni uteremsho utokao kwa (Allah) Mwenye hekima, Mwenye kuhimidiwa.[101]**

Kwa hivyo, lazima tafsiri iwe imejengeka katika lugha na iwe na mshikamano katika Aya zake hasa hasa zile Aya zilizo katika *siyaq* moja (zilizoko katika msururu mmoja).

Pili: ni kuwa tulifasiri neno ***Waliyyu (Walii)*** hapo kuwa maana yake ni rafiki au kipenzi. Na kwa hivyo, ukichukua Aya zilizopita pamoja na *Illa (Sababu)* iliomo katika Aya hii isemayo: **"Hakika *Walii* wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini tu…",** maana itakuwa: "musiwafanye makafiri kuwa ni rafiki zenu au vipenzi vyenu, kwa sababu Allah, Mtume wake na Waumini ndio marafiki zenu au ndio vipenzi vyenu". Utaona mshikamano 100% baina ya *Illa* (sababu) na *ma'alul* yaani – kwa hapa – ni lile katazo lenyewe: yani kuna mshikamano baina ya katazo na sababu ya katazo hilo: katazo ni lile lililomo katika Aya zilizotangulia kwamba **"Musiwafanye makafiri kuwa ni rafiki zenu",** na sababu ya katazo ni **"Kwa sababu Allah, Mtume wake na Waumini ndio marafiki zenu au vipenzi vyenu".** Hii ndio tafsiri sahihi kwa kutazama misingi hii ya tafsiri.

[100] - Sura 11 Aya 1.
[101] - Sura 41, Aya 41-42.

KANUNI NYENGINE YA KIUSULI

Aya inasema: **“Hakika *Walii* wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini tu: ***wale ambao*** wanasimamisha sala na wanatoa zaka nao ni wenye kurukuu”.**[102]

Neno la Kiarabu lililotumika kumaanisha ***wale ambao*** ni neno: **الَّذِيْنَ *Alladhiina.*** Neno hili – kama ilivyo katika usuli – ni miongoni mwa *siyaghu al-umum.*[103] Kwa hivyo, hapa wanaingia waumini wote: kila ambaye anaitwa Mu’umini.

Anasema Dr. Wahbat Al-Zuhaili, akitaja mambo yenye kumaanisha ujumla: **“Na katika hayo ni *Al-Asmau Al-Mawsulah* (Relative pronouns) kama vile (neno)…..*Alladhina”..***[104]

Anasema Sheikh Muhammad Al-Khudhari: **“(Miongoni mwa) njia za ujumla ni….*Al-Mawsulat* (Relative pronouns)”.**[105] Na kama unavyojua kwamba neno: *“Alladhina”* ni katika ***Al-mawsulat* (Relative pronouns)”.** Na hili ni mashuhuri liko katika vitabu tafauti.

Kwa hivyo, kwa kuzingatia ukweli kwamba katika Aya hio kuna neno ***“Alladhiina”*** ambalo linamaanisha *al-u’mum* (Ujumla jamala), basi huwezi tena kusema kwamba neno *Waliyyu **(Walii)*** katika Aya hio maana yake ni mtawala, kwani neno **“Wale walioamini”** linamaanisha ujumla jamala. Na kwa hivyo, ikiwa utalifasiri neno hilo kuwa maana yake ni mtawala, basi maana itakuwa: **“Hakika Mtawala wetu ni Allah, Mtume (s.a.w.) na wote walioamini”.** Kwa hivyo, kila aliyeamini ni mtawala wetu: mtawaliwa yuwapi?!

---

[102] - Sura 5 Aya 55.

[103] - *Siaghat al-umum* (form implying general sense) maana yake ni njia ya kuonesha ujumla jamala.

[104] - Al-Zuhaili *Usulu Al-Fiq-hi* j. 1, uk. 242.

[105] - Muhammad Al-Khudhari *Usulu Al-Fiq-hi* uk.179.

Ukiniambia kwamba: “Aaaa wewe hujafahamu vizuri! Unajua neno *Alladhina* kweli linamaanisha wingi; lakini katika lugha ya Kiarabu hutumika wakati mwengine wingi na hukusudiwa mmoja; na kwa hivyo aliyekusudiwa hapa ni Al-Imamu Ali”. Ukiniambia hivyo, nitakujibu kwamba kweli neno ***Alladhina*** linamaanisha wingi na kweli katika lugha ya Kiarabu hutumika wakati mwengine wingi na hukusudiwa mmoja, lakini hili linabomolewa na ukweli kwamba hata tukijaalia kuwa kweli Aya imemshukia Ali na kwamba neno *Waliyyu* ***(Walii)*** katika Aya hio maana yake ni mtawala, basi kanuni ni kuwa:

الْعِبْرَةُ بِعُمُوْمِ اللَّفْظِ لاَ بِخُصُوْصِ السَّبَبِ

Chenye kuzingatiwa ni ujumla uliomo katika lafdhi: si sababu (ya kwanini au kwa nani Aya imeteremka au Hadithi imenenwa.[106]

Kwa hivyo, hata kama Aya hio imemteremkia Ali, basi Ali atakuwa mtawala wetu na kila muumini naye atakuwa mtawala wetu au atafaa kuwa mtawala wetu, kwani lafdhi ya Aya ni ya ujumla **(لأَنَّ اللَّفْظَ عَامٌّ)**. Na hili bila shaka ni batili, kwa hivyo, hakuna tafsiri sahihi isipokuwa ile ile ambayo tumeitoa kabla, kwamba Waislamu wanatakiwa wamfanye Allah, Mtume (s.a.w.) na Waislamu wenzao kuwa ndio marafiki wao na vipenzi vyao, baada ya kuwa – katika Aya zilizotangulia na za baadae – wamekatazwa kuwafanya makafiri kuwa ndio marafiki wao. Hii ndio tafsiri sahihi ya Aya hio baada ya kuirudisha Aya hio katika fani za tafsiri: za lugha na usuli. Ama tafsiri kwamba Aya hio imemshukia Ali na kwamba ina maana ya kuwa yeye ni mtawala baada ya Mtume (s.a.w.), si tafsiri sahihi, na asili ya tafsiri hio ni zile riwaya zilizofinyangwa katika kiwanda cha Hadithi kule mjini Al-Kufa.

Mwisho natujiulize suala letu lile lile ambalo tutakuwa tukijiuliza sana: nalo ni kuwa ikiwa maana ya Aya hio:

> **Hakika *Walii* wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini tu”** ni **“Hakika Mtawala wenu au Msimamizi wa mambo yenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na Ali,”**

[106] - Dr. Wahbat Al-Zuhaili *Usulu Al-Fiq-hi* j. 1, uk. 265.

basi vipi tena Allah na Mtume wamekuwa watawala au wasimamizi wa mambo lakini Ali asiwe na hii ni habari kutoka kwa Allah tena neno lililotumika kumaanisha utawala huo wa viumbe wawili na Muumba mmoja, ni neno moja lililomo katika Aya moja?! Je kweli Allah anatoa habari ya kitu halafu habari hio haiwi?! Je unaonaje lau tutaambiwa kuwa Allah kasema: **"Hakika Kombo si mlevi"** halafu tukamkuta Kombo anapepesuka kwa bia, tutakubali kuwa aliyetoa habari hio ni Allah?! Au lau Allah atasema: **"Fulani ni kiongozi baada ya fulani"** halafu yule aliyebashiriwa kuwa kiongozi asiwe, tutakubali kuwa aliyetoa habari hio ni Allah?![107] Yote haya yanakuwekea wazi ukweli kwamba maana ya Aya hio ni: **"Hakika vipenzi vyenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na Waumini wote".**

[107] - Sheikh mmoja wa Zanzineti anasema kwamba hii ni kama vile Waislamu kulewa au kuzini ilhali wamekatazwa kufanya hivyo; kwa hivyo – anakusudia kusema kwamba – na hapa Masahaba waliasi tu kumfanya Ali kuwa ni khalifa. Lakini inaonesha kwamba Sheikh huyo kashindwa kujua kuwa kuna tafauti baina ya Allah kutoa amri na kutoa habari. Amri inawezekana watu wasiitekeleze, lakini habari ya Allah huwa ni kweli moja kwa moja: ikiwa ni habari ya jambo lililopita – kama vile kuangamizwa kwa watu wa Nabii Luti – basi huwa ni kweli jambo hilo lilitokea; na kama ni habari ya kitu kinachokuja – kama vile kiama – basi huwa ni kweli kitatokea. Hii ndio tafauti baina ya habari na amri: kwa hivyo, hapo katika Aya hio – ukisema kuwa Aya ina maana ya Uimamu na Ukhalifa wa Ali – basi jua kuwa unasema kwamba Allah katoa habari ya jambo ambalo halikuwa! Wala usijidanganye kwa kusema kwamba hapa Allah hakuwa akitoa habari, bali alikuwa akiamrisha tu kumfanya Ali kuwa ndiye khalifa baada ya Mtume (s.a.w.), lakini Masahaba wamekataa kuitekeleza amri yake! Kwani Aya hii ni habari (statement) na – kama tulivyobainisha katika *Mezani Ya Haki* – kwamba kuitoa habari na kuifanya kuwa ni amri, ni katika mlango wa majazi (metaphorical meaning), na kufanya hivyo haikubaliki ila kwa kuwepo *qarina* (*context* au ushahidi wa nje au ulio katika Aya hio hio) kwamba maana ya asili ya neno au sentensi si makusudio. Kwa hapa – licha ya kutokuwepo *qarina* (context) au ushahidi sahihi wa nje, basi *qarain* (*contexts*) zote zinaunga mkono tafsiri nilioitoa na zinaibomowa tafsiri ya Kishia.

KANUNI ZA KILUGHA

Katika *Mezani Ya Haki* kanuni hii tuliiruka. Tulifanya hivyo, kwani maelezo yake si mafupi na pia kwa kuzingatia ukweli kwamba kuifasiri kanuni hii na kuielezea kwa Kiswahili mpaka Mswahili wa kawaida akaweza kufahamu bila ya matatizo yoyote yale, kunahitaji juhudi ya ziada. Lakini hata hivyo, hapa nitajaribu kuielezea *nukta (point)* moja ya kilugha yenye kuhusiana na maudhui hii.

Neno la Kiarabu lililotumika kumaanisha "Hakika" katika Aya hio yenye kusema: **"Hakika *Walii* wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini tu…".** Ni neno **إِنَّمَا *Inna-maa.*** Asili ya neno ni **إِنَّ *Inna*** na **مَا *Maa*** imezidishwa. Na kwa kuzidishwa huko maana pia imezidi. Mwanzo ilikuwa ni herufi ya kutilia mkazo *(emphatic word)*, na kulitia jina *nasbu* (kwa lugha ya wote ni fat-ha); ilipoongezeka herufi **"ما"** imeongezeka faida zaidi: limekuwa sasa ni neno la kutilia mkazo na kukihusisha kitu na kitu kimoja tu: kisikivuuke kwenda kwenye kitu chengine, au kwa lugha ya kitaalamu ni **أَدَاةُ الْحَصْرِ وَالتَّوْكِيْدِ.** Yaani nikisema *Inna-maa uridu kadha* (Hakika ninachokitaka ni kitu kadhaa), basi hii kwa Kiarabu huitwa *Hasr* au *Qasru:*[108] yaani ninachokitaka ni kitu hicho tu: sitaki kitu chengine.

Sasa *hasr* au *qasru* ziko za namna tafauti. Moja ni ile iitwayo: ***"Qasru Qalb".*** Hii maana yake ni kuwa muhubiriwa (Addressee) anakuwa anadhania kitu kadha; wewe ukamwambia kinyume na vile anavyofikiria yeye na ikawa maneno yako umeyafungamanisha na kitu kimoja maalamu hicho hicho hayavuuki kwenda kwenye kitu chengine. Mfano ni kama Aya isemayo: **"Masihi mwana wa Maryamu hakuwa (vyengine) ila ni Mtume"..** Hii inaitwa ***"Qasru Qalb"*** (Kuyaletea maneno kinyume chake na kuyafunga yakawa na maana moja tu). Na hii ni kwa sababu Aya hii ni jawabu kwa Wakiristo wanaoitakidi kwamba Isa (a.s) ni mungu-mwana! Allah akaipindua itikadi yao hio na kuleta maneno kinyume na itikadi yao hio, kisha akayafunga maneno yake na kitu kimoja tu ambacho ndio itikadi

[108] - *Qasru* na *hasru* ni maana moja, kwa hivyo, usibabaike nikitaja hii na hii.

ya haki akasema: **"Masihi mwana wa Maryamu hakuwa (vyengine) ila ni Mtume".** Na hii kwa upande wa pili au kwa mazingatio mingine inaitwa **"*Qasru idhafi".***

Sasa ukirudi katika Aya **"Hakika *Walii* wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini tu…".** basi tunakuta kwamba pia kuna ***"Qasru Qalb".*** Na hii ni kwamba Aya zilizotangulia zinawakataza Waislamu wasiwafanye makafiri kuwa ni marafiki wao.[109] Na kwa hivyo, ndio maana ikaja Aya hii ikianzia na herufi إِنَّمَا ***Inna-maa*** yenye kumaanisha – kwa hapa – ***"Qasru Qalb"*** (Kuyaleta maneno kinyume chake na kuyafunga yakawa na maana moja tu), ili kuonesha kwamba hivyo munavyofanya au munavyodhani sivyo, bali vilivyo ndivyo ni hivi, navyo ni kuwa: "Hakika *Walii* wenu" yaani hawakuwa rafiki zenu (isipokuwa) **"Ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini tu…"..** Kwa hivyo, yote haya yanatubainishia ukweli kwamba neno *Waliyy (Walii)* lililomo katika Aya hio, maana yake si nyengine bali ni rafiki na kipenzi.

Ama tukilifasiri neno *Waliyy (Walii)* hapa kuwa maana yake ni mtawala – pamoja na kuizingatia ***"Qasru Qalb"*** iliomo ndani yake – basi:

a) Hapatokuwa na mfungamano baina ya katazo la kuwafanya makafiri kuwa ni vipenzi; na kumfanya Allah, Mtume (s.a.w.) na Ali tu kuwa ndio wasimamizi wa mambo yetu au watawala. Kwani kinyume cha kutokumfanya mtu kuwa ni rafiki na kipenzi ni kumfanya kuwa ni adui – si kumfanya kuwa ni mtawala; na kinyume cha kumfanya mtu kuwa ni adui ni kumfanya kuwa ni rafiki na kipenzi. Kwa hivyo, maana ni kuwa: "huyu mfanyeni adui; na yule mfanyeni rafiki na kipenzi". Na kwa hapa kutakuwa na muowano wa maana baina ya Aya husika na Aya zilizotangulia.
b) Maana itakuwa: **"Hakika mtawala wenu ni Allah na Mtume wake na wale walioamini tu".** Kisha ikiwa tutasema kuwa maana ya **"Wale walioamini tu"** ni Ali, basi maana itakuwa: **"Hakika ya mtawala wenu ni Allah na Mtume wake na Ali tu"** na kwa

[109] - Kwa bahati mbaya, hii imekuwa tabia ya Waislamu hadi leo, wakidhani kuwa hao wana urafiki na Waislamu.

hivyo, hata Maimamu wengine wa Ahlu-Al-Bait – ukiachilia mbali Abu Bakr na Umar – itakuwa hawamo.

USHAHIDI WA SHIA

Tumetangulia kueleza kwamba Shia wao wanaona kuwa maana ya neno *Waliyy (Walii)* katika Aya hio isemayo: **"Hakika *Walii* wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini tu"**, ni msimamizi wa mambo, na kwa hivyo maana ya Aya hio ni kuwa Allah ndiye *msimamizi* na muendeshashaji wa mambo, kisha Mtume na Ali (yaani hawa wawili ni kwa idhini ya Allah). Anasema Al-Tabrasi:[110]

> Kisha Allah akambainisha nani ni mwenye uwalii (utawala) juu ya viumbe na (mwenye) usimamizi wa mambo yao na (ambaye) kumtii kwake ni wajibu kwao, akasema: **"Hakika *Walii* wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake..[111]**

Kisha akasema Sheikh huyu – ambaye kama kawaida yake na wenzake kwenda kinyume na kananuni za tafsiri – akasema:

> Na Aya hii ni katika ushahidi wa wazi kabisa juu ya usahihi wa uimamu wa Ali baada ya Mtume (s.a.w.) bila ya kuwepo muachano (gap) baina yao.[112]

Kwa ufupi ni kuwa Shia wao wametegemea riwaya juu ya tafsiri yao hio. Lakini inatosha kuonesha wasiwasi mkubwa wa riwaya hizo, kwamba Aya – ukiiweka katika kila mezani miongoni mwa mezani za tafsiri – inaleta maana tafauti na riwaya hizo, na hii ni moja ya alama ya Hadithi za kufinyanga. Sasa na-tuzitazame riwaya hizo ambazo wamezitegemea katika tafsiri yao hio.

---

110 - Al-Tabrasi ni mwanachuoni wa Kishia aliyeishi karne ya sita. Jina lake ni Abu Ali, Al-Fadhlu bin Al-Hasan. Na huyu si yule Al-Tabrasi mwenye kitabu kiitwacho *Al-Ihtijaj* ambaye ni Abu Mansur Ahmad bin Ali. Lakini wote wameishi karne ya sita.

111 - Al-Tabrasi *Majmu'u Al-Bayaan* j. 3, uk. 264.

112 - K.h.j.

SABABU YA KUTEREMKA AYA

Riwaya wanayoitegemea Shia juu ya tafsiri yao hio, ni riwaya inayosema kwamba Aya hio ilimteremkia Ali wakati yumo katika kusali msikitini: yumo katika rukuu. Hapo alikuja masikini akaomba msaada ikawa hakuna mtu yoyote aliyemsaidia, Ali akavua pete yake – naye yumo katika rukuu – akamuashiria yule maskini kwa kidole chake akampa pete hio.[113] Basi hapo ndio ikateremka Aya hio:

> **Hakika *Walii* wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini tu: wale ambao wanasimamisha sala na wanatoa zaka nao ni wenye kurukuu.[114]**

Na zifuatazo ndio riwaya zenyewe:

RIWAYA KWA NJIA ZA KISUNNI

Anasema Ibn Abi Hatim:

> Ametusimulia Abu Said Al-Ashaj ametusimulia Al-Muharibi kutoka kwa Abdil-Malik bin Abi Sulaiman kasema: 'Nimemuuliza Abaa Ja'afar Muhammad bin Ali kuhusu kauli yake (Allah isemayo): **(((Hakika *Walii* wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini tu))),** akasema: 'Imemteremkia Ali.[115]

Riwaya hio kaisimulia pia Ibn Jarir Al-Tabari katika *Jaami'u Al-Bayaan*[116] kwa *sanad* mbili: katika moja miongoni mwa *sanad* mbili hizo, Sheikh wa Ibn Jarir katika masimulizi yake si Abu Said Al-Ashaj bali ni Ibn Wakii na katika riwaya ya pili Sheikh wa Ibn Jarir ni Hannad bin Al-Sariy. Nayo ni riwaya batili kwani katika *sanad* yake kuna Al-Muharibi. Jina lake ni

---

[113] - Nilipokituma kitabu hiki – wakati kilipokuwa makala – katika ukumbi wa zanzinet, mtu mmoja, aliuliza masuli yenye maana hii: Huyu Ali hakuwa na *khushuu* katika Sala? Je kulikuwa na dharura gani hata ikabidi Ali ashughulike na kutoa sadaka naye yumo katika sala? Labda na yako masuali mengine alioiuliza kwa sasa siyakumbuki.

[114] - Sura 5 Aya 55.

[115] - Ibn Abi Hatim *Tafsiru Al-Qur-ani Al-'Adhim* j. 4, uk. 1162.

[116] - J. 6, uk. 344.

Abdu-Rahman bin Muhammad bin Ziyad Al-Muharibi Abu Muhammad Al-Kufi, naye ni mwenye kukosea sana, mwenye kughushi na Hadithi zake zinagongana. Anasema Ibn Sa'ad: "Ni muaminifu, anakosea sana". Anasema Al-Imamu Ahmad bin Hanbal: "Imenifikia kwamba alikuwa akighushi (Hadithi)". Anasema Al-'Ijli: "Alikuwa akighushi (Hadithi). Anasema Al-Saji: "Ni mkweli anakosea ana *awham (Ilussion* yaani anakosea sana)".[117]

Pia yumo katika *sanad* ya riwaya hii Abdul- Malik bin Abi Sulaiman.Naye wametafautiana juu yake: wengine wakamkubali na wengine wakamuona kuwa ni mpokezi dhaifu. Kwa hali yoyote ile, dhahir ya maneno ya walio wengi ni kwamba inakubalika kuwa alikuwa akikosea. Tunasema**:** na Hadithi hii ni miongoni mwa alizozikosea.[118] Naye Abdul- Malik bin Abi Sulaiman anasema kwamba riwaya hii kamsikia Abu Ja'afar, Imamu wa Kishia akisema hivyo. Nasi tunasema kwamba Abu Ja'afar Imamu wa Kishia – hata ingelikuwa kweli ni Ma'asumu kama Shia wanavyodai[119] – lakini hakuwa akipata wahyi, naye hakusema riwaya hii kaisikia kutoka kwa nani. Abu Ja'afar huyu ni Abu Ja'far wa mwanzo, Muhammad bin Ali, kazaliwa mwaka 57 AH. Kwa hivyo, ilitakiwa aseme aliyemsimulia riwaya hii au apate wahyi! Kwa hali yoyote ile, kuwepo kwa udhaifu katika wapokezi wawili waliotangulia kunaifanya riwaya hii iwe dhaifu.

Ama *sanad* ya pili ya Ibn Jarir, utaona kwamba hayumo Al-Muharibi lakini yumo Abdul-Malik bin Abi Sulaiman huyo huyo tuliyemuelezea kabla na ambaye wametafautiana juu ya usahihi wake, na juu ya yote Hadithi hii ni *mursal* vile vile, kwani msimulizi ni yule yule Abu Ja'afar, Imamu wa Shia, naye hakusema alipoipata Hadithi hio.

---

[117] - Tazama *Tahdhibu Al-Tahdhi*b j. 6, uk. 237-238, *tarjama* na. 527.

[118] - K.h.j. uk. 352, *tarjama* na. 751.

[119] - Cha ajabu ni kuwa Maimamu hawa wanaambiwa kuwa ni Ma'asumu (hawakosei) lakini wao wenyewe wanatafautiana. Kwa mfano Al-Hasan bin Ali na ndugu yake Al-Husain bin Ali walikuwa na misimamo tafauti kuhusu suala la kufanya sulhu na Mu'awiya: Al-Hasan akafanya sulhu na akambaii Mu'awiya; Al-Husain akapinga vikali na akakataa kumbaii Mu'awiya. Ibn Al-A'atham *Al-Futuh* j. 4, uk. 161. Na hata baada ya kufa Al-Hasan, Al-Husain alimili katika vita na watu wa Banii Umayya badala ya sulhu.

Kisha Ibn Jarir akaipokea tena Hadithi hio, kutoka kwa U'qbat bin Abi Hakim, naye ni dhaifu. Anasema Ibn Ma'iin: "Hadithi zake ni dhaifu". Na akasema tena: "Naapa kwa jina la Allah ambaye hakuna Mola isipokuwa Yeye, hakika yake ni mwenye Hadithi *munkar".* Anasema Muhammad bin Awf: "Ni dhaifu". Anasema Al-Juzajani: "Si mwenye kuhimidiwa". Anasema Al-Nasai: "Ni dhaifu…si madhubuti".[120]

Kisha akaisimulia tena Ibn Jarir riwaya hii kwa *sanad* nyengine kutoka kwa Mujahid, lakini katika *sanad* yake kuna Ghalib bin Abdillah, naye hajulikani ni nani.[121] Na huenda ikawa kuna wapokezi wengine ambao hawajulikani.[122] Pia msimulizi wa riwaya hii ni Mujahid naye ni mfuasi wa Masahaba wala hakumtaja aliyemsimulia riwaya hio – kwa hivyo, ni riwaya *mursala,* na ni yenye *sanad* dhaifu – udhaifu juu ya udhaifu.

Ama Ibn Abi Hatim, yeye kasimulia riwaya nyengine, lakini katika *sanad* yake kuna Al-Rabi'u bin Sulaiman Al-Muradi, naye alikuwa na mughafala mkubwa kama ilivyoelezwa katika *Tahdhibu Al-Tahdhib*.[123] Pia katika *sanad* hii ya pili yumo Ayub bin Suwaid Al-Ramli, naye ni dhaifu sana, mwenye hifdhi mbovu, mwizi wa Hadithi za watu.[124] Hatimae tunakuta kwamba msimulizi wa Hadithi hii ni yule yule U'qbat bin Abi Hakim tuliyemuelezea kabla kidogo na ambaye ni dhaifu.[125]

Kisha akasimulia Ibn Abi Hatim riwaya nyengine, ambayo ndio iliotaja sadaka ya pete, lakini katika *sanad* yake kuna Al-Fadhlu bin Dukain naye ni muaminifu kasifiwa sana, lakini Ibn Shahin anasimulia kauli ya Ahmad bin Salih akisema: "Na alikuwa akighushi Hadithi munkar".[126] Pia yumo katika *sanad* hii, Musa bin Qais Al-Hadharami, naye ni katika *Ghulat* Shia (Extremist Shia yaani shia wenye siasa kali katika ushia wao), na hatuwezi kuwaamini Shia katika riwaya za Ushia, hasa hasa tukizingatia tabia waliokuwa nayo ya kutunga maelfu kama si malaki ya Hadithi. Naye

120 - Tazama *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 7, uk. 87, *tarjama* na. 201.
121 - Tazama *Lisanu Al-Mizan* j. 4, uk. 413, *tarjama* na.1265.
122 - Sikuweza kuwatafuta mara moja kwani hawakutajwa kwa majina yao kamili.
123 - J. 3, uk. 213, *tarjama* na. 473.
124 - Tazama *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 1, uk. 354, *tarjama* na. 745.
125 - K.h.j., j. 7, uk. 87, *tarjama* na. 201.
126 - K.h.j., j. 8, uk. 248, *tarjama* na. 505.

kaipokea kutoka kwa Salamat bin Kuhail, pia ni Shia wa Al-Kufa (Iraq), lakini ni imara katika Hadithi, hata hivyo, yeye ni mfuasi wa Sahaba na hakusema nani kamsimulia Hadithi hii, kwa hivyo ni Hadithi *mursal*, na Hadithi *mursal* ni dhaifu kwa wanavyuoni wa Hadithi. Inaonesha Hadithi hii Salamat bin Kuhail kaisikia kutoka kwa mmoja wa watunzi wao wa Al-Kufa (Iraq) ambaye hakumtaja!

Na riwaya nyengine kama hio, kaipokea Abdul-Razzaq kutoka kwa Ibn Abbas. Riwaya hii kainukuu Ibn Kathir katika tafsiri yake *Tafsiru Al-Qur-ani Al-'Adhiim* kwa *sanad* yake kamili. Nayo ni "Abdul-Razzaq katusimulia Abdul-Wahhab bin Mujahid kutoka kwa baba yake kutoka kwa Ibn Abbas".....kisha inafata Hadithi. Kisha akasema Ibn Kathir: "Abdul-Wahhab bin Mujahid hafanywi kuwa ni hoja".[127] <u>*Ninasema:*</u> Sufyan Al-Thauri kasema kuwa ni "Mwongo". Anasema Ahmad: "Si lolote si chochote: Hadithi zake ni dhaifu". Anasema Ibn Ma'iin na Abu Hatim: "Ni dhaifu". Anasema Al-Nasai: "Si mwenye kuaminika". Anasema Ibn Adey: "Hadithi zake zote hazifuatiwi".[128] Na wakasema Ali bin Al-Madini na Ibn Ma'iin – katika riwaya yake nyengine -: "Haandiki Hadithi zake: (naye) si lolote si chochote". Anasema Al-Daraqutni: "Si lolote si chochote: ni dhaifu". Anasema Al-Azdi: "Si halali kusimulia riwaya zake". Anasema Ibn Sa'ad: "Alikuwa dhaifu katika Hadithi". Anasema Al-Hakim: "Kasimulia Hadithi za kutunga". Kwa hivyo, hii ni *sanad* dhaifu sana.

Na riwaya nyengine kainukuu Ibn Kathir vile vile. Riwaya hio imesimuliwa na Ibn Mardawaih: "Kwa njia ya Sufyan Al-Thauri kutoka kwa Abi Sinan kutoka kwa Al-Dhahhaak (bin Muzahim) kutoka kwa Ibn Abbas". Nayo ni *sanad* dhaifu kwani Al-Dhahhaak – ambaye ndiye aliyeisimulia Hadithi hii kutoka kwa Ibn Abbas – hakupata kukutana na Ibn Abbas bali wala hakukutana na Sahaba yoyote yule. Anasema Shu'uba: "Nilimwambia Mushash: 'Dhahhak kasikia (Hadithi) kutoka kwa Ibn Abbas, akasema: 'Hakupata (hata) kumuona kamwe". Anasema Ibn Hibban: "Kawakuta Tabiina wengi, (lakini) hakupata kusema naye hata

[127] - *Tarjama* (biography) ya Abdul-Wahhab bin Mujahid iko katika Tahdhibu Al-Tahdhib j. 6, uk. 400, *tarjama* na. 839.

[128] - Hio ni lugha ya kitaalamu ikimaanisha kwamba hazina ushahidi.

Sahaba mmoja mdomo kwa mdomo. Na aliyedai kuwa kamkuta Ibn Abbas basi amekosea".[129] Anasema Ibn Adey: "Riwaya zake kutoka kwa Ibn Abbas na Abi Huraira na wote aliosimulia kutoka kwao, zote hizo ni za kufikiriwa (dhaifu)".[130] Kwa hivyo, *sanad* hii imekatika nayo inahukumiwa kuwa ni dhaifu.

Riwaya nyengine kaipokea Ibn Maghazil katika *Al-Manaaqib* na kuinukuu Al-Tabatabai katika *Al-Mizan*[131] kwa *sanad* hii:

> Katwambia Muhammad bin Ahmad bin Uthman kasema katupa habari Abu Bakr bin Ahmad bin Ibrahim bin Shadhan Al-Bazzaar kasema katupa habari Al-Hasan bin Ali Al-'Adawi kasema katupa habari Salamat bin Shabib kasema katupa habari Abdul-Razzaq kasema katupa habari Mujahid kutoka kwa Ibn Abbas…..kisha inafata Hadithi.

Nayo ni riwaya batili mno, kwani katika *sanad* yake kuna Al-Hasan bin Ali Al-'Adawi, maarufu kwa jina la *Dhi-ab*. Anasema Al-Daraqutni: "Ni mwenye kuachwa" (Hadithi zake zinaachwa)". Na mpokezi mwenye kuachwa, basi Hadithi zake zinahisabiwa kuwa ni katika Hadithi dhaifu sana. Anasema Al-Dhahabi baada ya kutaja Hadithi za uwongo za bwana huyu: "Ninasema: Sheikh huyu hana haya: hata hakufikiri katika uzushi wake anaouzuwa". Anasema Al-Hakim: "Ni mtu wa kufikiriwa: Qadhi Ismail alimfunga kwa kuyakanusha (yale anayoyasimulia ya uwongo wake)". Anasema Ibn Adey: "Yote anayoyasimulia ni ya kutunga isipokuwa machache, na tulikuwa tukimtuhumu (kuwa anatunga Hadithi) bali (baadae) ikatuthibitikia kwa yakini kuwa yeye ndiye anayezitunga (Hadithi hizo anazozisimulia)". Anasema Abu Muhammad Al-Hasan Al-Basri: "Abu Said Al-'Adawi ni mwongo mkubwa anamzulia Mtume (s.a.w.): anamsemea (mambo ambayo Mtume s.a.w.) hajayasema". Anasema Ibn Adey: "Kasimulia kutoka kwa waaminifu Hadithi zaidi ya elfu za kutunga".[132]

---

[129] - Ibn Hibban *Al-Thiqat* uk. 523, *tarjama* na. 8683.
[130] - Tazama *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 4, uk. 397-398, *tarjama* na. 794.
[131] - J. 6, uk. 22.
[132] - Tazama Al-Dhahabi *Al-Mizan* j. 2, uk. 29-32, *tarjama* na. 1903. Ibn Hajar *Lisanu Al-Mizan* j. 2, uk. 228-232, *tarjama* na. 987.

Kisha akanukuu tena Al-Tabatabai Hadithi nyengine kutoka kwa Ibn Al-Maghazili huyo huyo, kwa *sanad* dhaifu mno, nayo ni refu kidogo mwisho wake ni: "Kutoka kwa Muhammad bin Saib kutoka kwa Abi Saleh kutoka kwa Ibn Abbas". Nayo si *sanad* bali ni mauti, kwani Muhammad bin Saib ni Al-Kalbi – Shia wa kule kule mjini Al-Kufa (Iraq) kwenye kiwanda chetu cha kufinyangia Hadithi – kaitwa mwongo. Anasema Mu'utamir bin Sulaiman kutoka kwa baba yake: "Al-Kufa palikuwa na waongo wawili: mmoja wao ni Al-Kalbi". Anasema Laith bin Abi Sulaim: "Al-Kufa palikuwa na waongo wawili: mmoja wao ni Al-Kalbi na wa pili ni Al-Suddi". Anasema Yahya bin Main: "Si lolote si chochote". Na akasema katika riwaya ya pili: "Dhaifu". Bali Al-Kalbi huyu katuhumiwa hata katika Uislamu wake. Anasema Abu 'Amri bin 'Alaa: "Nashuhudia kwamba Al-Kalbi ni kafiri!.....nimemsikia akisema kwamba Jibril alimpa wahyi Mtume (s.a.w.), akasimama Mtume (s.a.w.) kwenda kwenye haja yake; Ali akakaa kitako (basi Jibril) akampa wahyi Ali![133]....Akasema Yazid (bin Zurai'i): 'Mimi sikumsikia akisema hivyo, lakini nimemsikia akisema: "Mimi ni Saibi". Anasema Al-'Uqaili: 'Nao (hao Masaibi) ni sehemu ya Al-Rafidha (Shia) wafuasi wa Abdullahi bin Sabaa.[134] Anasema Al-Asmai kutoka kwa Qurrat bin Khalid: "Walikuwa (wanavyuoni wa Hadithi) wakimuona Al-Kalbi kuwa anasema uwongo". Anasema Abu Hatim: "Wamekubaliana (wanavyuoni wa Hadithi) kuwa waziache Hadithi zake, Hadithi zake zinaporomoka, hazishughulikiwi". Anasema Al-Nasai: "Si mwenye kuaminika". Wanasema Ali bin Junaid, Al-Hakim na Al-Daraqutni: "Ni mwenye kuachwa". Anasema Al-Juzajani: "Ni mwongo mkubwa". Anasema Ibn Hibban: "Uwazi wa uwongo ndani yake uko dhahiri hauhitaji kuzama katika kuuelezea, kapokea (Hadithi za) tafsiri kutoka kwa Abi Salih kutoka kwa Ibn Abbas wakati Abi Salih hakupata kusikia (Hadithi yoyote) kutoka kwa Ibn Abbas". Anasema Al-Saji: "Hadithi zake zinaachwa na alikuwa dhaifu sana". Anasema Al-Hakim: "Kasimulia Hadithi za kutunga".[135] Hatimae nikakuta kwamba bwana Al-Kalbi mwenyewe kakiri kuwa yeye anasimulia Hadithi za uwongo. Anasema Al-Bukhari: "Katusimulia Yahya kutoka kwa Sufyan kasema:

---

[133] - Ndio maana tunasema itikadi za kumtukuza Ali kupindukia mipaka lazima ndugu zetu wazifikirie; utunzi ulikuwa mkali sana enyi ndugu zetu!

[134] - Hili linahitaji maelezo ya ziada hapa si mahala pake, lakini kwa ufupi ni kuwa kuwepo kwa mtu aliyeitwa Abdullahi bin Saba-a hakukuthibiti kwa riwaya sahihi.

[135] - Tazama *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 9, uk. 157, *tarjama* na. 268.

‘Kaniambia Al-Kalbi: ‘Kila nilichokusimulia kutoka kwa Abi Salih ni uwongo”.[136] Na Hadithi hii pia kaisimulia kutoka *Abi Salih* na kwa hivyo, ni uwongo mtupu.

Na Al-Kalbi kaisimulia Hadithi hio kutoka kwa Abi Salih kutoka kwa Ibn Abbas. Abi Salih, jina lake ni Baadham,[137] mtumishi wa Ummu Hani, naye ni dhaifu sana na ni mwenye kughushi na Al-Azdi anasema: “Ni mwongo mkubwa”. [138] Na tunamkuta katika wanavyuoni wa Hadithi, tafsiri na fiq-hi, Al-Imamu Jalalu Al-Din Al-Suyuti akisema: “Abu Salih ni dhaifu”.[139] Anasema Abdul-Razzaq Al-Mahdi katika maelezo yake juu ya tafsiri ya Al-Baghawi: “Abu Salih katika (riwaya zake alizozisimulia kutoka) kwa Ibn Abbas, si mwenye kuaminika”.[140] Na haya yamesemwa kabla na hao wanavyuoni wa wapokezi (U’lamau Al-Jarhi wa Al-Ta’adil) tuliowataja kabla. Kwa hivyo, Hadithi hii ni ufinyanzi wa kule kule mjini Al-Kufa!

Kisha akanukuu Al-Tabatabai Hadithi nyengine kutoka kwa Ibn Al-Maghazili huyo huyo, kwa *sanad* ambayo dhahir yake ina wapokezi wasiojulikana na dhaifu. Lakini katika *sanad* yake pia kuna Ibrahim bin Muhammad bin Maymun, kigogo cha Kishia. Naye anasimulia Hadithi za kutunga na Hadithi munkar. Anasema Ibn Hajar: “Kamtaja Al-Asadi katika (kitabu cha) wapokezi madhaifu, na akasema kwamba Hadithi zake ni munkar…kasimulia Hadithi ya kutunga….mtu huyu si mwenye kuaminika”.[141] Na msimulizi wa Hadithi katika *sanad* hio, ni Abdullah bin A’taa, naye ni mtu wa kule kule mjini Al-Kufa kwenye kiwanda cha utunzi wa Hadithi. *Tarjama* yake ni fupi katika *Tahdhibu Al-Tahdhib*.[142] Naye wametafautiana juu yake baina ya Ibn Ma’iin na Al-Nasai: Ibn Ma’iin anasema: “Ni mwenye kuaminika” Al-Nasai anasema: “Ni dhaifu”. Kanuni kwa mujibu wa *jumhur* ya watu wa Hadithi ni kutanguliza kauli ya wenye

---

136 - Tazama Al-Dhahabi *Al-Mizan* j. 5, uk. 3, *tarjama* na. 7574.

137 - Na pia huitwa Baadhan.

138 - Tazama maelezo yake kwa urefu katika *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 1, uk. 364-365, *tarjama* na. 770.

139 - Al-Suyuti *Asbabu Al-Nuzul* uk. 6, katika maelezo ya Aya 14, ya Sura ya 2.

140 - Tazama tafsiri ya Al-Baghawi *Ma’aalimu Al-Tanzil* j. 1, uk. 144, katika maelezo ya chini yaliotiwa na Abdul-Razzaq Al-Mahdi.

141 - Tazama *Lisanu Al-Mizan* j. 1, uk. 107, *tarjama* na. 318.

142 - J. 5, uk. 281-282, *tarjama* na. 551.

kujeruhi, yaani waliomdhoofisha. Kwa hali yoyote ile udhaifu mkubwa wa Ibrahim bin Muhammad bin Maymun unatosha kuibomoa riwaya hii.

Na akanukuu Al-Tabatabai riwaya nyengine kutoka kwa Abu Nuaim. Lakini *sanad* yake ni "Abu Zubair kutoka kwa Jabir". Nayo ni *sanad* dhaifu kwa ajili ya Abu Zubair huyu mwenye kughushi,[143] na Hadithi yake Hapa ni *mu'an'an.*[144] Nayo ni Hadithi dhaifu ikiwa itasimuliwa na mtu mwenye kughushi. Bali mbali na kughushi, Abu Zubair wengine wamemkataa kabisa. Na bila shaka kama ukisoma habari zake basi utaona kuwa hafai kuwa mpokezi wa Hadithi. Moja katika makosa yake ni kuwa Shu'uba anasema: "Nilikuwa kwanza nikipokea Hadithi kutoka kwake mpaka siku moja nikamkuta anampimia mtu kitu kwa mezani na kujizidishia upande wake", yaani anajizidishia yeye. Hii ni dhulma, na mtu kama huyu ambaye anathubutu kufanya hivi vipi asithubutu kuunda Hadithi. Na jengine ni kuwa anasema Shu'uba wakati siku moja kakaa mbele yake "Akaja mtu akamuuliza mas-ala akamwambia e Abu Zubair we! Unamzulia uwongo mtu Muislam!" Akamwambia: "Kwa sababu kanikera!" Sasa tazama wewe mtu kamkera ndio anamzulia uwongo vipi tutamuamini katika masimulizi ya Hadithi. Na kwa hivyo, wengine wamemkataa. Anasema Abdullahi bin Ahmad kutoka kwa baba yake – Al-Imamu Ahmad bin Hanbal – akisema: "Alikuwa Ayub akisema katuhadithia Abu Zubair, Abu Zubair, Abu Zubair". Nikamuuliza "Je alikuwa akimdhoofisha (yaani je alikuwa akisema kuwa ni dhaifu)?" Akasema: "Ndio". Na anasema Suwaid bin Abdul-'Aziz: "Aliniambia Shu'uba wewe unapokea Hadithi kutoka kwa Abu Zubair naye hajui hata kusali?" Na anasema Hushaim "Nilipokea Hadithi kutoka kwa Abu Zubair basi Shu'uba akachukua kitabu changu (chenye Hadithi hizo) akakichana-chana". Na anasema Abu Hatim: "Hadithi zake hazifai kuwa hoja". Kwa hivyo, kwa sababu ya "Kupunja katika mezani" na "Kumzulia mtu uwongo kwa sababu kamkera" inatubidi Hadithi yake tuiwache asije akatupunja katika masimulizi yake.

---

[143] - Tazama *Taqribu Al-Tahdhib* uk. 506, *tarjama* na. 6291.

[144] - Hadithu *mu'an'an* **(مُعَنْعَنٌ)** ni Hadithi ambayo msimulizi wake anatumia lafdhi: ((**عن فلان**)) ***A'n Fulan*** (Kutoka kwa fulani). Hadithi kama hii ni dhaifu ikiwa itasimuliwa na mpokezi *mudallis* (mwenye kughushi). Abu Zubair ni *mudallis* (mwenye kughushi) na Hadithi yake iko hivyo.

Kisha akanukuu Al-Tabatabai riwaya nyengine kutoka kwa Abu Nuaim vile vile, lakini ni Hadithi mursal, iliosimuliwa na Salamat bin Kuhail vile vile, naye hakusema ni nani kamsimulia wakati yeye si Sahaba: bali ni mfuasi wao na alikuwa Shia wa Al-Kufa kulikokuwa na tatizo la utunzi mkubwa wa Hadithi!

Riwaya nyengine kaisimulia Ibn Asaakir kwa *sanad* hii: "Issa kanihadithia baba yangu kutoka kwa baba yake kutoka kwa babu yake Ali". [145]

Issa ni "Issa bin Abdillah bin Muhammad bin Umar bin Ali bin Abi Talib (si Amiru-L-muuminin), na wengine humtaja kwa jina la "Issa bin Abdillah *bin Ubaidillahi* bin Muhammad bin Umar bin Ali bin Abi Talib, naye (Issa bin Abdillah) ni msimulizi wa Hadithi za kutunga; Hadithi munkar na Hadithi zake zinaachwa. Anasema Al-Daraqutni: "Hadithi zake zinaachwa". Anasema Al-Dhahabi baada ya kusimulia balaa zake: "Na hii huenda ikawa ni ya-kutunga".[146] Na akamtaja Ibn Hibban katika *Al-Thiqat*[147] na akasema: "Katika Hadithi zake kuna baadhi ya (Hadithi nyingi) munkar". Naye bwana huyu ana riwaya kwa kapu na magunia za kumtungia Al-Imamu Ali kazitaja Ibn Hajar katika *Lisanu Al-Mizan* na Al-Dhahabi katika *Al-Mizan.* Anasema Ibn Hibban: "Anasimulia kutoka kwa baba zake Hadithi za kutunga". Anasema Abu Nuaim: "Anasimulia kutoka kwa baba zake Hadithi (nyingi) munkar: haandiki Hadithi zake: hana maana". Na akasema Ibn Adey: "Katusimulia…..Hadithi hazina ushahidi….Hadithi (nyingi) munkar".[148]

Baba yake Issa ni: "Abdullahi bin Muhammad bin Umar bin Ali bin Abi Talib," naye ni *majhulu Al-hali* (Hali yake haijulikani: je ni mpokezi sahihi

---

[145] - Ibn Asaakir *Taarikh Dimashq* j. 48, uk 202, riwaya na. 10846, na katika j. 45, uk. 271, riwaya na. 9683.

[146] - Tazama Al-Dhahabi *Al-Mizan* j. 4, uk. 235, *tarjama* na. 6577 na *tarjama* na 6578: zote hizo ni *tarjama* za mtu mmoja lakini kamtaja mara mbili kwa sababu wengine hulitaja jina lake kwa urefu na wengine hulifupisha.

[147] - Uk. 799, *tarjama* na. 14614.

[148] - Ibn Hajar *Lisanu Al-Mizan* j. 4, uk. 399 *tarjama* na. 1217 na *tarjama* na 1218: zote hizo ni *tarjama* za mtu mmoja sawa na ilivyo katika *Al-Mizan* cha Al-Dhahabi.

au dhaifu). Katajwa katika *Tahdhibu Al-Tahdhib*[149] bila ya kunasibishwa na usahihi wala udhaifu – hali yake haijulikani.

Babu wa Issa ni "Muhammad bin Umar bin Ali bin Abi Talib," naye pia ni *majhulu Al-hali* (Hali yake haijulikani: je ni mpokezi sahihi au dhaifu). Anasema Al-Qattaan: "Hali yake haijulikani".[150] Kwa ufupi *sanad* hii imejaa wapokezi wasiojulikana hatuna haja ya kurefusha, na kwa hayo yaliotangulia inakubainikia kwamba hii ni *sanad* dhaifu au ukipenda sema *sanad* maudhui kwani mpokezi wa kwanza ni msimulizi wa riwaya za uwongo, za kutunga na bila shaka hii ni moja yao.

Na akaisimulia tena Ibn Asaakir kutoka kwa Salamat bin Kuhail,[151] lakini katika *sanad* yake kuna Muhammad bin Abdillah bin Al-Harith Al-Ramli. Anasema Al-Dhahabi katika *Al-Mizan*[152] na Ibn Hajar katika *Lisanu Al-Mizan*[153]:

> Kaleta habari (riwaya) batili. Kasema Al-Haj Al-Ishbili: 'Katusimulia huyu (Muhammad bin Abdillah bin Al-Harith Al-Ramli)…..kutoka kwa Jabir kasema: 'Kasema Mtume (s.a.w.)…". Kumtazama mwanamke mzuri kunazidisha nguvu ya macho ya kuona..

Hadithi hii ni vichekesho vyenye kuliza! Na pia *sanad* hii – dhahir yake ni kuwa – ina wapokezi wengi wasiojulikana. Na kwa hivyo, Ibn Kathir kasema katika tafsiri yake: "Na kwa ujumla, hakikusihi chochote (katika Hadithi hii) kwa sababu ya udhaifu wa *sanad* zake na kutokujulikana kwa wapokezi wake".[154] Hatimae ni kuwa Hadithi hii – kama tulivyosema – imesimuliwa na Salamat bin Kuhail naye ni Shia wa Al-Kufa (Iraq) – kwenye kiwanda cha kuchongea Hadithi – na hakusema nani kamsimulia Hadithi hii, kwa hivyo ni Hadithi mursal na ni dhaifu. Inaonesha – kama

---

149 - J. 6, uk. 16, *tarjama* na. 22.
150 - Tazama: *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 9, uk. 321, *tarjama* na. 601.
151 - Ibn Asaakir *Taarikh Dimashq* j. 45, uk. 272, riwaya na. 9684.
152 - J. 5, uk. 73, *tarjama* na. 7863.
153 - J. 5, uk. 255, *tarjama* na. 878.
154 - Ibn Kathir *Tafsiru Al-Qur-ani Al-'Adhim* j. 2, uk. 67, katika tafsiri ya Aya ya 55 ya sura 5.

tulivyosema mwanzo – Salamat bin Kuhail kaisikia Hadithi hii kutoka kwa mmoja wa watunzi wao wa Al-Kufa (Iraq) ambaye hakumtaja!

Riwaya hio ya Ali ya kutoa sadaka ya pete na kuteremkiwa na Aya hio isemayo: **"Hakika *Walii* wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini tu"** imesimuliwa pia na Al-Wahidi,[155] lakini *sanad* yake ni janga juu ya balaa, kwani katika *sanad* hio kuna Al-Suddi Al-Saghiir, naye ni Muhammad bin Mar-wan. Anasema Jarir bin Abdi Al-Hamid: "Mwongo". Anasema Al-Duuri kutoka kwa Ibn Ma'iin: "Si mwenye kuaminika". Anasema Salih bin Muhammad: "Alikuwa dhaifu na alikuwa akitunga (Hadithi)". Anasema Abu Hatim: "Hadithi zake zinaporomoka: Hadithi zake zinaachwa: Hadithi zake haziandikwi kamwe". Anasema Ibn Adey: "Udhaifu katika Hadithi zake uko bayana". Anasema Al-Juzajani: "Hadithi zake zinaporomoka". Anasema Ibn Hibban: "Si halali kuandika Hadithi zake ila kwa ajili ya kufatilia (*Sanad)*, na wala hafanywi kuwa ni hoja kwa hali yoyote". Anasema Al-Tabari: "Hadithi zake hazifanywi kuwa ni hoja". Anasema Abdullahi bin Numair: "Al-Suddi alikuwa mwongo mkubwa".[156]

Pia katika *sanad* ya Hadithi hio kuna Al-Kalbi. Naye kasemwa kuwa ni mwongo, msimulizi wa za Hadithi kutunga.[157] Tumesema kwamba Al-Kalbi kakiri mwenyewe kwamba kila Hadithi alioisimulia kutoka kwa Abi Salih ni uwongo".[158] Na Hadithi hii pia kaisimulia kutoka Abi Salih na kwa hivyo, ni uwongo mtupu. Abi Salih, jina lake ni Baadham, mtumishi wa Ummu Hani, naye pia ni dhaifu sana na ni mwenye kughushi na Al-Azdi anasema: "Ni mwongo mkubwa".[159]

---

155 - Al-Wahidi *Asbabu Al-Nuzul* uk. 145.

156 - Tazama *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 9, uk. 387, *tarjama* na. 721.

157 - Tumemuelezea kabla. Rejea sura ya kwanza chini ya kichwa cha habari: "Riwaya kwa njia za Kisunni".

158 - Tazama Al-Dhahabi *Al-Mizan* j. 5, uk. 3, *tarjama* na. 7574.

159 - *Sanad* hii pia tumeielezea kabla. Tazama maelezo ya Abi Salih kwa urefu katika *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 1, uk. 364-365, *tarjama* na. 770. Al-Suyuti *Asbabu Al-Nuzul* uk. 6, katika maelezo juu ya Aya 14, ya Sura ya 2.

Mwengine aliyeisimulia riwaya hio ni Al-Tabarani,[160] lakini katika *sanad* yake kuna Muhammad bin Ali Al-Saaigh. Anasema Ibn Nasir: "Haijuzu kupokea (Hadithi) kutoka kwake, kwani hayuko katika njia ya watu wa Hadithi, na mambo yake ni mashuhuri kwa watu".[161]

Naye kaipokea Hadithi hio kutoka kwa Khalid bin Yazid Al-'Amri. Abu Hatim na Yahya wanasema kwamba ni "Mwongo". Anasema Ibn Hibban: "Anasimulia Hadithi za kutunga kutoka kwa wapokezi thabiti.[162] Anasema Musa bin Harun: "Dhaifu".[163] Na huenda ikawa kuna madhaifu wengine wengi, sihangaiki kuwatafuta: hao wawili wanatutosha. Lakini hatimae nimekuta katika kitabu *Asbabu Al-Nuzul*[164] cha Al-Suyuti, akisema kwamba Hadithi hii: "Kaipokea Al-Tabarani katika *Al-Awsat* kwa *sanad* yenye wapokezi wasiojulikana". Kwa hivyo, huu ni udhaifu juu ya udhaifu.

Riwaya nyengine kaisimulia Al-Tabari,[165] lakini katika *sanad* yake kuna Asbaat, naye ni Asbaat bin Nasr, naye ni dhaifu. Anasema Harb: "Nilimuuliza (Al-Imamu) Ahmad (bin Hanbal) kuhusu Hadithi zake? Akasema: "Sijui" kana kwamba alimuona kuwa ni dhaifu". Anasema Abu Hatim: "Nimemsikia Abu Nuaim akisema kuwa ni dhaifu, na akasema Hadithi zake zote zinaporomoka, zimegeuzwa *sanad* zake". Anasema Al-Saji: "Anapokea Hadithi hazina ushahidi mwengine (yaani anazisimulia yeye tu wapokezi wengine wote hawakuzipokea Hadithi kama hizo)".

Na Asbaat kaipokea Hadithi hio kutoka kwa Al-Suddi.[166] Naye ni Ismail bin Abdil-Rahmaan Al-Suddi, Shia wa kule kule mjini Al-Kufa, aliyekuwa

---

160 - Al-Tabarani *Al-Awsat* j. 6, uk. 218, Hadithi na. 6232.

161 - Ibn Hajar *Lisanu Al-Mizan* j. 5, uk 307, *tarjama* na. 1030.

162 - Yaani ima yeye ndio mtunzi: kisha anawabandika nazo wao, au anazisikia Hadithi hizo kutoka kwa mtunzi kisha yeye anapozisimulia na kutaja wapokezi hamtaji mtunzi huyo: hutaja wale wapokezi thabiti tu. Lakini kwa vile yeye mwenyewe kaitwa kuwa ni "Mwongo" basi tuhuma kubwa zaidi iko kwake.

163 - Kwa urefu tazama *Lisanu Al-Mizan* j. 2, uk, 389, *tarjama* na. 1598.

164 - Uk. 106.

165 - Al-Tabari *Jami'u Al-Bayaan* j. 6, uk. 343-344.

166 - Tazama usije ukachanganya: Al-Suddi huyu siye yule tuliyemuelezea katika sura ya kwanza chini ya kichwa cha habari kisemacho *Riwaya kwa njia za Kisunn*: huyu ni Ismail

akiwatukana Abu Bakr na Umar. Naye ni dhaifu sana, bali kaitwa mwongo. Anasema Abdullah bin Habib bin Abi Thabit: "Nilimsikia Al-Sha'abi akiambiwa kuwa Al-Suddi kapewa hadhi ya Qur-ani. Akasema: "Al-Suddi kapewa hadhi ya ujinga". Na akasema Yahya kuwa ni "Dhaifu". Na akasema Abdullah bin Ahmad: "Nimemuuliza Yahya kuhusu wao (watu wawili Ibrahim bin Muhajir na Al-Suddi), akasema wanakaribiana kwa udhaifu". Na anasema Al-Duri kutoka kwa Yahya akisema: "Dhaifu". Na akasema Al-Juzajani kuwa ni "Mwongo mtukanaji. Anasema Al-'Uqaili: "Dhaifu: alikuwa akiwasema vibaya Mashekhe wawili (Abu Bakr na Umar)". Anasema Al-Tabari: "Hadithi zake hazifanywi kuwa ni hoja".[167] Na anasema Mu'utamir bin Sulaiman katika maelezo juu ya Muhammad bin Al-Saib Al-Kalbi, kutoka kwa Laith bin Abi Sulaim akisema kwamba: "Katika (mji wa) Al-Kufa kulikuwa na waongo wawili: mmoja ni Al-Kalbi na mwengine ni Al-Suddi".[168]

Na Al-Suddi ndiye msimulizi wa Hadithi hio, naye hakusema nani kamsimulia Hadithi hio, naye si Sahaba. Ukiongezea na udhaifu wake mkubwa, unapata janga juu ya balaa.

Hizo ndizo *sanad* za Hadithi hio ya Ali kutoa sadaka ya pete wakati yumo kwenye kurukuu iliosimuliwa na wapokezi wa Kisunni ambayo Shia wameitolea hoja juu ya tafsiri yao hio. Kwa ufupi ni kuwa, tunachoweza kukisema hapa ni kuwa katika ulimwengu wa Kisunni hakuna Hadithi yoyote sahihi juu ya Habari hii ya kuwa Aya hio ilimteremkia Ali kwa kutoa sadaka ya pete yake. Na anayedai kuwa kuna Hadithi sahihi na-atuletee Hadithi hio na *sanad* yake na kitabu inachopatikana. Bali ukweli ni ule ule aliousema Ibn Taymiya – kama alivyomnukuu Al-Tabatabai – kwamba Hadithi hizi zote ni za-kutunga. Ninasema: hakuna chenye kuonesha ukweli huu kuliko kule Aya kuonesha maana tafauti na Hadithi hio, na pia kule Aya kusema kitu halafu kisiwe – Allah na Mtume wamekuwa wasimamizi wa mambo yetu,[169] lakini Ali hakuwa na wote wamo katika neno moja lililomo katika Aya moja kama tulivyobainisha

---

bin Abdil-Rahmaan Al-Suddi; yule ni Al-Suddi Al-Saghiir, jina lake ni Muhammad bin Mar-wan. Na wote wamejeruhiwa sana lakini Al-Suddi Al-Saghiir kajeruhiwa zaidi.

[167] - Tazama *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 1 uk. 273.

[168] - Tazama *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 9 uk. 157.

[169] - Yaani Mtume kawa msimamizi wa mambo yetu kwa amri ya Allah.

kabla. Na cha kufahamu ni kuwa riwaya zenye kuzungumzia sababu za kuteremka kwa Aya na riwaya za tafsiri, kama zipo sahihi basi ni chache mno: asilimia kubwa ya riwaya hizi ni dhaifu na za kutunga. Anasema Sheikh Abu Al-Hasan,[170] katika mukhatasari wake wa tafsiri ya Al-Baydhawi:

> Hakika asilimia kubwa ya *tafsiru ma-athur*[171] imeingia kwa wasimulizi kutoka kwa mazindiki[172] wa Kiyahudi na Kifursi (Kiirani), na Waislamu waliokuwa (mwanzoni ni katika) Ahlu Al-kitab.[173]

TANBIHI

Ningependa kutoa *Tanbihi* juu ya dai lisilo na ukweli la mtunzi wa kitabu kinachoitwa *Al-Muraja'aat* ambacho kitabu chenyewe kimeandikwa juu ya mjadala wa kubuni: hauna ukweli, halafu ndani mumejaa mambo yasio na ukweli! Mtu huyu hana haya?! Bado anaendelea tu hadi leo kutaja mambo yasio na ukweli katika wakati ambapo kila kitu tayari kimeandikwa kwa *sanad?!* Alipokuwa akiizungumzia Aya hio tunayoijadili hapa, mtunzi wa kitabu hicho – bwana Sharafu Al-Din Al-Musawi – alisema: "Bali kuteremka (Aya hii) kwa Ali ni miongoni mwa mambo ambayo mufasirina wamekubaliana".[174] Kisha akatoa hoja kwa riwaya iliojaa wapokezi dhaifu na kuiita riwaya hio kuwa ni sahihi, kama tutavyobainisha katika sehemu ijayo ya riwaya za Kishia. Sasa yeye anatwambia kuwa wafasirina wamekubaliana kwamba Aya hio imemteremkia Ali; Al-Tabatabai –

---

170 - Yeye ni Mmisri lakini alichukua uraia wa Oman; alikuwa akisomesha hapa Oman, na kwa habari za mwisho nilizozipata ni kuwa kafariki dunia alipokwenda matibabu huko Misri. Inasemekana ni katika waliokuwa karibu sana na Sayyid Qutb.

171 - ***Tafsiru ma-athur*** iko ya namna tatu: moja ni tafsiri ya Qur-ani kwa Qur-ani. Hii ni tafsiri sahihi kuliko zote, nayo sio iliokusudiwa katika maneno hayo ya Abu Al-Hasan. Pili na tatu: ni tafsiri iliosimuliwa kutoka kwa Mtume (s.a.w.) na Masahaba. Hii ndio alioikusudia Abu Al-Hasan. Asilimia kubwa ya tafsiri ya aina hii haikuthibiti kwa riwaya sahihi. Lakini pia ziko riwaya nyengine zimethibiti.

172 - Mazindiki ni wanafiki: makafiri wanaojifanya Waislamu.

173 - Sheikh Muhammad, Abu Al-Hasan *Taysir Al-Baydhawi* uk. 8. Na – kwa asili – hayo ni maneno ya Ibn Kathir kama ilivyo katika *Manahilu Al-'Irfan* cha Al-Zarqani, j. 2, uk. 17.

174 - Tazama *Al-Muraja'at* uk. 373, katika *muraaja'a* na. 40.

mfasiri wa Kishia – katika *Al-Mizan*[175] anamtaja Ibn Taymiyya akinukuu makubaliano kuwa Hadithi hio ni ya kutunga! Sasa tumfate nani: Sharafu Al-Din anayedai makubaliano hewa au Al-Tabatabai anayenukuu tafauti na Sharafu Al-Din?

Kwa ufupi, ni kuwa tumenukuu maneno ya Ibn Kathir akisema: "Na kwa ujumla, hakikusihi chochote (katika Hadithi hii) kwa sababu ya udhaifu wa *sanad* zake na kutokujulikana wapokezi wake".[176] Pia Anasema aliyetia maelezo tafsiri *Al-Kashaf*[177] ya Al-Zamakhshari – baada ya kuwa Al-Zamakhshari ameileta riwaya hio (ya sadaka ya pete) – anasema mtiaji maelezo huyo kuhusu riwaya hio: "(Na riwaya) hii batili haina asili (msingi)".[178] Anasema Ibn Taymiyya katika *Al-Muqadimat Fii Usuli Al-Tafsir* kwamba Hadithi hii: "Hakika yake ni katika utunzi wa Rafidha (Shia)".[179] Ama Al-Qurtubi yeye amegusia riwaya tafauti tu, na alipokuja katika riwaya hii – dhahir ni kuwa – *matn* (text) yake kaidhoofisha. Anasema: "Na kulitafsiri (neno) zaka (lililotajwa katika Aya hio) kuwa maana yake ni kutoa sadaka ya pate, ni jambo lililo mbali".[180] Ama Ibn Jarir Al-Tabari, yeye kasema kuwa Aya hii imemterekia Ubaada bin Samit, kisha akaleta riwaya hio. Kisha akanukuu kauli nyengine na riwaya zao, lakini kauli yake yeye ni hio ya mwanzo kwamba Aya hio imemteremkia Ubaada bin Samit.[181]

Sasa yako wapi hayo makubaliano ya mufasirana alioyadai Sharafu Al-Din Al-Musawi katika kitabu chake *Al-Muraja'aat* kwamba Aya hii: **"Hakika *Walii* wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini tu…",** imemteremkia Ali bin Abi Talib?!

---

[175] - J. 6, uk. 25.

[176] - Ibn Kathir *Tafsiru Al-Qur-ani Al-'Adhim* j. 2, uk. 67, katika tafsiri ya Aya ya 55 ya sura 5.

[177] - J. 1, uk. 682.

[178] - Yaani si Hadithi kamwe!

[179] - Nimeinukuu kauli hii ya Ibn Taymiyya kutoka kwa aliyetia maelezo tafsiri ya Al-Zamakhshari *Al-Kashaf* j. 1, uk. 682.

[180] - Al-Qurtubi *Al-Jaami'u Liahkami Al-Qur-an* j. 6, uk. 208.

[181] - Tazama Ibn Jarir *Jami'u Al-Bayan* j. 6, uk. 343-344.

RIWAYA ZA KISHIA

UTANGULIZI

Sasa baada ya kutazama riwaya walizochomekewa wapokezi wa Kisunni,[182] na-tutazame riwaya zilizosimuliwa na Shia. Al-Tabatabai katunukulia riwaya si kidogo, nazo ni zenye *mutun* (texts) zenye mgongano. Na hapa hatuhitaji wala hatutopoteza wakati kwa kupekuwa wapokezi wake, bali tutazama *mutun* (texts) za riwaya hizo tu. Isipokuwa kuna riwaya moja tu ya Al-Tha'alabi – naye ni Sunni[183] – nimeinukuu katika sehemu hii kwa lengo la kuonesha jinsi gani riwaya hizo zinagongana, na pia kwa kuzingatia ukweli kwamba Al-Tabatabai na wengine kama Sharafu Al-Din Al-Musawi pia wanaonekana kuihusisha zaidi na kuitegemea zaidi riwaya hio katika vitabu vyao, kwa hivyo nimeihesabu kana kwamba imepokewa kwao. Riwaya hio, pamoja na kuonesha udhaifu wa *matn* yake, pia tutatazama *sanad* yake.

RIWAYA

Riwaya ya kwanza inasema:

> Hakika ya watu miongoni mwa Mayahudi walisilimu, miongoni mwao ni Abdillahi bin Salam na Asad bin Tha'alaba na Ibn Yaamin na Ibn Suriya, basi wakamjia Mtume (s.a.w.) wakamwambia: Ewe Nabii wa Allah! Hakika Musa aliusia kwa Yoshua bin Nun (kuwa Awe Khalifa baada yake), basi ni nani wasii wako (atayekuwa Khalifa baada yako) ewe Mjumbe wa Allah?[184] Na ni nani Walii (Msimamizi wetu) baada yako? Basi ikateremka Aya hii: "Hakika *Walii* wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini tu: wale ambao wanasimamisha sala na

[182] - Na hapa ndipo walipoteleza wasimulizi wa Kisunni: kukubali kusimulia riwaya kutoka kwa Shia, watu ambao ni mashuhuri kwa utunzi wa Hadithi kama wao wenyewe Maimamu wa Kisunni na watafiti wa Kisunni walivyoeleza. Na kwa hivyo, wameweza Shia kuwachomekea Sunni riwaya nyingi za kutunga hata katika vitabu muhimu kwa Sunni.

[183] - Sikuona alipoandikwa kuwa ni Sunni lakini tafsiri yake inaonesha hivyo.

[184] - Maneno haya yanaashiria kwa mbali kwamba suala la wasia juu ya uimamu na ukhalifa limetokana na Mayahudi waliosilimu. Riwaya nyengine zinasema kuwa muasisi wa fikra hii ni Myahudi aliyeitwa Abdullahi bin Saba-a, lakini ukweli ni kuwa hakuna riwaya thabiti juu ya kuwepo kwa kiumbe huyu kamwe.

wanatoa zaka nao ni wenye kurukuu".[185] Basi Mtume (s.a.w.) akasema: 'Simameni.' Basi wakasimama wakaja msikitini kutahamaki kuna muombaji yuko nje, akasema Mtume (s.a.w.): ewe muombaji je kuna yoyote aliyekupa kitu? Akasema: 'Ndio: pete hii.' Akasema (Mtume s.a.w.): 'Nani kakupa?' Akasema: 'Kanipa yule mtu anayesali. Akasema (Mtume s.a.w.): 'Katika hali gani kakupa?' Akasema: 'Alikuwa yuko katika rukuu, basi Mtume (s.a.w.) akapiga *takbiri*[186] (Allahu Akbar), na watu wote wa msikitini wakapiga *takbiri".* Basi Mtume (s.a.w.) akasema: "Ali ni *Walii* (Msimamizi) wenu baada yangu".[187]

Hio ni Hadithi ya kwanza aliotunukulia Al-Tabatabai. Sasa tazama tafauti ya Hadithi hio na Hadithi ya pili katika Hadithi alizotunukulia. Hadithi ya pili aliotunukulia – nafupisha – inasema:

Abu Rafii anasema: niliingia kwa Mtume (s.a.w.) siku moja naye kalala na nyoka yuko pembeni kwa nyumba. Nikachukia kumuua ili nisimuamshe Nabii (s.a.w.): nikadhani kuwa anapewa wahyi (wakati huo)….Basi akaamka naye anasoma:

إِنَّمَا وَلِيُّكُمُ اللهُ وَرَسُوْلُهُ وَالَّذِيْنَ آمَنُوْا الَّذِيْنَ يُقِيْمُوْنَ الصَّلاَةَ وَيُؤْتُوْنَ الزَّكَاةَ وَهُمْ رَاكِعُوْنَ

Hakika *Walii* wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini tu: wale ambao wanasimamisha sala na wanatoa zaka nao ni wenye kurukuu.

Kisha akasema: '*Al-hamdu Lillahi* Ambaye kaitimiza neema yake kwa Ali, na pongezi kwake kwa neema yake alioitimiza kwake……'.

---

[185] - Sura 5 Aya 55.

[186] - Tazama Hadithi hii inamfanya Mtume (s.a.w.) kuwa hakuuamini wahyi aliopewa mpaka baada ya kumuuliza muombaji ndio akauamini na kwa hivyo akapiga *Takbir* kwa furaha! Hadithi ya kutunga haisalimika kutokana na nukta (points) nyingi dhaifu.

[187] - Al-Tabatabai *Al-Mizan* j. 6, uk. 17, naye kainukuu kutoka katika kitabu *Al-Burhan* na *Ghayatu Al-Maram* kutoka kwa Al-Sadduq kwa *sanad* yake kutoka kwa Abi Ja'afar. Na hapa utaona kuwa Mtume (s.a.w.) katika maneno haya: **"**Ali ni *Walii* (Msimamizi) wenu baada yangu" anatoa habari ya jambo ambalo halikuwa!

Tazama tafauti baina ya Hadithi ya kwanza na Hadithiya pili! Ya kwanza Mayahudi waliosilimu walikwenda kwa Mtume (s.a.w.) wakamuuliza kuhusu khalifa ni nani baada yake, akashushiwa Aya hio kisha ndio akenda msikitini akamkuta masikini kapewa sadaka ya pete na Ali: hapa tunapata kwamba alipata wahyi wa Aya hio naye yumo usingizini tena aliyekuwepo ni Abu Rafii tu!

Sasa endelea kutazama tafauti iliopo baina ya Hadithi hizo mbili na Hadithi ya tatu. Hadithi ya tatu – kutoka kwa Abi Rafi'i vile vile – inasema:

> Muombaji alisimama kwa Ali bin Abi Talib naye yumo katika kurukuu katika sala ya *tatawu'i* (si ya lazima). Basi (Ali) akavua pete yake akampa muombaji (huyo), basi akamjia Mtume (s.a.w.) akamjuilisha hivyo, basi Mtume (s.a.w.) ikamteremkia Aya hii:
>
> > **Hakika *Walii* wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini tu: wale ambao wanasimamisha sala na wanatoa zaka nao ni wenye kurukuu.**
>
> Mtume (s.a.w.) akatusomea (Aya hio) kisha akasema: 'Yule ambaye mimi ni Mawla wake, basi na Ali ni Mawla wake'.

Mawla kwa tafsiri ya Kishia hapa ni msimamizi yaani mtawala, na maana ni: "Yule ambaye mimi ni msimamizi wa mambo yake, basi na Ali ni msimamizi wa mambo yake".

Tazama ukweli kwamba kule Aya imeteremka kwanza ndio Mtume (s.a.w.) akenda msikitini alikokuweko Ali na masikini mwenye kuomba: hapa masikini alipewa pete baadae yeye mwenyewe ndio akenda kwa Mtume (s.a.w.), na hapo ndio Mtume (s.a.w.) akateremshiwa Aya hio. Tena tunapata hapa kuwa Mtume (s.a.w.) baada ya hapo alisema: "Yule ambaye mimi ni *Mawla* wake, basi na Ali ni *Mawla* wake," wakati katika riwaya nyengine nyingi, tunapata kwamba maneno haya Mtume (s.a.w.) aliyasema katika sehemu iitwayo Ghadir alipokuwa akirudi katika Hijjatul-Wadaa – ufinyanzi wa Hadithi wajigonga wenyewe kwa wenyewe!

Tazama tena mgongano mwengine uliomo katika riwaya nyengine na hizo. Riwaya nyengine – ninafupisha – inasema kwamba Mtume (s.a.w.)

aliteremshiwa Aya hio na ikawa kwa mujibu wa Aya hio, Waislamu wameamrishwa wawatii Uli-L-Amri, ikawa hawakufahamu. Basi Mtume (s.a.w.) akatakiwa aibainishe (maana ya kuwatii Uli-L-Amri) kama alivyobainisha Sala, Zaka, Funga na Hija. Mtume (s.a.w.) akaogopa wasije wakartadi na kumkadhibisha (wakamwita yeye kuwa ni mwongo)![188] Basi ikawa ni dhiki kubwa kwake, na akarejea kwa Mola wake basi Allah akampa wahyi (wa Aya isemayo):

> **Ewe Mtume fikisha kile ulichoteremshiwa kutoka kwa Mola wako, na kama hukufanya basi hukufikisha ujumbe wake na Allah anakukinga kutokana na watu.[189]**

Basi (hapo Mtume s.a.w.) akapasua amri ya Allah na akautangaza *utawala* wa Ali siku ya Ghadir.[190]

Tazama tafauti iliopo! Kule katika Hadithi ya Abi Rafi'i tunapata: ((Mtume (s.a.w.) akatusomea (Aya hio)" yaani baada ya kuteremka Aya hio baada ya Ali kumpa muombaji pete: "Kisha akasema (Mtume s.a.w.): 'Yule ambaye mimi ni *Mawla* wake, basi na Ali ni *Mawla* wake". Wakati katika Hadithi hii, tunapata kwamba Mtume (s.a.w.) baada ya kupewa amri hio na kutakiwa awafasirie watu makusudio ya kumtii *Uli-L-Amri* na *Waliy (Walii),* akaogopa kufanya hivyo ili Masahaba wasije wakartadi na kumuona kuwa yeye ni mwongo! Kisha ikateremka Aya nyengine kumtaka lazima afikishe, basi akafanya hivyo siku ya Ghadir baada ya Hijjatu Al-wadaa! Tazama mgongano wa riwaya za kupakasa hizi: kule tangazo la ukhalifa wa Ali lilitolewa Madina mara tu baada ya kuteremka Aya hio; huku tangazo la ukhalifa wa Ali halikutolewa Madina mara tu baada ya kuteremka Aya hio, bali lilitolewa baada ya siku kupita katika sehemu ya Ghadir Khummi kwani kule Madina Mtume (s.a.w.) alihofia kwamba

---

[188] - Vipi wartadi na kumkadhibisha naye Mtume (s.a.w.) – kwa mujibu wa Shia – alikwisha kumtangaza Ali tangu huko Makka kabla yao kusilimu; na wengine ambao walikwisha kusilimu ndio wameshakuwa wala hawakurtadi, waje wartadi leo Madina baada ya kuwa wameshaingiwa na imani na kuwacha mali zao na jamaa zao huko Makka kwa ajili ya Uislamu?! E riwaya za kutunga maisha hazikai sawa wee!

[189] - Sura 5, Aya 67.

[190] - Al-Tabatabai *Al-Mizan* j. 6, uk. 16-17.

Masahaba watartadi na kumkadhibisha, hadi hapo ilipokuja Aya nyengine ikimuhimiza kufikisha ndio akafikisha naye yuko Ghadir: si Madina!

Pia tazama tena kitu chengine! Nacho ni kuwa huko Ghadir inadaiwa kuwa Mtume (s.a.w.) aliutangaza ukhalifa wa Ali kwa maneno yasemayo: "Yule ambaye mimi ni *Mawla* wake, basi na Ali ni *Mawla* wake". Sasa maneno haya si pia yamo katika Hadithi hio ambayo inadaiwa kuwa aliitamka huko Madina wakati ilipoteremka Aya hio isemayo: **"Hakika *Walii* wenu ni Mwenyezi Mungu…..**; sasa vipi tena isemwe kwamba Mtume (s.a.w.) huko Madina aliogopa kuifasiri maana ya Waliyy (Walii) ili Masahaba wasije wakartadi na kwamba aliifasiri maana hio huko Ghadir, ilhali maneno ya Hadith ya Ghadir ndio yale yale ya Hadithi ya Madina punde tu baada ya kuteremka Aya?! Sasa vipi na nini alichokiogopa?!

Utaona baadae – *In shaa Allah* – tutapoizungumzia Aya isemayo: "Na waonye jamaa zako wa karibu" kwamba pia kuna mgongano baina ya riwaya zao zenye kuihusu Aya hio na riwaya zao zenye kuihusu Aya hii: **"Hakika *Walii* wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini tu"...** Katika Aya **"Na waonye jamaa zako wa karibu"** – ambayo iliteremka Makka katika hatua za mwanzo za ulinganiaji – wenzetu wana riwaya kwamba Mtume aliwakusanya jamaa zake na kuutangaza ukhalifa wa Ali; wakati hapa katika Aya **"Hakika *Walii* wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini tu"..** wana riwaya kwamba Mtume (s.a.w.) aliogopa kumtangaza Ali ili Masahaba wasije wakartadi! Na hii ina maana kwamba Ali – kwa amri ya Allah – katangazwa kuwa ni khalifa si chini ya miaka 20 iliopita huko Makka; lakini Ali huyo huyo hakutangazwa – pamoja na Allah kutoa amri – kwa muda mrefu kwa hofu ya watu kurtadi huko Madina! Katangazwa lakini hakutangazwa! Kwa lugha nyengine, mtu ambaye ameshatangazwa miaka 20 iliopita huko Makka kwa amri ya Allah, na kwa hivyo – bila shaka – watu wote wanajua, vipi tena Mtume (s.a.w.) aogope kumtangaza huko Madina? Mgongano baina ya riwaya uko bayana.

Kisha Al-Tabatabai akatoa Hadithi nyengine iliokuja katika mapokezi ya Kisunni, nayo ni Hadithi alioisimulia Al-Tha'alabi katika tafsiri yake,[191]

[191] - Al-Tha'alabi *Al-Kashfu Wa Al-Bayan* j. 4, uk, 80.

lakini nayo pia inagongana na Hadithi nyengine zote. Katika Hadithi hii – nayo ni kutoka kwa Abu Dhar – anasema Abu Dhar:

> Nimemsikia Mtume (s.a.w.) kwa masikio yangu haya – vyenginevyo ayatie uziwi, na nikamuona kwa macho yangu haya vyenginevyo ayatie upofu – akisema: 'Ali ni kiongozi wa watu wema na ni mwenye kuwaua makafiri; atayemnusuru atanusuriwa; atayemuacha mkono naye ataachwa. Basi sikiliza! Hakika ya mimi (Abu Dhar) nilisali nyuma ya Mtume (s.a.w.) Sala ya adhuhuri……akaingia muombaji msikitini ikawa hakuna aliyempa…..na Ali alikuwa yuko kwenye rukuu akamuashiria kwa kidole chake cha ncha cha (mkono wa) kulia..akaja muombaji akachukua pete kutoka kwenye kidole chake cha ncha cha (mkono wa) kulia. Na hayo kwenye jicho la Mtume (s.a.w.)…Mtume alipomaliza kusali akanyanyua kichwa chake mbinguni akasema: E Allah! Hakika ya ndugu yangu Musa alikuomba akasema:
>
> > **Mola wangu kifunue kifua changu**Unirahisishie jambo langu**Unipe msaidizi kutoka katika watu wangu**Haruna ndugu yangu.[192]**
>
> Basi ikamteremkia Qur-ani[193] ikitamka: **'Tutautia nguvu mkono wako kwa ndugu yako; na tukupeni ushindi.[194]** E Allah na mimi Muhammad ni Nabii wako na mchaguliwa wako. Basi kifunue kifua changu**Unirahisishie jambo langu**Unipe msaidizi kutoka katika watu wangu**Ali, upe nguvu kwaye mgongo wangu". Anasema Abu Dhari: 'Wallahi Mtume hakukamilisha kusema ila na Jibril aliteremka na Aya kutoka kwa Allah..akasema: Ewe Muhammad soma….:
>
> > **Hakika *Walii* wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini tu: wale ambao wanasimamisha sala na wanatoa zaka nao ni wenye kurukuu.**
>
> Kisha akasema: "*Al-hamdu Lillahi* Ambaye kaitimiza neema yake kwa Ali, na pongezi kwake kwa neema yake alioitimiza kwake……

---

192 - Sura 19 Aya 25-31.

193 - Ha! Iliteremka Qur-ani zama za Nabii Musa? Au ikateremka Taurati? Usijeukaniambia: "Aaa ni Qur-ani kilugha", name nikakwambia: "uhakika wa Kisharia unatangulizwa kulikoni uhakika wa kilugha" **(الحقيقة الشرعية مقدمة على الحقيقة اللغوية).**

194 - Sura 28 Aya 35.

Tazama Hadithi hii ya kuundwa kule Al-Kufa kwa Al-A'amash – msimulizi wa riwaya hii – jinsi inavyogongana na riwaya nyengine! Hapa tunapata kwamba Mtume (s.a.w.) alikuwemo kwenye msikiti wakati tokeo hilo lilipotokea: riwaya inasema:

> Hakika ya mimi nilisali nyuma ya Mtume (s.a.w.)……akaingia muombaji msikitini ikawa hakuna aliyempa. Na inasema: 'Akaja muombaji akachukua pete kutoka kwenye kidole chake cha ncha cha (mkono wa) kulia. Na hayo (yalitendeka) kwenye jicho la Mtume (s.a.w.)….

Wakati riwaya hii hapa yatongoa hivi, kule katika riwaya nyengine tunaambiwa kwamba Mayahudi waliosilimu walikwenda kumuuliza Mtume (s.a.w.) kuhusu khalifa baada yake. Kisha ikateremka Aya hio, kisha yeye na wao wakaja msikitini wakati Ali anasali. Tena, kule sala ilikuwa ni ya nafila (si ya wajibu); huku walikuwa wakisali adhuhuri.

Jambo jengine lililomo katika Hadithi hii ni kuwa Hadithi inasema: "Akaja muombaji akachukua pete kutoka kwenye kidole chake cha (mkono wa) kulia. *Na hayo ni kwenye jicho la Mtume (s.a.w.)…".* *Ninasema:* Hii inamaanisha kwamba Mtume (s.a.w.) kalishuhudia tokeo hilo, wakati katika riwaya iliopita tunapata kwamba Mtume (s.a.w.) alimkuta maskini huyo nje ya Msikiti akamuuliza ni nani aliyempa pete hio na alikuwa katika hali gani? Akasema ni yule mtu yaani Ali na alikuwa katika hali ya kurukuu. Mtume (s.a.w) akapiga *takbiri.* Na hii – kama unavyoona – inaonesha kuwa Mtume (s.a.w.) hakushuhudia jambo hilo. Kwa hivyo, katika riwaya ya kwanza Mtume (s.a.w) hakulishuhudia tukio hilo; katika riwaya ya pili Mtume (s.a.w) kalishuhudia tukio hilo – kashuhudia lakini hakushuhudia! Inaonesha watunzi hawakuwa na *ijtimai* kabla ya utungaji wao!

Sasa tazama kitu chengine: nacho ni kuwa hapa – katika Hadithi hii – Mtume (s.a.w.) aliomba dua kwamba Allah amfanye Ali kuwa khalifa baada yake, na Allah akampokelea dua hio na akateremshiwa Aya hio kama ni habari na ahadi kutoka kwa Allah! Na Mtume (s.a.w.) akashukuru na kutoa pongezi kwamba dua yake imetakabaliwa, akasema: "*Al-hamdu Lillahi* Ambaye kaitimiza neema yake kwa Ali, na pongezi kwake kwa

neema yake alioitimiza kwake". Suali ni kuwa je Ali alikuwa khalifa baada ya Mtume (s.a.w.)?! Dua ya Mtume (s.a.w.) imekwenda wapi na ahadi ya Allah imekwenda wapi? Mtunzi wa Hadithi hii hakuwa hodari katika kazi yake ya kupakasa Hadithi kule mjini Al-Kufa!

Ama katika *sanad* ya riwaya hii, kuna Al-A'amash, Sulaiman bin Mihran, Shia wa kule kule mjini Al-Kufa, naye ni mwenye kughushi na Hadithi yake hapa ni *mu'an'an* (kutoka kwa fulani).[195] Anasema Wahb bin Zam'a Al-Mar-wazi: "Nimemsikia Ibn Mubarak anasema: 'Hakika wamezifisidi Hadithi za watu wa Al-Kufa Abu Is-haq (Al-Sabi'i) na Al-A'amash wenu". Na akasema: "Nimemsikia Mughirah anasema: 'Amewaangamiza watu wa Al-Kufa Abu Is-haq na Al-A'amash wenu huyu". Na akasema Al-Imamu Ahmad bin Hanbal: "Hadithi za Al-A'amash zinagongana". Anasema Al-Dhahabi: "Naye anaghushi, na huenda akaghushi kutoka kwa watu madhaifu". Anasema Ibn Al-Madini: "Al-A'amash alikuwa akikosea sana katika Hadithi za hawa (wapokezi) dhaifu".[196]

Pia yumo katika *sanad* ya riwaya hii Qais bin Al-Rabii, naye pia ni Shia wa kule kule mjini Al-Kufa kwenye kiwanda cha ufinyanzi wa Hadithi, tena ni dhaifu. Anasema: Amru bin Ali: "Yahya na Abdul-Rahman walikuwa hawasimulii (riwaya) kutoka kwake". Anasema Al-Imamu Ahmad: "Kasimulia Hadithi nyingi munkar". Na "Alikuwa Wakii akimdhoofisha (Akisema kwamba ni dhaifu)". Anasema Ibn Ma'iin: "Si lolote si chochote…..dhaifu…ndani yake kuna udhaifu….Hadithi zake ni dhaifu: hazina maana yoyote". Anasema A'ffan tulimuendea akawa anatusimulia basi wakati mwengine huziingiza Hadithi za Mughira katika Hadithi za Mansur". Yaani hajui hii imepokewa na nani na hii imepokewa na nani. Na hili linatosha kumjeruhi mpokezi. Anasema Abdullahi bin Ali bin Al-Madini: "Nilimuuliza baba yangu kuhusu yeye basi akamdhoofisha sana". Anasema Ibn Abi Shaiba: "Hifdhi yake ni mbaya sana; Hadithi zake zinagongana; anakosea sana; dhaifu katika riwaya; Hadithi zake ni zenye kuachwa". Na wako wengine wengi waliosema kuwa ni dhaifu.[197] Kisha

[195] - Tazama habari za Al-A'amash katika: *Taqribu Al-Tahdhib* uk. 254, *tarjama* na. 2615, na katika *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 4 uk. 195, *tarjama* na. 386.

[196] - Tazama Al-Dhahabi *Al-Mizan* j. 2, uk. 414, *tarjama* na. 3517.

[197] - Tazama maelezo yake kwa urefu katika *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 8, uk. 350, *tarjama* na. 698.

jambo jengine lililomponza bwana huyu ni kuwa pia alikuwa na mtoto wake ambaye alikuwa akitunga Hadithi halafu anaipenyeza katika kitabu cha baba yake! Hii ndio balaa ya Al-Kufa. Tazama utayakuta haya katika marejeo hayo hayo niliokupa hapo chini.[198]

Na riwaya nyengine alioitaja Al-Tabatabai, ni ile riwaya ya Al-Tabrasi katika kitabu chake kilichojaa riwaya za utunzi kiitwacho *Al-Ihtijaj*. Riwaya hio inasema:

> Wanafiki walimwambia Mtume wa Allah (s.a.w.): 'Je kimebaki kitu chochote kwa Mola wako juu yetu alichotufaradhishia – baada ya yale aliotufaradhishia – ili ututajie na nafsi zetu zitulie kwamba hakuna fardhi nyengine? Basi Allah akateremsha kuhusu hayo (Aya isemayo): **((Sema ninakuwaidhini kwa jambo moja tu))** yaani utawala. Allah akateremsha (Aya isemayo): **"Hakika *Walii* wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini tu: wale ambao wanasimamisha sala na wanatoa zaka nao ni wenye kurukuu".** Kisha akasema: "*Al-hamdu Lillahi* Ambaye kaitimiza neema yake kwa Ali, na pongezi kwake kwa neema yake alioitimiza kwake……

Tazama uwongo ulivyowazi katika riwaya hii! Vipi Aya hii **"Hakika *Walii* wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake…"** ifungamanishwe na Aya isemayo **''Sema ninakuwaidhini kwa jambo moja tu''**,[199] halafu jambo moja hilo lifasiriwe kuwa ni utawala wakati katika Aya hio hio: **''Sema ninakuwaidhini kwa jambo moja tu''**[200] Aya imejifasiri wenyewe kwa kulitaja jambo moja hilo ambalo tunawaidhiwa nalo?! Aya kiukamilifu inasema:

> **Sema ninakuwaidhini kwa jambo moja tu, ya kwamba musimame wawili-wawili na mmoja-mmoja kisha mufikiri; (mutaona kwamba) mwenzenu (huyu Muhammad) si mwenye wazimu: hakuwa yeye ila ni mwenye kukuonyeni kutokana na adhabu kali.**[201]

---

[198] - Na inawezekana kuwa kuna wapokezi wengi wasiojulikana, sikuweza kuwaona kwa upekuzi wa haraka haraka. Tazama maelezo ya Qais bin Al-Rabii kwa urefu katika *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 8, uk. 350, *tarjama* na. 698.

[199] - Sura 34 Aya 46.

[200] - Sura 34 Aya 46.

[201] - Sura 34 Aya 46.

Kwa hivyo, utaona kwamba jambo moja lenyewe tulilowaidhiwa kwalo Allah Mwenyewe kalieleza ni lipi nalo ni: **"Musimame wawili-wawili na mmoja-mmoja kisha mufikiri; (mutaona kwamba) mwenzenu (huyu Muhammad) si mwenye wazimu: …"..** Lakini bwana Al-Tabatabai akimnukuu Al-Tabrasi kutoka katika kitabu chake *Al-Ihtijaj* nacho bora angelikiita *Al-Mahjuj* anasema kwamba Aya hio **"Sema ninakuwaidhini kwa jambo moja tu' <u>Maana yake ni utawala".</u>** Hivi ndivyo, ndugu zetu wanavyozifasiri Aya kadha wa kadha za Qur-ani!

Kisha tazama tena mgongano uliokuwepo baina ya riwaya hii **"Wanafiki walimwambia Mtume wa Allah (s.a.w.): 'Je kimebaki kitu chochote kwa Mola wako juu yetu alichotufaradhishia …"..** Halafu tazama na riwaya nyengine zilizotangulia: kule sababu ya kuteremka Aya inayoambiwa kuwa ni ya utawala wa Ali ni:

1) Sadaka yake ya pete.
2) Mayahudi waliosilimu kutaka kujua mtawala baada ya Mtume (s.a.w.).
3) Dua ya Mtume (s.a.w.) apewe msaidizi miongoni mwa jamaa zake kama Musa alivyopewa Harun kuwa msaidizi wake – hizo ni sababu tatu tafauti.

Hapa tunapata kwamba Aya hio **"Hakika *Walii* wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake ……"** imeteremka kwa ajili ya kuibainisha na kuifasiri Aya isemayo: **"Sema ninakuwaidhini kwa jambo moja tu"** – mgongano wa wazi katika *mutun* za riwaya za kufinyanga.

Tazama pia ukweli kwamba riwaya hii inawaita Masahaba kuwa ni wanafiki.[202] Kwa hivyo, kinachotubainikia baada ya utafiti huu, ni kuwa

[202] - Na hili la kuwaita Masahaba kuwa ni makhiana, makafiri na wanafiki ndio ngoma yao? Sijui hawa watu wao ni wacha Mungu kiasi gani na wanatekeleza walioamrishwa na Mola wao kiasi gani hata wale wakawa ndio wanafiki katika mezani yao! Tukijaalia kwamba kweli ukhalifa ulikuwa ni wa Ali – nayo si sahihi – na Masahaba wamemchagua mtu mwengine, basi hilo litakuwa ni kosa moja lilofanywa na watu waliofanya kheri nyingi katika wakati mgumu; wakati sisi leo kwa siku tunamuasi Allah na Mtume wake makosa yasio na idadi wala hatuna kheri tunazozifanya ila chache sana. Sasa nani bora: yule aliyeasi kidogo na kufanya kheri nyingi au mimi na wewe ambao tunafanya maasi mengi na kheri kidogo? Hii ni kujaalia tu ili kwenda sawiya na akili za watu hawa,

riwaya hio ya kuwa Ali alitoa sadaka ya pete na ikawa hio ndio sababu ya kuteremka Aya hio, basi katika masimulizi yake ya Kisunni ***Ka-ramadi ni-shtaddat bihi Al-riihu fii yaumin 'Aasif*** ni kama jivu lililopigwa na upepo mkali katika siku ya kimbunga; riwaya hio katika masimulizi ya Kishia ***Kamathali l-ghaithi A'ajaba Al-kuffara Nabatuh Thumma Yahiju Fatarahu Musfaran Thumma Yakunu Hutaamaa*** ni kama mvua ambayo mimeya yake iliwafurahisha wakulima kisha ikakauka ukaiona imepiga umanjano kisha ikawa mabuwa – uwongo wa riwaya hio uko bayana.

KAULI NYENGINE JUU YA NANI IMEMSHUKIA AYA HIO

Sasa baada ya kuzitazama riwaya walizozitegemea Shia katika tafsiri yao ya Aya hio tulioijadili hapa, na-tutazame kidogo kauli nyengine. Hapa kuna kauli nyengine ya pili kwamba Aya hio imemteremkia 'Ubaada bin Samit. Riwaya hii kaipokea Al-Tabari,[203] lakini katika *sanad* yake kuna Yunus bin Bukair naye kuna tafauti juu yake: wengine wanamdhoofisha na wengine wanamuona kuwa ni mpokezi sahihi.[204] Pia yumo katika *sanad* hio Is-haq bin Yasar, naye pia kuna tafauti juu yake: wengi wamesema kuwa ni mwenye kuaminika, lakini Al-Daraqutni anasema: "Hafanywi kuwa ni hoja".[205]

Kisha Ibn Jarir akaipokea tena Hadithi hio kwa *sanad* nyengine, lakini kwa njia ya Atiyya Al-'Aufi naye ni dhaifu. Alipotajiwa Atiyya, Al-Imamu Ahmad bin Hanbal alisema: "Hadithi zake ni dhaifu". Na akasema Abu Hatim: "dhaifu". Na akasema Al-Nasai: "dhaifu".[206] Bali hata angelikuwa

---

vyenginevyo hakuna wasia wa Ali wala wa Pandu kuhusu ukhalifa: suala hili ni la uwongo uliotungwa katika siasa za kugombania madaraka tu.

[203] - Al-Tabari *Jaami'u Al-Bayaan* j. 6, uk. 343.

[204] - Tazama *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 11 uk. 382, *tarjama* na. 745.

[205] - Tazama *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 1 uk. 225, *tarjama* na. 484.

[206] - Tazama *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 7 uk. 200, *tarjama* na. 414. Na anasema Ibn Hajar: "Mkweli, anakosea sana, Shia, mwenye kughushi". Tazama Taqribu Al-Tahdhib Uk. 394, *tarjama* na. 4616.

ni msimulizi sahihi basi riwaya yake hapa isingelikubalika kwani ni *mursala.*[207]

Na akasimulia riwaya hio Ibn Abi Hatim,[208] lakini yeye kaihusisha riwaya hio na ‘Ubaada bin Samit katika sehemu ya mwisho tu ya Aya hio: sehemu yenye kusema: **“Na atayemfanya Allah na Mtume wake na waumini kuwa ndio vipenzi vyake, basi hakika ya kundi la Allah ni lenye kushinda”.** Lakini katika *sanad* yake kuna Al-Asbagh Al-Harani; sikumuona alipotajwa.[209] Pia yumo katika *sanad* hii, Is-haq bin Yasar, tumemuelezea katika *sanad* ya mwanzo ya Ibn Jarir na kwamba wametafautiana juu yake.

Na ziko kauli nyengine kwamba Aya hio imemteremkia Abu Bakr.[210] Lakini *sanad* yake si madhubuti kwani kuna Al-Mubarak bin Said naye wakati mwengine hukosea na Al-’Uqaili kamtaja katika *Al-Dhu’afaa* (kitabu cha wapokezi dhaifu).[211] Na Al-Mubarak bin Said kashirikiana katika kuisimulia Hadithi hii na Ammar bin Muhammad, naye anakosea sana. Anasema Ibn Hibban: “Ni miongoni mwa wanaokosea sana, na kukithiri makosa yao, basi akastahiki kuachwa”.[212] Na msimulizi wa Hadithi hio ni Said bin Masruq, baba yake Sufyaan Al-Thauri, naye anaisimulia Hadithi hio kutoka kwa Ibn Abbas, lakini dhahir ni kuwa Said bin Masruq hakusikia Hadithi yoyote ile kutoka kwa Masahaba kwani

---

[207] - Hadithi *mursal* au riwaya *mursala* ni ile ambayo mfuasi wa Sahaba anaisimulia kutoka kwa Mtume (s.a.w.) bila ya kumtaja Sahaba aliyemsimulia. Na huenda wakati mwengine ikaitwa Hadithi *mursal* au riwaya *mursala* ile ambayo mtu kaisimulia kutoka kwa mwengine bila ya kusema nani kamsikia.

[208] - Ibn Abi Hatim *Tafsiru Al-Qur-ani Al-’Adhim* j. 4, uk. 1163, Hadithi na. 6553.

[209] - Labda yuko katika vitabu vyengine ambavyo sinavyo; niliyemuona katika vitabu vingi ni Abu Al-Asbagh Al-Harani. Wapekuzi wanaweza kutafuta zaidi. Kwa hali yoyote ile ikiwa Aya hio imemuhusu Ubaada bin Saamit au haikumuhusu si muhimu sana katika mjadala huu, kwani maudhui yetu ni “Je Allah na Mtume wake wamemtangaza Ali kuwa ndiye khalifa?”

[210] - Al-Tha’alabi *Al-Kashfu Wa Al-Bayaan* j. 4, uk. 81.

[211] - Tazama *Tahdhibu Tahdhib* j. 10, uk. 26, *tarjama* na. 49.

[212] - Tazama *Tahdhibu Tahdhib* j. 7, uk. 355, *tarjama* na. 660.

hakuna katika Mashekhe wake waliotajwa katika *Tahdhibu Tahdhib*[213] hata mmoja aliyekuwa Sahaba.[214]

Na kuna kauli nyengine kwamba Aya hio imewateremkia Waislamu wote. Kauli hii imesimuliwa na Al-Tabari[215] kutoka kwa Al-Suddi na Abu Ja'afar, Imamu wa Mashia. Abu Ja'afar huyu ni Abu Ja'far wa mwanzo, Muhammad bin Ali. Lakini kauli hii – pamoja na kuwa ndio sahihi yao – inaweza ikazingatiwa kuwa ni moja tu ya kauli za Mufassirina, kwani hawa wote si Masahaba wala hawakusema wapi wamezitoa riwaya hizo. Pamoja na hayo hizo *sanad* zenye kutufikisha kwa Abu Ja'afar na Al-Suddi si *sanad* madhubuti.

Kwa hivyo, kwa ujmla tunachoweza kukisema ni kuwa hakuna Hadithi thabiti juu ya nani imemteremkia Aya hio inayosema: **"Hakika *Walii* wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini tu"...** Lakini hata hivyo, Hadithi inayosema kwamba Aya hio imemteremkia 'Ubaada bin Saamit hali yake ya kiisnadi haijambo zaidi kuliko zote, na kwa hivyo utaona kwamba Ibn Jarir, Ibn Kathir, Al-Tha'alabi na wengine wameitegemea riwaya hio ya kwamba Aya hii imemteremkia 'Ubaada bin Samit pasina riwaya nyengine kama ilivyo katika tafsiri zao.

MUKHTASARI

1) Tulioijadili hapa ni Aya isemayo:

إِنَّمَا وَلِيُّكُمُ اللهُ وَرَسُوْلُهُ وَالَّذِيْنَ آمَنُوْا الَّذِيْنَ يُقِيْمُوْنَ الصَّلاَةَ وَيُؤْتُوْنَ الزَّكَاةَ وَهُمْ رَاكِعُوْنَ

> **Hakika *Walii* wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini tu: wale ambao wanasimamisha sala na wanatoa zaka nao ni wenye kurukuu.[216]**

---

213 - Tazama *Tahdhibu Tahdhib* j. 4, uk. 73, *tarjama* na. 142.

214 - Shaqiq bin Salama, Abu Wail, ni katika Mashekhe wa Said bin Masruq, lakini Shaqiq bin Salama huyu aliuwahi tu wakati wa Mtume (s.a.w.) bila ya hata kumuona, kwa hivyo naye pia si Sahaba. Tazama *Tahdhibu Tahdhib* j. 4, uk. 317, *tarjama* na. 619.

215 - Al-Tabari *Jaami'u Al-Bayaan* j. 6, uk. 343.

216 - Sura 5 Aya 55.

2) Aya hii Shia wameichukua katika kuthibitisha dai kwamba suala la ukhalifa baada ya Mtume (s.a.w.) si suala la shura (mashauriano); bali ni suala ambalo limetokana na amri tukufu ya Mwenyezi Mungu Mwenyewe.

3) Na hii ni kwamba wao wanalifasiri neno ***Waliyyu (Walii)*** – lililotajwa katika Aya hio – kuwa maana yake ni msimamizi wa mambo, yaani mtawala. Na kwa hivyo, maana ya Aya hio ni:

> Hakika *msimamizi* wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na wale walioamini tu: wale ambao wanasimamisha sala na wanatoa zaka nao ni wenye kurukuu.

4) Kisha wakapokea riwaya zenye kusema kwamba makusudio ya maneno: **"Na wale walioamini tu: wale ambao wanasimamisha sala na wanatoa zaka nao ni wenye kurukuu"** ni Al-Imamu Ali (k.w.), na kwamba yalimteremkia hayo baada ya kutoa sadaka ya pete yake hali ya kuwa yumo katika sala anarukuu.

5) Tumethibitisha kwamba tafsiri hii haikubaliani na elimu ya tafsiri; kwani ni kinyume na kanuni zote za kilugha na za kiusuli.

6) Tumeona kwamba neno hilo ***Waliyyu (Walii)*** lina maana nyingi.

7) Kudai kuwa maana fulani ndio iliokusudiwa kunahitaji dalili (ushahidi).

8) Ushahidi waliotupa Shia ni Hadithi za kutunga: kila Hadithi ina *sanad* yenye wapokezi dhaifu sana au watunzi wa Hadithi. Na wote *taqriban* ni Mashia, na riwaya zote ni za wapokezi wa Al-Kufa, mji wa Mashia. Na riwaya zilizosimuliwa katika vitabu vya Kishia zinagongana kupita kiasi. Na hilo ndilo lile tulilotangulia kulinukuu kutoka katika kitabu cha Hadithi cha Kishia ambapo mtunzi wa kitabu hicho, Al-Tusi anasema:

> Amenikumbusha mmoja wa marafiki..kuhusu Hadithi za Sahibu zetu (Shia)…na kile kilichomo ndani yake miongoni mwa tafauti, kutokukubaliana (Hadithi hizo), migongano na kupingana….[217]

9) Hatimae tunaona kwamba kwa mujibu wa: *1) Sibaq* (Maneno yaliotangulia); *2) Siyaq* (Maneno yanayofatia); *3) Kanuni za kiusuli* (fundamentals of Islamic Jurisprudence) na *Kanuni za kilugha,* basi tafsiri sahihi ya Aya hio isemayo: **Hakika *Walii* wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini tu"** ni **"Hakika *vipenzi* vyenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini tu"** yaani vipenzi vyetu ni Allah (S.W.) Mtume (s.a.w.) na Waumini wa Kiislamu wote. Hii ndio tafsiri sahihi na ya wazi.

[217] - Al-Tusi *Tahdhibu Al-Ahkam* j. 1, uk. 2.

SURA YA PILI

KUHUSU AYA YA MAWADA

Mwenezi Mungu anasema:

قُلْ لا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْراً إِلاَّ الْمَوَدَّةَ فِي الْقُرْبَى

Qul *Laa* As-alukum ‘Alaihi ajran illa al-mawaddata fi-l qurbaa.[218]

Hii ni Aya nyengine katika Aya muhimu zao ambazo Shia wanatolea ushahidi kwamba Ali ndiye khalifa baada ya Mtume (s.a.w.), na kwamba kizazi chake ndicho chenye kurithi ukhalifa baada yake. Ama hoja yao juu ya hayo – sawa na hoja zao katika Aya tulioijadili katika sura iliotangulia – ni baadhi ya riwaya zilizopokewa kwamba Aya hii imewashukia Ali, Fatima na kizazi chao! Kisha baada ya kuzikubali riwaya hizo, Shia wakaweka *falsafa* zao ili kuthibitisha ukhalifa wa Ali na kizazi chake, kama tutavyobainisha baadae *In shaa Allah.*

Lakini kabla ya kuingia huko, kwanza tunakuta kwamba kuna tafauti ya ujumla yaani tafauti ya wanavyuoni wote – si ya Shia na *Jumhur* tu – katika baadhi ya vipengele fulani fulani vilivyomo katika Aya hio, jambo ambalo limepelekea kuwepo kwa tafauti ndogo ndogo nyengine za tafsiri ukiachilia mbali ile tafauti ya msingi ambayo iko baina ya Shia na *Jumhur.* Sheikh Abdullah Salih Al-Farisi – kwa mfano – anaifasiri Aya hio hivi:

قُلْ لا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْراً إِلاَّ الْمَوَدَّةَ فِي الْقُرْبَى

[218] - Sura 42, Aya 23.

Sema kwa haya (ninayokufundisheni) siombi, (sitaki) malipo yoyote kwenu; lakini (nataka) myapende mambo ya kukusogezeni (kwa Mwenyezi Mungu).

Na tafsiri hii ni moja ya tafsiri mbili zilizosimuliwa kutoka kwa Ibn Abbas nayo ni tafsiri ya Al-Hasan Al-Basri pia.[219]

Ama Al-Zamakhshari – mmoja wa Maulamaa wa lugha na tafsiri – yeye ameiletea Aya hio mielekeo miwili yaani uwezekano wa namna mbili, na yote mielekeo miwili hio, ina maana moja kwamba Aya hio maana yake ni: **"Sikuombeni juu yake (kufikisha huku) ujira isipokuwa huu: nao ni kuwa muwapende watu wa karibu yangu (jamaa zangu)".** Huo ni muelekeo wa kwanza alioutoa Al-Zamakhshari. Muelekeo wa pili ni: **"Sikuombeni juu yake (kufikisha huku) ujira katu, lakini hakika ya mimi ninakuombeni muwapende jamaa zanngu nao ni jamaa zenu".**[220] Na hio – ilio katika muelekeo wa kwanza – ndio tafsiri ya Shia wote[221] kama ilivyo katika *Al-Mizan*[222] cha Al-Tabatabai, baada ya kuzipinga tafsiri nyengine zote. Tafauti iliokuwepo baina ya tafsiri ya kwanza ya Al-Zamakhshari na tafsiri yake ya pili, ni kuwa katika tafsiri ya kwanza Mtume (s.a.w.) anaomba ujira juu ya kufikisha kwake na ujira wenyewe ndio huo wa kuwa tuwapende watu wake; wakati katika tafsiri ya pili, Mtume (s.a.w.) haombi ujira katu juu ya kufikisha kwake bali anachokitaka ni kuwa tuwapende watu wake – tafauti ya tafsiri mbili hizo ni kuwepo na kutokuwepo kwa ombi la ujira. Hili tutalizungumzia mahala pake *In shaa Allah.*

Ama Al-'Allama Sheikh Al-Sabuni, yeye kaifasiri Aya hio hivi:

---

[219] - Tazama Al-Baghawi *Ma'aalimu Al-Tanzil* j. 4, uk. 144.

[220] - Tazama Al-Zamakhshari *Al-Kashaf* j. 4, uk. 223.

[221] - Labda inawezekana ikawa wako Shia wenye kushikana na tafsiri ilio katika muelekeo wa pili, lakini cha msingi katika muelekeo wa kwanza na wa pili ni kuwa tuwapende watu wa karibu na Mtume (s.a.w.) nao – kwa mujibu wa Shia – ni Ahlu Al-Bait. Hii ndio kadiri ambayo Shia hawatafautiani kwa kadiri ninavyojua.

[222] - J. 18, uk. 47.

> Wambiye ewe Muhammad: sikuombeni kwa kufikisha ujumbe (huu) kitu (chochote) katika ujira wala mali, isipokuwa muilinde haki ya ujamaa wala musiniudhi, ili nifikishe ujumbe wa Mola wangu.[223]

Na mfano wake ni tafsiri ya Al-Imamu Ibn Kathir, ambapo katika kuifasiri Aya hio alisema:

> Sema ewe Muhammad kuwambia washirikina hao miongoni mwa makafiri wa kikureish sikuombeni kwa ufikishaji huu na kukunasihini (huku) munipe mali; bali ninakuombeni muizuie shari yenu kutokana na mimi na muniachie nifikishe ujumbe wa Mola wangu; kama hamuninusuru basi musinikere kwa sababu ya ujamaa uliopo baina yangu na baina yenu.[224]

Tafsiri hii na ilio kabla ya hii ni moja, nayo si tafsiri ya neno kwa neno, bali ni tafsiri ya maana iliokusudiwa tu kama vile kutia sherehe. Nayo tafsiri hii imesimuliwa pia kutoka kwa mwanachoni wa Umma *(Habru Al-ummah)* na mfasiri mkuu wa Qur-an baada ya Mtume (s.a.w.) naye ni Bahari Ibn Abbas (r.a.), na ikasimuliwa pia kutoka kwa Abu Malik, Ikrima, ‘Ataa, Mujahid, Al-Suddi, Ibn Zaid na Qatada.[225] Kwa hivyo, kwa tafsiri hizo tafauti ambazo wanavyuoni wamekwenda nazo, Aya hio ambayo inasema: **((قُلْ لا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْراً إِلاَّ الْمَوَدَّةَ فِي الْقُرْبَى))**, kwa Kiswahili itafasirika hivi:

1) **Sema kwa haya (ninayokufundisheni) siombi, (sitaki) malipo yoyote kwenu; lakini (nataka) myapende mambo ya kukusogezeni (kwa Mwenyezi Mungu).**

Hii ni tafsiri ya Sheikh Abdullah Salih Al-Farisi, Al-Hasan Al-Basri na ni moja ya riwaya zilizosimuliwa kutoka kwa Ibn Abbas.

2) **Sema sikuombeni juu yake (kufikisha huku) ujira isipokuwa muwapende watu wa karibu yangu (jamaa zangu).**

---

223 - Al-Sabuni *Safwatu Al-Tafasir* j 3, uk. 100.
224 - Ibn Kathir *Tafsiru Al-Qur-ani Al-‘Adhim* j. 4, uk. 99.
225 - Ibn Jarir Al-Tabari *Jaami’u Al-Bayan* j. 25, uk. 29-31.

Hii ni tafsiri ya Al-Imamu Al-Zamakhshari[226] nayo – kama tulivyosema – ndio tafsiri ya Shia.

3) **Sema (Ewe Muhammad): sikuombeni (kwa kufikisha ujumbe (huu) kitu (chochote) ujira wowote, isipokuwa muilinde haki ya ujamaa (wala musiniudhi ili nifikishe ujumbe wa Mola wangu).**

Wenye tafsiri hii – tukichukua tafsiri ya moja kwa moja – wanakusudia kusema: **"Sema: sikuombeni kwa kufikisha huku ujira wowote isipokuwa mapenzi kwa sababu ya ujamaa".** Hii ndio, tafsiri ya aghlabu ya wanavyuoni waliobakia kama vile Al-Sabuni,[227] Ibn Kathir,[228] Al-Alusi[229] na wengine na ndio ninayoiona kuwa ni tafsiri sahihi kwa sababu nitazozitoa *In shaa Allah*.

Sasa – kwa mtazamo wangu – wakati tumo katika kuipekuwa tafsiri ya Aya hio, basi kwanza tunahitaji kutazama mambo matano yaliomo katika Aya yenyewe na moja lililo nje ya Aya. Aya inasema:

قُلْ لا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْراً إِلاَّ الْمَوَدَّةَ فِي الْقُرْبَى

Qul Laa As-alukum 'Alaihi ajran illa al-mawaddata *fi*-l *qurbaa*.

Yaliomo katika Aya ni:

1) Kujua maana ya neno *Qurba* ambalo limo katika Aya hio.
2) Kujua maana za herufi *"Fii"* iliomo katika Aya hio.
3) Aina ya *Istithnaau (Exception)* iliomo katika Aya hio.
4) Siyaq (maneno yalio baada) na *Sibaq* (maneno yalio kabla) ya Aya hio.
5) Kuwepo kwa herufi yenye kukataa ambayo ni *Laa* ikifatiwa na herufi yenye kuonesha kukivua kitu kimoja katika jumla ya vitu yaani *Istithnaau (Exception).*

[226] - Naye kama ulivyoona kwamba kailetea tafsiri hii mielekeo miwili lakini katika mielekeo yote miwili hakuna tafauti kwamba wa kupendwa ni watu wa Mtume (s.a.w.): tafauti iko katika kuomba na kutoomba ujira.
[227] - Al-Sabuni *Safwatu Al-Tafasir* j. 3, uk. 100.
[228] - Ibn Kathir *Tafsiru Al-Qur-ani Al-'Adhim* J. 4, uk. 99.
[229] - Al-Alusi *Ruhu Al-Ma'aani* j. 25, uk. 30.

6) Yaliomo nje ya Aya ni riwaya zenye kuhusiana na Aya hio.

NUKTA YA KWANZA

MAANA YA NENO *QUR-BAA*

Neno *qurbaa* linatokana na neno la Kiarabu *Qaruba* (kitendo kilichopita) *Yaqrubu* (kitendo kilichopo na kijacho) na *Qarabatan* na *Quraban* na *Qurbatan* na *Qurbaa* (jina yaani *noun*), na maana yake ni kukaribia. Ilivyo au aghlabu ni kuwa kukaribia huku kuwe ni kukaribia kunakotokana na maumbile: si kunakotokana na bidii au matakwa ya mtu. Na hii ni kwa sababu kitendo cha Kiarabu ambacho muundo wake unakuja katika mezani hii: *"Fa'ula* (kitendo kilichopita)*…Yaf'ulu* (kitendo kilichopo na kijacho) kama ilivyo hapa *"Qaruba* (kitendo kilichopita) *Yaqrubu* (kitendo kilichopo na kijacho), basi huwa kitendo hicho ni kitendo ambacho kinaonesha kwamba kilichokuwa kutokana na kitendo hicho, basi ni kitu cha kimaumbile: si kwamba mtu kakifanya yeye. Kwa mfano vitendo kama: *Jamula* (kitendo kilichopita)*…Yajmulu* (kitendo kilichopo na kijacho), maana yake ni "Kawa mzuri", na hili ni jambo la kimaumbile ambalo liko nje ya uwezo wa kiumbe. Au neno: *Majuda* (kitendo kilichopita)*…Yamjudu* (kitendo kilichopo na kijacho) maana yake ni "Kawa mtukufu". Na kwa hivyo, wako wanaosema kwamba ikiwa neno "Kukaribia" *ree* yake katika neno la Kiarabu ina *dhamme* yaani likawa linatamkwa *"Qaruba….Yaqrubu"* basi linakuwa neno hilo limemaanisha kukaribia kiroho; na ikiwa *ree* yake – katika neno la Kiarabu – ina *kasra* (katika kitendo kilichopita) na ina *fat-ha* (katika kitendo kilichopo na kijacho) yaani likawa linatamkwa *Qariba…Yaqrabu* basi huwa neno hilo linamaanisha kukaribia kihisia au kimwili. <u>Ninasema:</u> Labda tunaweza kuwatolea ushahidi hawa kwa Aya ya Qur-ani kama: **" وَلا تَقْرَبَا هَذِهِ الشَّجَرَةَ"** ***Walaa Taqrabaa Hadhihi Al-Shajara,*** (Wala musiukaribie mti huu).[230] Neno kukaribia hapa *ree* yake – katika neno la Kiarabu – ina *kasra* (itapokuwa katika kitendo kilichopita) na ina *fat-ha* (katika kitendo

[230] - Sura 2, Aya 35.

kilichopo na kijacho). Na kuukaribia mti bila shaka si kitendo cha kiroho bali ni kitendo cha kihisia – cha kimwili.

Hio ndio maana ya msingi ya neno hilo. Na kwa uhusiano uliopo baina ya maana hio ya msingi na maana ya jamaa wa mtu wa damu,[231] basi jamaa wa mtu wa damu huitwa *Qarabatahu* au *Ulil-Qurba* yaani watu wake wa karibu kwa maana ya jamaa zake. Na hii ni kwa sababu jamaa wa mtu ndio watu wa karibu yake kwa nasaba (ubabani) au kwa *rahim* (umamani).

Kwa hivyo, utapojua kwamba neno *Qurbaa* (ni jina yaani noun), basi utakuwa umejua kwamba tafsiri ya msingi ya Aya hio Tukufu isemayo: **قُلْ لا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْراً إِلاَّ الْمَوَدَّةَ فِي الْقُرْبَى** ni **"Sema kwa haya, siombi malipo yoyote kwenu; isipokuwa mapenzi katika ukaribu".** Hii ndio maana ya msingi au ya neno kwa neno ya Aya hio kabla ya kuipa tafsiri hii na ile kwa mujibu wa fahamu tafauti za wataalamu.

Lakini baada ya kuitazama tafsiri hii ya msingi utaona kwamba ni tafsiri ambayo maana yake haijakamilika, kwani sehemu ya Aya isemayo: **"Isipokuwa mapenzi katika ukaribu,"** si lugha iliowazi. Na kwa hivyo, ni lazima itakuwa kuna hali moja katika mbili:

Moja: ni kuwa katika Aya iwe kuna neno limeondoshwa, nalo ni neno *Dhawi* au *Uli (Wenye au walio)*, na kwa hivyo, baada ya kulikadiria neno hilo, Aya iwe na maana hii: **قُلْ لا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْراً إِلاَّ الْمَوَدَّةَ فِي (ذَوِيْ أَوْ أُوْلِيْ) الْقُرْبَى** ..na tafsiri hapo itakuwa: **"Sema kwa haya, siombi malipo yoyote kwenu; isipokuwa mapenzi katika walio na ukaribu (yaani jamaa)".**

Dhahir, bali bila shaka, hii ndio tafsiri ya Shia. Na kwa ujumla ni kuwa kuondoshwa kwa neno katika Aya au Hadithi ni jambo lisilo na upinzani na mifano katika Qur-ani na Hadithi ni mingi mno. Miongoni mwa hio ni

---

[231] - *Uqaraba* wa kidamu japo kuwa asili yake ni wa kimwili kwa mazingatio yake ya kimsingi, lakini kwa mazingatio mengine ni wa kiroho kwa maana kwamba mtu si lazima awe karibu yako kimwili (physicaly) ndio aweze kuwa jamaa yako. Bali anaweza kuwa yuko Marekani nawe uko Pemba, na kwa mazingatio haya, ndio tumeweza kuuita ujamaa huo kuwa ni wa kiroho. Neno "Wa kiroho" halileti maana sawiya 100% na neno *Ma'anawiy* la Kiarabu, lakini tunajaribu kuleta maana iliokaribiana ili kuikurubisha maudhui katika fahamu za wasomaji.

Aya isemayo: **"وَجَاهِدُوا فِي اللَّهِ".**[232] Tafsiri yake ya neno kwa neno (literally) ni: **"Na fanyeni jihadi katika Mwenyezi Mungu".** Na mfano wa Aya hio, ni Aya isemayo: **"وَمَنْ كَانَ فِي هَذِهِ أَعْمَى فَهُوَ فِي الآخِرَةِ أَعْمَى وَأَضَلُّ سَبِيلاً".** Tafsiri ya neno kwa neno ni: **"Na atayekuwa kipofu katika hii basi yeye katika akhera ni kipofu na mwenye kupotea njia zaidi".**[233] Na mfano wake ni Aya yenye kusema: **"وَأُتْبِعُوا فِي هَذِهِ لَعْنَةً".** Tafsiri ya neno kwa neno ni: **"Na wakafatishiwa katika hii, laana"..**[234]

Katika Aya ya kwanza tunaona kwamba tunaamrishwa tufanye jihadi ***katika Mwenyezi Mungu***. Lakini je kuna kufanya jihadi ***katika Mwenyezi Mungu?*** Neno njia au dini hapa limeondoshwa, na makusudio ni: **"Na fanyeni jihadi katika *njia au dini* ya Mwenyezi Mungu".**[235] Maneno hayo yanafahamika kwa *Qarain muttasila (contexts)* na *qarain munfasilah* (maneno yalio nje ya Aya hio). Ama katika Aya ya pili, utaona kwamba neno *dunia* limeondoshwa. Aya inasema: **"Atayekuwa kipofu katika hii"** katika hii nini? Jawabu ni "hii dunia". Neno *dunia* limeondoshwa lakini linaeleweka katika *Qarinatun muttasila (Context).* Halkadhalika katika Aya nyengine inayofuata. Kwa hivyo, kwa ujumla kuondoshwa kwa neno ambalo linafahamika katika Aya, ni katika utaalamu wa lugha ya Kiarabu ambayo ndio lugha ya Qur-an. Bali wakati mwengine huondoshwa sentensi nzima kama ilivyo katika sehemu zinazoletewa *Al-faau* (fee) ambayo huitwa kinahau kuwa ni *Fau Al-fasiha.*[236]

Lakini, cha kuelewa ni kuwa tunapodai kuondoshwa kwa neno katika Aya au Hadithi basi ni lazima tujue kwamba tumedai kuwepo kwa *majaz*

---

232 - Sura 22, Aya 78.

233 - Sura 17, Aya 72.

234 - Sura 11 Aya 99. Na mfano wake ni Sura 28 Aya 42.

235 - Hata ikiwa tutaifasiri herufi *"Fii"* iliomo katika Aya: **"وَجَاهِدُوا فِي اللَّهِ" (Wajahidu *Fii* Allahi)** kuwa inamaanisha *Lamu ta'aliliya (Lamu yenye kumaanisha sababu),* au kuwa inamaanisha *Li-ajli* (kwa ajili ya…) basi bado tutalazimika kulikadiria neno "Dini" au "Njia" katika Aya hio, kwani uhakika ni kuwa hakuna kufanya jihadi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu kwani Yeye hanufaiki na chochote katika matendo yetu; bali uhakika wa mambo ni kuwa, tunapofanya jihadi huwa tunafanya kwa ajili ya dini ya Mwenyezi Mungu ili neno Lake liwe juu na neno la wale waliokufuru liwe chini. Kwa mazingatio hayo, basi maana ya Aya ni: **"Fanyeni jihadi kwa ajili ya dini ya Allah",** na kwa hivyo, hata kwa mujibu wa tafsiri hii basi bado kuna neno limeondoshwa nalo ni neno "Dini".

236 - Mfano ni kama Aya 8 ya Sura 28.

(metophor) katika Aya au Hadithi hio. Kwani kuondoshwa kwa neno ni katika *majaz* (metophor). Na kudai kwamba kitu fulani ni *majazi* haikubaliki ila kwa kuwepo *qarina* (context) au ushahidi wa nje wenye kuonesha kwamba maana ya asili ya neno hilo sio iliokusudiwa katika Aya hio au Hadithi hio. Kwa hali hii, kudai kwamba kuna neno limeondoshwa haikubaliki ila kwa ushahidi ima katika Aya yenyewe au ushahidi ulio nje ya Aya. *Tunasema:* ushahidi wa ndani ya Aya yenyewe wenye kuonesha kwamba neno *dhawi* au *uli (Wenye au walio)* limeondoshwa, ushahidi huo haumo katika Aya, kwani Aya hailazimishi kuifasiri kwa kulileta moja ya maneno hayo: bali inaweza kufasirika kwa tafsiri nyengine bila ya kulikadiria neno hilo. Kinyume chake – kama utavyoona – ushahidi uliomo ndani ya Aya unaipa uzito tafsiri tafauti na hio isemayo: **"Sema: sikuombeni juu yake (kufikisha huku) ujira isipokuwa huu: nao ni kuwa muwapende watu wa karibu yangu (jamaa zangu)"** kama tutavyoona wakati wa kutazama maana za herufi *"Fii"* iliomo ndani ya Aya hio.

Pili: iwe hakuna neno lililoondoshwa katika Aya na kwa hivyo tafsiri sahihi ya Aya isiwe hio iliojengaka juu ya kuyakadiria maneno *dhawi* au *uli*, bali iwe ni tafsiri nyengine iliojengeka kwa kuzitazama maana nyengine za neno *fii* lililomo katika Aya hio, kama inavyofuata katika maelezo yajayo. *Ninasema:* hii ni sahihi kwani kuzitazama maana tafauti za neno lililotajwa ni bora kuliko kulikadiria neno ambalo halikutajwa.

MAANA ZA HERUFI *FII* ILIOMO KATIKA AYA HIO

Jambo la pili hapa ni kuitazama maana ya herufi *"Fii"* iliomo ndani ya Aya hio, halafu kuifungamanisha maana ya herufi hio na neno *Qurbaa* lililo kabla yake. Herufi *"Fii"* – katika lugha ya Kiarabu – inaleta maana nyingi, lakini kwa hapa zote haziwezekeni isipokuwa tatu au moja katika tatu:

Moja ni: "Katika au ndani". Na hii ndio maana ya asili. Inapotumika kwa maana hii, herufi *fii* huambiwa kuwa imemaanisha *dharfiyya* (chombo). Maana hii ndio mashuhuri kwa watu wengi, na mfano wake ni kama mtu kusema: *"Muhammad fii L-bayt"* yaani Muhammad yumo *katika* au *ndani*

ya nyumba. Na katika Qur-an tuna Aya kama: ***"Fii*** **jannaatin wa 'uyun** **فِـيْ جَنَّـاتٍ وَعُيُوْنٍ"** maana yake ni: **"(Watakuwa)** ***katika*** **(au** ***ndani*** **ya) mabustani na chemchem (za maji safi)".[237]**

Maana ya pili ya herufi *"Fii"* ni kumaanisha *Sababiyya* (Sababu). Katika maana hii, herufi *"Fii"* inakuwa sawa – kimatumizi – na herufi *Bee (Al-baau).* Aghlabu ya wanavyuoni wa lugha huwa wanatoa ushahidi juu ya maana hii kwa Hadithi isemayo:

دَخَلَتِ امْرَأَةٌ النَّارَ فِيْ هِرَّةٍ حَبَسَتْهَا فَلا هِيَ أَطْعَمَتْهَا وَلا هِيَ تَرَكَتْهَا تَأْكُلُ مِنْ خَشَاشِ الأَرْضِ

Dakhalati mraatun Al-nnaara *fii* hirratin habasat-ha: fala hiya at'amat-ha walaa hiya tarakat-ha ta-akulu min khashaashi al-ardhi.

Neno *"Fii"* hapa limetumika kumaanisha *sababu,*[238] na maana ya Hadithi hio ni: "Mwanamke kaingia motoni kwa *sababu* ya paka aliyemfungia: hakumpa chakula wala hakumuachia akala vidudu vya ardhi".

Lakini pia inawezekana kutoa ushahidi wa kutumika neno *"Fii"* na kumaanisha *Sababiyya* (Sababu), kwa Aya isemayo:

إِنَّمَا يُرِيدُ الشَّيْطَانُ أَنْ يُوقِـعَ بَيْنَكُمُ الْعَدَاوَةَ وَالْبَغْضَاءَ فِي الْخَمْرِ وَالْمَيْسِرِ وَيَصـُدَّكُمْ عَنْ ذِكْرِ اللَّهِ وَعَنْ الصَّلاةِ

Hakika shetani anataka kukutilieni uadui na bughdha ***kwa sababu* ya ulevi na kamari na kukuzuieni kumkumbuka Allah na (kukuzuieni na) sala (musisali).[239]**

Herufi iliotumika katika Aya hii kumaanisha *kwa sababu,* ni herufi *fii.*

Maana ya tatu ya herufi *"Fii"* ni kumaanisha *"Illa"* na kwa maana hii itakuwa herufi *"Fii"* imefanya kazi ya herufi *Lamu ta'aliliyya* au imefanya kazi ya neno *liajli ta'aliliyya"*[240]. Mfano wa hii ni kama Aya isemayo:

---

[237] - Sura 44 Aya 52.

[238] - Tazama maelezo ya chini ya Muhyi-Din Abdul-Hamid katika *Sharhu Ibn 'Aqiil* j. 1, uk. 48, kaika mlango wa *Al-Mu'urab wa AlMmabni.*

[239] - Sura 5 Aya 91.

وَإِنِ اسْتَنصَرُوكُمْ فِي الدِّينِ فَعَلَيْكُمُ النَّصْرُ

Waini stansaruukum *fii* Al-Dini, fa'alaikumu nnasru. (Na wakikuombeni msaada *katika* dini, basi ni juu yenu kuwasaidia).[241]

Maana ya **"Wakikuombeni msaada *katika* dini"** ni wakikuombeni msaada kwa ajili ya dini. Na kwa hivyo, herufi *"Fii"* katika Aya hio, imetumika kwa matumizi ya *Lamu* au *"Li-ajili"* (Kwa ajili). Na mfano mwengine ni Hadithi isemayo: **"وَرَجُلانِ تَحَابَّا فِيْ اللهِ"** ***Wa rajulaani Tahaabaa Fii Allahi*** (Na watu wawili waliopendana *katika* Mwenyezi Mungu).[242] Maana ya 'Waliopendana *katika* Mwenyezi Mungu" ni waliopendana *kwa ajili* ya Mwenyezi Mungu. Na kwa hivyo, herufi *"Fii"* katika Hadithi hio, imetumika kwa matumizi ya *Lamu* au kwa matumizi ya *"Li-ajili"* (Kwa ajili).[243]

Sasa tukirudi kuitazama tena Aya yetu na kuyachanganya yaliomo humo na maana moja kati ya maana tatu hizo za herufi hii *"Fii"*, basi tafsiri sahihi ya Aya haiwezi kuwa ila moja katika mbili. Moja: ni kuwa Aya hio: **"Qul Laa As-alukum 'Alaihi ajran illa al-mawaddata fil-qurbaa,"** itafasirika hivi:

Sema sikuombeni juu yake (kufikisha huku) ujira wowote ule; isipokuwa mapenzi *kwa sababu ya* ukaraba (ujamaa uliopo baina yangu na baina yenu).

---

[240] - *"Lamu au liajli ta'aliliyyatain"* ni herufi "Lamu" au neno "Liajli (kwa ajili)" ambayo (maneno mawili hayo) yanaonesha illa (sababu) ya maneno yaliotangulia. Tafauti ya sababu tulioielezea katika namba 2, na "Lamu" na "Liajli (kwa ajili)" tulizozielezea katika namba 3, ni kuwa sababu ndio iliopelekea kitu fulani kikawa; wakati unaposema kwa ajili ni kuwa wewe umekifanya kitu fulani kwa lengo fulani yaani ili lengo hilo liwe. Aliyemuua paka – kwa mfano – hakumuua ili yeye ende motoni lakini kitendo chake hicho kimekuwa sababu ya yeye kwenda motoni; wakati aliyepigana kwa ajili ya dini ya Allah yeye kapigana kwa lengo hilo kwamba dini ya Allah iwe juu.

[241] - Sura 8, Aya 72.

[242] - Hii ni sehemu tu ya Hadithi. Kaipokea Al-Rabi'u bin Habib *Al-Jaami'u Al-Sahih* uk. 39, Hadithi na. 48. Muslim *Sahihu Muslim* uk. 399, Hadithi na. 1031. Al-Bukhari *Al-Sahih* Hadithi na. 6806.

[243] - Na mifano kama hii iko mingi sana.

Tafsiri hii ni kwa kuzingatia maana ya *Sababiyya* (Sababu) ya herufi hio *(Fii)*, ambayo ni ya pili kati ya maana tatu tulizozitaja kabla. Au maana iwe ni:

> **Sema sikuombeni juu yake (kufikisha huku) ujira wowote ule; isipokuwa mapenzi *kwa ajili ya* ukaraba (ujamaa uliopo baina yangu na baina yenu).**

Tafsiri hii ni kwa kuzingatia maana ya *Ta'aliliyya* ya herufi hio, ambayo ni ya tatu kati ya maana tatu tulizozitaja kabla.

Tawjih (muelekeo) ya maneno ya kwanza ni kuwa ujamaa uliopo baina ya Mtume (s.a.w.) umekuwa ndio sababu ya kuwepo mapenzi baina yake na jamaa zake; *Tawjih* (muelekeo) ya maneno ya pili ni kuwa panatakiwa pawe na mapenzi baina yao kwa ajili ya kuwepo ujamaa huo. Hatimae utaona kwamba tafsiri mbili hizo zote ni sawa sawa, kwa hivyo natuzifanye tafsiri hizo kuwa ni moja. Na ya pili: iwe ni tafsiri isemayo:

> **Sema sikuombeni juu yake (kufikisha huku) ujira, isipokuwa mapenzi (yaliomo) *ndani ya* ukaraba (ujamaa).**

Tafsiri hii ni kwa kuzingatia maana ya *dharfiyya* (chombo) ya herufi hio, ambayo ni ya kwanza katika maana tatu tulizozitaja kabla. *Tawjih* (muelekeo) ya tafsiri hii ya pili ni kuwa ujamaa umekuwa ni kama chombo ambacho ndani ya chombo hicho kuna mapenzi baina yake Mtume (s.a.w.) na baina yao Makureish – mapenzi hayo yamo ndani ya ukaraba.[244]

[244] - Muelekeo huu kautaja Al-Imamu Al-Zamakhashari katika *Al-Kashaf* j. 4, uk. 223.

MANENO YA DR. AL-QAZ-WINI

Lakini Dr. ‘Alaa Al-Din bin Al-Sayyid Amir Muhammad Al-Qazwini[245] – katika jawabu yake kwa Dr. Musa Al-Musawi alioiita *Ma’a Al-Dukturi Al-Musawi*[246] kaipinga tafsiri hio isemayo:

> **Sema sikuombeni juu yake (kufikisha huku) ujira wowote ule; isipokuwa mapenzi *kwa sababu* au *kwa ajili ya* ukaraba (ujamaa uliopo baina yangu na baina yenu),**

kwa madai kwamba uhusiano wote ulikatika baina ya Mtume (s.a.w.) na washirikina (makafiri) wa kikureish hata waliokuwa jamaa zake wa karibu kabisa. Anasema Dr. huyo:

> Na kwa hivyo, Allah alimkatalia Nuh utoto wa mwanawe alipomuasi baba yake kwa kauli yake (Allah aliposema): **‘Hakika yeye si katika watu wako, kwani yeye ni (mwenye kutenda) matendo si mazuri”.**[247] …….Na je inaingia akilini kwamba Mtume (s.a.w.) atake ujira kutoka kwa watu ambao wanataka kummaliza na kuimaliza da’awa yake baada (ya kuwa) kawaita wajinga na kuitia kasoro miungu yao (ya masanamu)?... (Allah anasema): **“Huwakuti watu wanamuamini Allah na siku ya mwisho (wakawa) wanawapenda wenye kumpinga Allah na Mtume wake hata wakiwa ni baba zao…”.**[248] Na kuna uhusiano gani baina ya washirikina (makafiri) na Mtume (s.a.w.) katika uhusiano wa ukaraba (ujamaa) ilhali Allah amewahukumu wao (Washirikina) kuwa ni najisi katika kauli yake (Allah aliposema): **“Hakika ya washirikina ni najsi”.**[249].

---

[245] - Vitabu vya waandishi – kikiwemo kitabu cha Dr. Alaa mwenyewe – vinaandika “Al-Qizwini” badala ya “Al-Qazwini”. Na hii bila shaka ni nasaba ya mtu aliyetoka katika mji. Kwa mujibu wa Yaqut Al-hamwiy katika *Mu’ujamu Al-Buldan* j. 7, uk. 46, mji huo unaitwa: “Qazwin”, na kwa maana hio nasaba sahihi ya mtu aliyetoka katika mji huo itakuwa ni “Al-Qazwini”: si “Al-Qizwini”. *Wallahu A’alam.*

[246] - Uk. 68-69.

[247] - Sura 11, Aya 46.

[248] - Sura 58, Aya 22.

[249] - Sura 9, Aya 28.

Hayo ndio maelezo ya Daktari huyu wa elimu, nayo si maelezo madhubuti. Ama kudai kwamba "Uhusiano wote ulikatika baina ya Mtume (s.a.w.) na washirikina (makafiri) wa kikureish hata waliokuwa jamaa zake wa karibu kabisa," utaona kwamba hayo ni madai yenye usahihi na makosa pamoja. Uhusiano uliokatika ni wa kidini na wa kiitikadi, na huu tangu mwanzo haukuwepo kwani Mtume (s.a.w.) hakupata kuabudu sanamu wala kuitakidi batili yao, lakini tafauti ya hali ya kabla ya Utume na ya baada ya Utume, ni kuwa kabla ya Utume hakutangaza rasmi ubatili wa ibada zao, wakati baada ya Utume alitakiwa afanye hivyo, akaambiwa: **"Pasua kile ulichoamrishwa na wapuuze washirikina (makafiri)".**[250]

Ama kosa lililokuwepo katika maneno ya Daktari huyo, ni kuchanganya mkatiko wa uhusiano wa aina hio na uhusiano wa kidamu. Uhusiano unaokusudiwa katika Aya tunayoijadili sisi inayosema:

> **Sema sikuombeni juu yake (kufikisha huku) ujira wowote ule; isipokuwa mapenzi *kwa sababu* au *kwa ajili ya* ukaraba (ujamaa uliopo baina yangu na baina yenu),**

ni uhusiano wa kidamu si wa kidini. Ami yake Mtume (s.a.w.), Abu Talib – kwa mfano – hakuwa Muislamu lakini alimlinda bega kwa bega kwa muda wa miaka hadi kufa kwake. Halkadhalika wako makafiri wengine waliokuwa wakimtetea Mtume (s.a.w.) kwa sababu ya ujamaa tu waliokuwa nao. Bali hata alipohajiri, Mtume (s.a.w.) kaongozwa njia ya kuelekea Madina Tukufu na kafiri. Kwa hivyo, wenye tafsiri isemayo:

> **Sema sikuombeni juu yake (kufikisha huku) ujira wowote ule; isipokuwa mapenzi *kwa sababu* au *kwa ajili ya* ukaraba (ujamaa uliopo baina yangu na baina yenu),**

wanaokusudia wao ni uhusiano huu wa ukaraba (ujamaa) wa damu: si wa dini. Na maana ni kuwa kama hawataki kumfuata katika dini basi wakumbuke udugu wa damu uliopo baina yao, na kwa hivyo, wasimuudhi: wamuache afanye kazi zake za kuwalingania watu.

---

[250] - Sura 15 Aya 94.

Ama maneno ya Daktari Alaa Al-Din aliposema:

> Na kwa hivyo, Allah alimkatalia Nuh utoto wa mwanawe alipomuasi baba yake kwa kauli yake (Allah aliposema): **'Hakika yeye si katika watu wako, kwani yeye ni (mwenye kutenda) matendo si mazuri'.**

Tunasema: mtoto wa Nabii Nuh (a.s.) ni mtoto wake hakuna shaka, na mtoto wake ni katika watu wake hakuna shaka, yaani watu wake kidamu. Na kwa hivyo, ni lazima itazamwe ni nini Allah anakikusudia aliposema kumwambia Nabii Nuh (a.s.): **"Hakika yeye si katika watu wako".** Utakumbuka kwamba maneno haya alioambiwa Nabii Nuh (a.s.) na Mwenyezi Mungu, aliambiwa wakati mtoto huyo amesha au kakaribia kughariki. Kwa hivyo, uhusiano anaoukataa Allah hapa baina ya Nabii Nuh (a.s.) na mwanawe si uhusiano wa kidunia wa kidamu bali ni uhusiano wa kiakhera wa kidini. Na ni kweli kabisa: akhera hakuna mwana wala baba. Hapa ilikuwa ni pahala ambapo waovu wanagharikishwa kwa sababu ya maovu yao. Na kwa hivyo, Aya hio baada ya kusema: **'Hakika yeye si katika watu wako"**, utaona kwamba maneno hayo yanaleta suali katika nafsi: "Vipi mwanangu si katika watu wangu". Ndio maana maneno yanayofuatia katika sehemu ya pili ya Aya hio hio, yakaja kwa kuanzia na herufi: **إِنَّ الْمَكْسُوْرَةُ الْمُشَدَّدَةُ *"INNA*** ambayo *hamza* yake *(Alifu* yake) ina *Kasra* na *Nuni* yake ina *Shada*," ili itoe jawabu na ioneshe sababu ya maneno yaliotangulia kabla **((لِتُفِيْدَ تَعْلِيْلا لِ ْلكَلامِ السَّابِقِ)),** sehemu hio ya Aya ikasema: **"إِنَّـهُ عَمَلٌ غَيْرُ صَالِحٍ " (Kwani yeye (ni mtendaji wa) matendo yasio mema).** Sababu ya yeye kutokuwa katika watu wako ni kuwa yeye ni mtendaji wa maovu.

Pili ni kuwa wanavyuoni wa lugha – kama ilivyo katika *Sharhu Ibni Aqil*[251] – wanasema kwamba katika Aya hio kuna neno limeondoshwa *(Mahdhuf),* na asili ya maneno ni: **'Hakika yeye si katika watu wako <u>*wataookoka*</u>"** yaani wataookoka kutokana na gharka. Neno kuokoka linafahamika katika *Qarain,* kwani kusema kwamba mtoto wa mtu si katika watu wake tu haikubaliki, ni lazima kuwe kuna maelezo ya ziada na maana maalumu iliokusudiwa: si katika watu wake vipi?

---

[251] - Ibn 'Aqiil *Sharhu Ibn 'Aqiil* j. 2, uk. 190, katika mas-ala ya mwisho kabisa ya mlango wa *Na'atu (Sifa).*

Ama maneno ya Daktari Alaa Al-Din aliposema:

> Na je inaingia akilini kwamba Mtume (s.a.w.) atake ujira kutoka kwa watu ambao wanataka kummaliza na kuimaliza da'awa yake baada (ya kuwa) kawaita wajinga na kuitia kasoro miungu yao (ya masanamu)?

Tunasema: kwamba suali hili lingekuwa sahihi lau ilikuwa Mtume (s.a.w.) alipata kuwaomba wao ujira kwa kulingania kwake. Lakini hakupata kufanya hivyo, wala Aya hii haina maana hio kamwe.[252]

Baada ya hapo, Daktari Alaa Al-Din alitoa hoja kwa Aya isemayo:

> **Huwakuti watu wanamuamini Allah na siku ya mwisho (wakawa) wanawapenda wenye kumpinga Allah na Mtume wake hata wakiwa ni baba zao….[253]**

Lakini Aya hii – kama unavyoona – haijibu hoja ya wenye tafsiri isemayo:

> **Sema sikuombeni juu yake (kufikisha huku) ujira wowote ule; isipokuwa mapenzi *kwa sababu* au *kwa ajili ya* ukaraba (ujamaa uliopo baina yangu na baina yenu),**

kwani Aya inayosema: **"Huwakuti watu wanamuamini Allah na siku ya mwisho (wakawa) wanawapenda wenye kumpinga Allah……",** inatukataza sisi kuwapenda makafiri na kuwafanya wao kuwa ndio vipenzi na marafiki zetu katika dini: si kwamba inakata uhusiano katika mambo ya kidunia na ujamaa wa kidamu, wakati wenye tafsiri isemayo:

> **Sema sikuombeni juu yake (kufikisha huku) ujira wowote ule; isipokuwa mapenzi *kwa sababu* au *kwa ajili ya* ukaraba (ujamaa uliopo baina yangu na baina yenu),**

[252] - Hili tutalieza kwa ufafanuzi zaidi katika sehemu inayofuata *In shaa Allah*.
[253] - Sura 58, Aya 22.

mapenzi wanayoyakusudia wao ni mapenzi ya kidunia yanayotokana na ujamaa wa kidamu. Na kwa hivyo, Mtume (s.a.w.) mwenyewe, katika kuifikisha *da'awa* kwa kipindi kirefu cha maisha yake ya Makka, kasaidiwa na ami yake ambaye hakuwa Muislamu.

Bali inawezekana pia ikawa makusudio ya Aya isemayo:

> **Huwakuti watu wanamuamini Allah na siku ya mwisho (wakawa) wanawapenda wenye kumpinga Allah na Mtume wake hata wakiwa ni baba zao…..**

ni kukata uhusiano wa aina zote na makafiri wenye kuipiga vita dini ya Kiislamu, baada ya kuwa wameshafahamishwa haki; na ikawa makusudio ya mapenzi yaliomarishwa katika Aya isemayo:

> **Sema sikuombeni juu yake (kufikisha huku) ujira wowote ule; isipokuwa mapenzi *kwa sababu* au *kwa ajili ya* ukaraba (ujamaa uliopo baina yangu na baina yenu),**

ni mapenzi ya kidunia ya kibinaadamu kwa wale wasioipiga vita dini. Na tafsiri hii inapata nguvu kwa Aya nyengine ambapo Allah (S.W.) anasema:

> **Allah hakukatazeni kutokana na wale ambao hawakukupigeni vita katika dini wala hawakukutoeni mijini mwenu kuwafanyia wema na kuwafanyia uadilifu……[254] …(Bali) Hakika Allah anakukatazeni kutokana na wale ambao wanakupigeni vita katika dini na wakakutoeni mijini mwenu na kusaidiana katika kukutoeni (Allaah anakukatazeni) kuwafanya marafiki (hao)…..[255]**

Kwa hivyo, maana ya yote haya ni kuwa katika Aya isemayo:

> **Sema sikuombeni juu yake (kufikisha huku) ujira wowote ule; isipokuwa mapenzi *kwa sababu* au *kwa ajili ya* ukaraba (ujamaa uliopo baina yangu na baina yenu),**

---

[254] - Sura 60, Aya 8. Maneno ***Kuwafanyia uadilifu*** Kiarabu chake ni: **"وتقسطوا إليهم" *(Watuqsituu ilayhim),*** na maneno haya wengine huyafasiri kuwa maana yake ni: **"Na muwape sehemu ya mali yenu".**

[255] - Sura 60, Aya 9.

basi Mtume (s.a.w.) – tukichukua tafsiri ya kuwa anatakiwa awaamrishe wampende yeye kwa sababu ya ujamaa wao – ni kuwa anawakataza tu kwamba wasimpige vita na kumuudhi ikiwa hawataki kusilimu; na kwamba wampende kwa sababu ya ujamaa uliopo baina yao. Mapenzi ya aina hii hayakukatazwa kwa wale wasioupiga vita Uislamu. Mtume (s.a.w.) – kwa mujibu wa tafsiri hio – anawataka watu wake wayahifadhi mapenzi hayo: si mapenzi ya kidini na kiitikadi.

Tunasema: bali hata ikiwa tumekatazwa kuwapenda makafiri kama alivyotoa hoja Daktari Alaa Al-Din kwa kutumia Aya hio isemayo:

> **Huwakuti watu wanamuamini Allah na siku ya mwisho (wakawa) wanawapenda wenye kumpinga Allah na Mtume wake hata wakiwa ni baba zao…..**

Jawabu ni kuwa Aya hii inawakataza Waislamu kuwapenda makafiri; wakati katika Aya isemayo:

> **Sema sikuombeni juu yake (kufikisha huku) ujira wowote ule; isipokuwa mapenzi *kwa sababu* au *kwa ajili ya* ukaraba (ujamaa uliopo baina yangu na baina yenu),**

Mtume (s.a.w.) anatakiwa awambie makafiri wampende yeye. Na bila shaka katika haya hakuna mgongano hata ikadaiwa kwamba Aya hio tulioitoa hapo ni kinyume na Aya hii.

MANENO YA AL-TABATABAI

Ama Al-Tabatabai, yeye katika kuipinga kwake tafsiri hio isemayo:

> **Sema sikuombeni juu yake (kufikisha huku) ujira wowote ule; isipokuwa mapenzi *kwa sababu* au *kwa ajili ya* ukaraba (ujamaa uliopo baina yangu na baina yenu),**

ana hoja kama au inayofana na baadhi ya yaliosemwa na Daktari Alaa Al-Din. Anasema:

> Na (jawabu yetu) katika (tafsiri) hio ni kuwa hakika maana ya ujira inapatikana ikiwa (umetolewa) kwa ajili ya *(in exchange for)* kazi ambayo mtoaji ujira anayo, basi humpa mfanya kazi ujira unaowiyana na mali alionayo…Basi kuomba ujira kutoka kwa Makureish ilhali walikuwa wakimkadhibisha (na) kuukataa ulinganio wake, basi kungefaa (huko kuomba ujira) tukijaalia kwamba wao walimuamini (Mtume s.a.w.), kwani tukijaalia kuwa walikuwa makafiri basi (hii ina maana kwamba) wao hawakuchukua kitu kutoka kwake hata wamlipe ujira. Na tukijaalia kuwa walimuamini (Mtume s.a.w.),…..basi kumchukia (ni jambo ambalo) huwezi kulifikiria ili mapenzi yawe ndio ujira.[256]

Labda maneno haya ya Al-Tabatabai hayako wazi kwa kila mtu. Anachokisema Al-Tabatabai ni kuwa katika Aya hio, Mtume (s.a.w.) anaomba ujira. Sasa ujira mtu huudai kwa kazi alioifanya baada ya makubaliano baina ya mwenye kazi na kibarua wake. Kazi alioifanya Mtume (s.a.w.) kwa hapa ni kulingania. Wenye kulinganiwa hawakuukubali wito wake. Sasa vipi yeye Mtume (s.a.w.) atawadai ujira ilhali kazi yake hawakuikubali? Kwa hivyo, natija ni kuwa Aya haina maana hio kwamba Mtume (s.a.w.) anawataka Makureish hapa waache kumuudhi, kwani hapa yeye anadai ujira kutokana na kazi yake ya kufikisha na waliofikishiwa hawakuikubali da'awa yake, sasa ujira huo ni wa nini? Maelezo haya – kama anavyosema mwenyewe Al-Tabatabai – ni sahihi tukijaalia kwamba hao wanaolinganiwa hapa hawakusilimu (yaani tukijaalia kuwa wahubiriwa hapa ni wale makafiri ambao hawakusilimu). Je tukijaalia kuwa walisilimu, jawabu ni nini? Jawabu ni kuwa baada ya kuwa wao ni Waislamu haingii akilini kuwa wamchukie Mtume (s.a.w.) hata ikabidi watakiwe kumpenda. Hii ndio maana ya maneno ya Al-Tabatabai.

---

[256] - Al-Tabatabai *Al-Mizan* j. 18, uk. 43-44.

Nawe – ndugu msomaji – unaona kwamba Sheikh Al-Tabatabai anajilazimisha kukipinga kitu hata kama kwa hoja dhaifu kama nyumba ya buibui *"Wa inna awhana Al-buyuti labaitu Al-ankabut"* (Na hakika nyumba dhaifu yao ni nyumba ya buibui). Maelezo yote ya Al-Tabatabai msingi wake ni kuwa Mtume (s.a.w.) katika Aya hio inayosema:

> **Sema sikuombeni juu yake (kufikisha huku) ujira wowote ule; isipokuwa mapenzi *kwa sababu* au *kwa ajili ya* ukaraba (ujamaa uliopo baina yangu na baina yenu),**

anatakiwa aombe ujira kwa ajili ya kazi yake ya ulinganiaji. Na Aya haina maana hio kamwe: Mtume (s.a.w.) hajapata (Bali Mitume hawajapata) kumuomba mtu ujira kwa kazi yao ya kufikisha: kufikisha ni wajibu juu yao, na tunashuhudia kwamba wamefikisha bila ya ujira. Bali Aya hio inakataa kwamba Mtume (s.a.w.) anaomba ujira juu ya ulinganiaji wake. Kwa ufupi ni kuwa, maudhui hii tutazungumzia katika sehemu inayofuata – *In shaa Allah* – hapa nilitaka ujue tu Al-Tabatabai ana nini cha kutwambia juu ya kuipinga kwake tafsiri hio isemayo:

> **Sema sikuombeni juu yake (kufikisha huku) ujira wowote ule; isipokuwa mapenzi *kwa sababu* au *kwa ajili ya* ukaraba (ujamaa uliopo baina yangu na baina yenu).**

<u>Jambo la tatu</u> la kutazamwa katika Aya hio, ni hii *Istithnaau*[257] (exception) ilioletwa na herufi **<u>إِلَّا</u> <u>(*illa):*</u>** je ni *muttasil* au *munqatiu?* Na hii ni kwamba *Istithnaau* zinagawika sehemu tafauti kwa mujibu wa nini kimezingatiwa. Katika baadhi ya mazingatio yake, *Istithnaau* hugawika sehemu mbili ziitwazo *istithnaau muttasil* (yaani yenye kushikana na maneno yaliotangulia) na *istithnaau munqatiu* (yaani iliokatika kutokana na maneno yaliotangulia).[258]

Katika Aya yetu isemayo: **"Qul Laa As-alukum 'Alaihi ajran *illa* al-mawaddata fil-qurbaa,"** tuna neno ***illa*** ambayo ni herufi yenye kumaanisha *istithnaau (exception):* je *Al-Istithnaau* hii ni *muttasil* (yenye kushikana na maneno yaliotangulia) au ni *munqatiu* (iliokatika kutokana na maneno yaliotangulia)? Ukisema ni *muttasil,*[259] basi maana ya Aya hio itakuwa hivi:

---

[257] - Lakini labda kwa wale wasiosoma Kiarabu kwanza wanahitaji kujua maana ya *Istithnaau* (exception) kabla ya kujua aina zake tafauti. Ama wasomaji wa Kiingereza wameshajua kwa sababu ya neno "Exception" nililolitia katika breketi. Kwa ufupi ni kuwa *Istithnaau* (exception) ni kukivua au kukitoa kitu au mtu (au vitu au watu) fulani kutoka katika ujumla wa vitu au watu wengine. Mfano utakuwekea wazi makusudio. Kwa mfano nikisema: "Watu wote wameondoka *isipokuwa* Salim". Utaona kwamba *Salim* tumemvua au tumemtoa kutoka katika jumla ya *watu* walioondoka kwa kutumia neno *isipokuwa* ambalo ni sawa na neno *illa* la Kiarabu au neno *except* la Kiingereza. Neno hili *isipokuwa* ndilo ambalo kwa Kiarabu huitwa *Istithnaau* au kwa Kiingereza huitwa (exception). Kwa hivyo, katika Aya: **"Qul Laa As-alukum 'Alaihi ajran <u>*illa*</u> al-mawaddata fil-qurbaa,"** *Istithnaau* ni neno ***illa*** yaani "Isipokuwa au ukipenda lifasiri hivyo hivyo: "ila".

[258] - Kwa ufafanuzi zaidi ni kuwa *Istithnaau muttasil* ni ile ambayo chenye kuvuliwa na kilichobakia au chenye kutolewa na kilichobakia ni jinsi moja. Mfano wake ni kama kusema: "Watu wote wamesimama isipokuwa Ali". Ali kavuliwa kutoka katika jumla ya watu waliosimama: watu waliosima ndio wenye kubakia na Ali ndiye aliyevuliwa au aliyetolewa, lakini Ali ni jinsi ya watu vile vile yaani naye ni mtu, kwa hivyo *Istithnaau* hapa ni *muttasil* yaani yenye kushikana na maneno yaliotangulia. Na *Istithnaau munqatiu* yaani iliokatika kutokana na maneno yaliotangulia, ni ile ambayo chenye kuvuliwa na kilichobakia au chenye kutolewa na kilichobakia ni jinsi tafauti. Kwa mfano nikisema: "Watu wote wamesimama isipokuwa punda". Punda kavuliwa kutoka katika jumla ya waliosimama, lakini punda na waliosimama – ambao ni watu – ni jinsi mbili tafauti, kwa hivyo *istithnaau* hapa ni *munqatiu* (yenye kukatika).

[259] - Nayo si sahihi: sahihi ni kuwa *Al-Istithnaau* hapa ni *munqatiu*.

> **Sema sikuombeni juu yake (kufikisha huku) ujira wowote ule; isipokuwa *<u>ujira ninaokuombeni</u>* ni mapenzi *katika*ukaraba au *kwa sababu* au *kwa ajili ya* ukaraba[260] (ujamaa uliopo baina yangu na baina yenu).**

Kisha ikiwa utalifasiri neno *Qurbaa (Ukaraba)* kuwa maana yake ni Ahlu Al-Bait (watu wa nyumba ya Mtume s.a.w.), basi utapata kwamba Mtume (s.a.w.) haombi ujira wowote (yaani kutoka kwetu kwa mujibu wa Shia), isipokuwa ***<u>ujira anaouomba kutoka kwetu ni kuwapenda Ahlu Al-Bait.</u>*** Na kwa kuwapenda Ahlu Al-Bait, basi tutakuwa tayari tumeshamlipa Mtume (s.a.w.) kwa kazi yake kubwa alioifanya ya kufikisha ujumbe! Na hivi ndivyo alivyosema Al-Tabatabai katika *Al-Mizan*[261] Anasema – baada ya maelezo:

> ……Hakuna shaka kwamba kuwajibisha kuwapenda wao (Ahlu Al-Bait),[262] na kukufanya kuwapenda huko kuwa ndio malipo ya utume; kwani hakika ilikuwa ni njia ya kuwarejesha watu kwao (Ahlu Al-Bait) kwa sababu ya (ule uwezo) waliokuwa nao (au sifa walizokuwa nazo za kuwa) ni marejeo (references) ya elimu.

---

[260] - Katika ukaraba yaani katika (wenye) ukaraba (yaani wenye ujamaa) nao ni jamaa wa Mtume (s.a.w.), kwa tafsiri moja au *kwa sababu* au *kwa ajili ya* ukaraba kwa mujibu wa tafsiri nyengine.

[261] - J. 18, uk. 47.

[262] - Lakini je kuwapenda munako kusisitiza ni kuwapenda Ahlu-Bait au ni kuwapenda Shia? Kwani sisi tunaona Shia hawawapendi Ahlu-Al-Bait wote bali wanaowapenda na kuwaheshimu ni Shia. Hawa Masharifu waliotoka Al-Yaman ni Al-Alawi (wanatokana na Sayyidna Ali), je wana hadhi kwa Shia Ithnashariyya? Bali hata Ahlu Al-Bait wa Shia Zaidiyya pia hawana hadhi kwa Shia Ithnashariyya. Kwa hivyo, AHLU AL-BAIT ni kisingizio tu, lakini makusudio ni Shia, au Ahlu Al-Bait katika Shia Ithnashariyya. Halafu nyinyi munategemea *Hadithi Thaqalain,* nayo imetaja kizazi cha Ali, kizazi cha Abbas, kizazi cha ‘Aqiil na kizazi cha Ja’afar. Kama Hadithi ilivyosema:

> Lakini watu wa nyumba yake ni wale walioharamishiwa sadaka baada yake. Akasema ni nani hao? Akasema (hao) ni kizazi cha Ali, kizazi cha Aqiil, kizazi cha Ja’afar na kizazi cha Abbas. Akasema (Husain): `Wote hawa wameharamishiwa sadaka?’ Akasema (Zaid bin Arqam): `Ndio’ (wote hawa wameharamishiwa sadaka).

Je hao wote wamo katika wajibu wa kuwapenda kwa mujibu wa Shia?

Hivyo ndivyo alivyyonena Sheikh Al-Tabatabai, lakini kwa kuzingatia kanuni kwamba: *"Khayru maa fussira bihi Al-qur-anu Al-qur-anu Nafsuh"* (kitu bora cha kuifasiria Qur-ani ni Qur-ani yenyewe) yaani Qur-ani inajifasiri yenyewe kwa yenyewe, basi hatimae utaona kwamba tafsiri hio ya kwamba Mtume (s.a.w.) hataki ujira katika kufikisha ujumbe isipokuwa ujira anaoutaka ni kuwa tuwapende Ahlu Al-Bait, ni kinyume na Aya nyengine kadha wa kadha ambazo Mtume (s.a.w.) anaelezewa na Mola wake kwamba:

وَمَا تَسْأَلُهُمْ عَلَيْهِ مِنْ أَجْرٍ

Na huwaombi juu ya (ufikishaji huu) ujira (wowote).[263]

Na akasema Allah:

قُلْ مَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ مِنْ أَجْرٍ

(Sema sikuombeni juu yake (kufikisha huku) ujira wowote ule juu yake (kufikisha huku).[264]

Na akasema Allah:

قُلْ مَا سَأَلْتُكُمْ مِنْ أَجْرٍ فَهُوَ لَكُمْ إِنْ أَجْرِيَ إِلاَّ عَلَى اللَّهِ

Sema chochote kile nilichokuombeni (kama nilipata kufanya hivyo) katika ujira, basi ni wenu (ujira huo chukueni nyinyi: mimi siutaki): haukuwa ujira wangu ila kwa Allah tu.[265]

Maneno yasemayo: **"Sema chochote kile nilichokuombeni (kama nilipata kufanya hivyo) katika ujira",** hayana maana kwamba Mtume (s.a.w.) aliwahi kuomba ujira, na dio maana Aya imemalizikia kwa maneno: **"Haukuwa ujira wangu ila kwa Allah tu".**

263 - Sura 12, Aya 104.
264 - Sura 38, Aya 86.
265 - Sura 34, Aya 47.

Ukiniambia: “Aaa! Unajua ujira ambao yeye haombi ni ujira wa pesa: si ujira wa kuwapenda watu wake”. Ukiniambia hivyo nitakujibu kwa jawabu mbili:

1) Ni kuwa **كلمة "أجر" في الآية نكرة في سياق النفي فهي تفيد العموم** neno *ajr* (malipo) lililotumika katika Aya hizo ni *nakira fii siyaaqi al-nafyi, (*yaani ni *nakira*[266] iliopo katika sentensi yenye kukataa) na hii ina maana kwamba neno hilo hapo limemaanisha ujumla jamala. Na kwa hivyo, kila unaoitwa kuwa ni ujira basi Mtume (s.a.w.) hautaki katika kufikisha kwake *da’awa* yake ya kufikisha Uislamu. Tena **جيء بحرف "من" لأجل ترسيخ هذا المعنى** imeletwa herufi *min* katika Aya hizo ili kuipa nguvu maana hio ya kukataliwa ujira kwa ujumla.
2) Pili: ni jawabu-suali! Nayo ni kujiuliza je huku kuwapenda Ahlu Al-Bait ni wajibu wetu wa Kisharia au si wajibu wetu? Jawabu yako itakuwa: “ni wajibu wetu”. Sasa vipi kitu ambacho ni wajibu na ni fardhi juu yetu kigeuke kuwa ndio malipo yetu kwa Mtume (s.a.w.) kwa ajili ya kazi yake. Unaonaje sala zetu, funga zetu, hija zetu n.k., je zinafaa kuwa ni malipo yetu kwa Mtume (s.a.w.) kwa sababu ya kazi yake?

Kwa hivyo, kwa mujibu wa Aya hizi, utaona kwamba Mtume (s.a.w.) katakiwa atangaze kwa uwazi kwamba yeye kwa kufikisha risala ya Allah, hataki malipo yoyote hapa duniani, bali malipo yake yako kwa Allah tu. Kwa maana hii, inatubainikia kwa uwazi kwamba kudai kuwa Aya hio isemayo: **“ قُلْ لا أَسْـأَلُكُمْ عَلَيْـهِ أَجْراً إِلاَّ الْمَـوَدَّةَ فِـي الْقُرْبَـى“** maana yake ni kuwa Mtume (s.a.w.) hataki ujira wowote isipokuwa ujira autakao ni kuwa tuwapende Ahlu Al-Bait na kwamba huo ndio ujira anaoutaka na ndio malipo yetu kwake, ni tafsiri ilio mbali na *tahqiq* za kielimu.[267] Kwa hivyo,

---

[266] - *Nakira* ni neno ambalo halikutiwa *alifu* na *lamu* kama ukisema *baytun,* au *baytin* au *baytan.* Na kinyume chake ni *ma’arifa* nalo ni neno lenye *alifu* na *lamu al-baytu* au *al-bayti* au *al-bayta.*

[267] - Ukweli ni kuwa hata tukiwapenda Ahlu Al-Bait na tukamsalia Mtume (s.a.w.) kwa siku mara laki moja, hatuwezi kumlipa Mtume (s.a.w.) hata ngamia akipenya kwenye tundu ya sindano. Ikiwa baba na mama hatuna cha kuwalipa kwa kuwa wao ni sababu tu ya sisi kuwepo hapa duniani, basi vipi tutamlipa mtu aliyekuwa sababu ya kuokolewa na moto wa jahannam na kuingizwa katika pepo?! *Allah atujaalie, Amin.*

ni wazi kwamba *Al-Istithnaau (Exception)* katika Aya hio, si *muttasil* (yenye kushikana na maneno yaliotangulia).

Kauli ya pili ni kuwa *Al-Istithnaau* hapa ni *munqatiu*[268] (iliokatika kutokana na maneno yaliotangulia). Na kwa maana hio, neno "malipo" au "ujira" lililomo katika sehemu ya kwanza – ya Aya hio – yenye kusema: **قُلْ لا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْراً (Sema sikuombeni juu yake (kufikisha huku) *malipo* yoyote…),** linakuwa neno hilo limemalizikia katika sehemu hio hio ya kwanza tu kama lilivyotamkwa: haliko wala halikadiriwi tena katika sehemu ya pili ya Aya hio. Na kwa hivyo, tukisema kwamba *Al-Istithnaau* hapa ni *munqatiu,* basi tafsiri ya Aya hio itakuwa hivi: **"Sema sikuombeni juu yake (kufikisha huku) ujira wowote ule isipokuwa mapenzi *kwa ajili (au kwa sababu)* ya uqaraba".** Kwa hivyo, natija ni kuwa – kwa mujibu wa msingi huu wa *Al-Istithnaau Al-Munqatiu* – Mtume (s.a.w.) haombi ujira wowote juu ya da'awa yake – kama Aya nyengine zilivyosema hivyo kwa uwazi – bali anawataka:

1) Makureishi – ikiwa hawataki kusilimu na kumpenda kwa misingi ya Uislamu basi – wampende kwa misingi ya ujamaa wao wa damu, na kwa hivyo wamuachie aendelee na *da'awa* yake wasimuudhi na kumuekea vizingiti katika ulinganiaji wake.
2) Au – kwa tafsiri ya pili – anachokitaka yeye si ujira kutoka kwao, bali anachokitaka ni kuwa wao wapende kujikurubisha kwa Allah kwa kusilimu na kufanya mambo mema. Lakini tafsiri hii ya pili ina udhaifu kama tutavyobainisha baadae.

Ama kudai kwamba Mtume (s.a.w.) anataka ujira kwa kazi yake ya ufikishaji wa risala; nao ujira wenyewe ni kuwa tuwapende Ahlu Al-Bait huo ndio ujira wake, hii si tafsiri sahihi. Naona watu wengine wanapenda kitu mpaka wanaamua kutoka kabisa katika *minhaj* (*methodology* au njia) sahihi ya tafsiri, basi kila Aya yenye sifa nzuri ni ya Ahlu Al-Bait tu! Hii ni tafsiri au ni kuichezea Qur-ani?! Ali ana sifa zake sahihi nyingi: hakuna haja ya kutungiwa Hadithi za uwongo, wala hakuna haja ya kupotoshewa tafsiri za Aya za Qur-ani bure. Ali anajulikana kuwa alikuwa shujaa, na ni

[268] - Nayo ndio sahihi, nayo ni kauli ya Al-Imamu Ibn Jarir Al-Tabari *Jami'u Al-Bayan* j. 25, uk. 33.

katika *fuqahaau Al-sahaba* (Masahaba wanavyuoni wakubwa sana), mwingi wa elimu na hekima na ucha Mungu wa hali ya juu na ni mkweli, n.k. Na hii haina maana kuwa yeye hakosei kama Shia wanavyotaka kumzidishia kitu ambacho Allah hakutupa sisi wanaadamu sote: "Binaadamu wote ni wenye kukosea na wabora wa wenye kukosea ni wenye kutubia". Yeye ni mtoto wa Adam kama mimi na wewe; kawa bora zaidi kwa sababu ya: usahaba wake, ucha Mungu wake, elimu yake, jihadi zake n.k.[269] Lakini leo watu wanataka kuwapachika Ahlu Al-Bait sifa ambazo Allah hakumpa kiumbe yoyote ilimradi wao wawe bora kuliko Masahaba wengine tu,[270] hadi watu kufika kutunga malaki ya Hadithi za uwongo na kupotosha mamia ya Aya za Qur-ani mpaka wakafikia kusimulia riwaya kadha wa kadha zenye kuifasiri Aya isemayo: **"مَـرَجَ الْبَحْـرَيْنِ يَلْتَقِيَـانِ" (Kazichanganya bahari mbili (zikawa) zinakutana).**[271] Wakasema kuwa maana ya bahari mbili hapa ni Ali na Fatima. Na Aya isemayo: **"بَيْنَهُمَا بَرْزَخٌ لا يَبْغِيَانِ"" (Baina yake kuna kizuizi haziingiliani).**[272] Wakasema kizuizi ni Mtume (s.a.w.).[273] Na Aya isemayo: **"يَخْرُجُ مِنْهُمَا اللُّؤْلُؤُ وَالْمَرْجَانُ" (Zinatoka humo (katika bahari mbili hizo) lulu na marijani).**[274] Wakasema kwamba lulu na marijani ni Hasan na Husain! Basi huku si kuichezea Qur-ani?! Anasema Al-Tabrasi katika tafsiri yake *Majmu'u Al-Bayan*,[275] akizisherehesha riwaya hizo za kutunga: "Wala hakuna shaka ya kuwa wao ni bahari mbili kwa kuenea kwa fadhila

---

269 - Wala usidhani kwamba yeye kawa bora kwa sababu ni Ahlu Al-Bait: Ahlu Al-Bait wako wengi – wenye kutokana na Ali – na wamekuwa udhia mkubwa kwa Waislamu na Uislamu. Kuna Masharifu wangapi wanamuasi Allah maasi makubwa na wengine – kule kwetu Zanzibar – hata walifika kukanusha kuwepo kwa Allah! Je na hawa nao pia ni bora katika mtazamo wa Uislamu kwa sababu ni *La'alawiyyin* (Wanatokana na Ali)?! Kuanzia hapa utaanza kuona kwamba ukweli ni ule ule alioutangaza Allah kwamba: **"Hakika ya mbora wenu zaidi ni mcha Mungu wenu zaidi".**

270 - Na ubora zaidi si kwa kuwa mtu ni Ahlu Al-Bait, bali ni kwa kuwa mcha Mungu zaidi kama Aya ilivyotangaza.

271 - Sura 55, Aya 19.

272 - Sura 55, Aya 20.

273 - Sasa Mtume (s.a.w.) kawazuia Ali na Fatima wasikutane, au yeye ndio kawakutanisha?! Huyu mtunzi anaonesha alikuwa bado anajifundisha kutunga: hajahitimu bado.

274 - Sura 55, Aya 22.

275 - J. 9, uk. 257.

zao na wingi wa kheri zao". Tazama pia riwaya hizo, katika tafsiri *Al-Mizan* ya Sheikh Al-Tabatabai.[276]

SIYAQ NA SIBAQ YA AYA HIO

Jambo la nne la kutazamwa katika Aya hio isemayo: **قُلْ لا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْراً (Sema sikuombeni juu ya hayo *malipo..*),** ni *Siyaq* (maneno yalio baada) na *Sibaq* (maneno yalio kabla) ya Aya hio. Aya hio imetanguliwa na Aya kadha wa kadha zenye kuhusu kiama, kutenda mema na mabaya, na malipo ya wema na wabaya. Aya iliokabla yake kabisa inasema:

وَالَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ فِي رَوْضَاتِ الْجَنَّاتِ لَهُمْ مَا يَشَاءُونَ عِنْدَ رَبِّهِمْ ذَلِكَ هُوَ الْفَضْلُ الكَبِيرُ

> **…..Na wale walioamini na kutenda mema (watakuwemo) katika mabustani ya pepo; watapata humo wanayoyataka kwa Mola wao; hio ndio fadhila kubwa (kabisa).[277]**

Halafu ndio ikaja Aya hio tunayoijadili, ambayo pia imetanguliwa na maneno yenye kuhimiza matendo mema, ikasema:

ذَلِكَ الَّذِي يُبَشِّرُ اللَّهُ عِبَادَهُ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ قُلْ لا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْراً إِلاَّ الْمَوَدَّةَ فِي الْقُرْبَى وَمَنْ يَقْتَرِفْ حَسَنَةً نَزِدْ لَهُ فِيهَا حُسْناً إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ شَكُورٌ

> **Hivyo ndivyo Allah anavyowabashiria waja wake walioamini na wakatenda mema; sema sikuombeni juu yake (kufikisha huku) ujira wowote ule isipokuwa mapenzi kwa sababu (au**

---

[276] - J. 19, uk. 107. Na ajabu ya mtu huyu, kuna sehemu tafauti ambazo yeye akifasiri hufasiri vyengine kisha akija katika utafiti wa riwaya huleta riwaya zinasema vyengine! Aya hizo yeye mwenyewe kazifasiri vizuri, kisha akaja kunukuu riwaya hizo bila hata kutaja kwamba ni riwaya za kutunga au ni riwaya dhaifu! Halkadhalika huyo aliyetangulia (Al-Tabrasi) naye kafasiri vyengine halafu akanukuu riwaya hizi na dhahir ni kuwa anaziunga mkono ndio maana akasema – baada ya kuzinukuu – kwamba: "Wala hakuna shaka ya kuwa wao ni bahari mbili kwa kuenea kwa fadhila zao na wingi wa kheri zao".

[277] - Sura 42, Aya 22.

> **<u>kwa ajili) ya ukaraba (ujamaa);</u> na atayechuma jema tutamzidishia ndani yake wema; hakika ya Allah ni Mwingi wa msamaha, Mwingi wa shukurani.**

Kwa hivyo, ukiyatazama maneno ya Aya ilio kabla na maneno ya mwanzo na ya mwisho mwa Aya yenyewe, utaona kwamba tafsiri zenye nguvu hapa ni tafsiri tatu (kwa mbili)[278] ambazo ndizo zenye muelekeo hapa. Moja ni ile tafsiri alioitumia Sheikh Abdullah Salih Al-Farisi, kwamba maana ya maneno yasemayo ***<u>Al-Mawadda fii Al-Qurba</u>*** ni **"Myapende mambo ya kukusogezeni (kwa Mwenyezi Mungu)".** Ndio maana Aya imezungukwa na Aya zenye kututaka tufanye mema ili tuingie peponi; kana kwamba Aya hio inasema:

> **haya tulioyataja hapa ya kutenda mema na kuacha maovu ili mupate pepo, sikulinganieni kuja katika hayo ili munipe ujira, bali ila kwa anayependa kujikurubisha kwa Allah kwa kuyatekeleza hayo.**

Ninasema: inaweza ikadaiwa kwamba tafsiri hio hapo – katika Aya nyengine – ni andiko la wazi, kama vile Aya yenye kusema:

قُلْ مَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ مِنْ أَجْرٍ إِلاَّ مَنْ شَاءَ أَنْ يَتَّخِذَ إِلَى رَبِّهِ سَبِيلاً

Sema sikuombeni juu yake ujira wowote isipokuwa anayependa kushika njia (ya kumfikisha) kwa Mola wake.[279]

Na tafsiri hio – mbali na kuwepo kwa *siyaq* na *sibaq* hizo pia – inapata nguvu kwa kuwepo herufi *Laa* na herufi *Illa* katika Aya hio, kama tutavyobainisha baadae *In shaa Allah.*

Lakini hatimae utaona kwamba mambo yote mawili hayo ambayo yanatarajiwa kuwa ni yenye kuipa nguvu tafsiri hio, ni mambo yenye kujibika. Ama kuhusu kuwepo kwa Aya zenye kututaka tufanye mema ili tuingie peponi katika Aya zilio kabla ya Aya hio isemayo:

---

[278] - Tatu kwa mbili kwani mbili katika hizo zimekurubiana sana: zina tafauti ndogo tu.

[279] - Sura 25, Aya 57. Yaani njia itayomfikisha katika rehema ya Mola wake.

قُلْ لا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْراً إِلاَّ الْمَوَدَّةَ فِي الْقُرْبَى

kunaweza kukajibiwa kwamba kutajwa kwa Aya hizo si **قَرِيْنَةٌ قَاطِعَةٌ** ushahidi wa mkato juu ya usahihi wa kuifasiri Aya hio kuwa maana yake ni: **"…….Myapende mambo ya kukusogezeni (kwa Mwenyezi Mungu)"**, kwani kutajwa kwa matendo mema na malipo ya pepo hakugongani pia na tafsiri isemayo: **"Sema sikuombeni juu yake (kufikisha huku) ujira wowote ule isipokuwa mapenzi kwa ajili ya ukaraba"** kwani – katika tafsiri hii ya pili – maana ni kuwa Mtume (s.a.w.) anawalingania watu wake kuja katika Uislamu ili waingie peponi bure: hataki malipo yoyote; na kama hawataki kumuitika basi wamuachie awalinganie watu wengine wasimkere na kumuekea vizingiti. Utaona kwamba kutajwa kwa Aya zenye kututaka tufanye mema ili tuingie peponi katika Aya zilio kabla, kama kunavyoafikiana na tafsiri isemayo: **"…….Myapende mambo ya kukusogezeni (kwa Mwenyezi Mungu)"**, ndivyo kunavyoafikiana na tafsiri isemayo: **"…Sema sikuombeni juu yake (kufikisha huku) ujira wowote ule isipokuwa mapenzi *kwa ajili* ya ukaraba".** Kwa hivyo, Aya hizo zilizotajwa kabla bado hazijawa ushahidi wa tafsiri hii wala tafsiri hile.

Ama Aya:

قُلْ مَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ مِنْ أَجْرٍ إِلاَّ مَنْ شَاءَ أَنْ يَتَّخِذَ إِلَى رَبِّهِ سَبِيلاً

Sema sikuombeni juu yake ujira wowote isipokuwa anayependa kushika njia (ya kumfikisha) kwa Mola wake,

utaona kwamba si andiko la wazi lenye kuafikiana na Aya yenye kusema: **"Qul *Laa* As-alukum 'Alaihi ajran *illa* al-mawaddata fil-qurbaa",** japo kuwa kuna kitu kilicho sawa baina ya Aya mbili hizo nacho ni kule kukataliwa kwa Mtume (s.a.w.) kuchukua ujira, lakini katika sehemu za mwisho za Aya mbili hizo kumekuwa na maneno tafauti, na hii inaifanya Aya ya pili isiwe andiko la wazi lenye kulazimisha kuwa Aya ya pili ifungamanishwe na ya kwanza na kuifanya Aya ya pili kuwa imeifasiri Aya ya kwanza – huku kumekataliwa ujira na kule kumekataliwa ujira; lakini huku kumethibitishwa mapenzi kwa ajili ya

ukaraba nalo ni jambo mahususi; wakati kule kumethibitishwa kushikana na njia ya kutufikisha katika rehema ya Allah nalo ni jambo la ujumla na lenye maana ilio pana zaidi.[280]

KUWEPO KWA HERUFI *LAA* NA HERUFI *ILLA*

Jambo la tano la kutazamwa katika Aya hio, ni kuwepo ndani yake kwa herufi *Laa* na herufi *Illa*. Tumekuwa tukizungumzia kuhusu *Qasru* katika makala na vitabu tafauti, kiasi cha kwamba itakuwa wengi wa waliozipitia makala hizo na vitabu hivyo, na ambao walikuwa mwanzo hawajui nini maana ya *Qasru*, sasa – watakuwa wameshaifahamu darsa hio vizuri. Hakuna ubaya kukumbushana kidogo hususan ukizingatia ukweli kwamba si kila mtu kasoma vitabu vyangu vyote. *Qasru* au *Hasru* ni kukifungamanisha kitu fulani au vitu fulani na kitu kimoja tu au na baadhi ya vitu tu; ikawa hakitoki au havitoki kwenda kwenye kitu au vitu vyengine. Kwa mfano, nikisema "asiingie humu ndani isipokuwa Muhammad", au nikisema: "sina niliyemuona ila Ali". Hii ina maana kwamba sina ninayemtaka mwengine yoyote aingie ndani ila Muhammad na sina mwengine niliyemuona isipokuwa Ali. Hio ni mifano tu, labda kupatikana maana ilio sawa 100% katika lugha ya Kiswahili ni tabu kidogo, lakini natarajia kwamba mifano hio imeweza kutoa muangaza juu ya *Qasru* au *Hasru* ni kitu gani.

Sasa *Qasru* ina njia nyingi katika muundiko wa lugha ya Kiarabu. Mashuhuri zaidi ni nne. Moja katika nne hizo ni ***Al-Nafyu wa Al-Istithnaa*** yaani ni pale inapoletwa herufi ya kukataa katika maneno kisha ikafatiwa na herufi ya *Istithnaau* (Exception) yaani herufi ya kukivua kitu kimoja au baadhi ya vitu. Katika Aya yetu isemayo:

قُلْ لا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْراً إِلاَّ الْمَوَدَّةَ فِي الْقُرْبَى

[280] - Yaani Aya inayosema: **"Sema sikuombeni juu yake ujira wowote isipokuwa anayependa kushika njia (ya kumfikisha) kwa Mola wake"** ni andiko la wazi katika maudhui inayozungumzwa na Aya hio; lakini si andiko la wazi lenye kuonesha kuwepo kwa mfungamano wa lazima baina ya Aya hio na Aya isemayo: **"…Sina ninachokuombeni juu yake (kufikisha huku) katika ujira isipokuwa mapenzi kwa ajili ya ukaraba".**

Qul *Laa* As-alukum Alaihi ajran *illa* al-mawaddata fil-qurbaa,

tuna herufi *Laa* ambayo ndio herufi ya kukataa na tuna herufi *illa* ambayo ndio herufi ya *Istithnaau* (Exception) yaani herufi yenye kuonesha kuvuliwa kwa kitu kimoja au baadhi ya vitu kutoka katika jumla ya vitu vilivyotajwa. Na kwa hivyo, tafsiri ya msingi ya Aya hio – kwa kuuzingatia mkatao uliokuwepo ndani yake na *Istithnaau* (Exception) iliokuwemo ndani yake – ni:

> **Sema sina ninachokuombeni[281] juu yake (kufikisha huku) katika ujira; isipokuwa mapenzi kwa sababu (au kwa ajili) ya ukaraba (ujamaa).**

Na kwa hivyo, basi utaona kwamba dhahiri ya Aya hii – kwa kuzingatia msingi huo wa kuwepo kwa herufi *Laa* na herufi *illa* – inaipa nguvu tafsiri hio tulioinukuu kutoka kwa Sheikh Al-Farisi inayosema:

> **Sema kwa haya (ninayokufundisheni) siombi, (sitaki) malipo yoyote kwenu; lakini (nataka) myapende mambo ya kukusogezeni (kwa Mwenyezi Mungu).**

Tunadai hivyo kwa sababu ni kweli kwamba Mtume (s.a.w.) hakuna alichokuwa akikitaka – kwa ulinganiaji wake – isipokuwa watu wafanye mema na waache mabaya ili wapate kurehemewa: basi hakuna zaidi. Na kwa tafsiri hii utaona kwamba maana ya *Qasru* katika Aya imepatikana.

Lakini – baada ya kufikiri sana – utaona kwamba na hoja hii pia inaweza ikajibiwa kwamba maana ya *Qasru* katika Aya hio inapatikana hata kwa mujibu wa tafsiri isemayo:

> **Sema sikuombeni juu yake (kufikisha huku) ujira wowote ule; isipokuwa mapenzi *kwa sababu* au *kwa ajili ya* ukaraba (ujamaa uliopo baina yangu na baina yenu),**

[281] - Kutoka kwa makafiri wa kikureish – kwa tafsiri moja – au kutoka kwa Waislamu kwa mujibu wa tafsiri nyengine.

kwani maana ya hayo ni kuwa baada ya kuwa makafiri wamekataa kuitika wito wa Mtume (s.a.w.), basi Mtume (s.a.w.) hataki kitu chengine chochote kutoka kwao ila waache kumuudhi tu – maana ya *Qasru* katika Aya kwa mujibu wa tafsiri hio pia imepatikana. Kwa hivyo, ni wazi kwamba tafsiri isemayo: **"…….Myapende mambo ya kukusogezeni (kwa Mwenyezi Mungu)"**, ni tafsiri yenye nguvu zake kwa mtazamo wa haraka haraka, lakini baada ya kuifikiri utaona ni tafsiri yenye udhaifu.

Sasa ikiwa tafsiri hio isemayo:

> **Sema kwa haya (ninayokufundisheni) siombi, (sitaki) malipo yoyote kwenu; lakini (nataka) myapende mambo ya kukusogezeni (kwa Mwenyezi Mungu),**

ni dhaifu kwa sababu yale ambayo yanaipa nguvu tafsiri hio pia yamo au yanawezekana kuzingatiwa katika tafsiri nyengine isemayo:

> **Sema sikuombeni juu yake (kufikisha huku) ujira wowote ule; isipokuwa mapenzi *kwa sababu* au *kwa ajili ya* ukaraba (ujamaa uliopo baina yangu na baina yenu),**

tunabakiwa na suali: je ni nini kimetufanya tuichague tafsiri hii ya pili pasina tafsiri ya kwanza. Sababu ni:

1) Kama tulivyosema kwamba chenye kuipa nguvu tafsiri ya mwanzo ni mambo mawili:

    a) Aya ilio kabla na maneno ya mwanzo na ya mwisho mwa Aya yenyewe: vyote hivyo vinatutaka tufanye mema ili tuingie peponi; kana kwamba Aya inasema kwamba haya tulioyataja hapa ya kutenda mema na kuacha maovu ili mupate pepo: sikulinganieni kuja katika hayo ili munipe ujira, bali isipokuwa kwa anayependa kujikurubisha kwa Allah kwa kuyatekeleza hayo. Lakini hili tumelijibu kwamba kutajwa kwa Aya hizo si **قَرِيْنَةٌ قَاطِعَةٌ** ushahidi wa mkato juu ya usahihi wa kuifasiri Aya hio, kwani kutajwa kwa matendo mema na malipo ya pepo kunaafikiana pia na tafsiri isemayo:

Sema sikuombeni juu yake (kufikisha huku) ujira wowote ule; isipokuwa mapenzi *kwa sababu* au *kwa ajili ya* ukaraba (ujamaa uliopo baina yangu na baina yenu),

kwani maana ni kuwa Mtume (s.a.w.) anawalingania watu wake kuja katika Uislamu ili waingie peponi bure: hataki malipo yoyote; na kama hawataki kumuitika basi wamuachie awalinganie watu wengine wasimkere na kumuekea vizingiti.

b) Jambo la pili lenye kuipa nguvu tafsiri ya mwanzo, ni kuwepo kwa maana ya *Qasru* katika tafsiri hio. Lakini na hili pia tumelijibu kwamba hata katika tafsiri ya pili maana ya *Qasru* pia inapatikana. Na kwa hivyo, utaona kwamba vimedhoofika hapa vyote vile vyenye kuipa nguvu tafsiri hio isemayo:

Sema kwa haya (ninayokufundisheni) siombi, (sitaki) malipo yoyote kwenu; lakini (nataka) myapende mambo ya kukusogezeni (kwa Mwenyezi Mungu).

2) Ama chenye kuipa nguvu tafsiri ya pili isemayo:

Sema sikuombeni juu yake (kufikisha huku) ujira wowote ule; isipokuwa mapenzi *kwa sababu* au *kwa ajili ya* ukaraba (ujamaa uliopo baina yangu na baina yenu),

ni kuwa katika Aya hio – katika matamshi yake ya Kiarabu – kuna herufi *Fii* na kuna neno *Qurbaa:* Aya inasema:

إِلاَّ الْمَوَدَّةَ فِي الْقُرْبَى

Illa Al-mawaddata <u>fii Al-qurbaa.</u>

Sasa cha kufahamu ni kuwa inapokusudiwa kusemwa **"Myapende mambo ya kukusogezeni (kukukurubisheni)"** basi katika Kiarabu huwa hakuna herufi *Fii* bali Aya katika Kiarabu ingesomeka ***Mawaddatu Al-Qurbaa***[282] na hapo tafsiri ingelikuwa

[282] - Na hapo *Al-baau (bee)* ingelikuwa na maana ya *Sababiya* yaani ingemaanisha "Sababu".

"Kupenda kujikurubisha". Kwani katika Kiarabu inapotakiwa kusemwa "kumpenda fulani" kwa kutumia neno *mawadda,* basi hapawekwi herufi ***fii*** ikasemwa: **مودة في فلان** ***Mwadatu fii Fulan*** (mapenzi katika fulani); bali husemwa **مودة فلان** ***Mawadatu Fulan*** (kumpenda fulani). Lakini kwa kuwa maneno ya Kiarabu ni ***"…Al-Mawaddata fii Al-Qurbaa",*** basi ukiwa utayafasiri maneno hayo kuwa maana yake ni **"Kupenda kujikurubisha"** basi utakuwa umeifanya herufi *Fii* kuwa haina kazi. Na hili halikubaliki ila kwa wale wanaosema kwamba katika Qur-ani kuna ziada, nayo ni kauli isiokubalika kabisa kwani ziada – kama alivyosema Sheikh Al-Mufassirin, Al-Khalili – huileta washairi katika mashairi yao ili wazifanye zile mezani za mashairi yao kuwa sawa baada ya kudharurika na kushindwa kuzifanya mezani hizo kuwa sawa bila ya ziada hizo; ama Allah (S.W.) Yeye hashindwi na kitu wala hadharuriki hata ikambidi alete ziada katika maneno yake ili maneno yake yapate kuwa sawa! Ninasema**:** bali ziada ni kufanya kitu kisichokuwa na faida; na matendo ya Allah yametakasika kutokana na kutokuwa na faida,[283] kwa hivyo, kila kilichotajwa katika Qur-ani kina faida wala hakuna ziada katika Qur-ani.[284] Kwa hivyo, tukizingatia msingi wa tafsiri hii na ile ni kuwa:

a) Tuikubali tafsiri hio isemayo:

> **Sema kwa haya (ninayokufundisheni) siombi, (sitaki) malipo yoyote kwenu; lakini (nataka) myapende mambo ya kukusogezeni (kwa Mwenyezi Mungu)"**,

[283] - Kama wanavyosema kwamba **أفعال الله منزهة عن العبث** Matendo ya Allah yametakasika kutokana na mchezo.

[284] **- اعلم – رحمك الله – أن الزيادة التي نفى وجودها العلماء في القرآن هي الزيادة التي تكون في المعنى لا الزيادة في الإعراب النحوي الممثل لها بقول القائل ((زيد ليس بموجود)) حيث يمكنك أن تقول ((زيد ليس موجودا).**

na kwa hivyo tuwe tumekubali kwamba herufi *fii* katika Aya hio ni ziada isioleta maana! Na bila shaka huu ni msingi batili, na kwa hivyo, natija ni kuwa hio ni tafsiri dhaifu.

b) Tuikubali tafsiri isemayo:

> **Sema sikuombeni juu yake (kufikisha huku) ujira wowote ule; isipokuwa mapenzi *kwa sababu* au *kwa ajili ya* ukaraba (ujamaa uliopo baina yangu na baina yenu),**

na kwa hivyo tuwe tumeipa herufi *fii* moja katika maana zake tafauti, nayo kwa hapa ima itakuwa:

1) Imetumika herufi hio kumaanisha *Al-Bau Al-Sababiyya* (Bee yenye kuonesha sababu).
2) Au imetumika kumaanisha *Lamu* au *Liajli ta'aliliyyatain* (Lamu au *Liajli* zenye kumaanisha: "kwa ajili ya").

Baada ya haya, utaona kwamba ushahidi uliomo ndani ya Aya yenyewe wa kilugha unaipa nguvu tafsiri moja (kwa mbili). Nasema moja kwa mbili kwani tafsiri mbili hizo – kama tulivyotangulia kusema – zimekurubiana sana: tafauti ni ndogo katika kuzingatia maana tafauti ya herufi *"Fii"*. Tafsiri hizo zenye nguvu hapa ni tafsiri yenye kusema:

> **Sema sikuombeni juu yake (kufikisha huku) ujira wowote ule; isipokuwa mapenzi *kwa sababu* ya ukaraba (ujamaa uliopo baina yangu na baina yenu).**

Hio ni tafsiri moja yenye nguvu kwani imeziingiza maana zote za herufi zilizomo ndani ya Aya. Pili ni:

> **Sema sikuombeni juu yake (kufikisha huku) ujira wowote ule; isipokuwa mapenzi *kwa ajili ya* ukaraba (ujamaa uliopo baina yangu na baina yenu).**[285]

[285] - Tafsiri hii na ya pili zimekurubiana sana: tafauti ni kwamba hapa imezingatiwa maana ya *Ta'aliliyya* (kwa ajili) ya herufi *"Fii"* wakati katika tafsiri iliotangulia

Tumesema hii ndio tafsiri sahihi na ndio tafsiri ya aghlabu ya wanavyuoni waliobakia, kama vile Al-Sabuni,[286] Ibn Kathir,[287] Al-Alusi,[288] Sheikh Al-Mufassirin, Badru Al-Din Al-Khalili, nayo ndio tafsiri ambayo Ibn Jarir Al-Tabari kasema kuwa ni sahihi kuliko zote.[289]

Ama tafsiri ya Shia yenye kusema:

> **Sikuombeni juu yake (kufikisha huku) ujira isipokuwa muwapende watu wa karibu yangu (jamaa zangu yaani Ahlul Bait),**

tafsiri hii inakosa ushahidi wa kilugha ndani ya Aya yenyewe. Suali lililobaki ni kuwa: kama tafsiri hio inakosa ushahidi wa kilugha ndani ya Aya yenyewe, je nini tegemeo la tafsiri hio? Tegemeo la tafsiri hio ni riwaya zilizopokewa juu ya nani ilimteremkia Aya hio. Sehemu inayofuata inazijadili riwaya hizo.

UTAFITI WA RIWAYA JUU YA

---

imezingatiwa maana ya Sababiyya (Sababu) ya herufi hio. Na iliosahihi zaidi ni tafsiri ya pili.

[286] - Al-Sabuni *Saf-watu Al-Tafasir* j. 3, uk. 100.

[287] - Ibn Kathir *Tafsiru Al-Qur-ani Al-'Adhim* j. 4, uk. 99.

[288] Al-Alusi *Ruhu Al-Ma'ani* j. 25, uk. 30.

[289] - Ibn Jarir *Jaami'u Al-Bayaan* j. 25, uk. 33. Bila shaka itakuwa pia kuna Wafasirina wengine wengi walioshikana na tafsiri hii ambao hatukizirejea tafsiri zao hasa hasa ukizingatia ukweli kwamba hii ni moja ya riwaya zilizosimuliwa na Ibn Jarir kutoka kwa Ibn Abbas, Ikrima, Abu Malik, Qatada, Mujahid, Al-Suddi, Al-Dhahhak, Ibn Zaid na Ataa bin Dinar. Mimi – *Walillahi Al-hamdu* – nilikuwa *namili* katika tafsiri hii zamani kabla hata ya kupekuwa maneno ya wanavyuoni kwani niliona kwamba herufi "Fii" hapa haina njia nyengine ya kuifasiri ila kuifasiri kuwa inamaanisha *Sababababiyya* (Sababu) au *Ta'aliliyya* (Kwa ajili). Hatimae nikamuuliza pia Sheikh Al-mufassirin Al-Imamu Badru Al-Din Al-Khalili (H.A.), akanijibu hivyo hivyo *Walillahi Al-hamdu.*

Jambo la sita: ni kutazama yaliomo nje ya Aya hio, nazo ni riwaya zenye kuhusiana na Aya hio. Kwa mujibu wa Shia – kama tulivyosema – Aya hio: **" قُلْ لا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْراً إِلاَّ الْمَوَدَّةَ فِي الْقُرْبَى "** imewashukia Ali, Fatima na watoto wao. Na kwamba tunachoamrishwa katika Aya ni kuwapenda wao ili iwe tumemlipa Mtume (s.a.w.) ujira kwa kazi yake ya kufikisha ujumbe. Nao wanategemea – kwa kauli yao hio – baadhi ya riwaya zilizokuja kwa njia chache, kama inavyofuata:

Riwa ya kwanza inasema:

> Ilipoteremka (Aya isemayo): **" قُلْ لا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْراً إِلاَّ الْمَوَدَّةَ فِي الْقُرْبَى "** (Masahaba) walisema: 'Ewe Mjumbe wa Allah! Na ni nani hao *qaraba* wako (jamaa zako) ambao imetuwajibikia kuwapenda?' Akasema (Mtume s.a.w.): 'Ali na Fatima na watoto wao".

Riwaya hio, kaisimulia Al-Tabarani,[290] Al-Tha'alabi,[291] na Ibn Abi Hatim.[292]

SANAD

Hadithi hii ni batili bila ya shaka kwani ina msururu wa wapokezi dhaifu nao ni Mashia wa kule kule mjini kwetu Al-Kufa, na hivi ndivyo zilivyo riwaya zote walizotungiwa Ahlu Al-Bait: wapokezi wake ni Mashia – hata kama riwaya hizo zimo katika vitabu vya Kisunni – tena aghlabu – kama si wote – basi ni Mashia wa Al-Kufa: riwaya zote za sifa za ziada za Ahlu Al-Bait ni utunzi wa Wairaki wa Al-Kufa *Wallahu Al-musta'aan!*[293]
Katika *sanad* ya riwaya hio, kuna Harb bin Hasan, naye ni Shia. *Tarjama* yake ni fupi katika *Lisanu Al-Mizan*.[294] Anasema "Al-Azdi: "Si mtu wa hivyo".

---

290 - Al-Tabarani *Al-Kabir* j. 3, uk. 47, Hadithi na. 2641.
291 - Al-Tha'alabi *Al-Kashfu Wa Al-Bayan* j. 8, uk. 310.
292 - Ibn Abi Hatim *Tafsiru Al-Qur-ani Al-'Adhim* j. 10, uk. 3277, riwaya na. 18477.
293 - Watu hawa wa Irak wamekuwa ni mtihani mkubwa kwa Waislamu katika historia yao yote na hadi leo wanaendelea kuwa mtihani kwa Waislamu!
294 - J.2, uk. 184, *tarjama* na. 827.

Na Harb bin Hasan kaisimulia Hadithi hio kutoka kwa Husain Al-Ashqar naye pia ni Shia wa Al-Kufa na ni dhaifu mno. Anasema Al-Bukhari: *"fihi nadharun* **فِيْهِ نَظَرٌ"** "Ni mtu wa kufikiriwa".[295] Na akasema tena Al-Bukhari: "Anasimulia (Hadithi nyingi) munkar". Anasema Abu Zur'a: "Hadithi zake ni munkar". Anasema Abu Hatim: "Si madhubuti". Anasema Al-Juzajani: "Ni *ghaali* (extremist, na ni) miongoni mwa wenye kuwatukana watu bora (Masahaba)". Kisha akataja Ibn Hajar riwaya zake alizozisimulia za kumtungia Ali na kuzinasibisha kwa Hujr Al-Madari na nyengine kwa Tawus ambazo Al-Imamu Ahmad kazikanusha na pia Ali bin Al-Madini kasema kuwa ni uwongo. Na Ibn Adey pia kazitaja riwaya zake *munkar* na akasema: "Balaa (yote hii) ninavyoona mimi inatoka kwa Al-Ashqar". Na wakasema Al-Nasai na Al-Daraqutni: "Si madhubuti". Na akasema Al-Azdi: "Ni dhaifu". Na akasema Abu Ma'amar Al-Hudhali: "Al-Ashqar ni mwongo". Anasema Al-Hakim: "Si madhubuti", nayo ndio lugha ya Al-Hakim kwa wapokezi dhaifu.[296]

Na Husain Al-Ashqar kaisimulia Hadithi hio kutoka kwa Qais bin Al-Rabii, naye pia ni Shia wa kule kule mjini Al-Kufa kwenye kiwanda cha ufinyanzi wa Hadithi, tena ni dhaifu kama tulivyomuelezea kabla.[297]

Na Qais bin Al-Rabii kaipokea Hadithi hii kutoka kwa Al-A'amsh, Sulaiman bin Mihran, naye pia ni Shia wa kule kule mjini Al-Kufa, naye ni mwenye kughushi na Hadithi yake hapa ni *mu'an'an* (kutoka kwa…).[298]

Hio ndio *sanad* ya Hadithi hio katika mapokezi yake yote, isipokuwa katika mapokezi ya Abu Hatim wako wapokezi watatu tu katika hao na mmoja ni mtu asiyejulikana: *sanad* imesema tu "katusimulia mtu aliyemtaja" basi ni hivyo "mtu aliyemtaja" hajulikani ni nani. Nao huo pia ni udhaifu mwengine mkubwa wa *sanad*.

---

[295] - Al-Bukhari anapotumia *lafdhi* hii humaanisha kwamba mpokezi huyo ni dhaifu sana.
[296] - Al-Bukhari *Al-Taarikh Al-Kabir* j. 2, uk. 384, *tarjama* na. 2862. Al-Dhahabi *Al-Mizan* j. 2, uk. 54-55, *tarjama* na. 1986. Ibn Hajar *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 2, uk. 291-292 *tarjama* na. 596. Al-Mizzi *Tahdhibu Al-Kamal* j. 2, uk. 648-649, *tarjama* na. 1307.
[297] - *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 8, uk. 350, *tarjama* na. 698.
[298] - Tazama Al-Dhahabi *Al-Mizan* j. 2, uk. 414, *tarjama* na. 3517.

HADITHI YA PILI

Hadithi ya pili inasema:

> Alipoletwa Ali bin Husain (r.a.) hali ya kuwa ni mateka, basi akasimamishwa katika njia za Dimashq[299] (mji mkuu wa Syria). Alisimama mtu miongoni mwa watu wa Sham akasema: 'Sifa zote zilio njema ni za Allah ambaye kakuuweni akaikata mizizi yenu na akakata jamaa wa fitna. Ali bin Husain (r.a.) akamwambia: je umesoma Qur-ani? Akasema: "Ndio". (Akasema Ali bin Husain kumwambia yule mtu, je): 'Umesoma watu wa *Hammim*?: (Akasema) 'Nimesoma Qur-ani na wala sikusoma watu wa *Hammim*'. Akasema: 'Hukusoma wewe (Aya isemayo) **قُلْ لا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْراً إِلاَّ الْمَوَدَّةَ فِي الْقُرْبَى** Akasema: "Je nyinyi ndio wao?" Akasema: "Ndio".

Kaipokea Ibn Jarir,[300] na Al-Tha'alabi.[301]

SANAD

Nayo pia Hadithi hii ni Hadithi dhaifu sana kwani katika *sanad* yake kuna Ismail bin Aban. Haikunibainikia ni yupi mmoja: je ni Ismail bin Aban Al-Warraq au ni Ismail bin Aban Al-Ghanawi. Wa mwanzo ni Shia wa Al-Kufa, lakini kahimidiwa na wengi wao, na wengine wachache wakamdhoofisha. Lakini dhahir ni kuwa watu hao waliomdhoofisha walimchanganyisha wa kwanza na wa pili.[302] Ama wa pili pia ni mpokezi wa Al-Kufa naye ni dhaifu, mwongo mwenye kutunga Hadithi na mwenye kuachwa.[303]

Na Ismail bin Aban kaisimulia Hadithi hio kutoka kwa Al-Aabah bin Yahya, naye pia ni Shia wa Al-Kufa na ni dhaifu. Anasema Al-Dhahabi: "Ni mwenye kuachwa, bali ni mwenye kutuhumiwa (kwa kutunga

---

299 - Riwaya nyengine ni kuwa jina sahihi la mji huo ni Dimishq, lakini *Jumhur* – kwa mujibu wa Yaqut Al-hamwiy – inauita mji huo Dimashq.

300 - Ibn Jarir *Jaami'u Al-Bayaan* j. 25, uk. 32.

301 - Al-Tha'alabi *Al-Kashfu Wa Al-Bayaan* j. 8, uk. 311.

302 - Tazama *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 1 uk. 236, *tarjama* na. 506.

303 - Tazama *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 1 uk. 237, *tarjama* na. 507.

Hadithi)". Na Al-Bukhari amemjeruhi vikali mpokezi huyu aliposema: **"فِيْهِ نَظَرٌ"** "ni mtu wa kufikiriwa".[304]

Na Al-Asabah bin Yahya, kaipokea Hadithi hio kutoka kwa Al-Suddi. Tumemuelezea katika sura ya kwanza. Naye ni Ismail bin Abdil-Rahmaan Al-Suddi, Shia wa kule kule mjini Al-Kufa, aliyekuwa akiwatukana Abu Bakr na Umar. Naye ni dhaifu sana, bali kaitwa mwongo.[305]

Kwa hivyo Hadithi hizi zote ni dhaifu sana hazifai kuwa *hujjatu Allahi Alaa Ibadihi* (hoja za Allah juu ya waja wake). Na kwa hivyo, hazifai kuzitumia katika kukifasiri Kitabu cha Allah, kwani ni dhaifu mno.

Baada ya haya, utaona kwamba Hadithi zote hizo zenye kutaka kuwapamba Ahlu Al-Bait mapambo ya sifa za ziada zimesimuliwa na wapokezi Mashia, na wengi wao wametajwa kwa sifa mbaya ya kuwa ni waongo na wote ni wa mji ule ule wa Kishia wa Al-Kufa kulikokuwa na kiwanda cha utunzi wa riwaya *Wala haula wala quwwata illa bi-Llah!*

MATN YA HADITHI

Anasema Sheikh Abdul-Razzaq Al-Mahdi[306] kwamba Sura hii imeteremka Makka na wakati huo Fatima bint Rasul (s.a.w.) hakuwa na watoto kamwe. Yaani anachokisema Sheikh huyu ni kuwa Sura nzima hii imeteremka Makka na wakati Mtume (s.a.w.) yuko Makka bado Bibi Fatima (r.a.) hana mtoto, sasa vipi Sura imeteremka kuwaamrisha Waislamu wawapende Al-Hasan na Al-Husain nao hawapo: hawajazaliwa? Al-Hasan bin Ali, mtoto wa Bibi Fatima na Al-Imamu Ali, alizaliwa Madina tarehe kumi na tano

[304] - *Tarjama* yake ni fupi katika *Al-Mizan* cha Al-Dhahabi j. 3, uk. 20, *tarjama* na. 3850, na Ibn Hajar *Lisanu Al-Mizan* j. 3, uk. 180, *tarjama* na. 729.

[305] - Tumetoa maelezo kuhusu Al-Suddi pamoja na kutoa marejeo huko nyuma.

[306] - Katika maelezo yake alioyatia katika tafsiri *Al-Kashaf* cha Al-Zamakhshari, j. 4, uk. 223.

(15) Ramadhan mwaka wa 3 H.[307] Na Al-Husain alizaliwa tarehe tatu (3) Shaabani mwaka 4 H.[308]

Kwa hivyo, Waislamu katika kipindi cha Makka wanaamrishwa kuwapenda watu hewa: hawapo katika ulimwengu – mtunzi hapa alighafilika!

FIQ-HI YA AYA

Tumeona kwamba kwa mujibu wa Shia Aya hio tunayoijadili hapa imewataremkia Ali, Fatima na watoto wao. Tumebainisha kwamba hakuna riwaya thabiti juu ya dai hilo, lakini tukijaalia kuwa ni hivyo, suali ni kuwa je kuna uhusiano gani wa Aya hii na dai la ukhalifa wa Ahlu Al-Bait?

Dr. ‘Alaa Al-Din bin Al-Sayyid Amir Muhammad Al-Qazwini – katika jawabu yake kwa Dr. Musa Al-Musawi alioiita *Ma’a Al-Duktur Al-Musawi*,[309] baada ya kuipinga tafsiri ya *Jumhur* ya Aya hio, anasema:

> Na kwa hivyo, inathibiti maana ya pili kuwa makusudio ya (Neno) *Al-Qurbaa* ni jamaa wa Mtume (s.a.w.) na watu wa nyumba yake – Ali na Fatima na Hasan na Husain. Na kwamba kuwapenda wao ni kuwapa Uimamu wao pasina wengine na hio ni kwa hoja inayofuata:
>
> Hakika kuwapenda Ahlu Al-Bait ni wajibu kwa mujibu wa Aya hio Takatifu, na kila yule ambaye kumpenda ni wajibu basi ni wajibu kumtii kwa mujibu wa kauli yake Allah: “Mukiwa munampenda Allah basi nifateni…”.[310] Na kwa msingi huu, ikiwa umethibiti uwajibu wa kupenda, basi umethibiti uwajibu wa kutii, na yule ambaye imekuwa wajibu kumtii basi Uimamu (Ukhalifa)[311] wake umekuwa wajibu. Basi inaundika kwetu hoja inayofuata:

---

307 - Tazama *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 2, uk. 257, *tarjama* na. 528. Pia tazama *Tangazo La Ghadir* cha Al-Sayyid Rizvi uk. 46.

308 - Tazama Tahdhibu Al-Tahdhib j. 2, uk. 299, *tarjama* na. 615. Pia tazama *Tangazo La Ghadir* cha Al-Sayyid Rizvi uk. 46.

309 - Uk. 69

310 - Sura 3, Aya 31.

311 - Uimamu na Ukhalifa una mafhumu (concept) tafauti kwa wanavyuoni wa Kishia (Tazama Tabatabai *Al-Mizan* j. 1, uk. 262…Khalid Abu Dhar *Al-Tashayyu’u Al-Muftaraa*

Aliyekuwa wajibu kumpenda Ni wajibu kumtii
Na kila aliyewajibu kumtii Uimamu (Ukhalifa) wake ni wajibu!

Basi natija (ni kuwa):

Aliyekuwa wajibu kumpenda Uimamu (Ukhalifa) wake ni wajibu!

Hayo ndio maneno ya bwana huyu, nayo – kama unavyoona ni – vichekesho vyenye kuliza, na ni hoja za kitoto! Sijui Dr. huyu ana akili gani?! Lakini hata ukikisoma hicho kitabu chake, utaona ni kheri kwake kama angenyamaza kuliko kumjibu Al-Musawi, kwani – kama tulivyobainisha katika utangulizi – anasubiri Sunni anukuu riwaya tu hata kama ni dhaifu kwa mtazamo wa Kisunni basi yeye huinukuu riwaya hio na akasema kwamba "Sunni kansema"! Sasa hatuna haja ya kuzungushana sana, tukijaalia kuwa Aya imewateremkia Ali, Fatima na watoto wao, tumeona kwamba hakuna riwaya sahihi juu ya dai hilo,[312] lakini tukijaalia kuwa ni hivyo; suali ni kuwa je Fatima naye yumo katika Aya au hayumo? Je na yeye awe Imamu (Khalifa) ili Maimamu sasa wawe 13: mmoja ni Imamu *ntu nke*?

Pili: kwani kuwapenda Waislamu wote au – kwa Kishia – kuwapenda Mashia wote si wajibu. Allah anasema:

وَالْمُؤْمِنُونَ وَالْمُؤْمِنَاتُ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ

Na waumini wanaume na waumini wanawake wenyewe kwa wenyewe ni vipenzi.[313]

'Alaihi uk. 196-199) lakini wakati mwengine huyatumia maneno hayo kwa lengo moja, kama alivyofanya muandishi huyu wa Kishia. Hata hivyo, kwao Imamu ndiye Khalifa wa Kisharia. Tafauti baina yao ni pale akiwa kaghibu – kama alivyofanya Al-Mahdi Al-Muntadhar – je kunakuwa na *"Wilayatu Al-Waqih"* yaani je mwanachuoni asiye *ma'asum* anakuwa muawakilishi wa Imamu Ma'asum (asiyetenda dhambi kwa itikadi ya Kishia). Al-Khomeni anasema: "Ndio"; wengine akiwemo Al-Musawi wanasema: "Sio". Nimehadithiwa na mmoja wa Mashia kwamba Al-Sistani pia ni katika wanaopinga siasa ya *"Wilayatu Al-faqih"* .

312 - Bali Al-Hasan na Al-Husain walikuwa hawajazaliwa kamwe iliposhuka Aya hio.

313 - Sura 9, Aya 71.

Na anasema:

إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ سَيَجْعَلُ لَهُمُ الرَّحْمَنُ وُدّاً

Hakika wale walioamini na kutenda mema Allah atawajaalia mapenzi (baina yao).[314]

Neno ***"Wudda"*** lililotumika katika Aya hii ni neno moja na neno *"Mawada"* lililotumika katika Aya hio tunayoijadili. Na Mtume (s.a.w.) anasema: **لاَ تُؤْمِنُوا حَتَّى تَحَابُّوا "Hamutoamini mpaka mupendane".**[315] Na hii – uhakika wake – ni amri, na amri inamaanisha uwajibu.[316] Na akasema katika Hadithi nyengine: **لا يؤمن أحدكم حتى يحب لأخيه ما يحب لنفسه "Haamini mmoja wenu mpaka ampendelee ndugu yake (Muislamu mwenzake) yale anayojipendelea yeye".**[317] Na akasema Allah katika Hadithi Qudsi: **وَجَبَتْ مَحَبَّتِي لِلْمُتَحَابِّينَ فِيَّ "Mapenzi yangu yamewawajibikia wale wanaopendana kwa ajili yangu".**[318] Kwa ufupi ni kuwa Aya na Hadithi zenye kuamrisha mapenzi baina ya Waislamu ni nyingi na hili halina khilafu.

Kwa hivyo, ikiwa anavyosema Daktari 'Alaa Al-Din ni sahihi kwamba:

Aliyekuwa wajibu kumpenda	Ni wajibu kumtii,
Na kila aliyewajibu kumtii	Uimamu (Ukhalifa) wake ni wajibu!

Basi maana ni kuwa:

Aliyekuwa wajibu kumpenda, Uimamu (Ukhalifa) wake ni wajibu!"

---

314 - Sura 19, Aya 96.

315 - Muslim *Sahihu Muslim* uk. 43, Hadithi na. 54.

316 - Kama ilivyo katika *Usuli* kwamba **"الأَمْرُ يَقْتَضِيْ الْوُجُوْبَ مَا لَمْ تَصْرِفْهُ عنه قَرِيْنَةٌ"** amri inamaanisha wajibu madamu hakuna Qarina (context) ilioigeuza (amri hio kutoka katika wajibu) huo.

317 - Muslim *Sahihu Muslim* uk. 39, Hadithi na. 45.

318 - Ibn Hibban *Al-Ihsan* j. 1, uk. 390-391, Hadithi na. 574. Al-Rabi'u bin Habib *Al-Jaami'u Al-Sahih* uk. 46, Hadithi na. 69.

Na natija ni kwamba: Tutakuwa na Maimamu na Makhalifa wengi, kwani kila Muumini ni wajibu kumpenda na kila aliyewajibu kumpenda ni wajibu kumtii na kila aliyewajibu kumtii ni wajibu kumfanya Imamu – natija ni kuwa Uimamu wake umetuwajibikia?! Hii ni mantiki ambayo haina kichwa wala miguu. Kwa ufupi ni kuwa:

1) Hakuna Hadithi sahihi kwamba Aya hio imewateremkia Ali na watoto wake.
2) Hata kama ingekuweko Hadithi sahihi, basi kuwapenda Ali na watoto wake haileti maana kuwa tuwafanye Makhalifa kwani kama tunavyotakiwa tuwapende wao vivyo hivyo tunatakiwa tuwapende Waislamu wote kwa ushahidi wa Aya nyingi na Hadithi nyingi.[319]

RIWAYA NYENGINE JUU YA SABABU YA KUTEREMKA AYA HIO

Bila kusahau kwamba, kuna riwaya nyengine tafauti na hio juu ya sababu ya kuteremka Aya hio. Riwaya hio inasema – ninafupisha – kwamba Maansar walijifakharisha kwa Ibn Abbas au kwa Abbas kwamba wao wamempokea Mtume na kumfanyia wema wa aina tafauti. Na kwa hivyo, wakasema kwamba wao ni bora kuliko wao (Ibn Abbas au Abbas na Makureish wengine). Habari hio ilipomfikia Mtume (s.a.w.), akawaendea Maansar katika majlisi yao akawambia: "Hamukuwa mumepotea Allah

---

[319] - Muandishi mwengine wa Kishia aitwaye Mahdi Ahmad Al-Fatlawi kaichukua Aya hio tunayoijadili hapa kuwa ni ushahidi kwamba Ahlu Al-Bait hawakosei. Kisha baada ya hapo ndio akatoa natija kwamba:

> Hakuna hekima yoyote ile ya Mwenyezi Mungu katika kuthibiti huku kwa *isma* (kutokufanya dhambi na kutokukosea) ya Ahlu Al-Bait isipokuwa kusimamia kwao kazi ya ukhalifa mtukufu baada ya Mtume (s.a.w.).

Tazama Mahdi Hamad Al-Fatlawi *Ma'a Al-Mahdi Al-Muntadhar* uk. 93-94. Lakini – kama ulivyoona – kwamba hakuna ushahidi kamwe wa kuwa Aya hio imewateremkia Ahlu Al-Bait: si katika Aya yenyewe wala si katika riwaya; bali ushahidi ulio katika Aya yenyewe ni kinyume kabisa na fikra hio kama tulivyobainisha. Kwa hivyo, maelezo yake hayo yote ni kama **جنة أصابها إعصار فيه نار فاحترقت** bustani iliopigwa na kimbunga ambacho ndani yake kina moto ikawaka yote bustani hio!

akakuongozeni kwa sababu yangu?" Wakasema: "Ndio". Akasema: "Basi hamuniitiki?" Wakasema: 'Unasema nini ewe Mjumbe wa Allah (ili tupate kuitika wito wako)". Akasema: "Si munasema nyinyi kwamba kwani hawakukutoa watu wako sisi tukakupokea; hawakukukadhibisha sisi tukakusadikisha...?" Basi Mtume (s.a.w.) akawa anaendelea kusema mpaka (Maansar) wakapiga magoti na wakasema: "Mali zetu na yote tulionayo mikononi mwetu ni vya Allah na Mtume wake". Basi ikateremka Aya hio: **"قُلْ لا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْراً إِلاَّ الْمَوَدَّةَ فِي الْقُرْبَى".**[320]

Fiq-hi ya Hadithi hii – kama unavyoona – inaonesha kuwa makusudio ya Aya hio isemayo: **"قُلْ لا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْراً إِلاَّ الْمَوَدَّةَ فِي الْقُرْبَى",** ni kuwapenda jamaa wa Mtume (s.a.w.). Na hii ni kuwa – kwa mujibu wa riwaya hio – Mtume (s.a.w.) aliyasema hayo baada ya Al-Ansar kumsumbulia Abbas au Ibn Abbas kwa takrima yao waliomfanyia Mtume (s.a.w.) na kwa hivyo wakajifanya wao kuwa ni bora zaidi kuliko Makureish na hata Abbas au Ibn Abbas ambao ni watu wa karibu zaidi na Mtume (s.a.w.).

Hivyo ndivyo riwaya inavyotongoa, lakini mbele haya kuna tatizo kwamba Sura hii iliteremka Maka: si Madina, na kwa hivyo kuihusisha na matokeo yaliotokea Madina si kitu sahihi. Hio ni kwa upande wa *matn (text)* ya riwaya hio. Ama kwa upande wa wapokezi, tunakuta kwamba katika *sanad* yake kuna Abdul-Salam bin Harb, naye ni dhaifu, anasimulia Hadithi munkar. Anasema Ibn Sa'ad "Alikuwa na udhaifu katika Hadithi". Na anasema Ibn Hajar: "Ana Hadithi (nyingi) Munkar". Na wengine wamemkubali.[321] Lakini pia yumo – katika *sanad* ya Hadithi hio – Yazid bin Abi Ziyad naye ni dhaifu, bila ya wasi wasi wowote ule.[322] Kwa hivyo, riwaya hio haikuthibiti.

RIWAYA NYENGINE: ni kuwa Aya hio imeteremka baada ya Makureishi kukataa kuitika wito wa Mtume (s.a.w.) wa kuja katika Uislamu. Sababu hii kaisimulia Al-Tha'alabi[323] kutoka kwa Qatada bila ya *sanad*, na mfano

[320] - Ibn Jarir Al-Tabari *Jaami'u Al-Bayaan* j. 25, uk. 32. Al-Tha'alabi *Al-Kashfu Wa Al-Bayaan* j. 8, uk. 312.
[321] - Tazama *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 6 uk. 282, *tarjama* na. 613, na *Taqribu Al-Tahdhib* uk. 355 *tarjama* na. 3067.
[322] - Tazama *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 11, uk. 287-288, *tarjama* na. 531.
[323] - Al-Tha'alabi *Al-Kashfu Wa Al-Bayaan* j. 8, uk. 310.

wake kaisimulia Ibn Jarir[324] kutoka kwa Ibn Abbas, na yenye kukurubiana na riwaya hio kimaana ni riwaya kutoka kwa Abi Malik ambayo pia imesimuliwa na Al-Tabari.[325] Na riwaya nyengie alizozitaja Al-Tabari ni za wafuasi wa Masahaba.[326]

Ama tukirudi katika riwaya ya Qatada, ni kama tulivyosema kwamba Al-Tha'alabi hakutaja *sanad*, na kwa hivyo hatuna cha kukijadili katika riwaya hio. Ama riwaya ya Ibn Abbas alioisimulia Al-Tabari, tunaona kwamba Al-Tabari kaisimulia riwaya hio kwa *sanad* mbili: ya kwanza katika *sanad* yake kuna Mu'awiya bin Salih naye wametafautiana juu ya usahihi wa Hadithi zake.[327] Na aliyeisimulia Hadithi hio kutoka kwa Ibn Abbas ni Ali bin Abi Talha naye ni dhaifu anasimulia Hadithi munkar, na juu ya yote hakupata kusikia Hadithi kutoka kwa Ibn Abbas. Kwa hivyo, baina yake na Ibn Abbas kuna mpokezi hakumtaja,[328] na kwa hivyo *sanad* hii ni dhaifu.

Ama *sanad* ya pili ya Hadithi ya Ibn Abbas, ina msururu wa wapokezi dhaifu, kuanzia babu hadi kufikia vijukuu! *Sanad* ya riwaya ya pili ni:

> Muhammad bin Sa'ad (bin Muhammad) kasema kanihadithia baba yangu (Sa'ad bin Muhammad bin Hasan bin Atiyya) kasema kanihadithia ami yangu (Al-Husain bin Hasan bin Atiyya) kasema kanihadithia baba yangu (Hasan bin Atiyya) kutoka kwa baba yake (Atiyya bin Sa'ad bin Junada Al-'Aufi) kutoka kwa Ibn Abbas.

Katika *sanad* hii kuna Atiyya bin Sa'ad Al-'Aufi, naye ni dhaifu na ni mwenye kughushi,[329] na Hadithi yake hapa ni *mua'an'an.* Pia yumo katika *sanad* hii Hasan bin Atiyya, naye ni dhaifu. Anasema Abu Hatim: "Hadithi zake ni dhaifu". Na akasema Ibn Hibban: "Hadithi zake si safi". Na ikaelezwa katika kitabu *Al-Dhu'afaa* kwamba: "Hadithi zake ni *munkar".*

---

[324] - Ibn Jarir Al-Tabari *Jaami'u Al-Bayaan* j. 25, uk. 30.

[325] - K.h.j.

[326] - Hizi si muhimu kwa hapa kwani itakuwa ni riwaya *mursala*.

[327] - Tazama *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 10 uk. 191, *tarjama* na. 392.

[328] - Tazama *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 7 uk. 298, *tarjama* na. 568.

[329] - Tazama *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 7 uk. 200, *tarjama na.* 414. Na anasema Ibn Hajar: "Mkweli, anakosea sana, Shia, mwenye kughushi". Tazama *Taqribu Al-Tahdhib* uk. 394, *tarjama* na. 4616.

[330] Pia yumo katika *sanad* hii Al-Husain bin Hasan bin Atiyya, naye ni dhaifu pia, kadhoofishwa na Ibn Ma'iin na wengine. Anasema Ibn Hibban: "Kasimulia mambo hayana ushahidi; wala haijuzu kumfanya kuwa ni hoja". Na Akasema Al-Nasai: "Dhaifu". Na akasema Abu Hatim: "Hadithi zake ni dhaifu". Anasema Al-Juzajani: "Hadithi zake ni *wahiy* (Dhaifu sana)". Anasema Ibn Sa'ad: "Alikuwa dhaifu wa Hadithi". Na Al-'Uqaili kamtaja katika *Al-Dhu'afaa.*[331] Pia yumo katika *sanad* hii Sa'ad bin Muhammad bin Hasan bin Atiyya. Anasema Al-Imamu Ahmad: "Huyu hakuwa mtu anayestahiki kuandikwa (kitu chochote) kutoka kwake, wala hakuwa mtu wa hayo (kamwe)".[332] Kwa hivyo, riwaya hii pia haikuthibiti.

MUKHTASARI NA NUKTA MUHIMU

1) Tulioijadili hapa ni Aya inayosema:

قُلْ لا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْراً إِلاَّ الْمَوَدَّةَ فِي الْقُرْبَى

2) Aya hii wametafautiana katika kuifasiri kwa tafsiri tafauti: tatu ndio muhimu zao. Tafsiri ya kwanza inasema:

> **Sema kwa haya (ninayokufundisheni) siombi, (sitaki) malipo yoyote kwenu; lakini (nataka) myapende mambo ya kukusogezeni (kwa Mwenyezi Mungu).**

Tafsiri ya pili inasema:

> **Sema: Sikuombeni juu yake (kufikisha huku) ujira wowote ule, isipokuwa mapenzi kwa *sababu (au kwa ajili)* ya ujamaa.**

Kimaana tafsiri hio ni sawa na tafsiri isemayo:

---

[330] - Tazama *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 2, uk. 255, *tarjama* na. 524.
[331] - Ibn Hajar *Lisanu Al-Mizan* j. 2, uk. 341-342, *tarjama* na. 2679.
[332] - Ibn Hajar *Lisanu Al-Mizan* j. 3, uk. 24, *tarjama* na. 3650.

Sema (Ewe Muhammad): sikuombeni (kwa kufikisha ujumbe (huu) kitu (chochote) ujira wowote, isipokuwa muilinde haki ya ujamaa (wala musiniudhi ili nifikishe ujumbe wa Mola wangu).

Tafsiri ya tatu inasema:

Sema sikuombeni juu yake (kufikisha huku) ujira isipokuwa muwapende watu wa karibu yangu (jamaa zangu).

Halafu zikapokewa riwaya kwamba jamaa zake wenyewe walikuwa ni Ali, Fatima, Al-Hasan na Al-Husain.

3) Tumebainisha kwamba tafsiri ambazo – kwa mujibu wa lugha – zina muelekeo ni ya kwanza na ya pili, lakini hata hivyo tafsiri ya kwanza – baada ya kuitafakari vyema – inaonekana kuwa ni tafsiri yenye udhaifu, na kwa hivyo tafsiri ya pili isemayo: **"Sema sina ninachokuombeni juu yake (kufikisha huku) katika ujira; isipokuwa mapenzi *kwa sababu* (au kwa ajili) ya ukaraba (ujamaa)"** ndio tafsiri sahihi.

4) Tafsiri ya tatu haina ushahidi wowote wa kilugha wala wa kifani yoyote.

5) Tegemeo la tafsiri ya tatu ni baadhi ya Hadithi zilizopokewa juu ya tafsiri hio.

6) Lakini Hadithi hizo ambazo zimetegemewa kuonesha kwamba Aya hio imewashukia Ali na watoto wake ni Hadithi za utunzi wa mjini Al-Kufa (Iraq). Hadithi hizo:

   a) Zote ni za wapokezi wa Al-Kufa (Irak).

   b) Kila Hadithi ina idadi ya wapokezi wa Kishia, na hutuwezi kuikubali riwaya ya Kishia yenye kutetea msimamo wa Kishia hasa hasa tukizingatia tabia yao ya kutunga Hadithi kwa wingi

katika vitabu vyao kama *Al-Kafi* na walizowachomekea Masuni katika vitabu vyao.[333]

c) Wapokezi hao wa Hadithi hizo si kwamba ni Shia tu, bali wengine ni waongo[334] watunzi wa Hadithi na wengine ni dhaifu sana na wengine wanaghushi Hadithi dhaifu. Kwa hivyo, Hadithi hizo ni za uwongo, za kutungwa.

d) Chengine chenye kuonesha utunzi wa riwaya hizo, ni kuwa Sura yenye Aya hio iliteremka Makka, na wakati huo Al-Sayyida Fatima alikuwa hajapata watoto – Al-Hasan na Al-husan. Vipi Sura iteremke kuwaamrisha Waislamu kuwapenda watu ambao hawajazaliwa. Mtunzi wa Hadithi hapa kaadhirika!

7) Hata tukijaalia kuwa kweli Aya hio imewashukia Ali, Fatima, Al-Hasan na Al-Husain bado Aya haina ushahidi wa ukhalifa na uimamu wao kwani:

a) Bibi Fatima naye yumo katika jumla ya tuliomrishwa tuwapende, naye si katika Maimamu 12. Kwa hivyo, kupenda ni kitu kimoja na ukhalifa ni kitu chengine.

b) Kama tunavyotakiwa tuwapende Ali na watoto wake ndivyo tunavyotakiwa tuwapende Waislamu wote kwa ushahidi wa Aya na Hadithi tulizozitoa.

Kwa hivyo natija ni kuwa Aya : **" قُلْ لا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْراً إِلاَّ الْمَوَدَّةَ فِي الْقُرْبَى"** ni haki lakini tafsiri ya Aya kwamba inamaanisha ukhalifa ni batili. Na kwa ufupi, tunasema kwamba suala zima la kuwa Allah na Mtume (s.a.w.) wamemchagua Ali na kizazi chake wawe ni Makhalifa baada ya Mtume, ni uwongo uliotungwa katika Irak ya kale katika wimbi la kugombania

[333] - Al-Bukhari tu ndio aliyewakera sana kwa kuwa hakuipokea Hadith *Al-Thaqalain* katika *Sahihu* yake. Bali riwaya zao nyingi za kupakasa kazipiga na ukuta, basi wakamsema sana.

[334] - Usije ukadhani kuwa mimi ndio ninayesema kuwa Mashia hao ni waongo, *Kalla (Sio hivyo)*: mimi ninanukuu tu yaliosemwa na wanavyuoni wa wapokezi, na nakubaliana nao baada ya kuzitazama asili mia kubwa ya riwaya za wapokezi hao walizozisimulia.

ushikaji wa hatamu za kisiasa baina ya Umawiyyin (Kizazi cha Umayya), Abasiyyin (Kizazi cha Abbas) na Al-'Alawiyyin (Kizazi cha Ali).[335] Na kila mmoja katika hawa ana Hadithi zake kwamba yeye ndiye anayestahiki kushika ukhalifa wa Dola ya Kiislamu, lakini wapambe wa kizazi cha Ali wao ndio matajiri wao katika Hadithi za namna hio! Lau watu wangelikuwa wanatumia akili zao vizuri au wanasali sala ya istikhara *li-Lahi* kabla ya kukumbatia itikadi wanazoletewa, basi asingepotezwa ila yule anayetafuta kujaza tumbo.

[335] - Jambo hili la kupigania madaraka baina ya makundi matatu haya liko wazi kabisa katika vitabu vya historia. Ndio maana utaona kwamba hata kizazi cha Ali pia kiligawika baina ya kizazi cha Hasan na kizazi cha Husain; kila mmoja anataka yeye awe ndio Khalifa. Na pia utakuta kwamba ukoo mmoja umekuwa na Ja'afar Al-Saadiq (Ja'afar mkweli) na umekuwa na Ja'afar Al-Kaadhib (Ja'afar mwongo). Na vikazuka vikundi tafauti vya Kishia kila mmoja anadai ukhalifa kwa kigezo cha Uahlul-Bait. Na wote wana Hadithi kwa kapu na magunia kwamba wao ndio wanaostahiki. Lakini ukweli ni kuwa Ahlu Al-Bait wa mwanzo walikuwa ndio watu wa mwanzo kuutetea ukhalifa kwa njia ya Shura, ndio maana Al-Imamu Al-Hasan bin Ali katika mkataba wake na Mu'awiya alishurutisha kwamba Mu'awiya akifa basi jambo la ukhalifa lifanyike kwa njia ya shura baina ya Waislamu. Mu'awiya alipokufa akarithiwa na mwanawe Yazid, basi hapo wafuasi wa Ahlu Al-Bait wakakasirika na wakasema kwamba Ahlu Al-Bait wana haki zaidi ya kulirithi jambo hilo la ukhalifa na hapo ndio ikaanza siasa hio ya kuwa Ahlu Al-Bait ndio wenye kustahiki kuurithi ukhalifa. Siasa hio ikaundiwa Hadithi na ikapotoshewa maana ya baadhi za Aya na baada ya muda ikawa ni mafunzo yatokayo kwa Allah na Mtume wake, ilhali jambo hilo lilikuwa halipo kamwe, bali ukisoma historia utaona kwa uwazi kwamba Shura ndio fikra iliokuweko katika zama za Ali na zama za Al-Hasan na wengine.

SURA YA TATU

KUHUSU AYA "NA WAONYE JAMAA ZAKO WA KARIBU"

Mwenyezi Mungu anasema:

وَأَنذِرْ عَشِيرَتَكَ الأَقْرَبِينَ

Na waonye jamaa zako wa karibu.[336]

Hii ni Aya nyengine muhimu katika jumla ya Aya ambazo Shia wanazitegemea katika dai lao la kuwepo wasia wa Allah na Mtume wake kwa Ali kwamba awe khalifa baada ya Mtume (s.a.w.). Katika Aya hii hatutokuwa na maelezo ya kilugha yenye kuhusiana na maudhui yetu, kwani hakuna katika Aya hii kitu ambacho kinapinga au kuunga mkono itikadi yao: hoja zote ziko katika riwaya tu ambazo zimesimuliwa kuhusiana na nini Mtume (s.a.w.) alikisema baada ya kuteremka Aya hii.

Aya hii ni katika Aya za mwanzo mwanzo kuteremka. Aya hii – kama unavyoona – inamuamuru Mtume (s.a.w.) awaonye jamaa zake wa karibu. Mtume (s.a.w.) alifanya hivyo. Lakini kilichopo ni tafauti ya riwaya juu ya nini Mtume (s.a.w.) alikitamka kuwambia watu wake baada ya kuteremka Aya hio. Kwa mujibu wa Shia, Mtume (s.a.w.) baada ya kuteremka Aya hio, aliwakusanya watu wa kabila lake la Banu Abdil-Muttalib bin Hashim, akawambia nani yuko tayari kuniunga mkono na kuwa pamoja nami na kunisaidia katika jambo hili (la kufikisha Uislamu) ili awe wasii wangu, ndugu yangu na khalifa wangu baada yangu? Watu wote wakanyamaza; Ali akanyanyuka – wakati bado ni mdogo – akakubali kumuunga mkono Mtume (s.a.w.). Na hapa kuna Hadithi moja tu iliokuja kwa *sanad* tafauti ambayo wanaitolea hoja hio.

[336] - Sura 26, Aya 214.

HADITHI

Katuhadithia Ibn Humaid katuhadithia Salama kanihadithia Muhammad bin Is-haq kutoka kwa Abdil-Ghaffar bin Al-Qasim kutoka kwa Al-Minhal bin Amri kutoka kwa Abdi-Llahi bin Al-Harith bin Naufal bin Al-Harith bin Abdil-Muttalib kutoka kwa Abdillahi bin Abbas kutoka kwa Ali bin Abi Talib kasema: 'Ilipomteremkia Aya hii: **"وَأَنذِرْ عَشِيرَتَكَ الأَقْرَبِينَ" (Na waonye jamaa zako wa karibu),** Mtume (s.a.w.) aliniita (mimi Ali) akaniambia Ewe Ali! Hakika ya Allah kaniamuru niwaonye jamaa zangu wa karibu…….Basi akasema (Mtume s.a.w. baada ya kuwakusanya jamaa zake): 'Enyi Bani Abdil-Muttalib! Hakika ya mimi *Wallahi* simjui kijana katika Waarabu aliyewajia watu wake na kitu bora kuliko nilichokujieni nacho mimi. Hakika mimi nimekujieni na kheri ya dunia na akhera na Allah kaniamuru nikulinganieni kwenye (kheri) hio. Nani katika nyinyi atanisaidia juu ya jambo hili ili awe ndugu yangu, wasii wangu na khalifa kwenu"…..*(Watu wote wakanyamaza na Ali akasema)*: "Mimi ewe Mjumbe wa Allah nitakuwa msaidizi wako juu yake (jambo hili). Basi (Mtume s.a.w.) akanishika shingo yangu na akasema: 'Huyu ni ndugu yangu, wasii wangu na khalifa wangu kwenu, basi msikilizeni na mumtii. Watu wakasimama huku wakicheka na kumwambia Abu Talib: 'Kakuamrisha umsikilize na kumtii mwanao![337]

Hadithi hii ndio ambayo Shia wanatolea ushahidi kwamba baada ya kuteremka Aya hio **"وَأَنذِرْ عَشِيرَتَكَ الأَقْرَبِينَ" (Na waonye jamaa zako wa karibu),** Mtume (s.a.w.) aliutangaza ukhalifa wa Ali bin Abi Talib. Nasi tunasema kwamba wakati tumo katika kulitafiti suala hili, basi inatubidi:

1) Kuitazama *sanad* ya riwaya hii.
2) *Matn* ya riwaya hii.
3) Riwaya nyengine zilizosimuliwa juu ya nini Mtume (s.a.w.) alikisema baada ya kuteremka Aya hio.
4) Kutazama *sanad* za riwaya hizo.
5) *Matn* za riwaya hizo.

[337] - Al-Tabari *Al-Taarikh* j. 2, uk. 228-229, na katika tafsiri yake *Jaami'u Al-Bayaan* j. 19, uk. 140, lakini katika tafsiri yake kuna maneno "Ili awe ndugu yangu" tu: maneno "Wasii wangu na khalifa kwenu" hayapo, na badala yake kuna maneno: "na kadha na kadha".

SANAD YA HADITHI HII

Ama ikiwa mimi na wewe tutastaajabishwa na kitu, basi natustaajabishwe na tatizo lenye kuendelea la ndugu zetu wa Kishia la kukombakomba kila Hadithi inayowafikiana na fikra zao hata ikiwa Hadithi hio ina udhaifu kiasi gani. Hadithi hii wanayoitegemea kuthibitisha dai lao hilo ni Hadithi dhaifu sana, kwani – tukianzia katika upande wa *sanad* – tunakuta kwamba katika *sanad* yake kuna:

1) Ibn Humaid. Jina lake ni Muhammad bin Humaid bin Hayyaan Al-Tamimi Al-Razi. Anasema Is-haq bin Mansur Al-Kawsaji kutoka kwa Ali bin Mihran akimzungumzia Muhammad bin Humaid: "Sijapata kuona mtu (anayejifanya) jasiri juu ya Mwenyezi Mungu (hamuogopi Mwenyezi Mungu) kuliko yeye: alikuwa akizichukuwa Hadithi za watu kisha akizigeuza". Na akasema tena: "Sijapata kuona mtu bingwa wa uwongo kuliko watu wawili – Sulaiman Al-Shaadhakuni na Muhammad bin Humaid". Na akasema Abu Abbas: …".Nimemsikia Ibn Khiraash anasema: 'Katusimulia Ibn Humaid na Wallahi alikuwa akisema uwongo". Na anasema Abu Hatim: "Imenifikia kutoka kwa Sheikh miongoni mwa *Khulqaniyyin* …. nilisimama nikamwambia mwenzangu: 'Hili (Ibn Humaid) ni jiongo halijui hata kudanganya". Na anasema Al-Nasai: "Si chochote si lolote" (yaani hana maana)". Akaulizwa: "Hata kidogo?" Akasema: "Hata kidogo". Na akasema katika sehemu nyengine: "Muhammad bin Humaid ni mwongo mkubwa". Na anasema Al-Bukhari: "Hadithi zake ni za kufikiriwa". Na akasema Abu Ali Al-Naysaaburi: "Nilimwambia Ibn Khuzaima lau ustaadh angesimulia Hadithi kutoka kwa Muhammad bin Humaid hakika ya Al-Imamu Ahmad amemsifu". Akasema: "Hakika yake hakumjua: kama angemjua kama tulivyomjua sisi basi asingemsifu". Na akasema Abu Nuim bin Adey: "Nimemsikia Abu Hatim Al-Razi nyumbani kwake na mbele yake alikuwepo Ibn Khiraash na kikundi cha mashekhe---- wakamtaja Ibn Humaid wakakubaliana kuwa yeye ni dhaifu sana katika Hadithi na kwamba anasimulia Hadithi wala hajaisikia (kwa mtu)". Na akasema Abu Qasim: "Nimemuuliza Abu Zur'a kuhusu Muhammad bin Humaid, akaniashiria kwa kidole chake mdomoni mwake. Nikamuuliza: "Mwongo?" Akatikisa kichwa chake: "Ndio" (mwongo). Nikamwambia alikwishakua mzee labda alikuwa

anafanyishiwa na kughushiwa, akasema: “Alikuwa anakusudia (kuzua uwongo)”.[338]

Pia yumo katika *sanad* hii:

2) Muhammad bin Is-haq, naye ni mwenye kughushi na juu ya hayo ni dhaifu. Maelezo yake ni marefu katika *Tahdhibu Al-Tahdhib*.[339] Na Hadithi hii ya Muhammad bin Is-haq – mwenye kughushi – hapa ni *mu’an’an*[340] **(مُعَنْعَنٌ),** nayo ni Hadithi dhaifu ikiwa itasimuliwa na mpokezi mwenye kughushi.

Pia yumo katika *sanad* hii:

3) Abdul-Ghaffar bin Al-Qasim (Abu Mar-yam), naye ni Shia gogo na ni dhaifu sana, mtunzi wa Hadithi za uwongo. Anasema Al-Dhahabi: “Rafidhi (Shia): si mwenye kuaminika”. Anasema Ali bin Al-Madini: “Alikuwa akitunga Hadithi”. Anasema Al-Bukhari: “Si madhubuti kwao (wanavyuoni wa Hadithi)”. Anasema Abu Daud: “Nashuhudia kwamba Abu Mar-yam (Abdul-Ghaffar bin Al-Qasim) ni mwongo”. Anasema Al-Imamu Ahmad bin Hanbal: “Alikuwa Abu ‘Ubaida akitusimulia kutoka kwa Abu Mar-yam (Abdul-Ghaffar bin Al-Qasim) watu husema hatumtaki (huyo)”. Wanasema Abu Hatim na Al-Nasai na wengine: “Hadithi zake zinaachwa”. Anasema Al-Dhahabi: “Shu’uba alipokea kutoka kwake ilipombainikia kwamba si mwenye kuaminika akamuacha”. Anasema Al-Ajurri: “Nimemuuliza Abu Daud kuhusu yeye akasema alikuwa akitunga Hadithi”. Anasema Al-Daraqutni: “Ni mwenye kuachwa”.[341]

Pia yumo katika *sanad* hii:

4) Al-Minhal bin Amri, naye si madhubuti. Anasema Abdullahi bin Ahmad: “Nimemsikia baba yangu akisema: “Shu’uba kamuwacha Al-

---

338 - Tazama *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 9 uk. 111 – 115, *tarjama* na. 181.

339 - J. 9, uk. 34-40, *tarjama* na. 50.

340 - Hadithu *mu’an’an* **(مُعَنْعَنٌ)** tumeielezea huko nyuma kwamba ni Hadithi ambayo msimulizi wake anatumia lafdhi: ((**فُلانٍ**)) **عَنْ *A’n Fulan*** (Kutoka kwa fulani).

341 - Tazama *Al-Dhahabi Al-Mizan* j. 3, uk. 354, *tarjama* na. 5147, na Ibn *Hajar Lisanu Al-Mizan* j. 4, uk. 42, *tarjama* na. 123.

Minhal (kaziwacha Hadithi zake) kwa kukusudia (si kwa bahati mbaya tu)". Na anasema Wahb bin Jarir kutoka kwa Shu'uba akisema: "Nilikwenda nyumbani kwa Al-Minhal nikasikia sauti ya gita (la muziki)". Na hivyo hivyo akasema Ibn Al-Madini. Na akasema Al-Ghallaabi: "Ibn Ma'iin alikuwa akimuangusha (akimponda) Al-Minhal (akimuona kwamba hafai)". Na akasema Al-Juzajani: "Mwenendo wake ni mbaya". Na akasema Al-Mughira "Hustaajabu wewe na huyu Al-A'amash mjinga, mimi nimemkataza asipokee Hadithi kutoka kwa Al-Minhal bin Amri na 'Abaya; tukaafikiana kwamba hatopokea kisha anapokea kutoka kwao. Nakuuliza kwa jina la Mwenyezi Mungu Mtukufu: je inafaa shahada ya Al-Minhal juu ya dirham mbili? Akasema: "E Mwenyezi Mungu! Haifai (Shahada yake)". Na akasema Al-Hakim: "Yahya bin Al-Qattaan kamtia kasoro Al-Minhal bin Amri". Na akasema Abu Al-Hasan bin Al-Qattaan: "Abu Muhammad bin Hazm alikuwa akimdhoofisha (akisema kuwa ni dhaifu) Al-Minhal".[342]

Kwa hivyo, baada ya haya, utaona kuwa Hadithi hii ni ya uwongo uliotungwa na bwana huyo wa Kishia aitwae Abdul-Ghaffar bin Al-Qasim, kisha wapokezi hawa madhaifu na wenye kughushi wakausimulia uwongo wake huo.

MATN YA HADITHI

Hakuna mwenye kuitazama *matn* ya Hadithi hii kwa utulivu kisha akailinganisha na Aya yenyewe akaweza kukubaliana na *matn* ya Hadithi hii, bali itambainikia kwa uwazi utunzi wa Hadithi hii. Tazama mambo yafuatayo:

1) Aya inamtaka Mtume (s.a.w.) awaonye jamaa zake wa karibu; wakati kwa mujibu wa Hadithi hii, Mtume (s.a.w.) hakuwaonya bali kawataka msaada.

2) Mtume (s.a.w.) – kwa mujibu wa Shia – katakiwa hapa autangaze ukhalifa wa Ali baada ya kuteremka Aya hio, yeye hakufanya hivyo moja

[342] - Tazama *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 10 uk. 283, *tarjama* na. 556.

kwa moja, bali kenda kutoa *offer* (tunuko) kwamba atayekubali kumsaidia ndiye atayekuwa wasii na khalifa. Kwa hivyo, Abu Lahab angekubali au mwengine yoyote yule angukuwa yeye ndiye khalifa. Ilivyo madamu hii ni amri ya Allah basi aseme tu kuwa silimuni enyi Banuu Abdil-Muttalib, na Allah kamchagua Ali kuwa ndiye khalifa wenu. Hili linamfanya kila anayetumia ubongo wake vizuri aone kwamba hii ni Hadithi ya kutunga.

3) Mtume (s.a.w.) katoa Ahadi – katika Hadithi hii – kwamba atayemsaidia basi atakuwa ndiye khalifa kwao. Tukiufasiri ukhalifa huu kuwa maana yake ni ukhalifa wa kuuongoza Umma wa Kiislamu – kama Shia wanavyosema – basi tunapata kwamba Ali kakubali kumsaidia Mtume (s.a.w.) lakini hakuwa khalifa baada yake – Ahadi ya Mtume (asiyetamka kitu kwa Matamanio: bali ni kwa wahyi) haikutimia! Je ni kweli Mtume (s.a.w.) anaahidi kutokea kitu kisha kisitokee, hasa hasa jambo kama hili la kufikisha ujumbe wa Allah?!

4) Hadithi inasema: "Huyu ni ndugu yangu, wasii wangu na khalifa wangu kwenu, basi msikilizeni na mumtii". Hivyo ndivyo Hadithi inavyotongoa, lakini cha kujiuliza ni kuwa vipi Mtume (s.a.w.) aseme maneno hayo kuwambia makafiri nao ni watu ambao yeye mwenyewe hawakumuamini: walikuwa wanamkadhibisha; sasa vipi tena awaamuru watu hao kuwa wamtii Ali ilhali yeye mwenye hawajamkubali kuwa ni Mtume wa kweli? Hii ni mantiki ya ajabu sana!

Hayo manne tulioyatanguliza ni kwa kuchukua kauli ya ndugu zetu wa Kishia kwamba hapa – katika Hadithi hii – Mtume (s.a.w.) alikuwa akiutangaza ukhalifa wa Ali. Vyenginevyo Hadithi hii – na nyengine kama tutavyoona, hata ikiwa ni Hadithi sahihi, basi – zinazungumzia ukhalifa wa kuisimamia familia ya Mtume (s.a.w.) tu: si ukhalifa wa kuuongoza Umma wa Kiislamu. Hadithi inasema: "Nani katika nyinyi atanisaidia juu ya jambo hili ili awe ndugu yangu, wasii wangu na khalifa kwenu". Na ikasema pia: "Huyu ni ndugu yangu, wasii wangu na khalifa wangu kwenu". Maneno "Khalifa wangu kwenu" Kiarabu chake ni: *"Khalifatii fii-kum"*, yaani katika nyinyi familia yangu. Na hivyo, ndivyo zilivyosema riwaya nyengine kwa uwazi, kama riwaya inayosema kuhusu tukeo hilo: "Nani atayenidhaminia dini yangu na miadi yangu na atakuwa pamoja

nami peponi na atakuwa khalifa katika *Ahli zangu (watu wangu)".*[343] Sasa cha kujiuliza ni kuwa je maneno haya wanaambiwa nani? Maneno haya wanaambiwa akina Abu Lahab – Makafiri. Na kwa hivyo Mtume (s.a.w.) anataka – kwa mujibu wa Hadithi hii ya kupakasa – msaada kutoka kwa makafiri, ili mmoja wao awe khalifa. Utaona wazi kwamba maneno sahihi ya riwaya hii ni yale tutayoyanukuu baadae kutoka kwa Al-Bukhari, Muslim, Al-Rabi'u bin Habib na wengine wengi, kwamba – baada ya kuteremka Aya hio – Mtume (s.a.w.) aliwahadharisha watu wake kutokana na adhabu ya moto na kwamba yeye hatowafaa kitu mbele ya Allah. Na mfano uko wazi katika Qur-an: Abu Lahab, Ami yake, ataingia motoni wala Mtume (s.a.w.) hawezi kumfaa kitu.[344]

TAKHRIJ NA MAELEZO

Hadithi hio tulioijadili hapa au mfano wa Hadithi hio kaipokea tena Ibn Jarir katika kitabu chake hicho hicho,[345] lakini huku maneno yake ni tafauti kidogo: huku Sayyidna Ali aliulizwa tu: "Ni kitu gani wewe kimekufanya umrithi bin Ami yako (Mtume s.a.w.) pasina ami zako (kumrithi yeye)". Sayyidna Ali akasimulia kisa hicho cha kukusanyika Banuu Abdil-Muttalib, kisha akanukuu maneno ya Mtume (s.a.w.) aliposema:

> Nani katika nyinyi atanibaii ili awe ndugu yangu, sahibu yangu na mrithi wangu? Hakuna aliyesimama; nikasimama mimi na nilikuwa ndiye mdogo wao…..Basi kwa sababu hio ndio nimemrithi bin Ami yangu (Mtume s.a.w.) pasina ami zangu (kumrithi yeye).

Nayo ni Hadithi ambayo *matn* yake ni yenye *mushkila*, kwani:

a) Ikiwa kurithi huku ni kurithi mali, Ali hakumrithi Mtume (s.a.w.) chochote.[346]

---

[343] - Ibn Asaakir *Taarikh Dimashq* j. 4, uk. 23, riwaya na. 837, na Al-Imamu Ahmad *Fadhailu Al-Sahaba* j. 2, uk. 807-808, Hadithi na. 1108.

[344] - Kama Uahlu Al-Bait unafaa, basi mtoto wa Nabii Nuh asingeliingia motoni! Ni wazi kwamba Allah anatazama usalama wa moyo na usafi wa matendo tu.

[345] - Ibn Jarir *Al-Taarikh* j. 2, uk. 229-330.

[346] - Na hili la kuwa Mitume (a.s.) hairithiwi, nilizungumza na Shia wakalipinga. Cha ajabu ni kuwa Hadithi hio ya kuwa Mitume hairithiwi imo katika *Al-Kafi* cha Al-Kuleini,

b) Ikiwa ni kurithi ukhalifa – nao labda ndio unaokusudiwa hapa basi – Ali hakumrithi Mtume (s.a.w.) ukhalifa pia, bali khalifa baada yake ni Abu Bakr.

c) Ikiwa ni kumrithi elimu na ujuzi. Basi hakuna yoyote mwenye elimu na ujuzi wa Mtume (s.a.w.) japokuwa Shia wanataka kumpachika Ali na Maimamu wao sifa hio ya kwamba walikuwa na elimu kama ya Mtume (s.a.w.).[347]

Na kwa ujumla, zingatia hapa Ahadi hii ya Mtume (s.a.w.) – ambayo pia iko katika Hadithi ya mwanzo – Hadithi hapa inasema: "Nani katika nyinyi atanibaii ili awe ndugu yangu, sahibu yangu na mrithi wangu? Hii – kwa ujumla – ni ahadi ya kuwa atayembaii atakuwa khalifa baada yake. Ali alimbaii, je alikuwa khalifa – ahadi ya Mtume (s.a.w.) imekwenda wapi?! Hii ni alama ya uzushi wa wazi wa Hadithi hii.

Ama katika *sanad* ya Hadithi hii ya pili, tunaona kwamba kuna Zakariyya bin Yahya Al-Dharir. Naye, dhahir ni kuwa, ni *Majhulu Al-hal* hali yake haijulikani (je ni mpokezi sahihi au vipi), kamtaja Al-Khatib Al-Baghdadi katika *Taarikh Baghdad* bila ya kutaja kwamba ni dhaifu au mwenye kuaminika.[348]

Pia yumo katika *sanad* ya Hadithi hio:

---

na Al-Imamu Al-Khomeni kasema kuwa ni Hadithi sahihi. Tazama Al-Khomeni *Al-Hukumatu Al-Islamiyya* uk. 143. Kweli Hadithi hio ya *Al-Kafi* haikutumia lafdhi "Mitume hairithiwi" lakini maana bila shaka ni hio kwani inasema: "Hakika ya Mitume hawakurithisha dinari wala dirhamu, lakini imerithisha elimu, basi atayeichukua na aichukue kwa wingi". Tazama Al-Kuleini *Al-Kafi* j. 1, uk. 83, Kitabu Al-'ilmi, mlango Thawabu Al-'aalim wal Muta'allim, Hadithi na. 1. Na katika uk. 79-80, mlango Sifatu Al-'ilmi wa Fadhlihi wa Fadhlu Al-'ulamaa. Hadithi na. 2. *Sanad* hii ya pili ni dhaifu, lakini *matn* yake ni sahihi kwani ni sawa na *matn* ya Hadithi ya mwanzo, ambayo ni sahihi.

[347] - Na hii ni ajabu kubwa sana: kumfanya mtu asiyepata wahyi kuwa sawa au kuliko Nabii. Mmoja wao (naye ni Sh. X mwenye makala zilizo mwisho wa kitabu hiki) niliwahi kujadiliana naye juu ya suala hili na akanitolea Hadithi za uwongo zilizojaa wapokezi waongo na madhaifu, nikamjibu juu ya Hadithi zake hizo jawabu ambayo natarajia kuitoa katika kijitabu kidogo au kuiunganisha na vitabu vyengine vijavyo *In shaa Allah*.

[348] - Al-Khatib Al-Baghdadi *Al-Taarikh* j. 8, uk. 459, *tarjama* na. 4571.

Abu Sadik Al-Azdi Al-Kufiy. Ya'aqub bin Abi Shaiba anasema ni "Mwenye kuaminika". Lakini Ibn Sa'ad anasema: "(Wanavyuoni wa wapokezi) wanamsema (wanamtia kasoro)".[349] Naye mpokezi huyu ni wa kule kule mjini Al-Kufa. Huko kunatisha sana jamani!

Pia yumo katika *sanad* ya Hadithi hio:

Rabia bin Naajidh. Naye pia ni bwana wa Ki-kufa: hajulikani au anakaribia kuwa hajulikani. Anasema Al-'Ijli: "Tabii mwenye kuaminika". Lakini Al-Dhahabi anasema: "Anakaribia kuwa hajulikani".[350] Ninasema: Ibn Hajar anasema kwamba mtu huyu hana ila Hadithi moja katika *Sunan Ibn Maja* na Hadithi moja katika *Al-Khasais* cha Al-Nasai. Ni wazi kwamba huyu ni mpokezi mwenye Hadithi chache sana na kwa hivyo kitendo cha Al-'Ijli cha kumwita mpokezi huyu kuwa ni mwenye kuaminika ni kosa la kiminhaj (Methodological error), na kimetokana na kawaida ya Al-'Ijli – kama Ibn Hibbaan – cha kuwaita wapokezi dhaifu na wasiojulikana kuwa ni wenye kuaminika.[351] Kwa hali yoyote ile Hadithi hii, ni ya utunzi wa wazi: haikuthibiti *sanad* yake kwa kuwa na wapokezi wasiojulikana; wala haikuthibiti *matn* yake kwa kutokukubaliana na hali ilivyo na matokeo yalivyotokea, bali pia na kwa kutokukubaliana kwake na Aya yenyewe tunayoijadili hapa.

---

[349] - Tazama *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 12, uk. 143, *tarjama* 605.

[350] - Tazama *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 3, uk. 228, *tarjama* na. 498.

[351] - Kwa mfano mpokezi aitwae Hisham bin Sa'ad Al-Madani. Wanavyuoni wa wapokezi wanakaribia kukubaliana kuwa ni dhaifu. Lakini Al-'Ijli anasema: "Hadithi zake zinafaa, naye Hadithi zake ni *hasan".* Mpokezi aitwae Al-Walid bin Qais bin Al-Akhram. Mpokezi huyu Al-Bukhari na Ibn Abi Hatim wamemtaja bila ya kubainisha hali yake, na kwahivyo ni *majhulul haal*. Lakini Ibn Hibbaan kamtaja katika kitabu cha wapokezi wenye kuaminika *Al-Thiqaat* na Al-'Ijli akasema: "ni mwenye kuaminika". Mpokezi aitwae 'Aasim bin Shumaikh. Mpokezi huyu, Ibn Hibbaan kamtaja katika kitabu cha wapokezi wenye kuaminika *Al-Thiqaat* na Al-'Ijli akasema: "ni mwenye kuaminika". Wakati wao watongoa hivyo, Abu Hatim anena: "*majhul (hajulikani)",* na Al-Bazzaar atongoa: "si mwenye kutambulika". Hio ni mifano mitatu; mifano iko mingi, na kwa hivyo, *minhaj (methodology)* ya Al-'Ijli isikushituwe sana ni sawa sawa na ile ya Ibn Hibbaan, na hilo limenenwa na wenye ujuzi.

HADITHI NYENGINE: kama hio, kaisimulia Al-Tha'alabi,[352] lakini katika *sanad* yake kuna Al-Hasan bin Ali bin Shabib. Kasifiwa na wengi; na wengine wakamponda. Na maelezo yake ni marefu katika *Lisanu Al-Mizan*,[353] lakini baada ya kuyatazama yote yaliosemwa utaona kuwa aliyetoa ufafanuzi mzuri ni Abdullahi bin Ahmad bin Hanbal kwamba: "Hakusudii kusema uwongo lakini alifuatana na watu miongoni mwa Wabaghdadi ambao walikuwa wakizidisha (katika Hadithi) na kuzinasibisha (na Mtume s.a.w. Hadithi ambazo hazitoki kwake)..na (tabia) hii ilikuwa hasa hasa kwa watu wa Baghdadi".

Pia yumo katika *sanad* hio:

'Abbad bin Ya'aqub, naye ni Shia mkubwa, mwenye siasa kali wa kule mjini Al-Kufa. Na anasimulia Hadithi munkar katika mambo ya fadhila na mambo ya kuwatia aibu Masahaba. Na kwa hivyo, wapokezi wengine wa Hadithi walimuacha.[354]

Pia yumo katika *sanad* hio:

Al-Sabbaah bin Yahya. Naye – kama tulivyomuelezea kabla – pia ni Shia wa Al-Kufa na ni dhaifu.[355] Imeelezwa katika *Al-Mizan* na *Lisanu Al-Mizan* kwamba Al-Sabbaah bin Yahya "Ni mwenye kuachwa, bali ni mwenye kutuhumiwa (kwa kutunga Hadithi)". Anasema Al-Bukhari: *"fihi nadharun* **فِيْهِ نَظَرٌ"** "Ni mtu wa kufikiriwa".[356]

Pia yumo katika *sanad* hio:

---

352 - Al-Tha'alabi *Al-Kashfu Wa Al-Bayaan* j. 8, uk. 182.

353 - J. 2, uk. 221-225.

354 - Tazama *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 5, uk. 95-96, *tarjama* na. 183.

355 - *Tarjama* yake ni fupi katika *Al-Mizan* cha Al-Dhahabi j. 3, uk. 20, *tarjama* 3850, na Ibn Hajar *Lisanu Al-Mizan* j. 3, uk. 180, *tarjama* na. 729.

356 - Tumesema Al-Bukhari anapotumia *lafdhi* hii humaanisha kwamba mpokezi huyo ni dhaifu sana.

Zakaria bin Maisara. Katajwa katika *Tahdhibu Al-Tahdhib*[357] bila ya kusemwa hali yake. Na kwa hivyo, ni *Majhulu Al-hal* (Hali yake haijulikani).

Pia yumo katika *sanad* hio:

Abu Is-haq, jina lake ni Amru bin Abdillahi bin Ubaidi-Llahi, Al-Sabi'i Al-Kufiy. Naye pia ni Shia wa kule mjini Al-Kufa, naye ni dhaifu mwenye kughushi na Hadithi yake hapa ni *mu'an'an.* Anasema Ibn Hibaan katika kitabu *Al-Thiqaat*: "Alikuwa akighushi". Na anasema Ma'an: "Wamezifisidi Hadithi za watu wa Al-Kufa Al-A'amash na Abu Is-haq (yaani kwa kughushi). Na Husain Al-Karaabisi na Abu Ja'afar Al-Tabari wamemtaja kuwa ni miongoni mwa wapokezi wenye kughushi.[358] Na imeelezwa katika kitabu *Jami'u Al-Tahsil Fii Ahkami Al-Marasil*[359] kuwa Abu Is-haq ni "Mwenye kukithiri kughushi". Na akasema Jarir bin Abd Al-Hamid: "Nimemsikia Mughira akisema: 'Amewaangamiza watu wa Al-Kufa Abu Is-haq na Aamash wenu huyu".[360]

Natija ni kuwa huu ni uwongo uliotoka huko mjini Al-Kufa, wapokezi wake ni hao Mashia, watunzi wa Hadithi, wenye kughushi, waongo na dhaifu.

RIWAYA NYENGINE: imesimuliwa na Ibn Asaakir, na Al-Imamu Ahmad. Lafdhi ya riwaya hio inasema:

> Nani atayenidhaminia dini yangu na miadi yangu na atakuwa pamoja nami peponi na atakuwa khalifa katika *Ahli zangu* (watu wangu).[361]

---

357 - J. 3, uk. 621.

358 - Tazama *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 8 uk. 56.

359 - Uk. 245, nukulu kutoka katika kitabu *Mizanu Al-Qist* cha Sh. Ali Al-Hijri, uk . 154.

360 - Na huenda ikawa kuna wapokezi wengine dhaifu au wasiojulikana sikuweza kuwaona kwa haraka haraka.

361 - Ibn Asaakir *Taarikh Dimashq* j. 4, uk. 23, Hadithi na. 837, na Al-Imamu Ahmad katika *Fadhaailu Al-Sahaba* j. 2, uk. 807-808, Hadithi na. 1108, na uk. 871, Hadithi na. 1196, na Ahmad vile vile katika *Al-Musnad* j. 1, uk. 324, Hadithi na. 883. Hadithi hii natarijia kwamba ina msururu wa wapokezi dhaifu au wasiojulikana, lakini kwa sasa sitaki kupoteza wakati kumpekuwa mmoja mmoja, ninataja wale niwajuao tu.

Lakini *sanad* yake haifurahishi, kwani yumo ndani yake Sharik. Naye ni Sharik bin Abdillah naye ni dhaifu: "Ana hifdhi mbaya sana……..ni mwenye kukosea sana…..…ni mwenye kuchanganyikiwa….si madhubuti…Hadithi zake zinagongana… mashuhuri kwa kughushi".[362] Na Hadithi ya Sharik hapa ni *muan'an.*

Pia yumo humu:

Al-A'amash. Naye ni Sulaiman bin Mihran. Tumemuelezea kabla, naye ni Shia wa Al-Kufa mashuhuri kwa kughushi Hadithi dhaifu. Na hapa Hadithi yake ni *mua'na'n.*[363]

Pia yumo humu:

Al-Minhal. Naye ni Al-Minhal bin Amri, naye hakukubalika. Tumemuelezea kabla. Tazama maelezo yake katika *sanad* ya Hadithi ya kwanza mpokezi na. 4.

Pia yumo humu:

Abbad bin Abdillahi Al-Asadi. Naye pia ni msimulizi wa Kishia wa kule kule mjini kwetu Al-Kufa. *Tarjama* yake ni fupi katika *Tahdhibu Al-Tahdhib.*[364] Anasema Al-Bukhari: **"فِيْـهِ نَظَرٌ"** "Ni mtu wa kufikiriwa". Anasema Ali bin Al-Madini: "Hadithi zake ni dhaifu". Anasema Al-Imamu Ahmad: "Hadithi zake ni munkar".

Hio ni *sanad* ya Ibn Asaakir na Al-Imamu Ahmad katika sehemu moja miongoni mwa sehemu mbili za kitabu chake *Fadhailu Al-Sahaba* na pia katika kitabu chake *Al-Musnad*. Kisha katika *sanad* ya Al-Imamu Ahmad kuna balaa nyengine ya ziada, nayo ni Yahya bin Abdil-Hamid Al-Himmani, naye pia ni Shia wa mjini Al-Kufa. *Tarjama* yake ni refu sana

[362] - Tazama vipande hivyo vya nukulu katika *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 4, uk. 293-296, *tarjama* na. 587.
[363] - Tazama *Taqribu Al-Tahdhib* uk. 254, *tarjama* na. 2615, na *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 4 uk. 195, *tarjama* na. 386.
[364] - J. 5, uk. 86, *tarjama* na. 165

katika *Tahdhibu Al-Tahdhib*.[365] Ufupisho wake ni kuwa alikuwa "Al-Imamu Ahmad anasema kuwa kasema uwongo". Na hii ni kuwa alikuwa bwana huyu akisema Al-Imamu Ahmad kanisimulia Hadithi hii, Al-Imamu Ahmad akiulizwa anasema si kweli mimi sijamsimulia. Na akasema Ibn Numair: "Al-Himmani ni mwongo". Kwa urefu tazama marejeo niliokupa. Ama Hadithi ya pili ya Al-Imamu Ahmad,[366] *sanad* yake ni hio hio. Kwa hivyo, riwaya hii ni ya kufinyanga![367]

RIWAYA NYENGINE: imesimuliwa na Ibn Abi Hatim.[368] Yumo katika *sanad* ya riwaya hii:

Abdullahi bin Abi Quddus. Naye ni Shia dhaifu sana. Anasema Ibn Ma'iin: "Si chochote si lolote (hana maana) Rafidhi (Shia) khabithi". Na anasema Muhammad bin Mihran: "Hakuwa na maana…..alikuwa kakaa kama mwenda wazimu, watoto wakimfuata huku wanamzomea". Na akasema Abu Daud: "Hadithi zake ni dhaifu". Na akasema Al-Nasai: "Dhaifu….si mwenye kuaminika". Na akasema Al-Daraqutni: "Dhaifu". Na akasema Ibn Adey: "Hadithi zake zote ni kuhusu fadhila za Ahlu-lbait".[369]

Pia yumo humu:

Al-A'amash. Tumemuelezea kabla kidogo, katika *sanad* iliotangulia, rejea umtazame.

RIWAYA NYENGINE: imesimuliwa na Al-Baghawi.[370] Lakini katika *sanad* yake kuna:

---

[365] - J. 11, uk. 213-218, *tarjama* na. 399.

[366] - Nayo ni Hadithi na. 1196.

[367] - Na huenda ikawa kuna wengine wengi dhaifu au wasiojulikana katika *sanad* ya Ibn Asaakir, hao tuliowataja wanatosha.

[368] - Ibn Abi Hatim *Tafsiru Al-Qur-ani Al-'Adhim* j. 9, uk. 2826, Hadithi na. 16015. Nayo pia riwaya hii huenda ikawa ina wapokezi wengi dhaifu, kwa sasa sitaabiki kuwapekuwa: nataja wale waliokaribu na kumbukumbu yangu tu.

[369] - Tazama habari za Abdullah bin Abdil-quddus katika Tahdhibu Al-Tahdhib j. 5 uk. 265, *tarjama* na. 516.

[370] - Al-Baghawi *Ma'aalimu Al-Tanzil* j. 3, uk. 480, Hadithi na. 1579.

Muhammad bin Is-haq. Naye ni dhaifu na ni mwenye kughushi na Hadithi yake hapa ni *mua'na'n.*[371]

Pia yumo humu:

Abdul-Ghaffar bin Al-Qasim. Naye ni Shia wa mjini Al-Kufa, mtunzi wa Hadithi za uwongo.[372]

Pia yumo humu:

Al-Minhal bin Amri. Naye pia si madhubuti.[373]

Hizo ndizo riwaya, walizozitegemea Shia katika dai lao kwamba ilipoteremka Aya hio: **"وَأَنذِرْ عَشِيرَتَكَ الأَقْرَبِينَ" "Na waonye jamaa zako wa karibu"**,[374] Mtume (s.a.w.) aliutangaza ukhalifa wa Ali. Utaona kwamba mbali na kuwa hizi ni riwaya za kutunga: zilizotungwa huko mjini Al-Kufa – kwani kila *sanad* ina wasimulizi wa Kishia wa Al-Kufa, waongo watunzi wa Hadithi – Hadithi hizi hazijengi hoja hio hata zingelikuwa sahihi, kwani Hadithi zote hizi zinasema: "Na atakuwa khalifa katika *Ahli zangu* (watu wangu)" na Hadithi ya kwanza inasema: "Na atakuwa khalifa kwenu (yaani kwa Banii Abdul-Muttalib bin Hashim)". Kwa hivyo, huu si ukhalifa wa umma ambao ulikuwa ukitangazwa hapa bali ni ukhalifa wa kuisimamia familia yake, bila shaka baada ya kufa kwake au wakati wa kutokuwepo kwake.[375] Na hayo, lau tukijaalia kuwa Hadithi hio ni sahihi, vyenginevyo tumeona kwamba ni Hadithi ambazo *sanad* zake ni kiza na *mutun* zake ni *Hashiman tadhruhu Al-riyaah* **(**Majani makavu yanayopeperushwa na upepo).

---

371 - Tumemuelezea kabla, rejea *sanad* ya Hadithi ya kwanza mpokezi na. 2.

372 - Tumemuelezea kabla, rejea *sanad* ya Hadithi ya kwanza mpokezi na. 3.

373 - Tumemuelezea kabla, rejea *sanad* ya Hadithi ya kwanza mpokezi na. 4.

374 - Sura 26, Aya 214.

375 - Utaona katika juzuu ya pili *In shaa Allah* maelezo yetu kuhusu Hadithi isemayo: **"Wewe nafasi yako kwangu ni kama nafasi ya Haruna kwa Musa…"** na Hadithi isemayo: **"Yule ambaye mimi ni mawla wake na Ali ni Mawla wake"** kwamba Hadithi zote hizi zina maana tafauti kabisa na madai ya Shia.

MANENO SAHIHI ALIOYATAMKA MTUME (S.A.W.) BAADA YA KUTEREMKA AYA HIO

Baada ya kuona riwaya hizo za kutunga juu ya nini inadaiwa kuwa Mtume (s.a.w.) alisema baada ya kuteremka Aya hio, sasa tunakunukulia maneno sahihi alioyatamka Mtume (s.a.w.), kisha kabla ya kutazama *sanad* za riwaya hizi, tazama maneno hayo yaliomo katika riwaya hizo, halafu yalinganishe na Aya inavyosema, basi hata ukiwa hujasoma hata *alifu* utajua ukweli ni upi.

Aya inasema: **"Na waonye jamaa zako wa karibu".** Kuonya inaeleweka nini maana yake. Riwaya zinasema:

> Ilipoteremka Aya hii: **"وَأَنذِرْ عَشِيرَتَكَ الأَقْرَبِينَ ((Na waonye jamaa zako wa karibu)),** Mtume (s.a.w.) akawa anayapitia makabila ya Kikureishi kabila moja moja mpaka akafika katika kabila la Banii Abdil Muttalib akasema: 'Enyi Banii Abdul Muttalib! Hakika Allah ameniamuru nikuonyeni, basi mimi sikufaeni kitu kutokana na Allah (huko akhera). Basi jueni kwamba vipenzi vyangu miongoni mwenu ni wacha Mungu.[376] Basi jueni kwamba wasinijie watu kesho (akhera) na dini (yao) mukanijia nyinyi na dunia munaibeba shingoni mwenu. Ewe Fatima binti Muhammadi! Na ewe Safiyya shangazi ya Muhammad zikomboweni nafsi zenu kutokana na (adhabu ya) Allah: mimi sikufaini kitu mbele ya Mwenyezi Mungu.[377]

---

[376] - Sio vipenzi vyangu ni Ahlu Al-Bait hata wakiwa wauaji au walevi! Bali vipenzi vya Mtume (s.a.w.) – kama Qur-ani ilivyoamuru – ni wacha Mungu tu.

[377] - Allahu Akbar, Allahu Akbar, Allahu Akbar! Tazama Hadithi ya haki! Wallahi ukiitamka ina nuru na mwili unakusisimka! Lafdhi hii nimeinukuu kutoka katika *Al-Jaami'u Al-Sahih* cha Al-Rabi'u bin Habib, uk. 381, Hadithi na. 1005. Hadithi hio kaisimulia pia Al-Tha'alabi katika *Al-Kashfu Wa Al-Bayan* j. 8, uk. 182, na mfano wake imo katika Al-Tabari *Al-Taarikh* j. 2, uk. 230, na Ibn Abi Hatim katika *Tafsiru Al-Qur-ani Al-'Adhim* j. 9, uk. 2825, Hadithi na. 16011-16012-16014, na Al-Bukhari katika *Al-Sahih* Hadithi na. 4771, na katika kitabu chake chengine *Al-Taarikh Al-Awsat* j. 1, uk. 86, Hadithi na. 214, na Muslim katika *Sahihu Muslim* uk. 105, Hadithi na. 204-245-246, na Ahmad *Al-Musnad* j. 8, uk. 356, Hadithi na. 26051, Al-Nasai katika *Al-Kubra* j. 10, uk. 207, Hadithi na. 11312-11313, na katika j. 6, uk. 159-161, Hadithi na. 6438-6439-6440-6441-6442, na Ibn Asaakir katika *Taarikh Dimashq* j. 37, uk. 149, Hadithi na. 7635, na Al-Tirmidhi *Al-Sunan* uk. 849, Hadithi na. 3184-3185, na Al-Tabarani katika *Al-Awsat* j. 8, uk. 238, Hadithi na. 8511, na Al-Tahhaawi katika *Sharhu Ma'aani Al-Athaar* j. 3, uk. 285, Hadithi na. 5388-5390, na pia kaipokea Hadithi hio Al-Baghawi katika tafsiri yake

SANAD YA HADITHI

Hadithi hii imekuja kwa njia na *sanad* tafauti, lakini kwa hapa tutatazama *sanad* tatu: mbili katika hizo ni kwa njia moja ya Al-Zuhri, na *sanad* moja ni kwa njia ya Al-A'araj: na zote ni *sanad* zenye kutufikisha kwa Abu Huraira (r.a.).

Kutoka kwa Al-Zuhri, Hadithi hio kaipokea Al-Tahhaawi[378] kwa *sanad* mbili. Moja ya hizo ni hii:

> Katuhadithia Yunus kasema katwambia Ibn Wahb kasema katwambia Yunus kutoka kwa Ibn Shihab kasema kaniambia Said bin Al-Musayyib na Abu Salama bin Abdil-Rahman kwamba Abu Huraira (r.a.) kasema…..*Kisha inafata Hadithi.*

Na mfano wake – *kisanad* na *matn* – ni riwaya ya Al-Nasai katika *Al-Kubra.*[379]

1) Yunus – mpokezi wa kwanza – ni Yunus bin Abdil-A'alaa, naye ni Imamu, mcha Mungu, mwingi wa elimu na ni mwenye kuaminika.[380]
2) Ibn Wahb – mpokezi wa pili – ni Abdullah bin Wahb bin Muslim Al-Qurashi, naye ni mwenye kuaminika, Imamu bingwa lakini anaghushi. Anasema Ibn Sa'ad: "Alikuwa mwingi wa elimu,

---

Ma'aalimu Al-Tanzil j. 3, uk. 482, Hadithi na. 1571582, na Ibn Jarir Al-Tabari katika *Jaami'u Al-Bayaan* j. 19, uk. 136-142 kwa *sanad* si chini ya kumi na nne, na Ibn Manda katika *Al-Aymaan* j. 2, uk.875-8832 Hadithi na. 933 hadi kufikia Hadithi na. 948, na Al-Bayhaqi katika *Al-Kubra* j. 9, uk. 393, Hadithi na. 12913-12914, na wengine wengineo. Nayo hii ndio Hadithi sahihi kwa *matn* na *sanad*. **TANBIHI:** Si kwamba wapokezi wote hawa wameisimulia riwaya hio kwa lafdhi moja: mwengine utakuta lafdhi moja; mwengine muna tafauti ndogo, lakini zote maana ni moja.

[378] - Al-Tahhaawi *Sharhu Ma'aani Al-Athaar* j. 3, uk. 285-286, Hadithi na. 5390. Na pia wameipokea wapokezi wengine wengi lakini kwa hapa tunatazama hii *sanad* moja ya Al-Tahhaawi tu.

[379] - Al-Nasai *Al-Kubra* j. 6, uk. 160, Hadithi na. 6440.

[380] - Ibn Hajar *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 11, uk. 387, *tarjama* na. 754.

mwenye kuaminika ikiwa atasema: 'Katuhadithia'[381] na alikuwa ni mwenye kughushi".[382] Katika *sanad* hii, Ibn Wahb kasema: "Kaniambia" na kwa hivyo, riwaya yake hapa inakubalika.

3) Yunus (mwengine) – mpokezi wa tatu – ni Yunus bin Yazid bin Abi Al-Nijaad, naye kadhoofishwa na Al-Imamu Ahmad na Ibn Sa'ad. Na wengine – kama Ibn Mai'n, Al-'Ijli, Al-Nasai na wengine wakamsifu kuwa ni mwenye kuaminika. Kanuni – kwa mujibu wa *Jumhur* – ni kutanguliza kauli ya wenye kusema kuwa ni mpokezi dhaifu hasa hasa ikiwa udhaifu wake umebainishwa. Lakini baada ya kuyatazama maneno ya wote – hata maneno ya Al-Imamu Ahmad mwenyewe – utaona kwamba Yunus bin Yazid huyu hakupondwa kwa uwongo au ufasiki, bali yeye ni mtu mkweli lakini mwenye hifdhi mbaya. Na hiki ndicho alichokisema Waki'i: "Nimemuona Yunus bin Yazid Al-Ayli na alikuwa na hifdhi mbaya".[383] Na kwa hivyo, Al-Hafidh Ibn Hajar anasema: "Ni mwenye kuaminika, isipokuwa riwaya zake kutoka kwa Al-Zuhri anasahau kidogo".[384]
4) Ibn Shihab – mpokezi wa nne – ni Al-Zuhri au kwa jina kamili ni Muhammad bin Muslim bin Ubaidi-Llahi bin Shihab Al-Zuhri, naye ni Imamu mwingi wa elimu mwenye kuaminika. *Tarjama* yake ni refu katika *Tahdhibu Al-Tahdhib*.[385] Ufupisho wake ni ule aliousema Ibn Hajar katika *Taqribu Al-Tahdhib* kwamba ni "Faqihi (Mwanachuoni wa fiq-hi) aliyeafikiwa katika utukufu wake na uwezo wake".[386] Lakini bila kusahau kwamba Al-Zuhri pamoja na ubingwa wake na uimamu wake alikuwa na kasoro mbili ambazo kwazo kapata lawama. Moja ni kujikurubisha kwa watawala wa Banii Umayya. La pili ni kughushi baadhi ya wakati. Anasema Al-Dhahabi: "Ni hafidh, hujja, alikuwa nadra (mara chache)

---

[381] - Yaani alikuwa ni mtu mwenye elimu na uwezo wa kuhifadhi lakini anaghushi na kwa hivyo ikiwa katika riwaya yake atatumia lafdhi "Katuhadithi au kanihadithia" basi riwaya yake hio inaaminika.

[382] - Tazama *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 6, uk. 65, *tarjama* na. 141.

[383] - Tazama *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 11, uk.395-396, *tarjama* na. 770.

[384] - Ibn Hajar *Taqrib* uk. 614, *tarjama* na. 7919.

[385] - Tazama *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 9, uk. 395-399, *tarjama* na. 734.

[386] - Ibn Hajar *Taqrib* uk. 506, *tarjama* na. 6296.

akighushi".[387] Ama kosa la mwanzo basi linatufanya tuziepuke riwaya zake za kisiasa tu ambazo zinawaunga mkono watawala hao. Ama ghushi – ni kama tulivyoeleza katika kitabu chetu *Ushahidi Uliowekwa Wazi* na vyengine kwamba – kanuni ni kuwa mwenye kughushi akiwa ni imara katika Hadithi, basi Hadithi yake inakuwa dhaifu ikiwa Hadithi hio ni *mu'an'an* **(مُعَنْعَنُ)** au ikiwa Hadithi hio ni **"مُؤَنَّنٌ** *muannan***".***[388]*** Pia zinaingia hapa namna zote za masimulizi atazozitumia msimulizi huyo mwenye kughushi, ikiwa namna hizo hazimaanishi kuwa yeye kaisikia Hadithi hio moja kwa moja kutoka kwa msimulizi aliye kabla yake. Al-Zuhri – katika *sanad* za Hadithi hii – amesema kwa uwazi kwamba: "Kaniambia". Kwa hivyo, Hadithi yake hapa inakubalika. Said bin Al-Musayyib – mpokezi wa tano – ni mfuasi wa Masahaba maarufu, naye ni Imamu mkubwa mwenye kuaminika bila khilafu yoyote, na katika waliopokea Hadithi kutoka kwa Abu Huraira, yeye ndiye imara kuliko wote.[389] Na Said bin Al-Musayyib kashirikiana katika kuisimulia riwaya hii pamoja na Abu Salama bin Abdil-Rahman, naye pia ni Imamu, mwingi wa elimu mwenye kuaminika.[390] Na Said bin Al-Musayyib na Abu Salama bin Abdil-Rahman wameisimulia Hadithi hii kutoka kwa Abu Hurara, naye ni Sahaba Mtukufu (r.a.). Kwa hivyo, *sanad* hii ina udhaifu mdogo sana kwa sababu ya kile alichokisema Al-hafidh Ibn Hajar kwamba Yunus bin Yazid Al-Ayli miongoni mwa waliomo katika *sanad* hii: "Ni mwenye kuaminika, isipokuwa riwaya zake kutoka kwa Al-Zuhri anasahau kidogo".

Na kwa ufupi ni kuwa Al-Zuhri anaisimulia Hadithi hii kutoka kwa "Said bin Al-Musayyib na Abu Salama bin Abdil-Rahman kutoka kwa Abu Huraira (r.a.)"... Njia hii ya Al-Zuhri, ina *sanad* nyingi baadhi yake ni dhaifu sana na nyengine ni dhaifu kidogo. Lakini Hatimae tunamkuta Muslim anaisimulia Hadithi hii kwa:

---

387 - Al-Dhahabi *Al-Mizan* j. 5, uk. 165, *tarjama* na. 8171.

388 - Hadithi ***"Muannan"*** ni Hadithi ambayo msimulizi wake anatumia herufi: **"أَنَّ"** *"Anna".*

389 - Na Hadithi hii kaipokea kutoka kwa Abu Huraira.

390 - Ibn Hajar *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 12, uk.127, *tarjama* na. 536.

Njia ya pili: Nayo ni:

> Kanisimulia Amru Al-Naqid katusimulia Mu'awiya bin 'Amri katusimulia Zaaida katusimulia Abdullahi bin Dhakwaan kutoka kwa Al-A'araj kutoka kwa Abu Huraira kutoka kwa Mtume (s.a.w.)….

1) Amru Al-Naqid – mpokezi wa kwanza – ni Amru bin Muhammad bin Bukair bin Saabur Al-Naqid na wengine humnasibisha pia na babu yake na kumwita Amru bin Bukair bin Saabur Al-Naqid kama ilivyo katika *Taqribu Al-Tahdhib*.[391] Anasema Al-Imamu Ahmad – kuhusu Amru bin Bukair huyu -: "Anatafuta ukweli". Anasema Abu Hatim: "Ni mwenye kuaminika, muaminifu, mkweli". Anasema Ibn Ma'in: "Si katika watu wa uwongo: ni mkweli". Anasema Al-Ajurri kutoka kwa Abi Daud: "Ni mwenye kuaminika". Anasema Al-Husain bin Fahm: "Ni mwenye kuaminika, imara, mtu wa Hadithi na alikuwa katika *Mahuffadh* (Wanavyuoni wakubwa waliohifadhi sana) wenye kuzingatiwa, na alikuwa faqihi (mwanachuoni wa sharia)". Lakini pamoja na hayo, baba yake Ali bin Al-Madini kaikanusha riwaya ya Amru Al-Naqid:

> kutoka kwa Ibn Abi Najih kutoka kwa Mujahid kutoka kwa Abi Ma'amar kutoka kwa Abdillah kwamba Al-Qurashi, Al-Thaqafi na Al-Ansari (Kureishi, Thakafi na Ansari) wako mbele ya mapazia ya Al-Kaba.

Akasema baba yake Ali bin Al-Madini: "Huu ni uwongo, Ibn Uyaina hakuisimulia hii bali ilikuwa (riwaya hii) kwa "Ibn Uyaina kutoka kwa Mansur kutoka kwa Mujahid kutoka kwa Abi Ma'amar kutoka kwa Abdillah" wala haikuwa katika Hadithi zake sahihi. Lakini maneno haya ya baba yake Ali bin Al-Madini, ukiyatazama utaona hakuna sababu ya kusema kuwa riwaya hio ni uwongo, kwani Amru Al-Naqid anaisimulia riwaya hio kutoka kwa: "Ibn Abi Najih kutoka kwa Mujahid kutoka kwa Abi Ma'amar kutoka kwa Abdillah" na baba yake Ali bin Al-Madini anaisimulia kutoka kwa: "Ibn Uyaina kutoka kwa Mansur kutoka kwa Mujahid kutoka kwa Abi Ma'amar kutoka kwa Abdillah" tafauti ni katika mpokezi mmoja: na hii haifikii daraja ya kuitwa mpokezi kuwa ni mwongo hasa hasa ikiwa mpokezi huyo kathibitishwa kuwa ni mwenye kuaminika

[391] - Ibn Hajar *Taqribu Al-Tahdhib* uk. 426, *tarjama* na. 5106.

kama alivyo Amru Al-Naqid huyu, bali hii inawezekana ikawa ni sahau tu. Na kwa hivyo, Al-Haafidh Ibn Hajar anasema kuhusu Amru Al-Naqid huyu kuwa ni: "Mwenye kuaminika, Haafidh (Mwanachuoni mkubwa aliyehifadhi sana) alisahau katika Hadithi".[392] Kwa hivyo, huyu ni mpokezi mwenye kukubalika, na udhaifu wake ni mdogo sana.[393]

Mu'awiya bin 'Amri – mpokezi wa pili wa *sanad* hii – ni mwenye kuaminika wala hakuna aliyemjeruhi.[394]

Zaaida – mpokezi wa tatu – ni Zaaida bin Qudama naye pia ni mwenye kuaminika wala hakuna aliyemjeruhi.[395]
Abdullahi bin Dhakwaan – mpokezi wa nne – ni Imamu mkubwa sana kaitwa Amirul-Mu-uminin (yaani katika Hadithi) naye hakuna tatizo lolote lile juu ya uaminifu na ukweli wake na ubingwa wake mkubwa sana.[396]

Al-A'araj – mpokezi wa tano – ni Abdul-Rahman bin Hurmuz, naye ni mwenye kuaminika wala hakuna aliyemjeruhi.[397]

Kwa hivyo, *sanad* hii – yenye udhaifu mdogo sana kwa sababu ya kuwemo Amru Al-Naqid, mpokezi wa kwanza ambaye ni mkweli lakini mara nyengine husahau – pamoja na *sanad* iliotangulia ambayo pia ina udhaifu kidogo – unaifanya riwaya hii iliosimuliwa kutoka kwa Abu Huraira iwe *hasan lidhatihi* na ifikie daraja ya usahihi *lighairihi*. Na ukichanganya Hadithi hii iliosimuliwa kutoka kwa Abu Huraira na Hadithi hii katika *sanad* na njia zake nyengine zinazofata, basi utakuta kwamba hii ni Hadithi sahihi bila mashaka. Na ukiongezea na ukweli kwamba Hadithi hii imesimuliwa kimaana katika mapokezi mingine tutayoyanukuu baadae – *In shaa Allah* – basi unapata dhahabu juu ya lulu.[398]

---

[392] - Ibn Hajar *Taqribu Al-Tahdhib* uk. 426, *tarjama* na. 5106.
[393] - Tazama *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 8, uk. 85-86, *tarjama* na. 156, Al-Khatib *Taarikh Baghdad* j. 12, uk. 201, *tarjama* na. 6667.
[394] - Tazama *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 10, uk. 194, *tarjama* na. 397.
[395] - Tazama *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 3, uk. 264, *tarjama* na. 571.
[396] - Tazama *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 5, uk. 178-179, *tarjama* na. 352.
[397] - Tazama *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 6, uk. 260, *tarjama* na. 569.
[398] - Usije ukadhani kwamba kila Hadithi dhaifu ikipokewa kwa *sanad* tafauti inapata nguvu na kufikia daraja ya Hasan au Sahihi! Laa (sio hivyo): Hadithi inayopata nguvu ni

Hizo ni baadhi tu ya *sanad*, tumezielezea kiasi cha kuthibitisha usahihi wa Hadithi hii, lakini Hadithi hii ina njia na *sanad* nyengine nyingi. Baadhi ya njia na *sanad* hizo ni:

Hadithi ambayo *sanad* yake ina mpokezi dhaifu kidogo kama vile mkweli lakini anasahau au anakosea kidogo au hifadhi yake si nzuri. Hadithi kama hii ikipata Hadithi nyengine yenye *sanad* kama hio inapata nguvu na kufikia daraja ya Hasan, nayo ni Hadithi iliochini ya Sahihi kidaraja lakini zote zinakubalika. Na zikikusanyika Hadithi za namna hio nyingi hufikia daraja ya usahihi. Ama Hadithi za waongo, mafasiki, watunzi wa Hadithi, wenye kuachwa, walio dhaifu sana, hawa kila wakiwa wengi na Hadithi yao inazidi kuwa dhaifu kwani wakiwa ni waongo – kwa mfano – basi huwa waongo wamekubaliana kusema uwongo. Anasema Ibn Al-Salaah:

> Wala hailazimu Hadithi kupokewa kwa njia tafauti kuwa ndio iwe (imepanda daraja na kufikia daraja ya Hadithi) Hasan, kwani udhaifu unatafautika: (udhaifu) mwengine huwa hauondoki kwa sababu ya kupokewa (Hadithi hio) kwa njia nyengine…kama vile riwaya za waongo na wenye kuachwa (na mfano wao); na (udhaifu) mwengine huwa unaondoka kwa sababu ya kupokewa (Hadithi hio) kwa njia nyengine, kama vile ikiwa mpokezi wake (Hadithi hio) ni mwenye hifadhi mbaya…Basi kupokewa kwake kwa *sanad* nyengine wakati huo kunaifaa (Hadithi hio) na kuiondoa kutoka katika muanguko wa udhaifu na kuipeleka katika kilele cha (kuzingatiwa kuwa ni Hadithi) *hasan* au sahihi.

Tazama *Al-Ba'ithu Al-Hathith* j. 1, uk. 134, akinukuu kutoka katika kitabu *'Ulumu Al-Hadith* cha Ibn Al-Ssalaah.

Na maneno kama hayo pia yamo katika *Muqaddimatu Ibn Al-Salaah* cha Ibn Al-Salaah uk. 31-32. Anasema Sheikh Ahmad Shakir – akisherehesha maneno hayo –:

> Na kwa hivyo, linabainika kosa la wanavyuoni wengi wa mwisho mwisho katika kuifanya kwao Hadithi dhaifu iliokuja kwa njia nyingi kuwa inapanda daraja (na kufikia daraja ya Hadithi) *hasan* au sahihi; kwani ikiwa udhaifu wa Hadithi ni kwa sababu ya ufasiki wa mpokezi au kutuhumiwa kwa uwongo, kisha ikaja (Hadithi hio) kwa njia nyengine ya aina hio hio (ya fasiki au mwongo) basi (Hadithi hio) huzidi udhaifu pamoja na udhaifu (wake wa mwanzo).

Tazama *Al-Ba'ithu Al-Hathith* j. 1, uk. 135. Bila kusahau kwamba Hadithi inapokuwa na udhaifu katika *matn (text)* yake, basi *sanad* sahihi au mjumuiko wa *sanad* nyingi pia hautoifaa kitu.

Njia ya ya Hisham kutoka kwa baba yake kutoka kwa Aisha. Kwa njia hii, Hadithi kaisimulia Al-Nasai,[399] Al-Tirmidhi,[400] Ibn Jarir Al-Tabari,[401] na Muslim.[402]

Njia ya Musa bin Talha kutoka kwa Abu Huraira. Kwa njia hii, Hadithi kaisimulia Al-Nasai,[403] Al-Tirmidhi,[404] Al-Tabarani,[405]Ibn Manda.[406] Al-Tahhaawi[407] na Muslim.[408]

Huu ni mukhtasari wa utafiti juu ya *sanad* za Hadithi hio, vyenginevyo Hadithi hii ina njia nyingi sana hatuwezi bali hatuhitaji kuzielezea zote, tunachotaka ni kuthibitisha tu usahihi wake, nao umeshathibitika *Walillahi Al-hamdu.*[409]

RIWAYA NYENGINE SAHIHI

Jambo jengine lililosimuliwa katika riwaya sahihi,[410] ni kuwa baada ya kuteremka Aya hio, Mtume (s.a.w.) alipanda katika kilima cha Al-Safa na akawaita jamaa zake na kuwaonya, akiwambia: "Mimi ni mwenye

399 - Al-Nasai Al-*Kubra* j. 10, uk. 207, Hadithi na. 11312. J. 6, uk. 161, Hadithi na.6442.
400 - Al-Tirmidhi *Al-Sunan* uk. 849, Hadithi na. 3184.
401 - Ibn Jarir Al-Tabari *Jami'u Al-Bayan* j. 19, uk. 136-137-141.
402 - Muslim *Sahihu Muslim* uk. 105, Hadithi na. 205.
403 - Al-Nasai *Al-Kubra* j. 6, uk. 159, Hadithi na. 6438.
404 - Al-Tirmidhi *Al-Sunan* uk. 849, Hadithi na. 3185.
405 - Al-Tabarani *Al-Awsat* j. 8, uk. 238, Hadithi na. 8511.
406 - Ibn Manda *Al-Aymaan* j. 2, uk. 875 Hadithi na. 933-934-935-936-937-938-939-940.
407 - Al-Tahhaawi *Sharhu Ma'aani Al-Athaar* j. 3, uk. 285, Hadithi na. 5388.
408 - Muslim *Sahihu Muslim* uk. 104, Hadithi na. 204.
409 - Nilikuwa nimezitafiti *sanad* za riwaya hii na nikakusanya maandishi marefu kabla ya kuzimaliza, nikaona nitamchosha msomaji Mswahili hususa wale ambao hawajui mambo ya elimu ya Hadithi, kwa hivyo, nikaona bora nifanye ufupisho wa *sanad* mbili tu kiasi cha kuthibitisha ili kufupisha maudhui kadiri inavyowezekana.
410 - *Sanad* chache za riwaya hii ambazo nimezipitia, nimeona kuwa *sanad* hizo ni sawa na *sanad* za Hadithi iliotangulia: ni dhaifu kidogo ambazo mkusanyiko wake unapeyana nguvu na kufika daraja ya usahihi. Lakini sikujilazimisha kuzipitia *sanad* nyingi sana za riwaya hii kwani hizo chache nimeona zinapeyana nguvu na pia maana ya riwaya hii ni sawa na riwaya iliotangulia.

kukuonyeni kutokana na adhabu kali". Na hii pia ni riwaya sahihi,[411] wala haipingamani na riwaya ya mwanzo, kwani zote ni kuwa aliwaonya watu wake kwa kuwatangazia kwa pamoja na kuwaonya mmoja mmoja.

MUKHTASARI NA NUKTA MUHIMU

1) Tulichokijadili katika sura hii, ni nini Mtume (s.a.w.) alikisema kuwambia watu wake baada ya kuteremka Aya ya Qur-ani yenye kusema: **"وَأَنذِرْ عَشِيرَتَكَ الأَقْرَبِينَ " ((Na waonye jamaa zako wa karibu)).**[412]

2) Shia wanadai kuwa baada ya kuteremka Aya hio, Mtume (s.a.w.) aliwakusanya watu wake na kuutangaza ukhalifa wa Ali.

3) Katika dai lao hilo wametegemea riwaya.

4) Lakini tumebainisha kwamba dai hilo ni batili, kwani:

a) Aya inamtaka Mtume (s.a.w.) awaonye watu wake, wakati kufanya hivyo wanavyodai wao si kuwaonya watu.

b) Tukijaalia kuwa maana ya Aya ni kuwa amtangaze Ali kuwa ni khalifa, basi utaona kwamba maneno yaliomo katika riwaya hizo hayamtangazi Ali kuwa ni khalifa moja kwa moja, bali yanatoa *offer* (tunuko au zawadi) kwa atakayekubali kufanya kadha atakuwa khalifa. Na kwa hivyo, Abu Lahab au Abu Talib wangekubali pengine mmoja wao ndiye angekuwa khalifa, hasa hasa tukizingatia vyeo vyao kwa Makureish. Na kwa hivyo, khalifa hakuchaguliwa na Allah.

c) Tena, tukijaalia kuwa hapa Mtume (s.a.w.) alimtangaza Ali kuwa khalifa baada yake naye akatoa ahadi hio kwamba atayembaii na kumsaidia atakuwa khalifa wake baadae, basi itakuwa ahadi ya Mtume (s.a.w.)

---

411 - Kaipokea Al-Tha'alabi *Al-Kashfu Wa Al-Bayaan* j. 7, uk. 183, na Ibn Abi Hatim *Tafsiru Al-Qur-aani Al-'Adhim* j. 9, uk. 2825, Hadithi na. 16012, na Al-Bukhari *Al-Sahih* Hadithi na. 4770, na Muslim *Sahihu Muslim* uk. 105, Hadithi na. 207-248, na Al-Nasai katika *Al-Kubra* j. 10, uk. 208, Hadithi na. 11314-11315, na wengi wengineo.

412 - Sura 26, Aya 214.

haikutimia kwani khalifa baada yake ni Abu Bakr: si Ali – ahadi ya Mtume (s.a.w.) haikutimia. Kwa hivyo, ni wazi kuwa dai hilo halina ukweli.

5) Riwaya hizo zinasema kuwa Ali kamrithi Mtume (s.a.w.). Lakini tunasema:

a) Ikiwa kurithi huku ni kurithi mali, Ali hakumrithi Mtume (s.a.w.) chochote.

b) Ikiwa ni kurithi ukhalifa – nao labda ndio unaokusudiwa hapa basi – Ali hakumrithi Mtume (s.a.w.) ukhalifa pia, bali khalifa baada yake ni Abu Bakr.

c) Ikiwa ni kumrithi elimu na ujuzi. Basi hakuna yoyote mwenye elimu na ujuzi wa Mtume (s.a.w.).

6) Riwaya hizo zinasema kuwa atayekubali kumsaidia basi atakuwa khalifa kwa watu wa nyumba yake. Kwa hivyo, hata riwaya hizo zingelikuwa ni riwaya sahihi, basi ukhalifa uliokusudiwa katika riwaya hizo si ukhalifa wa Umma wa Kiislamu.
7) Hayo tulioyatanguliza yote ni yenye kuihusu *mutun* (texts) za riwaya hizo kwa kujaalia kuwa riwaya hizo ni sahihi. Vyenginevyo, riwaya hizo zimesimuliwa na:

a) Wapokezi wa kule kule Al-Kufa, mji wa Shia.
b) Katika kila *sanad* kuna wapokezi Mashia.
c) Wapokezi hao ni waongo, watunzi wa Hadithi au dhaifu sana.

8) Kwa hivyo, natija ni kuwa dai hilo la kutangazwa ukhalifa wa Ali baada ya kuteremka Aya hio isemayo: **“Na waonye jamaa zako wa karibu”** halina ushahidi kutoka katika Aya hio wala kutoka katika riwaya wanazozitolea hoja, kwani Aya haikutaja ukhalifa na riwaya ni za kutunga – hakuna ushahidi!

9) La mwisho ni kuwa riwaya sahihi ni zile zenye kusema kwamba ilipoteremka Aya hio, Mtume (s.a.w.) aliwaonya watu wake, Makureish – kabila moja moja hadi kuwahadharisha watu wa nyumbani kwake akisema:

“Jikomboeni na moto kwani mimi sikufaini kitu mbele ya Allah”. Hii ndio riwaya:

a) Yenye *matn* (text) sahihi, kwani *matn* yake inakubaliana na Aya yenyewe: Aya inasema: “Waonye” na Hadithi inasema: “Aliwaonya”: sio Aya iseme: “Waonye” kisha yeye atangaze ukhalifa.
b) Yenye *sanad* sahihi.
c) Kwa hivyo, hadi hapa bado hatujapata ushahidi juu ya kutangazwa ukhalifa wa Ali na Allah na Mtume wake.

SURA YA NNE
KUHUSU MAJADILIANO

UTANGULIZI

Kama nilivyotangulia kusema kwamba kitabu hiki asili yake ni makala ambayo niliiandika na kuituma katika mtandao wa intaneti wa Wazanzibari (Zanzinet) na ukumbi wa Jifunzeuislamu. Sawa na upinzani nilioupata baada ya kuandika makala kuhusu *Hadithu Al-Thaqalain* na kuituma katika mtandao huo na baadae kuifanyia sehemu yake maalumu katika intaneti, jambo ambalo baadae lilipelekea kuwepo kwa mjadala baina yangu na watetezi wa Hadithi hio,[413] halkadhalika nilipoandika kitabu hiki – ambacho kilikuwa makala – na kukituma katika ukumbi huo wa Zanzinet na ukumbi wa Jifunzeuislamu, pia nilipata upinzani kutoka kwa wale wenye uoni tafauti na wangu. Mmoja wao aliandika makala za kunijibu,

[413] - Mijadala hio nimeiweka mwishoni: katika sura ya saba ya kitabu *Mezani Ya Haki*.

nami nikampa fursa mpaka amalize kisha na mimi nikamjibu makala zake. Kwa bahati mbaya baada ya hapo sikupata tena jawabu zake kuhusu makala hio ya ukhalifa ambayo kwa sasa ndio kitabu hiki. Kwa ajili ya kueneza faida na kuufikia ukweli na uhakika, nimeonelea bora kwamba majibizano hayo yote yaliofanyika baina yetu niyaweke katika kitabu hiki – kama nilivyofanya katika kitabu *Mezani Ya Haki* – ili watu waweze kufaidika zaidi. Humu – katika kitabu hiki – jina la Sheikh huyo tuliojadiliana nimeliondosha kwani labda hilo halitomfurahisha na lengo si majina ya watu bali ni uhakika wa jambo lenyewe tu. Ama ingelikuwa nanukuu kutoka katika kitabu chake hapo ningelazimika kumtaja kwani nikisema nimetoa katika kitabu fulani ni lazima nimtaje na mtunzi wake. Kwa hivyo humu nitatumia neno "Shekh X" kumaanisha Sheikh huyo niliejadiliana naye. Cha kufahamu ni kuwa Sheikh X huyu si yule anayehusika na kitabu cha Sala ya minazi na mipopoo.

Pia kuna mambo fulani fulani yaliomo katika makala humu hatuna budi kuyatoa kwani lugha ya kitabu ina maadili tafauti na lugha ya makala.[414]

JAWABU KWA MAKALA YA KWANZA YA SHEIKH X

بسم الله الرحمن الرحيم
الحمد لله رب العالمين وصلى الله على سيدنا محمد وعلى آله وأصحابه أجمعين

Nilikuwa nimeanza kuandika makala juu suala la ukhalifa. Kabla sijakamilisha kusema ninayoyasema, mara akaingia Sheikh X ili kunijibu makala yangu hio. Nadhani hio ilikuwa ni mbinu ya kutaka mimi niache kuandika makala yangu kama alivyofanya mbinu kama hio katika ukumbi wa Zanzinet[415] nilipokuwa nikimjibu makala yake juu ya Maimamu na elimu zao za ghaibu, ambapo nilikatisha makala zangu za kumjibu baada ya kuona kwamba hasemi kitu chenye kufahamika; bali mimi nikizungumzia Suala la Uimamu na Hadithi za Al-Kuleini, yeye ana Hadithi yake moja hio ya Barobaro anaileta; ikawa hakuna maelewano.

[414] - Yaani nilioibadilisha ni makala yangu tu: makala yake sina haki ya kuibadilisha isipokuwa spelingi tu, na ninapokuwa na nyongeza au maelezo basi huyaweka chini. Pia namna alivyotaja marejeo (references): katika baadhi ya sehemu nimebadilisha na kuyaweka marejeo hayo kwa mfumo mwengine.

[415] - Maneno haya niliyasema katika ukumbi wa Jifunzeuislamu.

Hapo mimi nikakatisha makala zangu, na hilo nadhani ndilo alilokuwa akilitaka nalo ni maslahi kwake. Labda na huku alikusudia kufanya hivyo hivyo, ili nikatishe maudhui yangu. Lakini mimi niliona nimuache aandike na mimi niandike,[416] mpaka hapo atapomaliza ikiwa ninahisi kuwa kuna haja ya kuwekwa wazi maneno yake basi nitafanya hivyo.

Sasa nadhani Sheikh X kanijibu kwa makala tano,[417] kama sikukosea. Kama nimekosea basi mutaweza kunikumbusha na kunijuilisha ipi katika makala zake sikuijadili. Nitaanza jawabu yangu kwa makala yake ya kwanza.

Katika makala yake ya kwanza, Sheikh X alianza kwa kuzungumzia maisha ya Mtume (s.a.w.) kwa ufupi hadi kufa kwake. Na haya yote hayana khilafu, wala hayahusiani na maudhui yetu. Bali sehemu kubwa ya makala yake haihusiani na maudhui yetu. Maudhui yetu ni: “Je Allah na Mtume wake wamemtangaza Ali kuwa ni khalifa?” Kwa hivyo, kazi yake ilikuwa fupi: kazi yake ilikuwa ni kutupa Aya na Hadithi tu zenye kusema hivyo.

Lakini Sheikh X – katika makala yake ya mwanzo – kawacha kabisa maudhui haya na badala yake akazungumzia maudhui ya ukhalifa wa Sayydna Abu Bakr (r.a.). Na katika hilo, anasema:

> Hivyo, si kila sahaba alidhani kuwa Seyyidna Abubakar (r) angekuwa Khalifa wa Waisilamu, bali kuna wale waliopinga jambo hilo, na haki hii haikukatazwa katika Uislamu. Palitokea watu kutoka katika sehemu mbali mbali waliopinga kuchaguliwa kwa Seyyidna Abubakar kuwa Khalifa wa Waisilamu ingawa baadae palipatikana huko kwa wengi kuunga mkono jambo hilo ingawa nguvu, hadaa pia ilitumika katika kutetea ukhalifa na kuchaguliwa kwa Seyyidna Abubakar, haya si mageni kwa wale waliosoma historia ya Kiislamu katika Vitabu Sahihi vya Historia na vile vya Hadithi.

[416] - Yaani nimuache anijibu na mimi niendeleze kuandika makala yangu tu bila kumjibu yeye hadi hapo atapomaliza jawabu yake kwangu.

[417] - Ziko makala nyengine mbili za ziada: moja nilikuwa sijaiona baadae nikaiona na nyengine – kumbukumbu yangu ni kuwa – aliituma baadae kabisa. Lakini zote zimetoka nje ya maudhui yetu: zote zimo humu nimezielezea.

Inavyoonyesha ni huko kwa Seyyidna Ali (k) kukataa kumpa kura yake Seyyidna Abubakar (r), hayo ni kwa sababu Ali alidhani ya kuwa yeye ndiye angestahiki kuwa Khalifa wa Waisilamu badala ya Abubakar, haya yamenakiliwa na Imam Tabari katika Tariikh yake kwa kusema: "Mtume (s.a.w.) amekufa na nimeona kuwa hakuna yoyote aliyebora kwa Ukhalifa kuliko mimi lakini watu wamemchaguwa Abubakar, nami nikawafuata. Kisha Abubakar naye akafa bado nilihisi kuwa hakuna aliyekuwa bora kwa jambo hilo kuliko mimi, lakini watu wakamchanguwa Omar, nami nikawafuata. Kisha Omar naye akauwawa bado niliona kuwa hakuna aliyefaa kwa jambo hilo kuliko mimi, bali walimchaguwa Othman badala yangu nami tena nikawafata.[418]

JAWABU

Kwa kuanzia, ningependa kukurejesha – hasa hasa – katika maneno yako uliposema: "Na haki hii haikukatazwa katika Uislamu". Tunasema kwamba ikiwa wewe unayakubali haya, basi elewa kwamba haya ulioyaeleza hapa ni uthibitisho wa wazi kwamba Khalifa baada ya Mtume (s.a.w.) hakutangazwa na Allah wala na Mtume (s.a.w.). Bali lilikuwa ni jambo la shura (mashauriano): "Na haki hii haikukatazwa katika Uislamu", kama ulivyonena. Na kama unavyojua kwamba katika mashauriano, wako wataokubali na wako wataopinga. Kwa hivyo, si vibaya katika uchaguzi huo wa khalifa, wengine kuona kuwa Ali ni bora na wengine wakaona kuwa Abu Bakr ni bora na wengine wakaona kuwa Sa'ad bin Ubaada ni bora. Lakini hatimae baada ya kuwa waliowengi (Majority) wa Masahaba (r.a.) walimuona kuwa Abu Bakr ndiye bora kwa ukhalifa na wakamchagua basi hakuna tena mwenye uwezo wa kutengua uamuzi huo.

[418] - *Tar-iikh At-Tabari,jalada la* 16, uk. Wa 51

Na kuukubali ukhalifa wake – baada ya kuchaguliwa na Waislamu – ni dini ya Allah ambayo ni wajibu kwa kila Muislamu kuifuata.[419]

Ama maneno yako uliposema: "Ingawa nguvu, hadaa pia ilitumika katika kutetea ukhalifa na kuchaguliwa kwa Seyyidna Abubakar". Ni bora ukatueleza ni nguvu zipi na ni hadaa gani iliopita katika uchaguzi huo, ili ikiwa tuna jawabu ya kukujibu tukujibu, na kama hatuna tukubaliane na wewe. Kwa ufupi, ni kuwa ikiwa unayakubali haya ulioyasema hapa, basi elewa kwamba unathibitisha ukweli kwamba sharia ya Allah ni kumchagua khalifa baada ya Mtume (s.a.w.) kwa njia ya Shura (Mashauriano). Vyenginevyo, hakuna maana ya kuwa wengine wamuone huyu kuwa ndiye anayefaa na wengine wamuone yule kuwa ndiye anayefaa, n.k. Na cha kufahamu ni kuwa, hakuna riwaya hata moja kwamba Ali mwenyewe alidai kuwa Allah na Mtume (s.a.w.) wamemchagua yeye kuwa ndiye khalifa baada ya Mtume (s.a.w.): riwaya zote ambazo zinasimulia kuwa Ali aliidai nafasi hio,[420] zinasema kwamba sababu alizokuwa akizitoa ni:

a) Ukaraba (ujamaa) wake na Mtume (s.a.w.).
b) Fadhila zake katika Uislamu.

Nami ninasema: kwamba ni vigumu kwa mtu anayejua dasturi na kawaida ya wacha Mungu, akakubali kwamba Ali aliidai nafasi ya ukhalifa kwa ajili yake binafsi kwa misingi ya ubora wake, kwani hakuna mcha Mungu anayeweza kudai ubora kwa ajili ya kabila na nasaba yake naye anaisoma Aya isemayo: **"Hakika mbora wenu zaidi kwa Allah ni mcha Mungu wenu zaidi".[421]** Halkadhalika si kweli kwamba Ali aseme kuwa mimi nina fadhila zaidi katika Uislamu kuliko Abu Bakr au Umar, bali hawezi kusema hata kuwa yeye ana fadhila zaidi kuliko mimi na wewe. Hata ingelikuwa kweli Ali ana fadhila zaidi kuliko Masahaba wote, basi akiwa

[419] - Si kwamba ni wajibu kumfuata kwa sababu yeye ni Abu Bakr, *"laa"* sio hivyo, bali ni wajibu kumfuata kwa kuwa yeye ni khalifa wa Waislamu aliyechaguliwa, kwani Allah katwambia tumtii Yeye na Mtume wake na Ulil Amri, yaani viongozi wa Kiislamu wenye kuhukumu kwa mujibu wa Sharia ya Allah.

[420] - Wakati riwaya nyengine nyingi zaidi zinaeleza kwamba Ali alipotaka kuchaguliwa kuwa khalifa baada ya kufa Uthman alikuwa hataki kabisa kuchaguliwa kuwa Khalifa, lakini Waislamu hawakumkubali mwengine yoyote isipokuwa yeye ndio akakubali.

[421] - Sura 49, Aya 13.

kama ni mtu mcha Mungu wa hali ya juu hawezi kusema maneno hayo, naye anaisoma Aya isemayo: **"Basi musizitakase nafsi zenu, Yeye (Allah) ndiye mjuzi zaidi wa afanyaye uchaji".**[422] Kwa hivyo, hayo maneno yaliomo katika riwaya hizo, naomba tuyafikirie upya kabla kuzitazama *sanad* za riwaya zenyewe. Sheikh X nina hakika 100% kwamba wewe hapo ulipo huwezi kusema kuwa wewe ni bora kuliko Muislamu mwengine hata kama wewe una hakika kuwa umempita kwa elimu na ibada, kwani hilo ni kinyume na tabia ya ucha Mungu: mcha Mungu hasemi kuwa mimi ni bora kuliko fulani.[423] Kwa hivyo, naona madai mawili haya ambayo ndio yenye kusimuliwa katika riwaya, basi ni madai yasio na ukweli.

Pili ni kuwa: madai haya ni kumfanya Ali kuwa alikuwa na uchu wa madaraka! Na hili pia ni vigumu kulikubali kwa mtu kama yeye, hasa hasa tukizingatia yale aliojifunza Ali kutoka kwa Mtume (s.a.w.) katika baadhi ya matokeo, ambapo baadhi ya Masahaba walikuwa wakimwambia Mtume (s.a.w.): "Nifanye kuwa *gavana* (liwali) wako", Mtume (s.a.w.) alikuwa akiwajibu: "Jambo hili hatumpi mwenye kuliomba".[424] Ninayo mifano mingi iliotokea katika historia ya watu ambao hatuna shaka kuwa ni chini ya Al-Imamu Ali kwa ujuzi na mingineo, ambao walikataa kuchaguliwa katika nafasi za uongozi wa dola ya Kiislam. Mfano mmoja ni Al-Imamu Salim bin Rashid Al-Kharusi. Huyu ni Imamu wa dola aliyechaguliwa Oman katika miaka kiasi cha 100+ iliopita. Oman ni nchi ambayo wakati mwengine huwa na mfumo wa kifalme kama sasa; wakati mwengine hugawika sehemu mbili: sehemu moja huwa kuna ufalme na ya pili huwa kuna Imam; na wakati mwengine huwa na Imam nchi nzima. Imamu huyu alipochaguliwa, alikataa kabisa. Mwanachuoni maarufu wa Oman wa zama hizo, Al-Imamu Al-Salimi (r.a.)[425] akamwambia kama ukikataa baada ya kuwa watu wote wameshakuchagua, basi tutakupiga upanga. Naye akajibu je baada ya kupigwa upanga, nitakuwa katika *al-walaya* (mapenzi ya Waislamu) au nitakuwa katika *al-baraa* (Waislamu watajitenga na mimi: watanichukia na sitopata dua zao)? Akamwambia watajitenga na wewe.

---

[422] - Sura 53, Aya 32.

[423] - Kama ilivyosimuliwa kutoka kwa Ibn Umar (r.a.) kwamba ucha Mungu ni kuwa wewe usijione bora kuliko yoyote yule. Al-Baghawi *Ma'aalimu Al-Tanzil* j. 1, uk. 82.

[424] - Al-Shaukani *Sharhu Al-Nayl* j. 8, uk. 258, Hadithi na. 3874.

[425] - Tazama *Nahju Al-Balagha* j. 1, uk 111, khutuba na. 87.

Basi alilia sana na hatimae – kwa sababu hio ndio – akakubali kuchaguliwa katika nafasi hio ya Uimamu wa dola.[426]

Mwenendo huu wa Al-Imamu Salim bin Rashid unatupa picha na tabia ya walivyo wacha Mungu. Kwa hivyo, bila shaka Al-Imamu Ali, aliyekulia chini ya madrasa ya wahyi, akapata nuru ya kukaa na Mtume (s.a.w.),[427] n.k., hawezi kugombania madaraka. Lakini mimi naona labda tumuache Ali mwenyewe ajieleze. Je Ali wewe kweli ulikuwa ukijiona bora kushika ukhalifa? Alipokufa Uthman na watu wakataka kumchagua Ali, Ali alisema hivi:

> Niacheni, tafuteni mwengine…na mukiniacha nitakuwa kama mmoja wenu. Na huenda nikawa ndio msikivu wenu na mtiifu wenu kwa yule mutayemtawalisha jambo lenu (la ukhalifa). Na mimi kuwa waziri ni kheri kwenu kuliko kuwa Amiri.[428]

Na baada ya *kubaiiwa* na kutokea fitna za Mu'awiya, Ali alisema: "*Wallahi* watu *wamenibaii* nami nalichukia jambo hili (la ukhalifa)".[429] Na akasema:

> Basi Allah anajua kwamba mimi nilikuwa nachukia kusimamia chochote katika mambo ya Umma wa Muhammad (s.a.w.), lakini watu waliyapinga (mambo) ya Uthman wakakubaliana kwamba wamuue wakamuua nami niko kwangu sikuamrisha wala sikukataza…na wakanitaja mimi kuwa wanibaii nikalichukia hilo.[430]

Haya ndio maneno yanayokubaliana na tabia ya mtu kama Ali na ucha Mungu wake. Lakini mingine yanayoelezwa ya kuwa alitaka kuwa yeye

---

[426] - Tazama tafauti baina ya mtu mwenye Imani na mtu asiyekuwa na Imani: Imamu huyu yuko tayari auliwe lakini asiwe kiongozi wa dola: wakati Maraisi wako tayari waue hata mamilioni ya watu lakini wapate uraisi wa miaka kumi! Hatimae wanaiacha dunia hivi hivi wanaondoka na matambara yao matatu meupe waliozongereshwa nayo tu.

[427] - Ingawa sitaki kusema kwamba kila aliyekaa na Mtume (s.a.w.) alikuwa mtu mwema, lakini Ali hakuna khilafu kwa Waislamu wote kwamba alikuwa ni mtu mwema.

[428] - Tazama *Nahju Al-Balagha* j. 1, uk 111, hutuba na. 87. Hiki ni kitabu muhimu cha Shia chenye kukusanya hutuba za Ali (k.w.).

[429] - Ibn Al-A'atham *Al-Futuh* j. 3, uk. 28.

[430] - Ibn Al-A'atham *Al-Futuh* j. 3, uk. 284-285.

ndiye awe khalifa, hayo ni kinyume na maneno yake haya na ni kinyume na tabia ya Ali; bali ni kinyume na tabia ya mcha Mungu yoyote. Ukweli ni kuwa:

a) Walikuwepo – katika Masahaba – waliona kuwa Ali ni bora, lakini hawa ni wachache sana, na hawakuwa na hoja isipokuwa ujamaa wa Ali na Mtume (s.a.w.). Na hoja hii ingefaa lau ingelikuwa Mtume (s.a.w.) alikuwa ni mfalme. Lakini yeye kaja kufunza usawa kwa watu wote na akatangaza kwamba:

> Hakuna ubora kwa Mwarabu juu ya asiyekuwa Mwarabu, wala kwa asiyekuwa Mwarabu juu ya Mwarabu, wala kwa mweusi juu ya mwekundu wala kwa mwekundu juu ya mweusi isipokuwa kwa ucha Mungu.

Na kabla ya tangazo lake hilo, Allah Mwenyewe alikwisha kutangaza kwamba: **"Hakika mbora wenu zaidi kwa Allah ni mcha Mungu wenu zaidi".** Kwa hivyo, hao waliomuona Ali kuwa ni bora zaidi msingi wao ni huo, nao haukubaliani na mafunzo ya Qur-an wala ya Hadithi za Mtume (s.a.w.).

b) Ali hakufurahishwa na ukweli kwamba uchaguzi wa Abu Bakr ulifanyika bila ya yeye kuwepo ili akaweza kushiriki katika shura (mashauriano). Na hili nadhani kila mtu anajua sababu yake ni nini? Sababu yake haikuwa maslahi binafsi. Vyenginevyo Umar na Abu Ubaida bin Al-Jarrah: kila mmoja kati yao angelisema nichaguweni mimi; na Abu Bakr naye angelisema nichaguweni mimi; lakini tunamkuta Umar na Abu Ubaida bin Al-Jarrah wanasema mchaguweni Abu Bakr; na Abu Bakr anasema mchaguweni Umar au Abu Ubaida bin Al-Jarrah.[431] Kwa hivyo, sababu kama unavyojua Sheikh X, ni kuwa Ansar – baada ya kifo cha Mtume s.a.w. – walikimbilia katika Saqifa yao ili wamchaguwe Khalifa miongoni mwao (Ansar) wakidhani kwamba wao ni bora kuliko Muhajirina kwa sababu ya ukarimu wao wa kumpokea Mtume (s.a.w.) baada ya kuingizwa katika dhiki kubwa huko

[431] - Al-Tabari *Al-Taarikh* j. 3, uk. 256, pia tazama uk. 265.

Makka. Wakati huo, Ali alikuwa kashughulika na maandalizi ya mazishi ya Mtume (s.a.w.).[432] Kwa hivyo, Abu Bakr na Umar, wakaona kuwa ukhalifa kuondoka kwa Muhajirina na kwenda kwa Ansar, unaweza kuleta siasa mbaya kwa Waarabu na hatimae kudhoofisha Uislamu, kwani Waarabu wote wa Bara Arabu walikuwa wakiwajali Makureish kuliko Waarabu wengine wote. Kwa hivyo, alichokifanya Abu Bakr na Umar – ambapo baadae pia waliridhiwa na Ansar wote *taqriban* – ni kuiokoa hali ya kisiasa ya Kiislamu ili kulifanya neno la Uislamu liwe na nguvu: na wala si uchu wa madaraka. Vyenginevyo, kila mmoja angejipigia kampeni yeye mwenyewe.

ANASEMA SHEIKH X

Mtu mwengine aliyepinga Ukhalifa wa Abubakar (r) alikuwa ni Saad bin Ubadah (r). Yeye ni katika waliofika kwanza katika jumba la Saqifa Bani Saidah akifatwa na wajumbe wengi wa kabila la Aws na Khazraji ingawa baadae alishindwa kwa hoja na baada ya kutokea kurushiana maneno kati ya Omar na Hubab Bin Mundhir! Hapa kuna baadhi ya Masahaba waliotowa hata wazo la kuuliwa kwa Saad bin Ubadah! Maneno kama *Qaatalaka-llah!* (Allah akulani) yalisikika yakitamkwa na baadhi ya wajumbe waliohudhuria katika tukio la uchaguzi wa Khalifa mpya.[433] Vipi basi tuambiwe kuwa Ukhalifa wa Seyyidna Abubakar (r) ulikuja na kutokea kwa njia isiyo na mashaka wala kibiru? Kwa ufupi hapakuwa na makubaliano ya moja kwa moja juu ya aliyefaa kuwa Khalifa baada ya Mtume isipokuwa baada ya hayo majadiliano marefu na yaliyojaa fujo na hatimae kukubaliana kuchaguliwa kwa Seyyidna Abubakar kuwa Khalifa.

JAWABU

[432] - Na hili ndilo wanalolitumia sana kubabaisha watu utasikia wanasema: "Ali anaukosha Mwili Mtukufu wa Bwana Mtume (s.a.w.), Ma-bwana wakubwa wako Saqifa wanagombania madaraka! Ndugu yangu Nassor Muhammad Al-Mazrui anasema katika maelezo yake alioyatia katika kitabu cha sira cha Sheikh Abdullah Salih Al-Farisi: "Kwani mtu hukoshwa na nani: si hukoshwa na jamaa zake wa karibu? Sasa Ali si ndiye mtu wake wa karibu?"

[433] - Al-Tabari *Al-Taarikh* j. 9, uk. 194.

Sa'ad bin Ubaada ni Sahaba wa Mtume (s.a.w.), kwa hivyo ana haki ya kuheshimiwa kwa usahaba wake. Lakini cha kufahamu ni kuwa:

a) Tokeo hili – kama unalikubali – basi – kama tulivyoeleza mwanzo – ni dalili tosha kwamba Mtume (s.a.w.) hakuchagua Khalifa baada yake. Vipi awe Mtume (s.a.w.) kachagua khalifa halafu Ansar wote wakusanyike katika Saqiifa kuchagua Khalifa miongoni mwao, yaani miongoni mwa Ansar!

b) Alipokuja Abu Bakr na Umar wasiwambie kwamba Mtume (s.a.w.) kasema kuwa Khalifa baada yake ni Ali. Na Ansar hawa – kama tulivyoeleza kwa urefu katika *Mezani Ya Haki* – ndio ambao Mwenyezi Mungu Mwenyewe kawasifu katika Kitabu Chake kwa sifa nzuru nzuri, kama Mtume (s.a.w.) Mwenyewe alivyowasifu pia.

c) Bali na vipi kuwe na agizo la Allah na Mtume wake juu ya ukhalifa wa Ali na kizazi chake, halafu Ali mwenyewe asitoe hoja hio wakati alipochaguliwa Abu Bakr na Umar na Uthman, na badala yake aseme yale tulioyanukuu kabla kwamba:

> Niacheni, tafuteni mwengine…na mukiniacha nitakuwa kama mmoja wenu. Na huenda nikawa ndio msikivu wenu na mtiifu wenu kwa yule mutayemtawalisha jambo lenu (la ukhalifa). Na mimi kuwa waziri ni kheri kwenu kuliko kuwa Amiri.

Na pia aseme: *"Wallahi* watu wamenibaii nami nalichukia jambo hili (la ukhalifa)".[434] Na pia aseme:

> Basi Allah anajua kwamba mimi nilikuwa nachukia kusimamia chochote katika mambo ya Umma wa Muhammad (s.a.w.), lakini watu waliyapinga (mambo) ya Uthman wakakubaliana kwamba wamuue wakamuua nami niko kwangu sikuamrisha wala sikukataza…na wakanitaja mimi kuwa wanibaii nikalichukia hilo.[435]

[434] - Ibn Al-A'atham *Al-Futuh* j. 3, uk. 28.
[435] - Ibn Al-A'atham *Al-Futuh* j. 3, uk. 284-285.

Na pia amwambie Mu'awiya – kile nilichokunukulia katika baadhi ya jawabu zangu – kwamba:

> Hakika wamenibaii watu ambao wamewabaii Abu Bakr na Umar na Uthmaan kwa masharti yale yale waliyowabaia wao. Aliyekuwepo hakuwa na haki ya hiari na aliyekuwa hayupo hakuwa na haki ya kukataa. *Hakika Shura (Kushauriana juu ya nani awe Khalifa) ni ya Muhajirina na Ansar. Wakikubaliana juu ya mtu watayemtaja kuwa ni Imamu, basi Mwenyezi Mungu analiridhia hilo.* Akitoka katika jambo lao mwenye kutoka kwa kuponda au kwa bidaa basi wanamrejesha katika kile alichotoka kutoka katika hicho. Na akikataa basi wamuue kwa sababu ya kufuata njia isio ya Waumini.[436]

Na akasema pia Al-Imamu Ali:[437]

> Kilichowajibu katika hukumu ya Allah na hukumu ya Uislamu juu ya Waislamu, baada ya kufa Imamu wao au kuuliwa…(basi) wasifanye kitu wala wasizuwe jambo wala wasitangulize mkono wala mguu wala wasianze chochote kabla hawajajichagulia Imamu mwenye kujizuia (na machafu) mjuzi, mnyenyekevu, mwenye marifa ya hukumu na Suna.[438]

Sasa baada ya yote haya, vipi mtu mwenye akili yake – licha ya mwenye elimu yake – atadai kwamba kuna wasia au tangazo la ukhalifa wa Ali kutoka kwa Allah na Mtume wake?

Ama kauli yako Ewe Sheikh X uliposema maneno haya:

> Hapa kuna baadhi ya Masahaba waliotowa hata wazo la kuuliwa kwa Saad bin Ubadah! Maneno kama *Qaatalaka-llah!* (Allah akulani) yalisikika yakitamkwa na baadhi ya wajumbe waliohudhuria katika tukio

[436] - Nimeinukuu riwaya hii kutoka kwa Al-Musawi *Al-Tas-hih* uk. 20, naye kainukuu kutoka katika *Nahju Al-Balagha* j. 3, uk. 7. Tazama pia Ibn A'atham *Al-Futuh* j. 2, uk. 374.

[437] - Na haya yote yamo kwenye vitabu vya Kishia.

[438] - Ahmad Al-Katib *Tatawwur Al-Fikri Al-Siyasi Al-Shi'i* uk. 443. Naye kayanukuu maneno haya ya Ali kutoka katika *Kitabu Sulaim bin Qais Al-Hilali* uk. 182, na Al-Majlisi *Biharu Al-Anwaaru* j. 8, uk. 555.

la uchaguzi wa Khalifa mpya. Vipi basi tuambiwe kuwa Ukhalifa wa Seyyidna Abubakar (r) ulikuja na kutokea kwa njia isiyo na mashaka wala kibiru.

Tunasema: kwamba kuuliwa kwa aliyepinga ukhalifa baada ya kuthibiti kwa maamuzi ya Waislamu, ni jambo ambalo kalitangaza Ali katika nukulu hio niliokupa kabla. Ali kasema:

> Akitoka katika jambo lao mwenye kutoka kwa kuponda au kwa bidaa basi wanamrejesha katika kile alichotoka kutoka katika hicho. Na akikataa basi wamuue kwa sababu ya kufata njia isio ya Waumini.

Hayo ni maneno ya Ali yaliomo kwenye kitabu cha Kishia chenye kukubalika. Kwa hivyo, sijui waliotoa rai hio walikuwa na kosa gani! Bali Ali mwenyewe alifunga safari kwenda kupigana na Mu'awiya kwa sababu ya kuukataa Ukhalifa wake, basi vipi alaumiwe aliyetoa wazo la kuuliwa aliyeukataa Ukhalifa wa Abu Bakr?!

d) Halafu la mwisho, ni kuwa vipi Allah na Mtume wake wawe wamemchagua Ali na kizazi chake na kumtaja Imamu mmoja mmoja na kuwa wao ndio waliochaguliwa kuwa ni Maimamu na kuwa Makhalifa wa kushika dola ya Kiislamu, halafu tunamkuta Al-Hasan bin Ali bin Abi Talib anakubali kujiuzulu kutoka katika nafasi yake ya ukhalifa na kumuachia Mu'awiya nafasi hio? Halafu Al-Hasan akashurutisha – katika barua yake ya sulhu baina yake na Mu'awiya – kwamba akifa Mu'awiya, basi utawala uwe kwa njia ya Shura, akasema katika barua hio ya mkataba wa sulhu:

> Hiki ndicho walichokubaliana Al-Hasan bin Ali bin Abi Talib na Mu'awiya bin Abi Sufyaan: (Al-Hasan) amekubaliana naye (Mu'awiya) kuwa ampe yeye usimamizi wa mambo ya waumini kwa sharti kwamba akitendee kazi Kitabu cha Allah na Suna za Nabii wake na mwenendo wa Makhalifa wema. Na wala Mu'awiya hana (haki) ya kumuusia yoyote (ukhalifa huo) baada yake, bali jambo hilo (la ukhalifa) liwe baada yake ni Shura (ushauriano) baina ya Waislamu.[439]

[439] - Ibn A'atham *Al-Futuh* j. 4, uk. 159-160.

Hayo ndio makubaliano yao. Sasa je Ali na Al-Hasan hawajui nao kuwa ukhalifa hauwi kwa njia ya shura hata waisisitize?![440] Na juu ya yote hayo, kwanini Ali naye aingie katika shura ya kumchagua Khalifa alipokufa 'Umar kama jambo hilo ni kinyume na Qur-ani na Sunna? Ndugu zetu naona haki hamuitaki: munataka na munapenda kudanganywa kwa riwaya za uwongo wa Al-Kufa.

JAWABU YA PILI KWA
MAKALA YA SHEIKH X

UTANGULIZI

بسم الله الرحمن الرحيم
الحمد لله رب العالمين وصلى الله على سيدنا محمد وعلى آله وأصحابه أجمعين

Katika jawabu yetu iliotangulia kwa Sheikh X, tulijibu *shubuhati* zake na kutapatapa kwake alikoandika, ambako – kama mmoja wa wasomaji alivyoniambia – hata aliyekuwa hajasoma anaona kwamba hoja zake ni hoja za kitoto.

Tulianza kujibu *shubuhati* za Sheikh X, si kwamba ni jambo lenye kustahiki kujibiwa katika ulimwengu wa elimu, lakini ni kwa ajili ya kuwasafishia wale wasiosoma na kuwaweka katika fikra sahihi. Na mimi nashukuru na napenda nikiona watu hawa wanajibu makala zangu ili nizidi kukuonesheni udhaifu wao, na jinsi walivyokuwa hawana hoja za kielimu. Na yatakubaikieni yote *In shaa Allah*, musitie wasiwasi. Wala

[440] - Hata Mu'awiya katika majibizano yake na Ali, alidai kuwa Ali awatoe waliomuua Uthman kisha ifanyike shura upya. Lakini hatuoni hata sehemu moja ambayo Ali alimjibu Mu'awiya kwamba khalifa hawi kwa njia ya shura bali anachaguliwa na Allah na Mtume wake. Kama ilikuwa khalifa katangazwa na Allah na Mtume (s.a.w.), basi Ali angelimjibu tu Mu'awiya kwamba Allah na Mtume wake wameshamtangaza Khalifa. Hili linatoa ushahidi wa wazi kwamba Hadithi zote za Kishia za ukhalifa wa Ali ni Hadithi za kutunga kwani alama moja ya Hadithi za kutunga ni kutokutumika au kutajwa wakati wa haja.

usidanganyike ewe Sheikh X kwamba mimi sitofanikiwi katika da'awa yangu ya kuwalingania watu wafate Qur-an na Suna na sio upotoshaji wenu wa kuweka neno "Ahlu Al-Bait," badala ya neno "Sunna", kwani nakwambia wako watu ambao kitabu changu *Mezani Ya Haki* kimewafika na walikuwa wamedanganyika na vijihadithi vyenu vya kutunga, na sasa – *Alhamdu Lillahi* – wamerudi katika haki.

MAUDHUI

Tumeijibu makala ya mwanzo ya Sheikh X. Katika jawabu yetu kwa makala yake hio, tulibakisha uporo wa alioyasema mwishoni mwa makala yake chini ya kichwa cha habari kisemacho: *Habari Muhimu.*

Hapa alileta vipengele vinne. Cha kwanza kinazungumzia tarehe ya kufa kwa Mtume (s.a.w.) na tarehe ya kuchaguliwa kwa Abu Bakr (r.a.). Hili si muhimu katika mjadala wetu kwani hatutafautiani. Kwa hivyo, naliruka.

Katika kifungu cha pili, Sheikh X anasema:

> Omar (r) alisimama huku anasema: nani miongoni mwenu ataacha kumbaii Abubakar ambaye Mtume mwenyewe alimpa kipau mbele? Kisha Omar akampa mkono wake Abubakar, baadhi ya watu wakamfuata Omar, lakini Ansar (watu wa Madina) wakasema, hatutompa kura zetu yoyote isipokuwa Ali.

JAWABU

Sheikh utakumbuka kwamba ulikuwa umetunukulia riwaya ya Al-Tabari kuhusu wale waliosema kuwa: "Allah amlani Sa'ad bin Ubada *(Qatalahu Allahu)".* Sasa nakuomba uirejee tena riwaya hio utaona kuna maneno haya: "(Abu Bakr) akanyoosha mkono wake nikambaii na Muhajirina wakambaii na Ansar wakambaii".[441] Halafu linganisha na maneno yako kwamba: "Lakini Ansar (watu wa Madina) wakasema, hatutompa kura zetu yoyote isipokuwa Ali". Pia linganisha maneno yako haya na maneno yako uliotwambia kabla kwamba: "Ingawa baadae palipatikana huko kwa

[441] - Al-Tabari *Al-Taarikh* j. 3, uk. 256-257.

wengi kuunga mkono jambo hilo". Tazama pia maneno yaliomo katika riwaya nyengine ya Al-Tabari – na *sanad* yake ni dhaifu mno, na asilimia kubwa ya *Taarikh* ya Al-Tabari ni batili lakini kwa sababu wewe umetolea hoja *Taarikh* yake nami nakunukulia – inasema: "Watu wakamchagua Abu Bakr uchaguzi wa Umma wote, baada ya kuchaguliwa katika Saqifa".[442] Na kwa ujumla ni kuwa riwaya zote zinaeleza kutokea mvutano kisha Bashir bin Sa'ad akawataka Ansar wenzake wamchague Abu Bakr naye akafanya hivyo na wengine wakafuatia. Kwa ufupi sina haja ya kurefusha, labda tuulize suali ili iwe ndio jawabu yako: suali ni kuwa riwaya yako inasema: "Lakini Ansar (watu wa Madina) wakasema, hatutompa kura zetu yoyote isipokuwa Ali". Je walimbaii Ali? Riwaya zote hapa zinakupinga, hata maneno yako mwenyewe ya huko nyuma – kama kawaida yako kujigonga – yanakupinga. Hatuna haja ya kuipekuwa riwaya yako hio kwani ubatili wake uko wazi. Labda kilichokuwepo ni baadhi ya watu tena wachache sana katika hao Al-Ansar walisema hivyo, lakini Umma ulimkubali na kumridhia Abu Bakr, na hili ndilo alilolisema Ali kama nilivyokunukulia maneno yake katika jawabu yangu ya mwanzo kutoka katika vitabu vyenu vya Kishia.

Suali jengine muhimu la kujiuliza ni kuwa maneno yanayowanukuu Ansar wakisema: "hatutompa kura zetu yoyote isipokuwa Ali" tukijaalia kuwa yametokana na riwaya sahihi, je maneno hayo yanamaanisha kwamba wao wanaona kuwa Ali ana haki zaidi ya ukhalifa kuliko wengine? Kama ni hivyo basi kwanini tena baada ya kufa Mtume (s.a.w) Ansar walikimbilia katika Saqifa yao ili wamchaguwe khalifa miongoni mwao? Je walimaanisha hapo sasa kwamba wao wanastahiki zaidi jambo la ukhalifa kuliko Ali?

Kifungu cha pili cha maneno ya Sheikh X, kinasema:

> Ali na Zubair hawakuwepo katika uchaguzi huo wa Abubakar. Ali na Zubair ni katika Masahaba kumi waliobashiriwa Pepo kwa mujibu wa Hadithi zinazokubaliwa. Zubair alitoa upanga wake na kusema kuwa hatompa kura yake mtu yoyote isipokuwa Ali bin Abi Talib (k), bali habari hizi zilipomfikia Seyyidna Abubakar alisema, mpigeni Zubair kwa mawe na mnyang'anyeni upanga wake.

[442] - Al-Tabari *Al-Taarikh* j. 3, uk. 256-257.

JAWABU

Tumeeleza katika jawabu yetu ya mwanzo sababu zilizomfanya Ali asiwepo katika uchaguzi wa ukhalifa wa Abu Bakr; kama tulivyoeleza sababu zilizomfanya Abu Bakr na Umar na wengine kukimbilia katika kumchagua khalifa. Kilichobakia ni kuwa je wewe unaamini kwamba Zubair kabashiriwa Pepo? Hebu tuambie Shia wana msimamo gani kwa Zubair? Sasa hapa sitaki kurefusha, lakini cha kufahamu ni kuwa tunapozungumzia kitu shura, si lazima kuwa awepo kila mtu, bali hili ni muhali hasa ukizingatia wingi wa Masahaba na hali zao za wakati wao. Lakini cha muhimu ni kuwa wataochagua wawe ni watu wenye kujua sifa za khalifa na hili Masahaba wote *taqriban* walikuwa wakilijua. Kwa hivyo, baada ya kuchaguliwa aliyechaguliwa basi Ali na Zubair ni lazima wamtii. Nimekunukulia mara elfu moja maneno ya Ali, na hii ya elfu mbili, kwamba Ali anasema:

> Hakika wamenibaii watu ambao wamewabaii Abu Bakr na Umar na Uthmaan kwa masharti yale yale waliyowabaia wao. Aliyekuwepo hakuwa na haki ya hiari na aliyekuwa hayupo hakuwa na haki ya kukataa. *Hakika Shura (Kushauriana juu ya nani awe Khalifa) ni ya Muhajirina na Ansar. Wakikubaliana juu ya mtu watayemtaja kuwa ni Imamu, basi Mwenyezi Mungu analiridhia hilo.* Akitoka katika jambo lao mwenye kutoka kwa kuponda au kwa bidaa basi wanamrejesha katika kile alichotoka kutoka katika hicho. Na akikataa basi wamuue kwa sababu ya kufata njia isio ya Waumini.[443]

Kwa hivyo, baada ya kuchaguliwa khalifa hakuna tena kuwa Kombo hakuwepo; Makame kankwenda bondeni; bali baada ya kuwa khalifa huyo ameshachaguliwa na wachaguwaji wakawa ni wajuzi, basi huwa ukhalifa wake umeshathibiti. Sasa Ali anatwambia kuwa walivyofanya Muhajirina na Ansar kuwachagua Makhalifa watatu waliotangulia Allah karidhika nako, wewe Sheikh X kwanini hutaki kuridhika na jambo ambalo Allah karidhika nalo. Sheikh X mkubali khalifa Abu Bakr, na ukubali kuthibiti ukhalifa kwa njia ya shura kama Ali anavyosema, vyenginevyo usijiite kuwa ni Shia wa Ali kwani humfuati.

---

[443] - Al-Musawi *Al-Tas-hih* uk. 20, naye kayanukuu kutoka katika *Nahju Al-Balagha* j. 3, uk. 7.

Kipengele cha tatu na cha mwisho cha Sheikh X kinasema:

> Ali aliogopa kutokea kwa fitna mara tu baada ya fitna ya kifo cha Mtume: fitna ambayo ingeung'owa Uislamu, hivyo, alikataa mapendekezo mengi yaliyoletwa kwake na baadhi ya waliomtaka awe Khalifa. Huyu hapa Ali anamkatalia Abu Sufiyan – ambaye alimjua kuwa bado alikuwa na athari za kijahiliyyah – wazo lake la kukusanya majeshi ya Makuraishi chini ya amri ya Ali kupambana dhidi ya Abubakar.[444]

JAWABU

Jamani enyi walimwengu wenzangu! Tazameni akili ya watu hawa! Mpaka lini akili zao hawa hazitoweza kufahamu?! Haya Allah – katika Qur-ani – na Mtume (s.a.w.) – katika Hadithi – wamemchagua Ali kuwa ndiye Khalifa; halafu Ali anakataa kuwa khalifa kwa kuogopa kutokea fitna! Natija ni kuwa Ali kaasi amri ya Mola wake na amri ya Mtume wake! Akili gani hii nyinyi munayompa Ali! Unaonaje lau kuwa kuna mtu anadai kuwa Mtume aliyechaguliwa na Allah kajitoa katika utume kwa kuogopa isitokee fitna, utakubali? Sheikh ikiwa munayakubali haya uliotueleza hapa – na munayakubali kwani yamo katika vitabu vyenu pia – basi elewa kwamba hata mwendaazimu anajua kwamba Ali kukataa kuwa khalifa – kama ilivyo katika riwaya hii na katika riwaya niliokunukulia mara nyingi kwamba:

> Niacheni, tafuteni mwengine…na mukiniacha nitakuwa kama mmoja wenu. Na huenda nikawa ndio msikivu wenu na mtiifu wenu kwa yule mutayemtawalisha jambo lenu (la ukhalifa). Na mimi kuwa waziri ni kheri kwenu kuliko kuwa Amiri,

ni hoja ya wazi kwamba ukhalifa haukuwa ni agizo la Allah na Mtume wake. Vyengineyo Ali asingesema maneno hayo. Sheikh X, bado

[444] - Sheikh X alikuwa kaandika hivi: "Chini ya amri ya Ali dhidi ya kupambana na Abubakar". Mimi nahisi ibara hii kaiweka kinyumenyume, na kwa hivyo nimeibadilisha na kuweka: "Chini ya amri ya Ali kupambana dhidi ya Abubakar". Ikiwa mimi ndiye niliyekosea, basi ibara yake yeye ndio hio, chukua kilichosahihi.

watapatapa tu: hujatupa ushahidi wa kuwa ukhalifa ni amri ya Allah na Mtume wake. Bado tunasubiri ushahidi.

JAWABU KWA MAKALA
YA PILI YA SHEIKH X

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَـٰنِ الرَّحِيمِ

الحمد لله رب العالمين , نحمده سبحانه وتعالى بما هو له أهل من الحمد ونثني عليه ونشهد أن لا إله إلا الله وحده لا شريك له ونشهد أن محمداً عبده ورسوله صلى الله عليه و على آله وأصحابه وسلم.....

Baada ya kuzijibu shubuhati za Sheikh X ambazo alizileta katika makala ya kwanza ya jawabu yake alionijibu – bila ya kujijua – akithibitisha ukweli wa kuthibiti ukhalifa kwa njia ya shura na pia – bila ya kujijua –

akithibitisha kuwa Allah na Mtume wake hakutangaza ukhalifa wa Ali, sasa na-tutazame nini alikisema katika makala yake ya pili. Baadhi ya yaliomo katika makala ya pili, niliwahi kuyajibu, lakini baadae baada ya kuona kwamba hapakuwa na mkamatano wa maudhui, basi niliona bora nimpe fursa aendelee. Katika makala yake ya pili pia alianzia kwa kutoa utangulizi mdogo wenye kusema kuwa *topic* (maudhui) hii ya ukhalifa wengine imewazidi kimo. Halafu akaelezea nini kimetokea baada ya kifo cha Sayyidna Abu Bakr. Na katika hayo, ana hiki cha kutwambia:

> Wakati Seyyidna Abubabakar (r) akiwa mahututi, aliusia aletewe kalamu na karatasi, Seyyidna Othman akawa ndiye mwandishi wa wasia huo, akaandika kwa amri ya Abubabakar (r) kuwa; "Baada yangu mimi khalifa atakuwa Omar Bin Al-Khattab (r). Hapana shaka kuwa Seyyidna Abubakar alifanya haya kwa ajili ya kuepusha zogo na fujo kati ya Waisilamu kama lile lililotokea wakati wa kuchaguliwa kwake. Hivyo kwa wasia huu ndio Omar (r) akawa Khalifa wa pili.

Ninasema: nimekujibu kwamba maudhui yetu ni je Allah na Mtume wake wamemtangaza Ali kuwa ndiye khalifa? Wewe unatutajia hapa wasia wa Abu Bakr kwa Umar. Nimekujibu sehemu hii pia – katika moja ya makala zangu – kwamba wasia huo ni pendekezo tu: haumlazimu Muislamu yoyote ila baada ya Waislamu kuuthibitisha.[445] Na hivyo ndivyo ilivyokuwa. Baada ya Uthman kuuandika wasia huo kwa amri ya Abu Bakr – kama ulivyosema – "Ulisomwa kwa Waislamu nao wakaukubali, kuusikia na kuutii".[446] Kwa hivyo, Umar hakushika ukhalifa kwa wasia wa Abu Bakr tu, bali ni kwa ridhaa ya Waislamu na hii ndio shura yenyewe. Hatuna haja ya kurefusha kwani jambo liko wazi. Isipokuwa hata ingekuwa Umar kawa khalifa kwa wasia wa Abu Bakr bila ya ridhaa ya Waislamu, basi hili bado halijatoa jawabu kwa suala letu: "Je Allah na Mtume wake wamemtangaza Ali kuwa ndiye khalifa?" Lakini kama tulivyosema kwamba Umar kawa khalifa kwa ridhaa zao, na kwa hivyo kawa khalifa kwa njia ya shura.

---

[445] - Na hivi ndivyo alivyosema Al-Imamu Ahmad bin Hanbal: "….Na 'Umar alipousiwa na Abu Bakr, basi hakika alikuwa Imamu baada ya (Masahaba) kumbaii na kumpa utiifu wao". Tazama maelezo yaliotiwa na Ammad Zaki Al-Baarurdi katika kitabu *Al-Ahkamu Al-Sultaniyya* cha Abu Al-Hasan Ali bin Muhammad Al-Baghdadi, uk. 23.

[446] - Ibn Kathir *Al-Bidaya Wa Al-Nihaya* j. 7, uk. 18.

Sheikh X anaendelea kwa kusema:

> Siku moja niliwahi kusoma makala ya Ustaadh Mazrui inayosema kuwa nasaba ya Mtume haitamfaa mtu yoyote kwa kuwa mbele ya Allah ni uchamungu tu, lakini maneno haya ya Sheikh wetu yanakanushwa na Seyyidna Omar (r) ambaye sasa tunazungumzia Ukhalifa wake, nimeona ni bora niyapachike maneno ya Seyyidna Omar yanayokanusha falsafa ya sheikh Juma Mazrui.
>
> Baada ya Hazrat Omar kutoa mahari ya dirham 40,000 kwa Hazrat Ali kwa ajili ya ndoa yake na Ummulkulthum (Dirham za wakati ule ambazo ni nyingi sana kulinganisha na mahari yaliyokuwa yakitolewa wakati ule), Seyyidna Omar alikuja katika minbar ya Mtume na akakaa baina ya minbar na kaburi la Mtukufu Mtume huku akizungukwa na Muhajirun na Masahaba wengine na akasema: "Nimemwoa Ummulkulthum, mtoto wa Ali ...kwani nimemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu akisema kila nasaba na njia zitakatika siku ya Kiama isipokuwa nasaba yangu na njia yangu, basi nimekuwa na Mtume na leo nimetaka kuongeza kuwa karibu naye zaidi kwa nasaba, hivyo msinikaripie kwa kuoa msichana mdogo".
>
> Ibnu Sa'ad ameongeza kwa kupokea kutoka kwa Al-Sha'abi na Al-Hessian[447] kuwa Al- Abbass alikuwa na haja kutoka kwa Omar (r) na akaja na kusema kuwambia Omar maneno haya: "Ewe, Kiongozi wa Waisilamu, mfano angekujia ami yake Nabii Musa ambaye ni Mwisilamu, wewe ungemfanyia nini? Omar akajibu kwa kusema: Wallahi, ningemtendea wema tu. Abbas (r) akasema tena: "Vyema, mimi basi ni ami wa Muhammad (s)". Omar (r) akasema: "Ewe Abu Al-Fadhli! Kwani unadhani wewe ni nani, ndio hivyo hivyo ulivyosema, *Wallahi*, baba yako Abdu Al-Muttalib ni bora kwangu kuliko baba yangu! Abbas akasema, umeapa *Wallahi!* Omar akasema wallahi nimeapa kwa hilo! Kisha Omar akaongeza kwa kusema, hayo ni kwa kuwa najua kuwa Abdu Al-Muttalib ni bora kwa Mtume wa Allah kuliko baba yangu mwenyewe, hivyo naona bora mapenzi ya Mtume kuliko mapenzi yangu mwenyewe".

[447] - Hivi ndivyo alivyoandika Sheikh X, sijui kama kakusudia "Al-Husain" au "Al-Hessian" ndio jina sahihi la msimulizi huyo; sikuwa na wakati wa kutosha ili nikaweza kutazama katika marejeo aliotupa Sh. X, ili kuhakikisha.

Mtu mmoja alimvunjia heshima Ali basi Omar aliposikia alisema: "Unamjua huyu aliyezikwa hapa? Huyu ni Muhammad ibn Abdillahi ibn Abd Al-Muttalib na huyu Ali ni mtoto wa Abu Talib ibn Abd Al-Muttalib. Basi usimtaje Ali isipokuwa kwa kheri na kama humpendi utamkosesha raha huyu aliyezikwa hapa", yaani Mtume (s). Hadithi hii imepokewa na Ahmad kwa *sanad* sahihi.[448] Basi Sheikh Juma haifai mimi kukukumbusha jambo hili, umesema kuwa hakuna sahaba aliyekuwa akirejea kwa Ali Bin Abu Talib (k.w), haya nayasubiri kufikia kwa pahala pake *Inshaallah*. Amma hili la kuheshimika kwa Ali na Masahaba karibu wote nimelitaja ili kutaka kuendelea na mjadala huu wa Ukhalifa. Hivyo kwa hakika Omar alikuja katika Ukhalifa kwa baraka ya wasia wa Hazrat Abubakar (r) na si kwa baraka ya kura za Waisilamu. Amma huko kulikubali kwa Masahaba jambo hili la wasia ni kulinda mafunzo ya Mtume Muhammad (s) yanayowataka "Kusikia na kutii" hata kama aliyechaguliwa ni mwenye nywele kama zabibu (mtumwa mweusi) au kama ulivyowahi kutwambia maneno haya pale uliposema kuwa ubora ni uchamungu na si kutokana na Ahlul Bayt au kizazi cha Mtume (s). Hivyo, Masahaba walimsikiliza Seyyidna Abubakar (r) na hawakutoka katika *Ijmaa*[449] kwa kulinda mafunzo ya Mtukufu Mtume na kwa ajili ya kuiondowa fitna!

JAWABU

Suala la kwamba nasaba haifai kitu na Hadithi yako hii ulioiita sahihi, nimeijibu katika moja ya makala zangu. Hapa – pamoja na kuondosha mambo mingine kwa ajili ya kufanya mukhtasar na kuzidisha mambo mingine kidogo – naikariri tena jawabu hio: hakuna mapya isipokuwa sehemu moja moja tu, lakini lengo langu kwa kuikariri jawabu hio ni kutaka jawabu zangu ziende kwa mujibu wa makala zako. Kwa vile nilikujibu makala yako ya kwanza, sasa nakujibu ya pili kisha ya tatu hadi tumalize *In shaa Allah.*

Tunasema: kwanza nakuomba:

[448] - Al-Imamu Ahmad *Fadhailu Al-Sahaba* j. 2, uk. 641, Hadithi na.1089.
[449] - *Ijmaa* maana yake ni makubaliano.

1) Ukitupa riwaya utupe marejeo kamili. Habari mbili hizi za Umar (r.a.) hukutwambia ulipozitoa. Kwa ufupi ni kuwa riwaya hii iko sehemu tafauti na huitaja wanavyuoni wa tafsiri wanapoifasiri Aya isemayo:

فَإِذَا نُفِخَ فِي الصُّورِ فَلا أَنسَابَ بَيْنَهُمْ يَوْمَئِذٍ وَلا يَتَسَاءَلُونَ

Litapopulizwa parapanda, basi hapatokuwa na nasaba siku hio wala hawatoulizana.[450]

Nimesema katika *Mezani Ya Haki* kwamba Hadithi hio[451] inagongana na Aya hii tulioinukuu hapa, bali inagongana na kamusi nzima ya Qur-an ambapo tunaona kwamba mtoto wa Nabii Nuh nasaba haikumfaa kitu baada ya kuwa anafanya maasi. Bali inagongana Hadithi hio na Hadithi nyengine nyingi, kama Hadithi sahihi tulioinukuu katika sura ya tatu – ya kitabu hiki – isemayo:

> ….Enyi Banii Abdul Muttalib! Hakika Allah ameniamuru nikuonyeni, basi mimi sikufaeni kitu kutokana na Allah (huko akhera). Basi jueni kwamba vipenzi vyangu miongoni mwenu ni wacha Mungu. Basi jueni kwamba wasinijie watu kesho na dini (yao) mukanijia nyinyi na dunia munaibeba shingoni mwenu. Ewe Fatima binti Muhammadi! Na ewe Safiyya shangazi ya Muhammad zikomboweni nafsi zenu kutokana na (adhabu ya) Allah: mimi sikufaini kitu mbele ya Mwenyezi Mungu".

Bali pia Hadithi hio inagongana na Aya: **"Na waonye jamaa zako wa karibu".**[452] Pia inagongana Hadithi hio na Hadithi nyengine kadha wa kadha tulizozitaja katika *Mezani Ya Haki*.[453]

2) Bila ya kupoteza wakati kwa kuzichungulia riwaya mbili hizo za Umar (r.a) ili kuthibitisha usahihi au udhaifu, ningependa nikukumbushe *minhaj* (Methodology au njia) yako ya kuipima riwaya na Qur-an. *Minhaj* yako ni kuwa ikiwa riwaya itapingamana na Qur-an basi huikubali. Ninasema: hii

---

[450] - Sura 23, Aya 101.

[451] - Yaani Hadithi isemayo: "Nasaba zote zitakatika siku ya kiama isipokuwa nasaba yangu".

[452] - Sura 26, Aya 214.

[453] - Hapa tutanukuu baadhi yake tu ili kufupisha.

ni *minhaj* sahihi na nzuri, lakini kwa bahati mbaya hapa hukuitumia, kwani Hadithi hio inapingana na Aya kadha wa kadha za Qur-ani ambazo zinaonesha au zinasema kwamba hakuna mazingatio ila kwa ucha Mungu tu na kwamba nasaba na kabila si vyenye kuzingatiwa. Sasa ukirudi kuyatazama maneno hayo uliotunukulia kutoka kwa Umar, utakuta yanazungumzia kitu chengine na mimi nazungumzia kitu chengine. Umar anazungumzia kuwaheshimu jamaa[454] wa Mtume (s.a.w.); wakati mimi nililolizungumzia ni ubora kwa mujibu wa Nasaba. Hili ndilo ambalo halipo katika Uislamu. Na nimetoa ushahidi kwa Aya kama: **"Basi litapopulizwa parapanda, hapatokuwa na nasaba baina yao siku hio wala wao hawatoulizana".[455]** Na Aya isemayo:

> Enyi watu hakika Yetu Sisi tumekuumbeni kutokana na mwanamume (mmoja, Adam) na mwanamke (mmoja Hawaa) na tukakujaaliyeni mataifa (mbali mbali) na makabila (mbali mbali) ili mupate kujuana, hakika ya mbora wenu kwa Mwenyezi Mungu ni mcha Mungu wenu (zaidi), hakika ya Allah ni Mjuzi, Mwenye habari (ya kila kitu).[456]

Ni wazi kwamba mbora kwa Allah ni mcha Mungu. Sasa sijui mimi nina kosa gani kusema kuwa ubora ni kwa ucha Mungu. Na kumbuka kuwa maneno ya Umar au Sahaba yoyote au mtu yoyote yule yanarejeshwa katika Qur-an na Suna, yakiafikiana basi hio ni haki hatuna uwezo wa kuipinga; yakiwa ni kinyume basi Sahaba huyo au mtu huyo huwa kakosea. Nami nasema kuwa – ikiwa riwaya uliotunukulia ni sahihi – basi Umar hajakosea kwani yeye hazungumzii ubora wa Ali na Al-abbass bali anazungumzia kuwaheshimu.

Pili: ni kuwa niliposema hivyo, pamoja na kunukuu Aya hizo, pia nilinukuu riwaya kadha wa kadha zenye kusema kwa uwazi kwamba hakuna ubora wa nasaba. Na hapa nazinukuu tena baadhi ya riwaya hizo:

إنَّ الله لا ينظرُ إلى صُورِكُم وأموالِكم ، ولكن ينظرُ إلى قلوبكم وأعمالكم

---

454 - Na mimi nahimiza hilo, lakini kwa sharti awe ni Muislamu mcha Mungu.
455 - Sura 23 Aya 101.
456 - Sura 49, Aya13.

Hakika ya Allah hatazami sura zenu na mali zenu lakini anatazama nyoyo zenu na matendo yenu”. [457]

Na riwaya nyengine inasema:

إن الله لا ينظر إلى أحسابكم ولا إلى أنسابكم ولا إلى أجسامكم ولا إلى أموالكم ولكن ينظر إلى قلوبكم فمن كان له قلب صالح تحنن الله عليه وإنما أنتم بنو آدم وأحبكم إليه أتقاكم

Hakika ya Allah hatazami usharifu (utukufu) wenu wala nasaba zenu wala miili yenu wala mali zenu, lakini anatazama nyoyo zenu. Atayekuwa na moyo mwema basi Allah atamuhurumia. Na hakika yenu ni watoto wa Adam, na kipenzi zaidi kuliko nyote kwake (kwa Allah) ni mcha Mungu wenu zaidi.[458]

Na riwaya nyengine inasema:

انظر، فإنك لست بخير من أحمر ولا أسود إلا أن تفضله بتقوى

Tazama hakika yako si mbora kuliko (mtu) mwekundu wala (mtu) mweusi isipokuwa umpite kwa ucha Mungu”. Kainukuu Ibn Kathir katika tafsiri yake kutoka kwa Al-Imamu Ahmad. [459]

Na riwaya nyengine inasema:

المسلمون إخوة، لا فضل لأحد على أحد إلا بالتقوى

Waislamu ni ndugu hakuna ubora kwa mmoja juu ya mwengine ila kwa ucha Mungu.[460]

---

[457] - Muslim *Sahihu Muslim* Hadithi na. 33/2564 na 34/2564. Anasema Ibn Kathir: “Na kaipokea Ibn Majah”.

[458] - Kainukuu Al-Qurtubi katika tafsiri yake katika tafsiri ya Surat Al-Hujurat.

[459] - Tazama Ibn Kathir *Tafsiru Al-Qur-ani Al-‘Adhim* j. 4, uk. 195.

[460] - Tazama Ibn Kathir *Tafsiru Al-Qur-ani Al-‘Adhim* j. 4, uk. 195.

Na riwaya nyengine inasema:

يا أيها الناس ألا إن ربكم واحد وإن أباكم واحد ألا لا فضل لعربي على عجمي ولا عجمي على عربي ولا لأسود على أحمر ولا لأحمر على أسود إلا بالتقوى ألا هل بلغت ؟ قالوا نعم قال ليبلغ الشاهد الغائب

Enyi watu hakika ya Mola wenu ni Mmoja, baba yenu ni mmoja, basi eleweni kwamba hakuna ubora kwa Mwarabu juu ya asiyekuwa Mwarabu, wala kwa asiyekuwa Mwarabu juu ya Mwarabu, wala kwa mweusi juu ya mwekundu wala kwa mwekundu juu ya mweusi isipokuwa kwa ucha Mungu. Je nimefikisha? (Masahaba) wakasema: "ndio". Akasema: 'basi aliyepo amfikishie asiyekuwepo'.[461]

Hizi ni baadhi ya riwaya ambazo zinasema kwa uwazi kwamba nasaba na rangi na kabila sivyo vyenye kuzingatiwa: bali ucha Mungu tu ndio unaozingatiwa. Na Aya nyengine zinasema:

وَمَا أَمْوَالُكُمْ وَلا أَوْلادُكُمْ بِالَّتِي تُقَرِّبُكُمْ عِنْدَنَا زُلْفَى إِلاَّ مَنْ آمَنَ وَعَمِلَ صَالِحاً

Na si mali zenu wala watoto wenu vitavyokukurubisheni na Sisi, isipokuwa atayeamini na kutenda mema.[462]

Na Aya:

لَنْ تَنفَعَكُمْ أَرْحَامُكُمْ وَلا أَوْلادُكُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ يَفْصِلُ بَيْنَكُمْ

Hawatokufaeni arhamu (jamaa) zenu wala watoto wenu, siku ya kiama, (Allah) atapambanua baina yenu (atakufarikisheni nao).[463]

---

[461] - Kainukuu Al-Qurtubi katika *Al-Jaami'u Lil-Ahkaam* j. 16, uk. 293 kutoka kwa Al-Tabari katika kitabu chake *Adaabu Al-Nufuus.*

[462] - Sura 34, Aya 37.

[463] - Sura 60, Aya 3.

Na Aya inayosema:

قَدْ كَانَتْ لَكُمْ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ فِي إِبْرَاهِيمَ وَالَّذِينَ مَعَهُ إِذْ قَالُوا لِقَوْمِهِمْ إِنَّا بُرَآءُ مِنْكُمْ وَمِمَّا تَعْبُدُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ .....

Kwa hakika pamekuwa na kigezo chema kwenu kwa Ibrahim na waliopamoja naye waliposema kuwambia watu wao: 'Hakika ya sisi tunajitenga kutokana na nyinyi na kutokana na munavyoviabudu visivyokuwa Allah…….[464]

Na Aya inayosema:

لا تَجِدُ قَوْماً يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الآخِرِ يُوَادُّونَ مَنْ حَادَّ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَلَوْ كَانُوا آبَاءَهُمْ أَوْ أَبْنَاءَهُمْ أَوْ إِخْوَانَهُمْ أَوْ عَشِيرَتَهُمْ .....

Hukuti watu wanamuamini Allah na siku ya mwisho (wakawa) wanampenda anayempinga Allah na Mtume wake, hata wakiwa baba zao au watoto wao au ndugu zao au ukoo wao……[465]

Aya zote hizi zinatoa mafunzo ya wazi kwamba Uislamu hautazami nasaba, kabila wala tabaka.

Nadhani hadi hapa tafauti baina ya ubora na kuheshimu imebainika kama vile ambavyo imebainika nini mimi nilikisema na nini riwaya uliotupa inasema: mimi nilikanusha – kwa ushahidi wa Aya na Hadithi hizo nilizokunukulia – kuwepo ubora kwa misingi ya ukabila na nasaba; wakati katika riwaya uliotupa inaeleza kwamba U'mar anachukizwa na kitendo cha kuvunjiwa heshima Ali; na – katika riwaya ya pili – anaahidi kumtendea wema Abbas, na haya ni mambo matatu tafauti.

Sasa tuje katika riwaya yako uliotunukulia kikamilifu na kutupa marejeo. Nayo ni riwaya isemayo:

---

464 - Sura 60, Aya 4.

465 - Sura 58, Aya 22. Na mfano wake ni Aya 23-24 ya Sura 9.

> Mtu mmoja alimvunjia heshima Ali basi Omar aliposikia alisema: "Unamjuwa huyu aliyezikwa hapa, huyu ni Muhammad ibn Abd Allah ibn Abd Al-muttalib na huyu Ali ni mtoto wa Abu Talib ibn Abd Al-muttalib. Basi usimtaje Ali isipokuwa kwa kheri na kama humpendi utamkosesha raha huyu aliyezikwa hapa", yaani Mtume (s). Kisha ukasema ewe Sheikh X: "Hadithi hii imepokewa na Ahmad kwa *sanad* sahihi..

Ninasema: Riwaya yenu hii inajenga msimamo tafauti na misimamo yenu mingine juu ya Umar (r.a.). Mmoja wa wahadhiri wenu wakuu wa Afrika Mashariki, anatwambia kwamba Umar aliposema kuwa: "Wakome wanafik kusema kuwa Mtume s.a.w. kafa" yaani baada ya kifo cha Mtume (s.a.w.) "Aliwakusudia Ali na Abbas kuwa ndio wanafiki"! Na vitabu vyenu vingi vinatwambia hivyo kuwa Umar alikuwa akimfanyia Ali uadui na hasad. Mara munatwambia hapa kwamba Umar alikasirika kwa kuvunjiwa Ali heshima!

Sasa kabla ya kuitazama *sanad* ya Hadithi hii ulioiita sahihi, tunasema kuwa Hadithi hii – hata ikiwa ni Hadithi sahihi basi – elewa kwamba Umar hapa anakanusha kuvunjiwa heshima Ali kama riwaya inavyosema. Na kwanini Ali avunjiwe heshima hata kama hakuwa Muislamu? Madamu yeye hajamvunjia Muislamu au Uislamu heshima, basi Uislamu unatutaka tumuheshimu.

Ama kuhusu Hadithi yako hio, basi waliosema kuwa ni sahihi wanahitaji kuwa na ushahidi kwani katika *sanad* yake kuna:

1) Al-Fadhlu bin Hubab.
2) Ibn Lahi'a.

Ama Al-Fadhlu bin Hubab, wametafautina juu ya usahihi wake kiasi cha kwamba kwa uchache tunaloweza kulisema ni kuziwacha tu riwaya zake bila ya kuzidhoofisha wala kuzikubali.[466]

[466] - Tazama *Lisanu Al-Mizan* j. 4, uk. 438, *tarjama* na. 1340.

Ama Ibn Lahi'a, yeye ni dhaifu bila ya wasi wasi na ni mwenye kughushi Hadithi, na Hadithi yake hio ni *mua'nn'an* nayo ni Hadithi dhaifu ikiwa itasimuliwa na msimulizi mwenye kughushi kama tulivyoeleza katika sehemu tafauti. Anasema Al-Bukhari: "Yahya bin Said (Al-Qattaan) alikuwa hamuoni kuwa ni chochote (Alikuwa hamthamini)". Anasema Ibn Mahdi: "Sichukui kingi wala kidogo kutoka kwake". Na Al-Imamu Ahmad ana riwaya tafauti kuhusu Ibn Lahi'a, moja kati ya hizo inamdhoofisha. Anasema Ibn Khuzaima: "Na Ibn Lahi'a sizisimulii Hadithi zake humu akipwekeka nazo (Yaani akizipokea yeye pekee)". Na akasema Abdul-Karim bin Abdul-Rahman Al-Nasai kutoka kwa baba yake akisema: "Si mwenye kuaminika". Na akasema Ibn Ma'iin: "Alikuwa dhaifu: Hadithi zake si hoja". Na akasema Ibn Sa'ad: "Alikuwa dhaifu". Na akasema Ibn Hiban: "Nilizichunguza habari zake nikamgundua kuwa alikuwa akighushi". Anasema Al-Juzajani: "Hadithi zake hazitegemewi wala haitakiwi kufanywa kuwa ni hoja wala mtu asidanganyike nazo". (Kama Sheikh X alivyodanganyika nazo). Anasema Abu Zur'a: "Hawezi kudhibiti (Hadithi)". Na alipoulizwa Abu Zur'a kuhusu Ibn Lahi'a na Al-Ifriqi, akasema: "ni madhaifu wawili: na Ibn Lahi'a Hadithi zake zinagongana". Anasema Al-Hakim: "Hadithi zake zinaporomoka". Anasema Al-Tabari: "Akili yake ilichanganyikiwa mwishoni mwa umri wake".[467] Kwa hivyo, Sh. X Hadithi ulioiita kuwa ni sahihi si sahihi.

Sheikh X anaendelea kwa kusema:

> Inakutosha maneo ya Sahaba Abu Dardaa kuwa ni ushahidi wa yale yaliyokuwa yakitendwa katika zama za Makhalifa na watu waliokuwa hawajali nini wanafanya, huyu hapa Sahaba mwerevu na mchamungu Abu Darda-a (r) katika Hadithi iliyosimliwa na Salim anasema:

[467] - Tazama *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 5 uk. 327-332, *tarjama* na. 648. Bila ya kusahau kutoa tanbihi ya kitu kimoja muhimu: nacho ni kauli ya Al-Azdi kwamba riwaya za Abadila (Wenye majina ya Abdala wote) kutoka kwa Ibn Lahi'a ni sahihi. Kauli hii wameitegemea watu wengine akiwemo Al-Albani. Lakini dhahir ya kauli hii imejengeka kwa kutazama kwamba Ibn Lahi'a alichanganyikiwa na kwa hivyo riwaya za Abadila kutoka kwake – labda – wamezisimulia kabla ya yeye kuchanganyikiwa na kwa hivyo ni riwaya sahihi. Lakini hivyo ingekuwa sawa lau Ibn Lahi'a alikuwa na kasoro hio tu ya kuchanganyikiwa, lakini yeye – mbali na udhaifu huo – pia ni mpokezi mwenye kughushi *(Mudallis)* na Hadithi yake Hapa ni Mu'an'an. Kwa hivyo, hii ni riwaya dhaifu kwa hali yoyote ile.

Amesimulia Salim kuwa: "Nilimsikia Ummu Ad-darda' akisema: 'Mara moja Abu Ad-darda alikuja nyumbani akiwa amekasirika na kuhuzunika sana, nikamwambia, nini kilichokukasirisha hivyo? Akasema: *'Wallahi* siwaoni wafuasi wa Muhammad kufanya yale mazuri tuliyokuwa tukiyafanya zama za Mtukufu Mtume (s) isipokuwa huku kusali kwa jamaa.[468]

Maneno haya Abu Dardaa aliyasema katika kipindi cha mwisho cha Ukhalifa wa Othman Bin Affan. Sasa ukijiuliza, ni mambo gani hayo ambayo Sahaba Abu Dardaa aliyahuzunikia, hapa itabidi kuendelea na makala hii *Inshallah*….[469]

JAWABU

Nahisi Sheikh X umechanganya uliposema: "Inakutosha maneo ya Sahaba Abu Dardaa kuwa ni ushahidi wa yale yaliyokuwa yakitendwa katika zama za Makhalifa" ingawa baadae umekiri kwamba: "Maneno haya Abu Dardaa aliyasema katika kipindi cha mwisho cha Ukhalifa wa Othman Bin Affan". Kwa hivyo, matatizo anayoyazungumzia Abu Al-dardaa yalitokea katika miaka sita ya pili ya utawala wa Uthman, na kipindi hiki bila shaka kilijitokeza matatizo bila ya khilafu yoyote kwa Waislamu. Lakini hapa kuna mambo mawili ya kufahamu:

a) Uthman hakuwa mtu muovu, lakini alikuwa dhaifu katika uongozi kwa sababu ya uzee wake.
b) Katika kipindi cha Ali pia yalijitokeza matatizo makubwa, hadi Ali kugombana na Ibn Abbas. Nami ninaamini 100% kwamba Ali hakuwa mtu muovu, lakini simuepushi na kukosea kama mwenyewe alivyosema – katika riwaya ya Kishia – kwamba:

---

[468] - Marejeo aliotupa Sheikh X ni Al-Bukhari *Al-Sahih* Hadithi na. 1.622.

[469] - Tazama huyu mtu anasema anajibu makala yangu ya ukhalifa lakini utaona kwamba tangu kaanza kutoa jawabu yake hadi hapa bado hajajibu chochote katika yale nilioyasema, bali anatoka nje ya maudhui kabisa, lakini mimi nakwenda naye hivyo hivyo kwa mujibu wa akili yake.

> Mimi katika nafsi yangu sikuepukana na kukosea wala sijiaminishi na hilo kutokana na matendo yangu, isipokuwa ikiwa Allah atanitosheleza na nafsi yangu kile ambacho yeye anakimiliki zaidi kuliko mimi.[470]

Kwa hivyo, makosa na matatizo yalijitokeza katika Makhalifa wawili wa mwisho na wote hawakuwa watu waovu katika nafsi zao na kheri walizozifanya ni nyingi sana. Kwa hali yoyote ile, ninachotaka kukisema ni kuwa ikiwa ni kulaumiwa basi tuwalaumu wote, au tunyamaze na hili ni bora kwetu.

Sheikh X anaendelea kwa kusema:

> Kwa hivyo, utaona kuwa Ukhalifa wa Abubakar (r) umekuja kwa uchaguzi (election) na Ukhalifa wa Omar (r) ulikuja kwa wasia (appointment) na Ukhalifa wa Othman kama utakavyoona umekuja kwa njia ya makubaliano ya watu wachache walioteuliwa na Omar (r) labda njia hii twaweza kuisema kuwa ni (selection) kama neno hili litakuwa ni sahihi kwa hali hio!
>
> Sasa suala, kwa nini hawakupewa fursa watu kumchaguwa Omar wala Othman kama kuna Aya inayosema **"Waamruhum shura bainahum"?**[471] **(Na mambo yao hushauriana wao kwa wao kwa pamoja)?** Mbona kulikuwa na wasia wa Abubakar? Mbona Omar aliteua kikundi cha wachache kufanya kazi hio? Je, haya si mambo ya kizota au Chama cha wachache? Naomba majibu kwa Ndugu yangu Sheikh Juma Mazrui juu ya suala hili.*[472]*

Ninasema: Haya yote nimeshakujibu kwamba:

---

[470] - Ahmad Al-Katib *Tatawuru Al-Fikr* uk. 24. Al-Kuleini: *Rawdhatu Al-Kafi* uk. 292-293. Al-Majlisi *Biharu Al-Anwar* j. 8, uk. 555, chapa ya zamani. Kama kweli Ali ni *maasum* asingelisema maneno haya, bali angesema: "mimi nina hakika kuwa sikosei kwani ni maasum".

[471] - Sio kama kuna Aya; Aya ipo kweli, sema kama Aya ina maana hio?

[472] - Unazidi kuona kwamba Sheikh wetu maudhui imemshinda: maudhui ni: "Je kweli Allah na Mtume wake wamesema kuwa khalifa baada ya Mtume (s.a.w.) ni Ali?" Sheikh anaelemea kwengine kabisa!

1) Wasia wa Abu Bakr ni pendekezo tu: haukuwalazimu watu: watu wangeona vyengine kuwa ndio bora basi wangeliubatilisha wasia huo, na wakafanya wanavyoona wao kuwa ndio bora.
2) Watu walisomewa wasia huo na wakaukubali. Kwa hivyo, uchaguzi wa Umar ulitimia kwa njia ya shura, kwani hio ndio shura yenyewe.
3) Kuchaguliwa kwa Uthman na baadhi ya watu ambao ndio kikundi chenyewe alichokiteua Umar, hakujaonesha kwenda kinyume na shura, kwani shura si lazima wawepo watu wote, bali ni lazima wachaguzi wawe wenye kufaa. Na wote walioingia katika Shura ni Masahaba Maulamaa.
4) Kama hili lilikuwa ni kosa basi na Ali naye kalifanya, kwani naye alikuwemo katika shura wala hakusema **"Jamaa twanchagua Uthman kwa shura ela mwajua kuwa shura haifai?".** Lakini madamu Ali ni *ma'asumu* (Hakosei) kwenu, basi elewa kwamba uchaguzi ulikwenda kwa mujibu wa sharia ya Allah, na Ali naye kashiriki, na hili – tena kwa upande mwengine – linathibitisha uhalali wa shura na linathibitisha kosa kwa wanaodai kuwepo uteuzi wa Allah na Mtume wake wa khalifa.
5) Ali mwenyewe kauhalalisha uchaguzi huo uliofanyika kwa njia ya shura kwa maneno yake mwenye katika risala aliompelekea Mu'awiya ambayo nimekunukulia sana huko nyuma.

Sheikh X, anamalizia kwa kusema:

> Ndugu wasomaji, haya ndio mambo ambayo yanafaa kuzingatiwa, kusiwe na lawama tu kwa Mashia au wale ambao hawakubaliani na falsafa zinazotolewa kuwa Ukhalifa haukuwa na matatizo wala dosari lolote. Ni jambo la wazi kwa Waisilamu na hasa wale ambao hawakuwahi kupitia kwenye vyuo vya kidini kutokudanganywa na makala za watu wenye kutaka kuikadhibisha historia na kutuletea wazo kuwa hakukuwa na matatizo yoyote ili kutaka kuwalaumu kwa hayo watu wengine.
>
> Angalia jinsi uhasama juu ya kugombea Ukhalifa ulivyoutia hasara Uislamu na bado tunaambiwa kuwa hakukuwa na ugomvi wala matatizo bali watu wote walikubaliana. Huyu hapa Imam Al-Bukhari, anasema kuwa: "Imesimliwa na Said Bin Al-Musayyib kuwa Jubeir Bin Mut'im (r) amesema: "Pale fitna ya kwanza ilipotokea kwa kuuwawa kwa Othman

Bin Affan (r), haikumbakisha yoyote kuwa hai katika walioshiriki katika vita ya Badr; kisha pakatokea vita ya wenyewe kwa wenyewe huko Madina, fujo la Al-Harra, tukio hilli halikumbakisha hai yoyote kati ya walioshiriki katika sulhu ya Hudaybiyyah; kisha fitna ya tatu ikatokea na haikuondoka isipokuwa baada ya kuudhalilisha Ummah huu na kuufanya (kuwa) dhaifu sana".[473]

Basi, kama mambo yalifanywa kwa mujibu wa Qur'ani na Sunnah kama tunavyoambiwa na Masheikhe zetu humu, tusengeona haya yaliyotokea kati ya Masahaba: huko kunyanyuka kwa watu wakapigana na kuwaua baadhi ya Viongozi wa Ummah huu kati ya hao Makhalifa amma ilitokana na makosa ya Ukhalifa huo, au udhalimu wa hao wafuasi wa Makhalifa hao, jambo hili haliwezi kuachiliwa bila ya kuzungumzwa na kutanabahisha watu wenye kupenda haki.

Tunasema: Haya yote ulioyasema hayahusiani na maudhui yetu ya asili ya "Je Allah na Mtume wake wamemtangaza Ali kuwa ndiye khalifa?" Wala hayahusiani na maudhui yako wewe ulioileta ya uchaguzi wa Makhalifa; mingine katika haya yalitokea katika miaka 12 ya uchaguzi wa Uthman na mingine yalitokea baadae zaidi – Uthman hayupo tena. Sisi maudhui yetu si hio: maudhui yetu ni kuwepo amri ya Allah juu ya ukhalifa wa Ali, nawe ukazidisha suala la shura na uchaguzi wa makhalifa. Ilitakiwa mazungumzo yaishie hapo ili tusiwe tunawababaisha wasomaji. Maneno hayo ungeyaleta, lau ingekuwa maudhui yetu ni je katika zama za Makhalifa kulitokea mgogoro au haukutokea? Lakini maudhui ni nyengine kabisa na wewe kazi yako wadapiadapia hiki na kile! La mwisho ni kuwa, ikiwa tutachukulia matatizo yaliotokea katika ukhalifa kuwa ni sababu ya kuujeruhi ukhalifa huo, basi na Ali naye hatosalimika kwani matatizo katika zama zake ni mengi zaidi. Napenda niishie hapa.

[473] - Marejeo aliotupa Sheikh X ni Al-Bukhari *Al-Sahih* 5. 358.

JAWABU KWA MAKALA
YA TATU YA SHEIKH X

بسم الله الرحمن الرحيم
الحمد لله رب العالمين وصلى الله على سيدنا محمد وعلى آله وأصحابه أجمعين

Usisahau kwamba mjadala huu ni kuwa je Allah na Mtume wake wamemtangaza Ali awe ndio khalifa baada ya Mtume (s.a.w.). Hadi hapa, ni wazi kwamba jawabu hio bado haijapatikana: kuna kubabaika tu! Katika makala ya tatu ya jawabu yake kwangu, Sheikh X, alisema yafuatayo:

> Jee, kulitokea nini Siku ya Ghadir Khum?
>
> Ghadir Khum ni sehemu iliyoko maili kadhaa kutoka Makka katika njia inayoelekea Madina. Wakati Mtume (s.a.w) alipopita sehemu hio tarehe 18 Dhul'Hijja (10 March 632) wakati anarudi kutoka Hijja yake ya mwago, Aya, **"Ewe Mtume fikisha uliyoteremshiwa…",** iliteremshwa, kwa hio alisimama ili kutangaza kwa Mahujaji ambao

alifuatana nao kutoka Makka na ambao walikuwa watawanyike njia panda hapo kila mtu kuelekea sehemu yake. Kwa amri ya Mtume (s.a.w) mimbari maalum ilitengenezwa kwa kutumia matandiko ya ngamia kwa ajili yake. Baada ya Sala ya mchana, Mtume .(s.a.w) alipanda mimbari na akatoa Khutuba yake ya mwisho mbele ya mkusanyiko mkubwa kabla ya kifo chake miezi mitatu baadae.

Sehemu ya kuvutia ya Khutuba yake, ni pale alipomchukuwa ‘Ali (a.s) kwa mkono wake, Mtume s.a.w. aliwauliza wafuasi wake iwapo yeye ana mamlaka zaidi (awla) kwa waumini kuliko wao wenyewe. Kundi kubwa lile la watu likaitikia kwa sauti kubwa “Hivyo ndivyo ilivyo , Ewe Mtume wa Allah”.

Kisha akatangaza: “Yule ambaye kwamba mimi ni (mawla) mwenye kumtawalia mambo yake, huyu Ali vile vile ni (mawla) mwenye kumtawalia mambo yake. Ewe Allah, kuwa rafiki kwa yule ambaye ni rafiki, na uwe adui kwa yule ambaye ni adui kwake”.[474]

Mara tu baada ya Mtume (s.a.w) kumaliza khutuba yake, Aya ifuatayo iliteremshwa:

“……. Leo nimekukamilishieni dini yenu, na kuwakamilishieni neema yangu kwenu, na nimewaridhieni kwamba Uislamu ndiyo dini yenu”.[475] Baada ya khutuba yake, Mtume (s.a.w) alimtaka kila mtu kula kiapo cha utii kwa ‘Ali (a.s) na kumpongeza. Miongoni mwa waliofanya hivyo ni Umar bin al-Khattab, ambaye alisema: “Hongera Ali Ibn Abi

[474] - Bila ya kwenda mbali, maneno: “Ewe Allah, kuwa rafiki kwa yule ambaye ni rafiki, na uwe adui kwa yule ambaye ni adui kwake” yanatosha kuonesha kuwa makusudio ya neno *“Mawla”* hapa ni rafiki na kipenzi. Hii katika Balagha huitwa **مُراعَاةُ النَظِيْرِ** *Muraa’aatu Al-Nadhir*, nako ni kuyafanya maneno ya mwisho yakawa yananasibiana na maneno ya mwanzo kimaana. Na hii yote, ikiwa tutaijaalia kuwa hii ni Hadithi sahihi.

[475] - Sura 5 Aya 3.

Talib! Leo umekuwa bwana[476] wa waumini wote wanaume na wanawake.[477]

JAWABU

Kwa ufupi ni kuwa Hadithi hio inayoitwa Hadithi ya "Ghadir Khumm" ni katika jumla ya yale ambayo nakusudia kuyaandika. Na kama nilivyogusia kwamba Hadithi hii haitaki kujadiliwa katika karatasi mbili tatu kama hivi, bali ina maelezo marefu. Na kwa sababu, mimi nakusudia kuiandika[478] – *In shaa Allah* – kiukamilifu, basi kwa hapa sitoijadili sana, lakini nitaashiria mambo mawili matatu kuhusiana na Hadithi hio na yaliobaki yatakuja wakati wake ukifika *In shaa Allah*. Mambo muhimu tutayotazama hapa ni:

1) Maana ya neno *Mawla* lililomo katika Hadithi hio.

2) Sababu ya kusemwa maneno hayo tukijaalia kuwa hii ni Hadithi sahihi.[479]

3) Na hatimae kutazama utabiri uliomo katika Hadithi hio.

MAANA YA NENO *MAWLA*

Mawla ni neno la kiarabu linalotokana na kitendo kilichopita *Waliya;* na kitendo kilichopo na kijacho *Yalii* na jina (Noun) ni *Walyan* au *Wilayatan.* Nalo, kwa chimbuko na maana, ni sawa sawa na neno *Waliyy* tulilolijadili katika sura ya mwanzo: ni neno lenye maana nyingi kama ifuatavyo:

---

[476] - Katika riwaya hakuna neno *"Bwana"* bali kuna neno *"Mawla".* Kwa hivyo, kwanza usilipe tafsiri hii wala ile mpaka tukubaliane neno hili lina maana gani hapa.

[477] - Sasa Sheikh X alau kaingia katika maudhui!

[478] - Bali nimeshaiandika bado kuikamilisha tu.

[479] - Nami nakubaliana na Maulamaa wanaosema kuwa maneno yasemayo "Yule ambaye mimi ni *mawla* wake basi na Ali ni *mawla* wake" ni maneno sahihi; na kwamba maneno yasemayo: "e Allah! Mpende ampendae na kuwa adui wa yule aliye adui wake" ni maneno yaliozidishwa katika asili ya Hadithi. Lakini cha kufahamu ni kuwa hata kama maneno haya ni sahihi: hayakuzidishwa, basi yanaipa nguvu tafsiri ya waliosema kuwa neno *mawla* katika Hadithi hii maana yake ni kipenzi, kwani kama tulivyoeleza kabla kwamba maneno hayo ni **مراعاة النظير** *muraa'aatu al-nadhir.*

1) Hutumika neno *mawla* kwa maana ya *Waliyyu* yaani msimamizi wa jambo la mwengine. Na maana hii ndio tunayoitumia kumwita kiongozi wa Dola kuwa ni *Waliyyu l-amri* yaani msimamizi wa mambo ya raiya au – kwa kutumia lafdhi yenyewe ya neno hilo – humwita *Mawla-na* yaani msimamizi wetu.[480]

2) Pia Hutumika neno *mawla* kwa maana hio hio ya *Waliyyu*, lakini kwa maana nyengine, nayo ni maana ya rafiki au kipenzi.[481] Na maana hii imetumika katika Qur-an katika Aya yenye kusema: **"..Hakika Allah ndiye kipenzi chake…"**[482] Neno lilitumika katika Aya hii kumaanisha kipenzi ni neno: "Mawla".

3) Maana nyengine ya neno *mawla* ni mtu muliefungamana (**حَلِيْفٌ** au Ally) na kuahidiana kwamba mutakuwa pamoja na kusaidiana hasa hasa dhidi ya mtu mwengine.[483] Maana hii huwa tunaisoma sana katika vitabu vya sira, nayo ndiyo maana iliomo katika baiti la shairi lisemalo:

وَنَنْصُرُ مَوْلانَا وَنَعْلَمُ أَنَّهُكَمَا النَاسِ مَجْرُوْمٌ عَلَيْهِ وَجَارِمُ**[484]

Na tunamnusuru yule tuliyefungamana naye na tunajua kwamba yeye – kama walivyowatu (wengine) – anafanyiwa makosa naye pia anafanya.

4) Maana nyengine ya neno *mawla* ni msaidizi au mtetezi.[485]

5) Maana nyengine ya neno *mawla* ni mtu aliyekombolewa kutoka utumwani (freed slave).[486] Maana hii pia imo katika vitabu vingi vya Hadithi kama kuitwa Salim kuwa ni "Mawla Abi Hudhaifa".

---

480 - Ibn Mandhur *Lissanu Al-'Arab* j. 15, uk. 401-402.
481 - Ibn Mandhur *Lissanu Al-'Arab* j. 15, uk. 402.
482 - Sura 66, Aya 4.
483 - Ibn Mandhur *Lissanu Al-'Arab* j. 15, uk. 402.
484 - **الأصل أن ما إذا زيدت بعد الكاف كفتها عن العمل ولكن قد ورد قليلا زيادتها بعدها من غير الكف ومن ذلك هذا البيت. راجع شرح ابن عقيل ج 2 ص .**
485 - Ibn Mandhur *Lissanu Al-'Arab* j. 15, uk. 402.

6) Maana nyengine ya neno *mawla* ni kinyume cha maana namba 5 iliotangulia, naye ni mtu aliyemkomboa mtumwa.[487]

7) Maana nyengine ya neno *mawla* ni *Asaba*.[488] *Asaba* ni jamaa wa karibu wa mtu wa upande wake wa kuume ambaye hakuna mwanamke aliyekuepo baina yake na wao katika uhusiano wao. Kama vile: ami, bin ami, kaka kwa baba tu au kwa baba na mama, n.k.

8) Maana ya nane nimeiona katika kitabu *Tadhkiratu Al-Khawwaas* cha Sibt Ibn Al-Jawzi, nayo ni *mawla* kwa maana ya *aula* (yaani - mwenye kustahiki zaidi au aliye bora zaidi).[489] Kisha akatoa ushahidi kwa Aya isemayo: **مَأْوَاكُمُ النَّارُ هِيَ مَوْلاكُم (Makazi yenu ni moto, huo ndio unaokustahikieni).[490]** Lakini bila kusahau kwamba wanavyuoni wametafautiana hapa kuhusu tafsiri ya neno *mawla* lililomo katika Aya hii. Hio aliotupa yeye ni tafsiri moja ya Aya hio, na wengine wakasema kuwa tafsiri ya Aya hio ni: **(Makazi yenu ni moto, huo ndio *mawla* wenu yaani sehemu ambayo mutaambiwa kuwa hiki ndicho munachostahiki).[491]** Na wengine wakasema kuwa tafsiri ya Aya hio ni **(Makazi yenu ni moto, huo ndio utaokunusuruni leo (yaani hakuna wa kukunusuruni)".[492]**

Sasa baada ya haya na-turejee katika Hadithi yetu isemayo: "Man kuntu Mawlahu fa-Aliyyu Mawlahu" (Yule ambaye mimi ni *mawla* wake na Ali ni *mawla* wake)". Hatimae ni kuwa hakuna khilafu baina yetu kwamba maana zote hizi sizo zilizokusudiwa katika Hadithi hio: "Man kuntu Mawlahu fa-Aliyyu Mawlahu" (Yule ambaye mimi ni *mawla* wake na Ali

---

486 - Ibn Mandhur *Lissanu Al-'Arab* j. 15, uk. 402.
487 - Ibn Mandhur *Lissanu Al-'Arab* j. 15, uk. 402.
488 - Ibn Mandhur *Lissanu Al-'Arab* j. 15, uk. 402.
489 - Sibt Ibn Al-Jawzi *Tadhkiratu Al-Khawwaas* uk. 59-60.
490 - Sura 57, Aya 15.
491 - Tazama Al-Zamakhshari *Al-Kashaf* j. 4, uk. 474. Lakini tafsiri hii na ya kwanza zinakaribiana.
492 - Tazama Al-Sabuni: *Al-Saf-wa* j. 3, uk. 230.

ni *mawla* wake): tafauti yetu ni katika maana mbili za mwanzo:[493] *mawla* kwa maana ya msimamizi wa jambo la mwengine, ambayo ndio chaguo la Shia; na *mawla* kwa maana ya kipenzi ambao ndio chaguo la wengine – tukijaalia kuwa hii ni Hadithi sahihi.

KANUNI

Tumeeleza huko nyuma kwamba Wanavyuoni wametafautiana juu ya neno lenye maana nyingi *(mushtarak)* likitumika katika Aya au Hadithi: je huwa maana zote hizo zimekusudiwa? Wengine wakajuzisha kuwa maana zote zizingatiwe; na wengine wanaona kwamba ikiwa kuna *Qarina* (context au ushahidi) itayobainisha maana moja iliokusudiwa basi itazingatiwa na kama hakuna basi itabidi neno hilo liachwe mpaka tupate ushahidi juu ya maana iliokusudiwa. Na tumesema kwamba kauli kwamba neno lenye maana nyingi *(mushtarak)* linaachwa kama lilivyo hadi kuwe na ushahidi juu ya maana iliothibiti ndio kauli ya *Jumhur* (majority) ya Umma. Na bila shaka ukitafakari hapa husiti kuona kwamba kauli hio ya *Jumhur* ndio kauli sahihi. Kauli hii tunaweza kuipa nguvu kwa kutazama ukweli kwamba neno lenye maana nyingi lina uwezekano wa kuwa maana yake hii au maana yake ile ndio iliokusudiwa – hatujui ni ipi katika hizo. Na kwa hivyo, kwa kuzingatia kanuni ya ki-usuli inayosema kwamba: **"الدَّلِيْلُ إِذَا طَرَقَهُ الاحْتِمَالُ سَقَطَ بِهِ الإِسْتدلاَلُ"**, (Dalili ikiwa na maana nyingi basi ushahidi wake huporomoka), basi hatuwezi kudai maana moja maalumu ila kwa ushahidi wa *Qarina* (context) au ushahidi wa nje. Kwa hivyo, hadi hapa ni wazi kwamba wote – Shia, Suni na Ibadhi – wanaambiwa kuwa hawana ushahidi: kila mmoja alete ushahidi mwengine ama ulio ndani ya Hadithi hio au ulio nje ya Hadithi hio wenye kuthibitisha madai yake.

USHAHIDI

Baada ya hayo, sasa tumebakiwa na suali la hoja za pande mbili: je nini ushahidi wa Shia kwa kuichagua maana ya msimamizi wa mambo ya neno *mawla* lililomo katika Hadithi hio? Na kwa upande wa pili tuna hoja gani katika kutokukubaliana na tafsiri yao hio na – kinyume chake – kuichagua

[493] - Wengine hutolea hoja kwa maana ya nane lakini hii kimaana haina tafauti na maana ya pili: zote zinapeleka katika lengo moja kwamba Ali ni mtawala.

kwetu maana ya kipenzi ya neno *mawla* lililomo katika Hadithi hio? Elewa kwamba hapa tupo katika kujaalia tu kuwa Hadithi hio ni sahihi: vyenginevyo nimekwambieni kuwa Hadithi hio ina maelezo marefu na Al-Bukhari kasimulia kuwa mtu wa kwanza kuisimulia Hadithi hio ni Abu Is-haq Al-Sabi'i Shia wa Al-Kufa baada ya kurudi Al-Khurasan (Iran) kisha watu wakamfuata. Tena Abu Is-haq ni dhaifu na ni *mudallis* (Mwenye kughushi). Kwa vile kama nilivyokwambieni kwamba mimi Hadithi hii nimeanza kuiandika na nina kama peji 40, na makusudio ni kuifanyia kitabu,[494] kwa hivyo kwa sasa sitojadili chochote kile kwa urefu, kwani Hadithi hii nitaielezea kwa urefu – *In shaa Allah* – katika kitabu chake maalumu. Na kwa hivyo kwa hapa sitojadili shubuhati walizoshikana nazo Shia katika Hadithi hii,[495] bali nitawabainishia udhaifu wa dai la akina Sheikh X na wenzake wenye itikadi kama yake kwa dalili mbili tu: na maelezo zaidi yatakuja baadae *In shaa Allah.* Dalili zetu mbili za udhaifu wa dai lao ni kama inavyofuata:

Moja – kama tulivyosema – ni kutazama "Sababu ya kusemwa maneno hayo: "Yule ambaye mimi ni *Mawla* wake na Ali ni *Mawla* wake". Sababu ya kuteremka Aya au ya kutamkwa Hadithi huwa ndio miongoni mwa mambo muhimu yenye kubainisha makusudio ya Aya hio au ya Hadithi hio. Na hii haina maana kwamba ikiwa Aya au Hadithi zinatoa hukumu fulani kwamba hukumu hio huhusishwa na sababu hio tu, lakini sababu huwa inaweka wazi makusudio ya Aya na Hadithi kisha hukumu inawahusu watu wote.

Katika riwaya zote *taqriban*, kisa, asili na sababu ya kusemwa maneno hayo ni kuwa Buraida na Ali walitumwa na Mtume (s.a.w.) kwenda Al-Yaman. Buraida ikawa hakupata *muamala*[496] mzuri kutoka kwa Ali au aliona – yeye (Buraida) na wenzake – mambo ambayo hayakuwafurahisha. Waliporudi, Buraida akamshitakia Mtume (s.a.w.), basi uso wa Mtume (s.a.w.) ukapiga wekundu (kwa hasira) kisha akasema: "Ewe Buraida yule ambaye mimi ni *Mawla* wake, basi Ali pia ni *Mawla* wake".[497] Na tokeo

[494] - Jua kwamba haya ninayoyasema hapa yote ni kwa kuwa huu ni mjadala niliouandika kama ni makala tu katika intaneti: hiki mwanzo hakikuwa kitabu.

[495] - Maelezo kamili yatakuja katika juzuu ya pili ya kitabu hiki *In shaa Allah.*

[496] - Ushirikiano.

[497] - Al-Nasai *Al-Khasais* uk. 74, Hadithi na. 80-81.

hili limefasiriwa pia na riwaya iliopokewa na Al-Tabari kwa *sanad* dhaifu sana. Riwaya hio inasema: "Watu walimshitaki Ali" yaani katika khutuba ya *Hijjat Al-Wada'a* baada ya Ali kurudi kutoka Al-Yaman pamoja na wenzake akiwemo Buraida, Mtume (s.a.w.) akasema: "Enyi watu: musimshitaki Ali, kwani naapa kwa (jina la) Allah yeye ndiye mwenye kumuogopa Allah kuliko nyote…".[498] Kwa hivyo, kwa ufupi tu, hivi ndivyo kisa na sababu ya kusemwa maneno hayo yasemayo: "Yule ambaye mimi ni *Mawla* wake, basi Ali pia ni *Mawla* wake". Riwaya nyengine inasema kuwa baada ya watu kumshitaki Ali, Mtume (s.a.w.) alisema: "Munamtakia nini Ali: Ali anatokana na mimi; na mimi ninatokana na Ali, naye ndiye Waliy wa kila Muumini baada yangu".[499]

Sasa kabla ya kuendelea na maelezo, ni kuwa hatuna budi kusema kuwa ni vigumu kwa Muislamu mwenye kuitumia vizuri akili yake na kutafakari vyema kuyakubali maneno haya. Vipi Mtume (s.a.w.) akasirike kwa kushitakiwa Ali bila ya kwanza kuisikiliza kesi? Je huu ndio uadilifu uliohimizwa na Qur-an na Suna zake mwenyewe Mtume (s.a.w.). Je si ndiye Mtume mwenyewe aliyesema: "Lau angeiba Fatima bint Muhammad, basi ningemkata mkono wake?"[500] Pili ni kuwa sababu iliotolewa katika Hadithi ni kuwa Ali asishitakiwe kwa sababu ni Mcha Mungu! Suali: kwani mcha Mungu hashitakiwi? Na sababu nyengine iliotolewa ni kuwa "Ali anatokana na Mtume". Jiulize wewe anatokana na Mtume (s.a.w.) vipi? Ikiwa kwa ujamaa uliokuwepo baina yao, basi kizazi cha Abbas, Aqil, Ja'afar wote hawa wakikosea wasishitakiwe kwani uhusiano wao na Mtume (s.a.w.) ni sawa sawa na uhusiano wa Ali na Mtume (s.a.w.)?! Na kwa hivyo, kwanini Al-Abbasiyyina walaumiwe? Bali vipi Fatma aliyetoka katika mgongo wa Rasul (s.a.w.) angekatwa mkono lau aliiba; lakini Ali iwe ni haramu hata kumshitaki? Kuanzia hapa

---

498 - Al-Tabari *Al-Taarikh* j. 3, uk. 223, katika maelezo juu Hijjatu Al-Wada'a.

499 - Al-Nasai *Al-Khasais* uk. 79, Hadithi na. 89.

500 - Tazama Hadithi hii katika *Sahihu Muslim* j. 6, katika *Sharhu Al-Nawawi* uk. 247, Hadithi na. 8 – 4386, na 9 – 4387 na 11- 4389. "Mlango wa kukata mkono wa mwizi sharifu na mwengineo". Na Al-Bukhari Hadithi na. 2648, na 3475, na 3733, na 4304, na 6787, na 6788. Ibn Majah Hadithi na. 2547 na 2548. Al-Tirmidhi, Hadithi na. 1430, na wengineo.

utaanza kuona ukweli aliousimulia Al-Bukhari katika *Al-Taarikh Al-Kabir*,[501] kutoka kwa Abu Husain akisema:

> Hatukuisikiapo Hadithi hii[502] mpaka alipokuja huyu (Abu Is-haq Al-Sabi'i) kutoka Khurasan (Iran) akaipigia kelele (kwa lugha ya vijana akaipigia debe)…basi watu wakamfuata.

Abu Is-haq – kama tulivyosema – ni Shia wa Al-Kufa dhaifu sana na ni mwenye kughushi.

Sasa baada ya hapo na-tukubali kidogo – kwa ajidili ya mjadala – kuwa hii ni Hadithi sahihi. Kwa kukubali huku, basi tunaona wazi nini sababu ya kusemwa maneno hayo: "Yule ambaye mimi ni Mawla wake, basi Ali pia ni Mawla wake". Ikiwa tutalifasiri neno *mawla* kuwa maana yake ni mwenye kuyatawala mambo (yaani mtawala), na kuifungamanisha tafsiri hio, na sababu ya hayo yaliotokea ya kutokufahamiana vyema huko Al-Yaman baina ya Ali na wenzake, ambayo yalisababisha Buraida na wenzake kuchukizwa na baadhi ya yaliofanywa na Ali, basi maana itakuwa: "Musimshtaki Ali kwa sababu yeye ni mtawala wenu kama nilivyo mimi". Suali la kujiuliza hapa ni: je enzi ya Mtume (s.a.w.) watawala walikuwa wangapi? Je Ali naye alikuwa mtawala? Ukiniambia *"laa"* haya ni *majazi* tu ***bi-I'itibari maa sayakunu*** **هَذَا مَجَازٌ بِاعْتِبَارِ مَا سَيَكُوْنُ**, *Hii ni mithali tu kwa kuzingatia kitu kitachokuwa baadae* yaani Mtume (s.a.w.) hapa alizingatia kuwa Ali atakuwa msimamizi wa mambo yenu (Waislamu) baada yake. Ukiniambia hivyo nitakuuliza je Ali alikuwa msimamizi wa mambo (mtawala) baada ya Mtume (s.a.w.) kama Hadithi yako inavyosema? Kwa hivyo, Mtume (s.a.w.) hapa kabashiri kitu ambacho hakikutokea – Utabiri wa Mtume haukuwa! Kwa hivyo, Hadithi hii bado haijawa hoja ya ukhalifa wa Ali kutoka kwa Allah na Mtume wake, kwani maneno "Yule ambaye mimi ni Mawla wake, basi Ali pia ni Mawla wake" hayafasiriki ila katika njia mbili au moja katika mbili:

---

[501] - J. 6, uk. 79, *tarjama* na. 8348.

[502] - Yaani Hadithi: "Yule ambaye mimi ni Mawla wake, basi Ali pia ni Mawla wake". Ninavyoona mimi ni kuwa asili ya Hadithi ni sahihi, lakini ina nyongeza nyingi na vipengele vingi vilivyopokewa katika masimulizi tafauti ambavyo ni ziada ya watunzi.

a) Ama useme kuwa Ali ndiye au naye alikuwa mtawala wakati wa Mtume (s.a.w.). Na hili bila shaka si sahihi kwa mtu yoyote yule!
b) Au useme kwamba Mtume (s.a.w.) hapa alikusudia kuwa Ali atakuwa mtawala baada yake. Na hapa utabiri wa yule **"Asiyetamka (chochote) kwa matamanio yake: bali ni (kwa) wahyi anaopewa"** haukutimia! Sasa chagua moja ewe Sheikh X ili tukusajili katika orodha ya wachekeshaji wenye kuliza!

TUNAENDELEA NA JAWABU YETU
KWA MAKALA YA TATU YA SHEIKH X[503]

بســـــــم الله الرحمــن الرحيــم
الحمــد لله رب العالمين و صلى الله على سيدنا محمد و على آله و صحابته أجمعين
وبعد:

Tunaendelea na jawabu yetu kwa makala ya Sheikh X, kuhusiana na yaliotokea hapo Ghadir Khum, baada ya dai la Shia la kwamba Mtume (s.a.w.) alimtangaza Ali kuwa khalifa. Je baada ya tangazo hilo la kubuni, nini kilitokea kwa mujibu wa Shia? Sheikh wetu anasema:

> Mwarabu mmoja aliposikia tukio la Ghadir Khum, alikuja kwa Mtume (s.a.w) na akasema: "Ulituamrisha tushuhudie kwamba hakuna mungu

[503] - Jawabu hii ni ya makala ile ile ya tatu ya Sheikh X lakini nililazimika kuigawa mara mbili na kuituma katika Zanzinet mara mbili ili nisiwachoshe wasomaji, kwani lau niliituma yote labda ingelikuwa refu kwa wengine.

isipokuwa Allah na kwamba wewe ni Mjumbe wa Allah, tumekutii. Umetuamrisha kusali sala tano kwa siku, tukakutii. Umetuamrisha kufunga (saumu) mwezi wa Ramadhani, tumekutii. Kisha umetuamrisha kwenda kuhiji Makka tukakutii. Lakini hukutosheka na yote haya ukamnyanyua binamu yako kwa mkono wako na ukamuweka juu yetu kama mtawala kwa kusema 'Ali ni *mawla* wa yule ambaye mimi ni mawla kwake: je, amri hii yatoka kwa Allah au yatoka kwako wewe?" Mtume (s.a.w) akasema: "Kwa jina la Allah ambaye ndiye Mola Pekee! Haya yanatoka kwa Allah, Mwenye nguvu na Mtukufu".

Aliposikia jibu hili, aligeuka na kuelekea aliko ngamia wake jike huku akisema: "Ewe Allah! Kama asemayo Muhammad ni sawa, basi vurumisha jiwe juu yetu kutoka angani na tupatie sisi adhabu kali na mateso". Kabla hajamfikia ngamia wake Allah alimvurumishia jiwe ambalo lilipiga juu ya kichwa chake na kupenyeza ndani ya mwili wake na kumuacha akiwa amekufa. Ni katika tukio hili kwamba Allah (S.W.) aliteremsha Aya ifuatayo:

> **Muulizaji aliuliza juu ya adhabu itakayotokea. Kwa makafiri ambayo hapana awezaye kuizuia. Kutoka kwa Allah, Mola wa mbingu za daraja.[504]**

Kama unakumbuka, niliwahi kusema kuwa nimeeleza maelezo ya ziada ili mpate kuyafahamu hayo nitakayoyaandika baadae, hapa nitapenda kuwaeleza kuwa nimeleta ushahidi wa maneno ya Hazrat Ali mwenyewe ya kwamba alikuwa akiamini kuwa Ukhalifa ni wake[505] ingawa alikubaliana na wenzake baada ya fujo na kutoelewana juu ya suala hilo kutokea: Je, Wanachuoni wa Ki-Sunni wanaliona tukio hili kuwa ni sahihi.

JAWABU

[504] - Sura 70, Aya 1-3. Maneno *Dhi Al-Ma'arij* wameyafasiri kwa namna kama tano, moja yao ni hio alioitaja Sheikh X. hapa: **"mwenye mbingu zenye daraja".**

[505] - Maneno haya nimeshayajibu kwa ufafanuzi huko nyuma.

Katika makala iliotangulia tumekujibu kitandawili chenu cha Hadithi "Yule ambaye mimi ni *Mawla* wake basi na Ali ni *Mawla* wake". Sasa hapa tunaendelea na Hadithi yako hii nyengine uliotuletea. Tazameni ndugu Waislamu jinsi watu hawa wanavyozipotosha maana za Aya! Na hii ndio kawaida yao kuzipotoa Aya nyingi za Qur-an ili ziwafikiane na itikadi yao hata ikiwa hazikubaliani na akili ya binaadamu yoyote yule duniani! Haikusalimika kutokana na kutungiwa kijihadithi hata *Qulhuwa-Allahu* nayo pia imetungiwa Hadithi akapachikwa nayo Ali! Bali – kama nilivyotangulia kusema katika utangulizi kwamba – mpaka Aya isemayo: **وَلِلَّهِ الأَسْمَاءُ الْحُسْنَى فَادْعُوْهُ بِهَا (Na Allah ana majina mazuri (matukufu) muombeni (au muabuduni) kwa hayo)**,[506] pia imetungiwa riwaya itokayo kwa Abu Abdillah (Ja'afar Al-Saadiq) akisema:

> Sisi (Maimamu wa Ahlu-lbait) Wallahi ndio majina matukufu (yenyewe) ambayo Allah haikubali kutoka kwa waja amali yoyote ila kwa kutujua (kututambua) sisi!

Sasa ikiwa watu hawa wamefikia hadi ya kuzipotoa Aya namna hii na kutunga riwaya ambazo ubatili wake haujifichi kwa kila mtu,[507] vipi leo tutazikubali riwaya zao ambazo wamezisimulia wao tu kuhusu Uimamu na mingineo?!

Naturudi katika Hadithi ya bedui aliyeteremshiwa adhabu ya mawe. Tunasema kwamba uwongo huu hauihitaji kuwa mtu awe *Ruhullah* au *Ayatullah* ili aweze kuugundua, bali Aya yenyewe uliotunukulia inatosha kukujibu. Aya inasema:

> **Muulizaji aliuliza juu ya adhabu itakayotokea. Kwa makafiri ambayo hapana awezaye kuizuia. Kutoka kwa Allah, Mola wa mbingu za daraja.**[508]

---

[506] - Sura 7, Aya 180.

[507] - Hata siku moja walikuwa baadhi ya vijana katika intaneti ya Oman wakijadiliana na mkiristo wa Lebanoni, akawaletea Qur-ani ilioko kwa Mashia, baadae yeye mwenyewe akasema wachilia mbali hii ni ya kutunga bila shaka!

[508] - Sura 70, Aya 1-3.

Na tafsiri nyengine ya Aya ya mwisho ni: **“Kutoka kwa Allah mwenyewe utukufu mkubwa”.**[509] Hizo ndizo Aya ulizotunukulia. Sasa soma Aya za mbele yake. Aya za mbele yake zinasema:

> **Malaika na Roho hupanda kwake katika siku ambayo kiwango chake ni miaka elfu khamsini*Basi subiri kwa subira njema*Kwani wao wanaiona (adhabu hio au siku hio ya kiama) iko mbali*Nasi tunaiona iko karibu….**[510]

Kisha zinafuata Aya nyengine nyingi mfululizo zenye kusimulia habari ya siku hio ya Kiama na adhabu zake. Kwa hivyo, hata kipofu anaona kwamba hapa anachouliza mwenye kuuliza huyo ni adhabu ya akhera. Lakini ndugu zetu wakaona hapo hapo wapatize na kututungia riwaya – kama kawaida yao – wakiinasibisha na tokeo la Ghadir, lakini Qur-ani yenyewe imekataa – Hadithi ya kutunga maisha haikai sawa.

Pili: ni kuwa Sura hii imeteremka Makka baada ya Suratu *Al-Haaqqa.* Kwa hivyo, kuinasibisha Sura hii na tokeo la Ghadir lililotokea – kwa mujibu wenu – mwaka wa *Hijjatu Al-Wadaa* ambao ni mwaka wa 10 H., ni kuchanganya mambo.[511]

Ama yale yaliomo katika riwaya nyengine kwamba Aya hizi **“Muulizaji aliuliza juu ya adhabu itakayotokea. Kwa makafiri …”..** zimeteremka baada ya muulizaji huyo kuomba kuwa ikiwa hii ni haki basi Allah amteremshie adhabu, kwa kusema:

اللَّهُمَّ إِنْ كَانَ هَذَا هُوَ الْحَقَّ مِنْ عِنْدِكَ فَأَمْطِرْ عَلَيْنَا حِجَارَةً مِنْ السَّمَاءِ أَوِ ائْتِنَا بِعَذَابٍ أَلِيمٍ

---

509 - Na ziko tafsiri nyengine.

510 - Sura 70, Aya 4-6.

511 - Imeteremka Makka katika hatua za mwanzo kabla ya Mtume (s.a.w.) kwenda Madina.

E Allah ikiwa hii ni haki kutoka kwako basi tunyeshee mvua ya mawe yatokayo mbinguni au tuletee adhabu kali.[512]

Riwaya hii pia haikupini nguvu nyinyi, kwani Aya inayofuatia baada ya Aya hio, inasema:

وَمَا كَانَ اللَّهُ لِيُعَذِّبَهُمْ وَأَنْتَ فِيهِمْ وَمَا كَانَ اللَّهُ مُعَذِّبَهُمْ وَهُمْ يَسْتَغْفِرُونَ

Na haiwi kuwa Allah awaadhibu wao nawe uko pamoja nao; na haiwi kuwa Allah awaadhibu wao nao wanaomba msamaha.[513]

Kwa hivyo, kwa mujibu wa Aya hizi, walioomba washushiwe adhabu, basi adhabu hio hawakushushiwa kwa sababu ambazo Allah mwenyewe kazitaja, wakati kule – katika riwaya yenu – munatwambia kuwa adhabu ya mawe ilishushwa.

Kwa ufupi ni kwamba hapa kuna riwaya tafauti: hio yenu ni moja. Na kwa hivyo, bila ya kupoteza wakati kwa kutazama *sanad* za riwa hizo[514] basi natuseme kwamba kuna riwaya za namna mbili mashuhuri zaidi:

Moja: ni riwaya yenye kusema kwamba muulizaji – yaani kwa mujibu wenu – kwa maana ya muombaji aliomba aadhibiwe ikiwa kitendo hicho cha Mtume (s.a.w.) cha kumtangaza Ali ni haki. Riwaya hii inapingana na Aya zenyewe kwani Aya zinazofuata kama vile: **"Basi subiri kwa subira njema*Kwani wao wanaiona (hio adhabu au siku ya kiama) iko mbali*Nasi tunaiona iko karibu…",** ni maandiko ya wazi kwamba kinachoulizwa au kinachoombwa ni adhabu ya kiama si ya dunia.

Pili: ni riwaya zenye kusema kuwa muulizaji – naye ni Al-Nadhru bin Harith au Abu Jahl – alikuwa hapa anauliza kwa maana ya kuhoji usahihi wa kuwepo adhabu ya siku ya kiyama. *Siyaaq* (maneno yanayofatia) ya Aya, inakubaliana na riwaya hizi. Na kwa hivyo, hata Al-Tabatabai –

[512] - Sura 8, Aya 32.
[513] - Sura 8, Aya 33.
[514] - Ingawa nyengine kuzifunguwa tu nimeona wapokezi madhaifu tele.

pamoja na kawaida yake ya kujigonga: akifasiri hufasiri vyengine halafu akileta riwaya huleta riwaya zenye maana nyengine – basi anasema:

> Jambo lenye kuoneshwa na *siyaq* ya Sura (hii) ni kuwa Sura (hii) inaelezea (habari za) siku ya Qiyama na maandalizi ya adhabu kali zilizoandaliwa ndani yake……kisha ikataja siku ambayo adhabu (hio) imeandaliwa kisha wakavuliwa Waumini (kwamba wao hawatoadhibiwa).[515]

Kwa hivyo, sina haja ya kurefusha na kutafuta *sanad* bure: Hadithi yako inaonesha kitu chengine na Aya zenyewe zinaonesha kitu chengine: Hadithi inaonesha kuwa adhabu ilitokea duniani; Aya zinaonesha kuwa kinachoulizwa au kinachoombwa ni adhabu ya kiama, ndio maana Aya ikasema: **“Wao wanaiona iko mbali*Nasi tunaiona iko karibu”** – mgongano baina ya riwaya na Aya uko bayana!

Anasema Sheikh X:

> Idadi ya mabingwa wa Ki-Sunni ambao wamesimulia tukio hili[516] kwa urefu na kwa mukhtasari, hushangaza akili! Tukio hili la kihistoria lilisimuliwa na Masahaba 110 wa Mtukufu Mtume (s.a.w); wafuasi wa Masahaba 84 na kisha likasimuliwa na mamia mengi ya wanachuoni wa ulimwengu wa Ki-Islamu, kuanzia karne ya kwanza mpaka kwenye karne ya kumi na nne AH (Karne ya 7-20 AD).
>
> Tak-wimu hizi hujumuisha tu wapokezi waliomo katika simulizi zilizoandikwa na wanachuoni wa Ki-Sunni!

[515] - Al-Tabatabai *Al-Mizan* 20, uk. 5.

[516] - Yaani Hadithi “Yule ambaye mimi ni *Mawla* wake na Ali ni *Mawla* wake”.

Sehemu ndogo ya vyanzo (Souces) hivi inatolewa hapa chini.[517] Wengi wa wanachuoni hawa hawakunukuu tu tangazo hili la Mtume (s.a.w) bali vile vile wanaliita sahihi.

Hapa ni lazima kutaja kuwa Sheikh Juma Mazrui ataliona tukio hili kuwa halikusihi, hizi ndio mbinu zake kubwa za kutaka watu waendelee kudanganywa na kuona kuwa Shia wametoa habari hizi kutoka kwenye mifuko yao. Mbinu hizi hazitafanikiwa, watu siku hizi wanarejea vitabu vinavyothibitisha habari hizo, Maulamaa wote hao wamethibitisha ukweli wa habari hizo isipokuwa huyo anayesema kuwa anajuwa kila hukmu ya Hadithi inayotajwa humu, basi tazameni Maulamaa hao nini wamesema na mtazame nini Sheikh Juma Mazrui anawaambieni, kisha mpime maneno yake na maneno ya Maulamaa hawa, na akili kichwani mwenu *Inshaallah*))).

JAWABU

Sheikh X kuhusu wasimulizi wa Kisunni ni kweli kama unavyosema kuwa Hadithi hio wameipokea. Lakini bado una kazi mbili:

Moja: ni kuthibitisha kuwa wao wanasema kuwa hio ni Hadithi sahihi. Kazi hii nitakupunguzia, nayo ni kuwa wao wametafautiana juu ya usahihi

[517] - 1) Al-Hakim Al-Naysaburi, *Al-Mustadrak 'Ala Al-Sahihyn* (Beirut), juzuu 3, uk . 109-110, uk . 133, uk . 148, uk . 533. Ameelezea kwa uwazi kwamba Hadithi hii ni sahihi kwa mujibu wa vigezo vya Bukhari na Muslim. Al-Dhahabi alithibitisha hukumu yake. 2) Al-Tirmidhi, *Sunan,* (Cairo), juzuu 5, uk . 633. 3) Ibn Majah, *Sunan,* (Cairo , 1952), juzuu 1, uk . 45. 4) Ibn Hajar Al-'Asqalani, *Fath Al-bari bi Sharh Sahih Al-Bukhari,* (Beirut , 1988), juzuu 7, uk . 61. 5) Al-'Ayni, '*Umdat Al-Qari Sharh Sahih Al-Bukhari,* juzuu 8, uk . 584. 6) Al-Suyuti, *Al-durr Al-Manthur,* juzuu 2, uk . 259 na uk. 298. 7) Fakhr Al-Din Al-Razi, *Tafsir Al-Kabir,* (Beirut , 1981), juzuu 11, uk . 53. 8) Ibn Kathir, *Tafsir Qur'an Al-adhim,* (Beirut) juzuu 2, uk . 14. (9) . Al-Wahidi, *Asbab Al-Nuzul,* uk. l64. (10) Ibn Al-athir, *Usd Al-Ghaba fi Ma'rifat Al-Sahaba,* (Cairo , 1932), juzuu 3, uk.92. (11) Ibn Hajar Al-'Asqalani, *Tahdhib,* (Hyderabad , 1325), juzuu 7, uk . 339. (12) Ibn Kathir, *Al-bidayah wa Al-Nihayah,* (Cairo , 1932), juzuu7, uk . 340, juzuu 5, uk. 213. (13) Al-Tahawi, *Mushkil Al-Athar,* (Hyderabad , 1915), juzuu 2 uk . 308-9. (14) Nur Al-Din Al-Halabi Al-Shafi'i, *Al-Sirah Al-Halabiyya,* juzuu3, uk . 337. (15) Al-Zarqani, *Sharhu Al-Mawahib Al-Ladunniyya,* juzuu 7, uk . 13.

wa Hadithi hii: wengine wanaona kuwa ni sahihi kama Al-Albani;[518] na Sibt Ibn Al-Jawzi;[519] na wengine wanaona kuwa ni Hadithi ambayo haikuthibiti kama Ibn Taymiyya,[520] na ndio dhahir ya mtazamo wa Al-Bukhari kama nilivyokunukulia riwaya yake katika makala iliotangulia kutoka katika kitabu chake *Al-Taarikh Al-Kabir*[521] aliposema kwamba mtu wa mwanzo kuisimulia riwaya hio ni Shia wa Al-Kufa aitwaye Abu Is-haq Al-Sabi'i, kisha watu wakamfuata. Na wengine wanaona kwamba Hadithi hio haifai kuwa ni hoja kwani si *mutawatir* kama Al-Qurtubi kama ilivyo katika tafsiri yake.[522] Kisha – baada ya kusema hivyo – akasema Al-Qurtubi:

> Abu Daud Al-Sijistani na Abu Hatim Al-Razi wameiponda (Hadithi hio) na wakatoa ushahidi wa ubatili wake kwamba Mtume (s.a.w.) kasema: 'Muzaina na Juhaina na Ghifar ni *Mawla* wangu mimi tu pasina watu wengine wote: Hawana *mawla* isipokuwa Allah na Mtume wake.[523]

Na akasema Abdul-Razzaq Al-Mahdi katika maelezo yake alioyatia katika tafsiri ya Al-Qurtubi:

> Na katika mlango huu (yaani katika Hadithi hii) kuna ushahidi mwengine unaoipa nguvu (Hadithi hii) pamoja na kuwa kuna (wanavyuoni) wengi walioidhoofisha.[524]

Kwa hivyo, si kwamba wanavyuoni wa Kisunni wote wanaiona kuwa Hadithi hii ni sahihi. Hilo ni mosi nimekusaidia.

---

518 - Al-Albani *Al-Sahiha* j. 4, uk. 330-344.
519 - Sibt Ibn Al-Jawzi *Tadhkiratu Al-Khawaas* uk.55-62.
520 - Ibn Taymiyya *Minhaju Al-Bida'a* j. 4, uk. 103-104.
521 - J. 6, uk. 79, *tarjama* na. 8348.
522 - Al-Qurtubi *Al-Jami'u Lil-Ahkam* j. 1, uk. 307-308 katika tafsiri ya Aya ya 30 ya Sura 2.
523 - Al-Bukhari *Al-Sahih* Hadithi na. 3512, Muslim *Al-Sahih* Hadithi na. 2520 na wengineo.
524 - Abdul-Razzaaq Al-Mahdi, katika maelezo yake alioyatia katika tafsiri ya Al-Qurtubi j. 1, uk. 307.

Pili: ni kuwa tukijaalia kuwa wanavyuoni wote wa Kisunni wanasema kuwa hio ni Hadithi sahihi, suali ni kuwa je wanasema kuwa maana ya neno *"Mawla"* lililomo katika Hadithi hio maana yake ni mtawala? Na kwa hivyo maana ya Hadithi – kwa mujibu wao – ni "Yule ambaye mimi ni mtawala wake basi na Ali ni Mtawala wake?" Nadhani hii ndio kazi nitayokupa? Masuni hata wanaosema kuwa Hadithi hii ni sahihi, hawasemi kuwa neno "*Mawla*" lililomo katika Hadithi hio maana yake ni mtawala; bali wanasema kuwa maana yake ni "Kipenzi".[525] Na hii ndio tafsiri pekee inayowiyana na sababu ya kutamkwa kwa maneno hayo kama nilivyobainisha kabla. Kwa hivyo, vitabu vya Kisunni juu ya hili havikusaidii, kwani tatizo letu si kuwepo kwa riwaya hio, bali tatizo letu ni maana ya riwaya hio. Tumesema – katika darsa iliotangulia – kwamba maneno: "Yule ambaye mimi ni *Mawla* wake, basi Ali pia ni *Mawla* wake" ikiwa utayafasiri kuwa maana yake ni msimamizi wa mambo, basi hapa hayafasiriki ila katika njia mbili au moja katika mbili:

a) Ama useme kuwa Ali ndiye au naye alikuwa mtawala wakati wa Mtume (s.a.w.). Na hili hakuna alisemae: si Shia wala si Suni wala si Ibadhi.
b) Au useme kwamba Mtume (s.a.w.) hapa alikusudia kuwa Ali atakuwa mtawala baada yake, na hapa utabiri wa yule **"Asiyetamka (chochote) kwa matamanio yake: bali ni (kwa) wahyi anaopewa"** utakuwa haukutimia!

Nimesema: Kwa hivyo, hatukubakiwa isipokuwa na tafsiri ya wale wanaosema kwamba neno *"Mawla"* katika riwaya hio maana yake ni kipenzi. *Tahriri* ni kuwa wenzake Ali huko Al-Yaman walichukizwa na baadhi ya walioyaona kutoka kwake, na hii ina maana kuwa walimchukia

[525] - Sikuona katika Maulamaa wa Kisunni aliyesema kuwa neno "Mawla" lililomo katika Hadithi hio maana yake ni mtawala isipokuwa Sibt Ibn Al-Jawzi katika *Tadhkiratu Al-Khawwaas* uk. 60. Labda yuko mwengine ambaye sikuiona kauli yake. Kwa hali yoyote ile, madhehebu za Kisunni zinakubaliana kwamba Mwenyezi Mungu na Mtume wake hawakutoa amri ya kuwepo Khalifa baada ya Mtume (s.a.w.), bali ukhalifa ulikuwa ni jambo la kushauriana. Huu ndio msimamo wa Kisunni; Sunni atayesema kinyume na hivi, basi hio ni kauli yake binafsi haikufikia daraja ya kuitwa kuwa ni kauli ya Kisunni; sawa na Shia Ithnashariy anayeona kuwa hakukuwa na wasia juu ya ukhalifa; hii hatuwezi kuiita kuwa ni kauli ya Kishia; bali ni kauli yake binafsi.

kwa sababu hio, kwa hivyo, kana kwamba Hadithi inasema musimchukie Ali kwani: "Yule aliye mpezi wangu basi na awe mpenzi wake au anipendae mimi basi na-ampende na yeye pia". Hii ndio maana peke yake ambayo inawezekana kuletewa Hadithi hio hasa hasa ukiifungamanisha Hadithi hio na sababu yake ya kutamkwa. Nadhani umefahamu ikiwa unataka kufahamu.

Sheikh X anasema:

> Sheikh Juma Mazrui Aya ya 55-56 ya Sura ya 5 (Al-Maidah) imeshuka kwa shani ya Imam Ali (a.s). Jambo hili najua unaweza kulikataa lakini huwezi kulifuta katika vitabu vilivyoandikwa kabla ya wewe hujazaliwa. Jambo hili limetajwa katika vitabu vya Shia na Sunni, miongoni mwa vitabu vya Shia vilivyotaja jambo hili ni (kama inavyofata chini).[526]
>
> Amma Vitabu vya Sunni vilivyosema kuwa tukio la Aya hio lilikuja kwa shani ya Imam Ali (a.s) ni vingi sana, miongoni mwa Vitabu hivyo ni (kama inavyofata chini).[527]

JAWABU

Anachokizungumzia Sheikh X ni Aya isemayo:

---

[526] - *Bihar Al-Anwar*, cha Allama Al-Majlisi, *Tafseer Al-Mizan*, cha Allama Al-Tabatabai, *Tafseer Al-kashaf*, cha Allama Muhammad Jawad Mughniyah, *Al-ghadir*, cha Allama Abdul Husain Ahmad Al-Amini na *Ithbat Al-Hudate*, cha Allama Muhammad Ibn Hasan Amuli.

[527] - 1) *AL-Tafsir Al-kabir* ya Imam Ahmad Ibn Muhammad Al-Tha'labi, chini ya maelezo ya aya ya Sura ya 5 aya ya 55-56. (2) *Al-Tafsir Al-Kabir* ya Imam Ibn Jarir Al-Tabari, jalada la 6, kurasa za 186, 288-289. (3) *Tafsir Jamiu Ahkam Al-Qur-an* ya Imam Muhammad Ibn Ahmad Qurtubi, jalada la 6, uk. wa 219. (4) *Tafsir Al-Khazin*, jalada la 2, uk. wa 68. (5) *Tafsir Al-Durr Al-Manthoor* ya Imam Al-Suyuti, jalada la 2, uk. wa 293-294. (6) *Tafsir Al-Kashshaf* ya Imam Al-Zamakhshari, chapa ya Misri mwaka 1373, jalada la 1 uk. wa 505 na 649. (7) *Asbab Al-Nuzool* cha Imam Jalaluddin Al-Suyuti, chapa ya Misri ya mwaka 1382, jalada la 1 uk. wa 73, Hadithi ya Ibnu Abbass (r). (8) *Asbab Al-Nuzool*, cha Al-Wahidi, kutoka kwa Ibn Abbas. (9) *Al- Musnad* ya Imam Ahmad Ibn Hanbal, jalada la 5, uk. wa 38.

Hakika *Walii* wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini tu: wale ambao wanasimamisha sala na wanatoa zaka nao ni wenye kurukuu.[528]

Nayo tumeshaijadili kwa marefu na mapana katika sura ya kwanza ya kitabu hiki. Tatizo letu Sheikh X sio kutajwa kwa riwaya au kutotajwa. Suali ni kuwa je riwaya hio ni sahihi? Umetaja marejeo mengi hapa, lakini katika marejeo haya wapokezi wa Hadithi ni watatu tu: Al-Tha'alabi, Al-Tabari na Al-Wahidii naye ni mwanafunzi wa Al-Tha'alabi: waliobakia ni wenye kunukuu tu riwaya,[529] kwa hivyo wao si muhimu hapa. Sasa kwa ufupi ni kuwa nimekubainishia *sanad* zote za riwaya yenu ya sadaka ya pete kwamba ni utunzi wa waongo wa Al-Kufa: sasa wewe niletee hio riwaya yenye *sanad* sahihi.

Ama kusema kuwa riwaya hio wameipokea Shia; *Tunasema:* kwanini Shia wasiipokee na wao ndio walioitunga?! Ni vigumu kwa mtu atayesoma vitabu vya riwaya vya Kishia akaweza kukubaliana na riwaya zao. Je si ndio Shia waliopokea riwaya ziliofika daraja ya mutawatir kwamba Qur-ani imepunguzwa na kubadilishwa?[530] Nilikunukulieni katika *Mezani Ya Haki* kauli za wanavyuoni wenu wakisema:

---

[528] - Sura 5 Aya 55.

[529] - Hapa linathibiti lile nililokwambieni katika utangulizi kwamba watu hawa wanapenda kuwaghushia watu: hunukuu Hadithi kutoka kwa wapokezi wawili watatu kisha wakatoa idadi kubwa ya walioitaja Hadithi hio katika vitabu vyao. Asiyejua hudhani kwamba wote hao wameipokea Hadithi hio, kumbe wapokezi ni wawili watatu.

[530] - Hapa kuna kitu kimoja ambacho ni vyema kukitolea tanbihi: nacho ni kuwa ndugu zetu wa Kishia wanapopata lawama hii ya kusema kuwa Qur-ani imepotoshwa, husema hata katika Sunni pia ziko riwaya zenye kuonesha kuwa Qur-ani imepotoshwa. Sasa tafauti iliokuwepo hapa ni kuwa Wanavyuoni wa Kishia au baadhi ya wanavyuoni wa Kishia wao wanasema kuwa Qur-ani imepotoshwa na kupunguzwa; na Aya zenyewe zilizopunguzwa ni zile za ukhalifa wa Ali. Wakati Sunni wao hawasemi hivyo; Sunni wanasema kwamba kuna Aya za Qur-ani zilizofutwa lafdhi yake; na kuna Aya nyengine zilizofutwa lafdhi na hukumu; na kuna Aya nyengine zilizofutwa hukumu bila ya lafdhi. Kwa hivyo, wao riwaya zao ni zenye kusema kwamba kuna Aya zilizofutwa na Allah Mwenye: hawasemi kuwa Pandu na Makame wamezipotosha au kuzifuta Aya hizo, na hii ni tafauti na Shia wanaoona kuwa kuna Aya zimetolewa na nyengine kupotoshwa na binaadamu, kama ilivyo katika vitabu vyao vingi! Ama Hadithi ya Sayyida Aisha (r.a.) iliomo katika *Sahihu Muslim* kuhusu kunyonya mara kumi na kufutwa idadi hio hadi kuwa mara tano na kwamba hio ilikuwa ni sehemu ya Qur-ani hadi kufa kwa Mtume

> Na wala haijifichi kwamba habari (riwaya) hii na riwaya nyingi sahihi ziko wazi kuhusu ***kupunguzwa Qur-ani na kuibadilisha.*** Na kwa mtazamo wangu habari (riwaya) katika mlango huu ni ***Mutawaatir.*** [531]

Anasema mwengine:

> Hakika ya kusalim amri kwa *utawaatur* wake *(utawaatur* wa visomo saba) kutoka katika Wahyi Mtakatifu, na kuwa Roho Mtakatifu kaiteremsha, kunapelekea kuzitupa habari (riwaya) *mustafidha* (nyingi) bali *mutawaatir* zenye kuonesha kwa uwazi kwamba katika Qur-ani kumetokea upotoshaji wa maneno, maudhui na irabu, pamoja na kuwa Wanavyuoni wetu wamekubaliana juu ya usahihi wa riwaya hizo.[532]

Huyu Mwanachuoni mwengine wa Kishia anasema kuwa Hadithi zenye kuonesha kuwa Qur-ani imepunguzwa na kubadilishwa ni *mutawaatir* .

Anasema mwengine:

> Jua kwamba haki ambayo haina njia ya kuikimbia kwa mujibu wa habari (riwaya) *mutawaatir* zenye kufuata na nyenginezo, ni kwamba hii Qur-ani

---

(s.a.w.), ni Hadithi iliodhoofishwa na wanavyuoni wengi wa Kisunni kama alivyobainisha Al-Imamu Al-Qannubi katika *Al-Tufan* j. 3, sehemu ya pili uk. 403-415. Na wale ambao hawakuidhoofisha Hadithi hii kama Al-Imamu Al-Nawawi, wao wameitolea tafsiri ya undani (ta-awil). Anasema Al-Imamu Al-Nawawi:

> Na maana yake ni kuwa kufutwa unyonyaji wa mara kumi kwa kufanywa mara tano kumechelewa sana (kufutwa huko) hata Mtume (s.a.w.) akafa na baadhi ya watu wakawa bado wanasoma mara tano na wanaifanya kuwa ni Qur-ani yenye kusomwa kwa sababu ya kuwa kwao haikuwafikia kwamba imefutwa kwa sababu ya kuwa muda wake (wa kufutwa) bado ni wa karibu sana.

Tazama Al-Nawawi *Sharhu Sahihi Muslim* j. 5, uk. 374, katika sherehe ya Hadithi na. 3572. Kwa hivyo, kwa ujumla ni kuwa wanavyuoni wa Kisunni wamekubaliana kuwa Qur-ani haikupotoshwa wala kubadilishwa na Hadithi ambazo dhahir yake iko hivyo, basi ama wamezikataa au wameziletea tafsiri ya undani inayokubaliana na itikadi sahihi ya Kiislamu; wakati *Jumhuri* ya wanavyuoni wa Kishia wamezikumbatia riwaya za namna hio.

[531] - Al-Majlisi *Mir-aatu Al-'Uqul Fii Sharhi Akhbari Al-Rasul* j. 12, uk. 525.

[532] - Ni'imatu Allah Al-Jazairi *Al-Anwaaru Al-Na'amaaniyya* j. 2, uk. 257.

> ilio mikononi mwetu, hakika imetokea ndani yake kubadilishwa baada ya Mtume (s.a.w.). [533]

Anasema mwengine:

> Jua kwamba habari (riwaya) kutoka kwa Maimamu Waliotakasika (Maimamu kumi na mbili wa Kishia) zimemiminika (ziko kwa wingi) kuhusu kuingia ziada na kupunguzwa Qur-ani.[534]

Na tumekunukulia kabla kidogo, upotoshaji wenu wa Aya isemayo: **"وَلِلَّهِ الأَسْمَاءُ الْحُسْنَى فَادْعُوْهُ بِهَا" (Na Allah ana majina mazuri (matukufu) muombeni (au muabuduni) kwa hayo)**, ambapo munatwambia kuwa *Al-asmau Al-husnaa* (Majina Matukufu) yenyewe ni Maimamu! Sisi bado tuendelee kukubali riwaya zenu tu?[535] Kwa hivyo, Sheikh X riwaya za Shia sisi si hoja kwetu hata wakitumiminia kwa kapu na magunia, kwani utunzi wa riwaya kwao ulipindukia mipaka kama walivyosema wapekuzi mabingwa, bali na kama riwaya hizo za kupotolewa kwa Qur-ani zinavyotoa ushahidi huo.

Sheikh X anasema:

> Hapa tunayo Tafsir ya Imam Thaalabi ambaye jina leke hasa ni Abi Is'haq Ahmad Ibn Muhammad ibn Ibrahim Nisaboori Al-Tha'labi. Imamu huyu amekufa mwaka 337 AH. Mwanachuoni Mkubwa wa Historia ya Kiislamu Ibn Khallikan amesema juu yake kuwa "Imam

---

[533] - Abu Hasan Al-'Amili, katika utangulizi wa pili wa tafsiri yake *Mir-aatu Al-Anwaar Wa Mishkaatu Al-Asraar* uk. 36.

[534] - Al-Khurasani *Bayaanu Al-Saada Fii Muqaddimati Al-Ibaada* j. 1, uk. 12.

[535] - Wala mtu asiniambie kwamba "Kwani hakuna kwao riwaya zenye *sanad* sahihi?" Kwani ikiwa Al-Kuleini kapokea riwaya 17,000 halafu Al-Majlisi – kama alivyotwambia mmoja wa Mashia – anasema kwamba 6000 tu ndio sahihi; na kitabu kilichokuwa na vitabu 30 leo kina vitabu 50, sisi hatuwezi kuzikubali riwaya zao ila zikipatikana sharti tatu nilizozitaja katika utangulizi, kwani aliyethubutu kutunga riwaya akamzulia Allah uwongo hashindwi kutunga *sanad* akamzulia mtu uwongo. Na mfano wa wazi ni riwaya hizo za kupotoshwa Qur-ani na riwaya hio ya kuipotosha Aya ya *AlAasmaau Al-Husnaa* kuwa ni Maimamu, riwaya ambayo – bila shaka kwa mujibu wa Shia – ina *sanad* sahihi. Je ndio tuikubali kwa sababu *sanad* yake ni sahihi?

Thaalabi alikuwa wa pekee katika kuifasiri Kur'ani na tafsiri yake ndio bora zaidi kuliko tafsiri nyengine".[536]

Imam Thaalabi alipofika kwenye Sura 5:55-56 amenakili maelezo ya Hadithi yenye simlizi za Sahaba Abu Dhar al Ghifari (r) kuwa amesema:

"Masikio yangu yote mawili yawe hayasikii tena na macho yangu mawili yapofuwe kama ninasema uongo! Nimemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu, rehma na amani ziwe kwake akisema, "Ali ni Kiongozi wa wachamungu na ni Muuwaji wa makafiri, atakayemsaidia atakuwa mshindi pamoja naye na atakayemwacha naye ataachwa". Siku moja niliswali na Mtume Muhammad (s), masikini akaja kwa ajili ya sadaka, lakini hapakuwa na yoyote aliyempa sadaka hio, wakati huo huo Ali alikuwa katika hali ya kurukuu na akamuashiria masikini huyo kuchukuwa pete yake kwenye kidole chake, hapo Mtukufu Mtume akamtukuza Allah na kusema "Allahu Akkbar"! Kaka yangu Musa (a.s) alikuomba akisema: **"Ewe Mola wangu, ukunjuwe moyo wangu kwa kuifanya kazi yangu nyepesi na niondolee utata uliopo kwenye ulimi wangu ili waweze kunifahamu, na mchaguwe kutoka miongoni mwa ahli zangu Harun ambaye ni ndugu yangu awe waziri wangu na nitie nguvu kwa ajili yake na mfanye ashiriki kwenye kazi yangu ili tuweze kukutukuza na kukukumbuka wewe kila mara. Kwa hakika unatuona".[537]** Na ewe Mola wangu ukamwambia Musa kuwa, ewe Musa, nimekutakabalia maombi yako. Ewe Allah! Mimi ni mja wako na Mtume wako. Ungarishe moyo wangu pia na nifanyie kazi yangu iwe nyepesi na mfanye Ali ambaye ni miongoni mwa ahli zangu kuwa waziri wangu na mfanye yeye awe ni nguvu kwangu". Kisha Abu Dhar akaendelea kusema; Wallahi! Mtume hakumaliza dua yake isipokuwa Siddiq Jibriil alishuka na Aya hii:

[536] - Tazama *Wafayaatu Al-A'ayaan*. **Ninasema:** Lakini kauli hii ni kinyume na wanavyoona – karibu – Umma mzima kwamba tafsiri bora – katika tafsiri za awali – ni ya Ibn Jarir. Na pamoja na hayo wanavyuoni hawakukubaliana naye katika sehemu kadha wa kadha za tafsiri yake.

[537] - Sura 20, Aya 25-35.

INNA-MA WALIYYUKUM ALLAH .... Hakika Allah ndiye Msimamizi wa mambo yenu, na Mtume wake pia na wale walioamini ambao wanasimamisha Swala na kutowa Sadaka[538] hali wao wanarukuu".[539] Na yoyote atakayemfanya Allah na Mtume wake na wale walioamini kuwa ndio wasimamizi wa mambo yake, hakika kundi la Allah ndilo litaloshinda.[540]

Sheikh Juma Mazrui, jee Imam Thaalabi hakujua ipi Hadithi sahihi na ipi Hadithi dhaifu, na kwamba wewe unajua zaidi zipi Hadithi sahihi na zile zisizokuwa sahihi.

JAWABU

Sheikh X unaonesha hata hio makala yangu niliozungumzia Aya hio hukuisoma. Riwaya hii niliijibu hivi:

Tazama Hadithi hii ya kuundwa kule Al-Kufa kwa Al-A'amash – msimulizi wa riwaya hii – jinsi inavyogongana na riwaya nyengine! Hapa tunapata kwamba Mtume (s.a.w.) alikuwemo kwenye msikiti wakati tokeo hilo lilipotokea: riwaya inasema: "Hakika ya mimi nilisali nyuma ya Mtume (s.a.w.)……akaingia muombaji msikitini ikawa hakuna aliyempa", na inasema: "Akaja muombaji akachukua pete kutoka kwenye kidole chake cha ncha cha (mkono wa) kulia. Na hayo ni kwenye jicho la Mtume (s.a.w.)…". Wakati kule katika riwaya nyengine tunaambiwa kwamba Mayahudi waliosilimu walikwenda kumuuliza Mtume (s.a.w.) kuhusu khalifa baada yake. Kisha ikateremka Aya hio, kisha yeye Mtume (s.a.w.) pamoja na wao wakaja msikitini wakati Ali anasali. Tena, kule sala ilikuwa ni ya nafila (si ya wajibu); huku walikuwa wakisali adhuhuri.

---

538 - Qur-an haikusema sadaka bali imesema zaka.

539 - Sura ya 5 Aya 55-56. Lakini mbona Allah kawa ni Mwenye kuyatawala mambo yetu, na Mtume naye kawa hivyo kwa idhini ya Allah, lakini Ali hakuwa na wote habari ya utawala wao imo katika neno moja lililomo katika Aya moja?!

540 - *Tafsir al-Kabir,* ya Imam al-Tha'labi chini ya maelezo ya Sura 5:55-56. Sheikh X aliandika **"Hakika kundi la Allah ndilo litakalofaulu"**. Na hii ni Aya nyengine: si hio hapo.

> Jambo jengine lililomo katika Hadithi hii ni kuwa Hadithi inasema: "Akaja muombaji akachukua pete kutoka kwenye kidole chake cha (mkono wa) kulia. *Na hayo ni kwenye jicho la Mtume (s.a.w.)…". Ninasema:* Hii inamaanisha kwamba Mtume (s.a.w.) kalishuhudia tokeo hilo, wakati katika riwaya iliopita tunapata kwamba Mtume (s.a.w.) alimkuta maskini huyo nje ya Msikiti akamuuliza ni nani aliyempa pete hio na alikuwa katika hali gani? Akasema ni yule mtu yaani Ali na alikuwa katika hali ya kurukuu. Mtume (s.a.w) akapiga *takbiri.* Na hii – kama unavyoona – inaonesha kuwa Mtume (s.a.w.) hakushuhudia jambo hilo. Kwa hivyo, katika riwaya ya kwanza hakushuhudia; katika riwaya ya pili kashuhudia – kashuhudia lakini hakushuhudia! Inaonesha watunzi hawakuwa na *ijtimai* kabla ya utungaji wao!
>
> Sasa baada ya hayo, tazama kitu chengine: nacho ni kuwa hapa – katika Hadithi hii – Mtume (s.a.w.) aliomba dua kwamba Allah amfanye Ali kuwa khalifa baada yake. Hadithi inasema kwamba Allah akampokelea dua hio na akateremshiwa Aya hio kama ni habari na ahadi kutoka kwa Allah! Suala je Ali alikuwa khalifa baada ya Mtume (s.a.w.)! Dua ya Mtume (s.a.w.) imekwenda wapi na ahadi ya Allah imekwenda wapi? Mtunzi wa Hadithi hii hakuwa hodari katika kazi yake ya kupakasa Hadithi kule mjini Al-Kufa!

Hayo Sheikh X ndio nilioyasema kuhusu *matn* (text) ya riwaya hii. Sasa wewe unaendelea kuinukuu riwaya tu bila ya kunijibu hoja nilizozitoa. Kisha baada ya hapo nikazungumzia *sanad* (wapokezi) ya riwaya hio, nikasema:

> Ama katika *sanad* ya riwaya hii, kuna Al-A'amash, Sulaiman bin Mihran, Shia wa kule kule mjini Al-Kufa, naye ni mwenye kughushi na Hadithi yake hapa ni *mu'an'an* (kutoka kwa fulani).[541] Anasema Wahb bin Zam'a Al-Mar-wazi kuhusu Al-A'amash huyu: "Nimemsikia Ibn Mubarak anasema: 'Hakika wamezifisidi Hadithi za watu wa Al-Kufa Abu Is-haq (Al-Sabi'i) na Al-A'amash wenu". Na akasema: "Nimemsikia Mughirah anasema: 'Amewaangamiza watu wa Al-Kufa Abu Is-haq na Al-A'amash wenu huyu". Na akasema Al-Imamu Ahmad bin Hanbal: "Hadithi za Al-A'amash zinagongana". Anasema Al-Dhahabi: "Naye anaghushi, na huenda akaghushi kutoka kwa watu madhaifu". Anasema Ibn Al-Madini:

[541] - Tazama habari za Al-A'amash katika: *Taqribu Al-Tahdhib* uk. 254, *tarjama* na. 2615, na *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 4 uk. 195, *tarjama* na. 386.

> "Al-A'amash alikuwa akikosea sana katika Hadithi za hawa (wapokezi) dhaifu".[542]
>
> Pia yumo katika *sanad* ya riwaya hio Qais bin Al-Rabii, naye pia ni Shia wa kule kule mjini Al-Kufa kwenye kiwanda cha ufinyanzi wa Hadithi, tena ni dhaifu.[543] Na inawezekana ikawa kuna wapokezi wengi wasiojulikana, sikuweza kuwaona kwa upekuzi wa haraka haraka.

Hayo ndio nilioyasema kuhusu *sanad* ya riwaya hio. Sasa Sheikh yote hayo wewe hukunijibu: jawabu yako ni hii:

> Sheikh Juma Mazrui, jee Imam Thaalabi hakujua ipi Hadithi Sahihi na ipi Hadithi Dhaifu, na kwamba wewe unajuwa zaidi zipi Hadithi sahihi na zile zisizokuwa sahihi?

Ninasema: kauli hii inafaa isemwe na mtu wa sokoni: si mtu aliyekwenda kukaa chuoni miaka saba anasoma dini! Lakini labda hio ndio lugha ambayo wewe unaweza kuifahamu, na kwa hivyo na mimi nikuulize – kama kawaida yetu sisi Waswahili tukiulizwa na sisi huuliza:

1) Wewe ulipoikataa Hadithi ya kunyonyeshwa barobaro[544] ulikuwa mjuzi zaidi kuliko Al-Imamu Muslim?!

2) Wewe unapozikataa Hadithi za kuonekana kwa Allah, je inamaanisha kuwa wewe ni mjuzi zaidi kuliko Al-Bukhari na Muslim na Ahmad na wengine?!

Nadhani ikiwa tutakuwa tukitoa hoja hizi basi hatuna haja ya kujadili kitu kwani sisi si wajuzi hata kuliko hao Maulamaa walioko leo Afrika Mashariki. Sheikh tunapojadili huwa hatumjadili mtu, bali tunajadili ushahidi aliotupa kisha tunauweka katika misingi yake na kuupima.

---

542 - Tazama Al-Dhahabi *Al-Mizan* j. 2, uk. 414, *tarjama* na. 3517.

543 - Tazama maelezo yake kwa urefu katika *Tahdhibu Al-Tahdhib* j. 8, uk. 350, *tarjama* na. 698.

544 - Yaani Hadithi alioipokea Muslim na wengine ya kujuzu mwanamke kumnyonyesha mtu aliyefikia balegh ili iwe kamuharamikia. Tazama Muslim *Al-Sahih* Hadithi na. 3585 na zinazofata.

Vyenginevyo labda wewe hujakaa na wanavyuoni wa tafsiri na Hadithi: wala hujishughulishi na kutaka kuyajua waliotuandikia! Al-Imamu Ahmad bin Hanbal ni mjuzi zaidi wa mambo ya Hadithi kuliko Al-Tha'alabi, japo kuwa Al-Tha'alabi anaweza akawa labda ni mjuzi zaidi wa mambo mingine, naye Al-Imamu Ahmad anaona kuwa riwaya za tafsiri hazina msingi kamwe,[545] ingawa dhahir si kwamba Al-Imamu Ahmad anakusudia kuzikanusha riwaya zote za tafsiri; bali – dhahir ni kuwa – anakusudia kutokuwepo usahihi kwa asilimia kubwa ya riwaya hizo kama alivyosema Al-Zarqani.[546] Na Al-Tha'alabi uliyemtaja, tafsiri yake ni mashuhuri kwa Hadithi za kutunga. Anasema Abdu-Razzaq Al-Mahdi katika utangulizi wake alioutia katika tafsiri ya Al-Baghawi:

> Jua ewe ndugu Muislamu kwamba vitabu vyote vya tafsiri vimekusanya Hadithi dhaifu na za kutunga na riwaya za Kiisraili munkar na visa vibovu havina haja hata ya kuvitaja. Na katika hizo ni Hadithi zilizotungwa kuhusu fadhila za Qur-ani sura moja moja alizozisimulia *Al-Tha'alabi* katika tafsiri yake….na Maimamu wameeleza kwa uwazi kuwa ni za kutunga.[547]

Nakusubiri Sheikh X uniambie: "Je Maimamu hao wanajua kuliko Al-Tha'alabi?" Anasema Ibn Al-Jawzi baada ya kutaja Hadithi ya kutunga:

> Na ameitawanya Hadithi hii *Al-Tha'alabi* katika tafsiri yake..na akafuatiwa na Abu Al-Hasan Al-Wahidi katika hayo, nayo si ajabu kwao kwani wao si watu wa (elimu ya) Hadithi.[548]

Nakusubiri tena ewe Sheikh X uniambie: "Je Ibn Al-Jawzi anajua kuliko Al-Tha'alabi?" Nami nitakujibu: "ndio: Ibn Al-Jawzi katika uwanja wa Hadithi ni bingwa zaidi kuliko Al-Tha'alabi".

---

545 - Al-Zarqani *Manaahilu Al-'Irfaan* j. 2, uk. 17.

546 - Al-Zarqani *Manaahilu Al-'Irfaan* j. 2, uk. 17.

547 - Abdul-Razzaq katika maelezo yake juu ya Tafsiri ya Al-Baghawi *Ma'aalimu Al-Tanzil* j. 1, uk. 11.

548 - Tazama maelezo haya katika *Al-Maudhu'aat* (Hadithi za kutunga) cha Ibn Al-Jawzi, j. 1, uk. 240, milango yenye kuhusiana na Qur-an: mlango wa fadhila za Sura.

Ama tukija katika Hadithi yako hio ya pete; tunamkuta Juma Mazrui anasema kwamba imetungwa. Je wanavyuoni wanasemaje? Nimekunukulia maneno ya Ibn Kathir na Ibn Taymiyya kuhusu Hadithi hio, na hapa nakuongeza maneno ya mjuzi mwengine naye Abdul-Razzaq Al-Mahdi huyo huyo tuliyemtaja kabla. Katika utangulizi wake alioutia katika tafsiri ya Al-Baghawi,[549] anazungumzia:

> HADITHI ZA KUTUNGA KATIKA VITABU VYA TAFSIRI NI NYINGI: miongoni mwa hizo kwa mfano ni Hadithi ya Ali na kutoa kwake sadaka ya pete kwenye sala, hakika yake ni ya kutunga kwa makubaliano ya wanavyuoni.

Nakusubiri tena ewe Sheikh X uniambie: "Basi wanavyuoni hao waliokubaliana wanajua zaidi kuliko Al-Tha'alabi?"

Kwa hivyo, Sheikh kwa mukhtasari ninataka uelewe mambo haya:

1) Si kila Hadithi ambayo wanavyuoni wanainukuu huwa wanadai kuwa ni sahihi, bali wao huwa wanazinukuu kuonesha kauli mbali mbali zilizokuwepo pamoja na tegemezi zao katika riwaya. Na huu ndio mfumo wa Al-Tabari na huyo Al-Tha'alabi uliyemtaja. Bali mfano mzuri wa kulifahamu hili, ni hio hio Hadithi ulioinukuu hapa yenye kuhusiana na Aya hio isemayo:

   > **Hakika *Walii* wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini tu: wale ambao wanasimamisha sala na wanatoa zaka nao ni wenye kurukuu.**

   Sasa sijui tafsiri ya Al-Tha'alabi unayo au umetazama yaliosemwa na mwenye kitabu cha *Murajaat* tu. Ikiwa tafsiri hio unayo au unaweza kuipata, basi rejea uitazame utaona kwamba tafsiri ya Al-Thaalabiy kuhusu Aya hio ni sawa sawa na tafsiri ya Al-Tabari, Ibn Kathir na wengine kwamba Aya hio: **"Hakika *Walii* wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini tu…"**

[549] - Tazama Al-Baghawi *Ma'aalimu Al-Tanzil* j. 1, uk. 15.

imemteremkia Ubaada bin Samit.[550] Kisha akasema Al-Tha'alabi: "Na akasema Al-Suddi, Utbat bin Hakim na Thabit bin Abdillah…", kisha ndio akasimulia riwaya hio ulionukuu wewe. Hii ni kusema kwamba riwaya hio ulionukuu wewe, Al-Tha'alabi hakuikubali, bali ni riwaya walioitolea hoja watu wengine yeye kanukuu hoja yao tu, nayo kama nilivyosema riwaya hio imejaa wapokezi Mashia dhaifu, bali kama walivyosema vigogo kwamba ni riwaya ya kutunga. Upo?

2) Jambo la pili ni kuwa sisi tunataka ushahidi hatutaki jina la mtu.

3) Jambo la tatu ni kuwa, ikiwa hio ndio *minhaj* (methodology) yako, basi Hadithi ya kunyonyeshwa barobaro sasa uikubali kwani wewe si mjuzi kuliko Al-Imamu Muslim.

JAWABU KWA MAKALA YA NNE YA SHEIKH X

Bila shaka makala ya nne ya Sheikh X haina tafauti na makala yake ya tatu: zote zinasimulia tokeo la Ghadir na zinatoa ushahidi – taqriban – ule ule aliotupa katika makala ya tatu. Katika makala ya nne, ana maelezo yasemayo:

[550] - Al-Tha'alabi *Al-Kashfu Wa Al-Bayaan* j. 4, uk. 80. Sasa ikiwa Sheikh X anamkubali Al-Tha'alabi kama alivyosema, na kwamba hakuna tafsiri bora kuliko yake, basi sasa naafuate kauli yake kwamba Aya hii imemteremkia Ubaada bin Saamit.

Allah amesema: **“Ewe Mtume, fikisha uliyoteremshiwa kutoka kwa Mola wako; na kama hutafanya, basi hujafikisha ujumbe wake, na Mwenyezi Mungu atakulinda na watu”.**[551]

Shia wanaamini kwamba agizo lililotajwa na Aya hio ya Qur’an lilitekelezwa na Mtume (s.a.w.w.) alipomteua Imam ‘Ali bin Abi Talib (a.s.) kuwa wasii wake kwenye siku ya Ghadir Khumm.

Aliposikia majibu haya, yule mtu aligeuka na kumuelekea ngamia wake huku akisema: **“Ee Mwenyezi Mungu! Ikiwa haya ayasemayo Muhammad ni sahihi, basi tuteremshie jiwe kutoka mbinguni na utuadhibu vikali”.** Basi mtu huyo kabla hajamfikia ngamia wake, Mwenyezi Mungu alimteremshia jiwe lililomwingia mwilini mwake kupitia kichwani kwake na kumwacha akiwa amekufa. Ilikuwa katika tukio hili ndipo Mwenyezi Mungu Mtukufu alipoteremsha Aya ifuatayo:

Muulizaji aliuliza juu ya adhabu itakayotokea. Juu ya Makafiri - ambayo hapana awezaye kuzuia. Kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mwenye utukufu mkubwa.[552]

Maelezo haya tumeshayajibu katika jawabu yetu kwa makala ya tatu ya Sheikh X, na kubainisha kwamba Aya hii inazungumzia adhabu ya kiama: hatuna haja ya kukariri jambo lilo kwa lilo.

Pili: ni dai la Sheikh X kwamba Mtume (s.a.w.) alimteua Ali siku hio ya Ghadir kuwa ni Khalifa wake, yaani Mtume (s.a.w.) aliposema katika hutuba yake: **“Yule ambaye mimi ni *Mawla* wake basi na Ali ni *Mawla* wake”.** Dai kwamba neno *“Mawla”* kwenye Hadithi hio maana yake ni mtawala tumeshalijibu: hatuna haja ya kukariri.

Tumebakiwa na Aya isemayo:

---

[551] - Sura 5, Aya 67.

[552] - 70:1-3.

> **Ewe Mtume, fikisha uliyoteremshiwa kutoka kwa Mola wako; na kama hutafanya, basi hujafikisha ujumbe wake, na Mwenyezi Mungu atakulinda na watu.**

Shia – kama alivyosema Sheikh X – wanaamini kwamba Aya hii imeteremka katika tokeo hilo la Ghadir, na kwamba hapa Mtume (s.a.w.) aliamrishwa kuutangaza ukhalifa wa Ali! Jawabu juu ya dai hili ni refu sana: nimeielezea Aya hio kiurefu katika kitabu maalumu juu ya Hadithi hio ya Ghadir Khumm isemayo: **"Yule ambaye mimi ni Mawla wake na Ali ni Mawla wake".** Kwa hapa na-tutazame nukta (points) zile zile tulizozigusia kabla. Nayo ni kuwa Aya inamtaka Mtume (s.a.w.) afikishe. Kufikisha huku kumefasiriwa kuwa ni kufikisha habari ya Allah kwamba Ali ndiye Mawla baada ya Mtume (s.a.w.). Neno "Mawla" hapa limefasiriwa kuwa maana yake ni mtawala. Kwa hivyo, Allah anampa wahyi Mtume wake aseme: **"Yule ambaye mimi (Muhammad) ni Mtawala wake na Ali ni Mtawala Wake".** Yaani Mtawala wake baada ya kufa Mtume. Sasa tunaona kwamba Muhammad kawa mtawala lakini Ali hakuwa: ilhali wote wameripotiwa na habari hii moja ya mbinguni kuwa ni watawala! Sasa je kweli hii ni habari ya Allah na Mtume wake? Na kama hii ni Habari ya Allah na Mtume wake, je kweli neno Mawla katika Hadithi hio lina maana hio ya mwenye kuwatawalia mambo au mtawala? Nadhani tumeeleza vya kutosha katika jawabu yetu iliotangulia. Al-Hasan bin Al-Hasan bin Ali, mjukuu wa Sayyidna Ali, alipoulizwa: "Je Mtume hakusema kwamba yule ambaye mimi ni *Mawla* wake basi na Ali ni *Mawla* wake?" Akajibu: "Ndio, lakini hakukusudia Uimamu na Utawala, na lau alikusudia hivyo basi angeliwaambia kwa uwazi".[553] Na Abdullah bin Al-Hasan, kitukuu cha Al-Imamu Ali alikuwa akisema:

> Sisi hatuna katika jambo hili (la utawala, haki) wasiokuwanayo wengine (yaani Waislamu wote ni sawa katika ukhalifa), na alikuwa akikanusha dai kwamba uimamu wa Ali ni agizo kutoka kwa Allah.[554]

---

[553] - Tazama *Tatawuru Al-Fikr* uk. 31.

[554] - Tazama *Tatawuru Al-Fikr* uk. 31, naye kainukuu kutoka katika kitabu *Basaairu Al-Darajaat* uk. 153,156.

Kwa hivyo, bado tuna kazi ya kuthibitisha sababu ya kuteremka Aya hio isemayo:

> **Ewe Mtume, fikisha uliyoteremshiwa kutoka kwa Mola wako; na kama hutafanya, basi hujafikisha ujumbe wake, na Mwenyezi Mungu atakulinda na watu",**

nalo ni suala lenye riwaya nyingi tafauti, zenye mgongano.[555] Pia bado tuna kazi ya kubainisha maana iliokusudiwa ya neno "Mawla" katika Hadithi hio ya Ghadir.

Na hapa kuna jambo moja muhimu kuhusu Aya hio, jambo ambalo pia tumeligusia katika Aya zilizotangulia. Jambo lenyewe ni kuwa wataalamu wa Kishia wanatwambia kwamba ilipoteremka Aya inayosema: **"Hakika *Walii* wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini tu…",** ilikuwa ni amri ya Allah kwamba Ali ndiye khalifa baada ya Mtume (s.a.w.). Waislamu ikawa hawakulifahamu hilo, kwa hivyo Mtume (s.a.w.) akatakiwa awafasirie Waislamu kama alivyowafasiria Sala, Zaka n.k. Lakini Mtume (s.a.w.) aliogopa kufanya hivyo kwa kuhofia Waislamu wasije wakartadi na kumkadhibisha!!! Basi Allah ndio akateremsha Aya hii **"Ewe Mtume, fikisha uliyoteremshiwa kutoka kwa Mola wako…",** wakati alipokuwa akirejea kutoka katika Hijjat Al-Wadaa hapo Ghadir, na akamtangaza Ali akisema: "Yule ambaye mimi ni Mawla wake basi na Ali ni Mawla wake". Na bila shaka huu ni mgongano wa riwaya ambapo riwaya yao nyengine inasema kwamba ilipoteremka Aya **"Na waonye jamaa zako wa Karibu"** ambayo iliteremka katika hatua za mwanzo za Da'awa huko Makka, Mtume (s.a.w.) alilikusanya kabila la Banii Abdil-Muttalib na hapo kumtangaza Ali kuwa ndiye Wasii na Khalifa wake. Sasa vipi Mtume aogope Madina kumtangaza mtu aliyemtangaza Makka miaka mingi iliopita ?! Kamtangaza Makka na watu ni makafiri na wakasilimu; lakini anaogopa kumtangaza Madina kwa Waislamu wasije wakartadi! Tazama jinsi ambavyo Aya hazikubaliani na tafsiri zao; na jinsi riwaya zao zinavyogongana!

[555] - Maelezo zaidi juu ya Aya hio yako katika kitabu kingine *In shaa Allah*.

JAWABU KWA MAKALA
YA TANO YA SHEIKH X

Sheikh X anasema:

SHEIKH JUMA MAZRUI NA HADITH AL-THAQALAYN

Assalam Alaikum! Ndugu Waisilamu!

Hadith Al-thaqalayn ni Hadithi mutawatir na imepokewa na Masahaba wengi sana na matabii, Sheikh Juma katika kupinga kwake fadhila za Ahlul Bayt (a.s) amechukuwa juhudi kubwa za kutapakaza yale anayoyaita utafiti juu ya Hadithi Thaqalayn, lakini utafiti wake unampotezea muda wake mwingi sana ambao huenda usizae matunda yoyote[556] na hasa kwa vile Hadith Thaqalayn imo katika vitabu vingi sana ambavyo vimeandikwa na Maulamaa Wakubwa sana wa Kiislamu katika madhehebu zote mbili hizi za Sunni na Shia.

Juhudi ya Sheikh Juma haitaza matunda yoyote, na hasa kwa vile Hadithi hii ni *mutawatir*[557] na imepokewa na kusimliwa na watu wengi sana, na imekuja kwa njia nyingi pia, yote haya yanathibitisha kuwa Hadithi hii ni sahihi licha ya wasomi hawa waliokuja baadae kuanza kuikadhibisha kwa faida zao chache za kidunia[558] lakini haki itabakia pale pale *Inshaallah.*[559]

Hadithi ya Thaqalayn inayowataka Waisilamu washikamane na Kitabu cha Allah na Ahlul Bayt (a.s) imo katika *Sahih Muslim, juzuu ya* 7, *Kitab fadha'il alSahabah, chapa ya* Maktabat wa Matba`at Muhammad `Ali Subayh wa Awladuhu ya Cairo, uk. wa 122-123.

---

556 - Ama kwa wenye kutafuta kujaza matumbo kweli utafiti huo haufai kitu, kwani wao wanajua wakifanyacho; lakini kwa wanaotafuta madhehebu kwa ikhlas, basi *Al-hamdu Lillahi,* utafiti huo umefaa na unaendelea kufaa mpaka siku ya Kiyama *In shaa Allah.*

557 - Hata Hadithi za kupotolewa Qur-ani pia ni *mutawatir*! Je tuzikubali?

558 - Sijui faida gani hio ya kidunia! Labda ni kweli kwamba mwizi anadhania kuwa watu wote ni wezi!

559 - *Amin!*

Imam Al-Hakim ambaye ni Mkuu zaidi kwa elim ya Hadithi kuliko Sheikh wetu Juma Mazrui amesema hivi juu ya Hadith Thaqalayn:

> Hadithi hii ni sahihi kwa mujibu wa methodology **(**Njia) na *conditions* (Sharti) za kuthibitisha usahihi wa Hadithi zilizowekwa na Imam Al-Bukhari na Imam Muslim, ingawa Al-Bukhari hakuitia katika sahih yake.[560]

Sheikh Juma Mazrui mimi naona kama Imam Al-Hakim ambaye pia ni Al-Hafiz, vyeo hivi viwili amepewa kutokana na elimu yake kubwa ya Hadithi aliyokuwa nayo, basi kama wewe hukubaliani naye itabidi wewe uwe mtambuzi zaidi kuliko Imam huyu na jambo hili sijuwi kama linawezekana!

Kuna kama aina nne ya Hadithi ya Thaqalayn kutoka kwa Sahaba Zayd ibn Arqam na usahihi wa Hadithi hii umethibitishwa katika vitabu vya Kisunni, inasikitisha kuwa moja katika *excuse* (kisingizio) anayotoa Sheikh Juma katika kuikataa Hadithi hii ni kusema kuwa Sahaba mmoja katika hao waliosimlia alikuwa ni mzee tayari na hakumbuki anayoyasema, basi huenda akawa amesema maneno ambayo si sahihi![561]

Maa shaallah! Haya Sheikh nakupa mkono wa pongezi kwa hoja zako na *Inshaallah* watu wataendelea kukufuata na kuikataa Hadithi hii sahihi, lakini *Wallahi,* utajua kama umekosea na *Wallahi* itafika siku utajua haya wewe mwenyewe, na nakuomba tafadhali siku hio ikifika usiache kuniambia na kuwaambia wale wote uliowapoteza kwani huku ndiko kumcha Mwenyezi Mungu…… Maa salaam.

JAWABU

[560] - Tazama: Al-Imam Al-Hafiz Abu Abd Allah Al-Hakim Al-Naysaburi, *AlMustadrak Ala Al-Sahihayn;* Dar Al-Ma`rifah li Al-Tiba`ah wa Al-Nashr, chapa ya Beirut , juzuu ya 3 uk. wa 109-110 na uk. wa 148.

[561] - Sikusema mimi bali ni Sahaba huyo kasema hivyo yeye mwenyewe kwenye Hadithi hio hio *(Hadithu Al-Thaqalain).*

Nadhani aliyesoma utafiti wangu juu ya *Hadithi Al-Thaqalain*, anaona kuwa Sheikh X hakujibu chochote katika nilioyasema. Isipokuwa amekariri dai lile lile ambalo nimelijibu katika kitabu changu *Mezani Ya Haki*.

Katika makala hii ya Sheikh X, tunapata hoja mbili: moja ni ya kielimu; na ya pili ni ya sokoni :

1) *Hadithi Al-Thaqalain* ni mutawatir. Na hii ndio ngoma yao.

2) Al-Hakim kasema kuwa Hadithi hio ni sahihi, kwa mujibu wa sharti ambazo wameziweka Al-Bukhari na Muslim, na Al-Hakim ni mjuzi kuliko Juma Al-mazrui.

Jawabu kwa hoja ya kwanza nimeitoa kwa urefu katika *Mezani Ya Haki* – kwa hapa nafupisha tu – nayo ni kuwa dai hilo si sahihi, kwani ili Hadithi iitwe *mutawatir* ina masharti yake: si wingi wa wapokezi tu kwamba ndio unaifanya Hadithi iwe *mutawatir*: wingi wa wapokezi katika tabaka tatu za mwanzo: Tabaka ya Masahaba, Matabiina, na Tabii Tabiina, ni sharti moja tu ya utawatir. Miongoni mwa masharti yake mingine muhimu ni kuwa isisimuliwe na watu wenye maslahi ya pamoja tu. Sasa Hadithi *Al-Thaqalain* katika *sanad* zake zote au karibu *sanad* zake zote za Kisunni imesimuliwa na wasimulizi wa Iraki na aghlabu yao ni wasimulizi wa Al-Kufa, nao ni mji wa Mashia.[562] Kwa hivyo, imesimuliwa na watu wenye maslahi ya pamoja na kwa hivyo imepoteza sifa ya kuitwa *mutawatir*.

Anasema Al-Imamu Abdu-llahi bin Mas'ud Al-Mahbubi, Al-Bukhari (Sadru Al-sharia):

> Maana ya *mutawatir* – kwa muktadha wa maneno yake – ni ile ambayo wasimulizi wake wanakuwa katika kila zama, ni watu ambao idadi yake haihisabiki wala haiwezekani kuwa waafikiane katika kusema uwongo kwa sababu ya wingi wao na uadilifu wao na kwa sababu makazi yao (yako) mbali mbali…..hata lau walitoa habari idadi (kubwa sana)

[562] - Nililitupia macho suala hili kwa haraka hara sikuona isipokuwa *sanad* moja tu ndio iliosimuliwa na watu wa Basra, lakini yote ni Iraki hio! Labda uchunguzi wa kina zaidi unahitajika. Kwa hali yoyote ile iwayo, Hadithi hii ina ubovu katika *matn* yake zaidi hata kuliko *sanad* zake.

> isiohisabika (lakini) kwa kitu ambacho inajuzu wakakubaliana kusema uwongo kwa sababu ya (kuwa) na lengo (moja) katika malengo, basi haiwi *mutawatir*.[563]

Na anasema – mwanachuoni wa Kishia – Mohd Baqir Al-Sadr:

> Na shuruti za *tawatur* ni wingi wa idadi, lakini hakuna mpaka wa kina wa daraja ya wingi huo……kwa sababu hilo linaathirika kwa sababu *(factors)* za kielimu na za kibinafsi….Ama sababu za kielimu miongoni mwa hizo ni aina ya mashahidi kutokana na uaminifu na uhodari. Na katika (sababu) hizo ni kutafautika mwenendo wao (watoaji habari hao) na hali (circumstances) zao, kwa sababu kadiri wanavyokuwa mbali mbali na wanavyotafautika (katika misimamo na mitazamo) inakuwa uwezekano wa kushirikiana kwa pamoja – katika kuwa habari hii maalumu ni yenye maslahi binafsi yenye kuwafanya watoaji habari hao wote (watoe habari hio) – ……uko mbali.[564] .

Hivi ndivyo ilivyo katika elimu ya usuli ewe ndugu yangu Sheikh X. Tazama maneno hayo ya wanavyuoni wawili hao, wa Kishia na wa Kisunni! Katika nukulu ya kwanza, tunapata miongoni mwa masharti ya Hadithi mutawatir:

> Ni (ile iliosimuliwa na) watu ambao idadi yake haihisabiki wala haiwezekani kuwa waafikiane katika kusema uwongo kwa sababu ya wingi wao na uadilifu wao *na kwa sababu makazi yao (yako) mbali mbali".*

Sanad zote za *Hadithi Al-Thaqalain* ni za Kiiraki na aghlabu yake ni zina wasimulizi wa Al-Kufa, kwa hivyo, hii ni habari iliotoka katika mji mmoja tu.

Pili tunapata katika maelezo hayo kwamba:

> Hata lau walitoa habari idadi (kubwa sana) isiohisabika (lakini) kwa kitu ambacho inajuzu wakakubaliana kusema uwongo kwa sababu ya (kuwa) na lengo (moja) katika malengo, basi haiwi *mutawatir*.

563 - Tazama *Al-Tanqihu Ma'a Sharhihi Al-Musamma Bi Al-Tawdhih* j. 2, uk. 6.
564 - Tazama *Durusu Fii Usuli Al-Fiqhi* sehemu ya 3 uk. 22.

Na kwa hivyo, wasimulizi wa madhehebu moja hawaifanyi Hadithi kuwa ni *mutawatir* hata wakiwa wengi. *Hadithi Al-Thaqalain* imesimuliwa na Shia hata katika vitabu vya Kisunni! Na kwa hivyo, imesimuliwa na watu wenye lengo moja – natija ni kuwa hio ni Hadithi Ahadi: si *mutawatir*.

Katika nukulu ya pili ambayo ndio ya mwanachuni wa Kishia, tunapata haya yafuatayo:

> Kwa sababu kadiri wanavyokuwa mbali mbali na wanavyotafautika (katika misimamo na mitazamo) inakuwa uwezekano wa kushirikiana kwa pamoja – katika kuwa habari hii maalumu ni yenye maslahi binafsi yenye kuwafanya watoaji habari hao wote (watoe habari hio) – ……uko mbali.

Nadhani umefahamu Sheikh X! Ni lazima watoaji habari hao – pamoja na kuwa idadi yao ni kubwa – wawe mbali mbali na wawe na misimamo tafauti: si watu wenye (common interest) maslahi ya pamoja katika suala hilo. Kwa hivyo, Hadithi Al-Thaqalain katika vitabu vya Shia wasimulizi ni Shia; *Hadithi Al-Thaqalain* katika vitabu vya Kisunni wasimulizi ni Shia wa Al-Kufa – Hadithi yenu ni Ahadi: si mutawatir. Hii ni kwa ufupi, kwa urefu tumeeleza katika *Mezani Ya Haki* nawe hukutujibu.

Ama dai lako la pili uliposema:

> Sheikh Juma Mazrui mimi naona kama Imam Al-Hakim ambaye pia ni Al-Hafiz, vyeo hivi viwili amepewa kutokana na elimu yake kubwa ya Hadithi aliyokuwa nayo, basi kama wewe hukubaliani naye itabidi wewe uwe mtambuzi zaidi kuliko Imam huyu na jambo hili sijuwi kama linawezekana.

Tunasema: Mashaa Allah, jawabu yako ni ya kielimu sana! Hizi ndizo jawabu za Sheikh huyu anapokosa cha kujibu. Tumekwambia ewe Sheikh X kwamba jawabu hii wewe haikufai kwani:

1) Itabidi uikubali Hadithi ya kunyonyeshwa barobaro, kwani wewe si mjuzi kuliko Muslim, nawe Hadithi hio huikubali.

2) Uzikubali Hadithi za kuonekana kwa Allah kwani huyo Al-Hakim ni miongoni mwa wenye kuziona Hadithi hizo kuwa ni sahihi. Na kwa hivyo naye ni miongoni mwa waliozisimulia.[565] Wewe unazikataa, sasa wewe umekuwa mjuzi kuliko Al-Hafidh Al-Hakim, Al-Bukhari, Muslim, Ahmad, Al-Tirmidhi, Ibn Maja na Ibn Hajar na wanavyuoni wote wa Hadithi wa Kisunni?! Sheikh X hoja hio haikufai wewe: itakudhuru mwenyewe usiikimbilie: tafuta *shubuha* nyengine uandame ili uweze kuukimbia ukweli, hapo bado hujapata njia ya kuukimbia.

Ama kuhusu kauli ya Sheikh X aliposema kwamba Al-Hakim kasema:

> Hadithi hii ni sahihi kwa mujibu wa methodology (Njia) na *conditions* (Sharti) za kuthibitisha usahihi wa Hadithi zilizowekwa na Imam Al-Bukhari na Imam Muslim, ingawa Al-Bukhari hakuitia katika sahiih yake",

inaonesha Sheikh X labda hata hapotezi wakati wake kurejea vitabu vya elimu ya Hadithi. Al-Hakim kaziita sahihi Hadithi nyingi ambazo ni dhaifu sana. Na kasema mwahala kadha kuwa hii ni sahihi kwa sharti ya Al-Bukhari na Muslim wala si hivyo kamwe. Na hili limebainishwa pia na wajuzi wengi. Anasema Abu Is-haq bin Ibraahim:

> Al-Hakim kakusanya Hadithi nyingi alizodai kuwa ni kwa sharti za Al-Bukhari na Muslim…miongoni mwa hizo ni Hadithi: "Yule ambaye mimi *Mawla* wake, basi na Ali ni *Mawla* wake". Basi wanavyuoni wa Hadithi wakampinga. [566]

Anasema Ibn Kathir kuhusu kitabu *Al-Mustadrak* cha Al-Hakim:

> Katika kitabu hiki kuna Hadithi nyingi, kati yake zimo sahihi zenye kudirikiwa (ambazo Al-Bukhari na Muslim hawakuzisimulia katika

[565] - Al-Hakim *Al-Mustadrak* j. 2, uk. 553, Hadithi na. 3880, katika tafsiri ya Surat Al-Qiyaamah.

[566] - Tazama utangulizi ulioandikwa na Mustafa Abdul-Qadir Ataa katika *Al-Mustadrak* j. 1, uk. 15.

> Sahihi zao mbili) nazo ni chache; na zimo nyengine sahihi…na zimo dhaifu na za kutunga pia.[567]

Anasema Al-Suyuti kuhusu kitabu hicho *Al-Mustadrak* cha Al-Hakim:

> Na Al-Dhahabi amekifanyia mukhtasari (kitabu hicho) *Al-Mustadrak* na akamfuatishia kwa kuzidhoofisha na (kusema kwamba Hadithi zake nyengine ni) munkar na akakusanya juzuu moja ya Hadithi zilizomo ndani yake, nazo ni za kutunga, akazitaja kiasi cha (Hadithi) mia.[568]

Kisha akanukuu Al-Suyuti maneno ya Al-Maaliini akisema:

> Nimekichungulia (kitabu) *Al-Mustadrak* alichokitunga Al-Hakim mwanzo hadi mwisho sikuona ndani yake hata Hadithi moja (alioisimulia) kwa mujibu wa sharti zao (Al-Bukhari na Muslim).[569]

Ingawa kauli hii imepingwa na Al-Dhahabi, na akasema:

> Na hii ni israfu (kupindukia mpaka) kwa Al-Maaliini, vyenginevyo ndani yake (kitabu hicho *Al-Mustadrak*) kuna mkusanyiko mkubwa (wa Hadithi alizozisimulia) kwa mujibu wa sharti zao (Al-Bukhari na Muslim)…..na zilizobaki – nazo ni kiasi cha robo (ya kitabu) ni munkar na dhaifu sana hazikusihi na katika baadhi ya hizo kuna (Hadithi) za kutunga.[570]

Kwa hivyo, katika kitabu *Al-Mustadrak* kuna Hadithi kadha wa kadha ambazo Al-Hakim kasema kuwa kazisimulia kwa mujibu wa sharti za Al-Bukhari na Muslim nazo si kwa sharti zao, na nyengine ni kwa sharti za mmoja tu, na nyengine kazipandanisha *sanad* za huyu na huyu. Yote haya yameelezwa katika vitabu mbali mbali. Lakini Ibn Hajar anamtakia udhuru Al-Hakim – kwa hayo – kwamba ilikuwa lengo lake ni kuzichuja riwaya hizo lakini hakuwahi mauti yakamfikia.[571]

---

[567] - Ibn Kathir *Al-Baa'ithu Al-Hathith* j. 1, uk. 113.
[568] - Al-Suyuti *Tadribu Al-Rawi* uk. 94.
[569] - Tazama *Tadribu Al-Rawi* uk. 94.
[570] - Tazama *Tadribu Al-Rawi* uk. 94.
[571] - Tazama *Tadribu Al-Rawi* uk. 94. Na tazama pia maelezo ya Ahmad Shakir katika *Al-Baa'ithu Al-Hathith* j. 1, uk. 113.

NUKULU YA HADITHI AL-THAQALAIN

Sasa baada ya maelezo hayo, na-tuitazame *Hadithi Al-Thaqalain* ambayo Sheikh X amenilaumu kwa kusema kwangu kuwa haikuthibiti kutoka kwa Mtume (s.a.w.).

Hadithi Al-Thaqalain ni hii:

> Katuhadithia Zuhair bin Harb na Shujaa bin Makhlad wote kutoka kwa Ibn Uliyyah. Kasema Zuhair katuhadithia Ismail bin Ibrahim kanihadithia Abu Hayyan kanihadithia Yazid bin Hayyan kasema: 'Niliondoka mimi na Husain **(حُصَيْنٌ)** bin Sabra na Umar bin Muslim kwenda kwa Zaid bin Arqam. Tulipokaa naye, Husain akamwambia: 'Ewe Zaid! Kwa hakika umekuta kheri nyingi: umemuona Mtume (s.a.w.) na umesikia Hadithi zake na umekwenda vitani pamoja naye, na ukasali nyuma yake: kwa hakika umekuta kheri nyingi ewe Zaid! Tuhadithie ewe Zaid yale ulioyasikia kutoka kwa Mtume (s.a.w.). Akasema (Zaid bin Arqam) ewe mwana wa ndugu yangu! Wallahi, miaka yangu imekuwa mikubwa (nimeshakonga), na umri wangu umekuwa mkongwe, na nimesahau baadhi ya yale niliokuwa nimeyahifadhi, basi nitachokusimulieni kikubalini na nisicho (kusimulieni) basi musinikalifishe. Kisha akasema: 'Alisimama Mtume (s.a.w.) siku moja pamoja nasi akahutubia katika (sehemu yenye) maji yanayoitwa 'Khumman' baina ya Maka na Madina. Basi akamuhimidi Allah na kumsifu na akatoa mawaidha na kukumbusha. Kisha akasema: 'Baada ya hayo, Enyi watu! Hakika yangu mimi ni mtu (ambaye) amekaribia kunijia Mjumbe wa Mola wangu nami nitaitika. NA MIMI NAKUWACHIENI VIZITO VIWILI: CHA MWANZO CHAO NI KITABU CHA ALLAH. Ndani yake kuna uongofu na nuru, basi kishikeni Kitabu cha Allah na mushikamane nacho.' Basi akahimiza juu ya (kushikamana na) Kitabu cha Allah na kuwataka (watu) wakipende. Kisha akasema: 'NA AHLU BAITII (WATU WA NYUMBA YANGU), NAKUKUMBUSHENI ALLAH KUHUSU WATU WA NYUMBA YANGU, NAKUKUMBUSHENI ALLAH KUHUSU WATU WA NYUMBA YANGU, NAKUKUMBUSHENI ALLAH KUHUSU WATU WA NYUMBA YANGU.' Akasema Husain (kumwambia Zaid bin Arqam): 'Kwani watu wa nyumba yake ni nani ewe Zaid: kwani wake zake si watu wa nyumba yake (si Ahlu Al-Bait)?' Akasema (Zaid bin Arqam): 'Wake

zake ni AHLU BAITIHI (ni watu wa nyumba yake) lakini watu wa nyumba yake ni wale walioharamishiwa sadaka baada yake. Akasema ni nani hao? Akasema (hao) ni kizazi cha Ali, kizazi cha Aqiil, kizazi cha Ja'afar na kizazi cha Abbas. Akasema (Husain): 'Wote hawa wameharamishiwa sadaka?' Akasema (Zaid bin Arqam): 'Ndio' (wote hawa wameharamishiwa sadaka).

MATN YA HADITHI HIO

Hapa nagusia kila kitu kidogo kidogo tu kwani Hadithi hii, tumeileza kwa urefu hatuna haja ya kukariri. Tunasema: kwa mujibu wa Hadithi hii tunapata kwamba Ahlul-Bait ni:

a) Kizazi cha Ali.
b) Kizazi cha Aqil.
c) Kizazi cha Abbas.
d) Kizazi cha Ja'afar.
e) Wake wa Mtume (s.a.w.).

Haya ikiwa wewe Sheik X unaiamini Hadithi hii kuwa ni sahihi, je unakubali kwamba wote hawa ni Ahlu-bait ili uwe umeiitakidi *Hadithi Al-Thaqalain?* Hapa ndipo utapoona ajabu ya watu hawa: kupiga kelele *"Hadithi Al-Thaqalaini* weee *Hadithi Al-Thaqalain*" wala wao wenyewe hawaiamini! Shia wanasema kwamba wake wa Mtume si Ahlu Al-Bait – wakitegemea Hadithi za kupakasa kule mjini Al-Kufa, kama tulivyobainisha katika *Mezani Ya Haki* – wakati *Hadithi Al- Thaqalain* inasema kwamba nao ndiwo; Shia wanawalani Abbasiyyin (Kizazi cha Abbas) na kwa mujibu wa *Hadithi Al-Thaqalain* nao ni Ahlu Al-Bait. Sasa Hadithi hii munaimamini au hamuiamini? Naona mumemega kiasi chenu: kidogo tu hata robo haikutimia!

Kwa leo sina zaidi, Hadithi hii nimeifanyia kitabu kizima chenye kurasa 213,[572] na kwa hivyo maelezo yote yako huko. Hadi hapa nitakuwa nimemaliza kujibu makala 5 za Sheikh X.[573]

---

[572] - Katika kitabu nilichokiita **"القسطاس المستقيم"** au kwa Kiswahili *Mezani Ya Haki*.

[573] - Baada ya hapa Sheikh X hakuandika tena chochote kuhusu maudhui haya, bali alirukia maudhui nyengine, ambayo sitopenda kuishirikisha katika kitabu hiki ili tusitoke nje ya maudhui, bali nitaiashiria tu. Aliandika makala ya sita akazungumzia kwamba mimi nazipinga Hadithi za Mashia kwa sababu wao ni Mashia tu ilhali Maimamu

wakubwa kama Al-Bukhari na wengineo wamesimulia riwaya zao. Nami nafupisha jawabu kama ifatavyo:

1) Kuna tafauti kubwa baina ya Shia wa zamani waliokuwa katika zama za Masahaba na Shia wa leo au waliokuja baadae: Shia wa zama hizo, ushia wao ulikuwa ni kusema kuwa Ali ni bora kuliko Abu Bakr na Umar, basi ni hivyo tu: mambo mengine yote ni sawa na Waislamu wengine; wala walikuwa hawawatukani Makhalifa wengine bali wakiwapenda na kuwaombea dua, suala lilikuwa nani bora zaidi tu. Ushia huu kwa sasa uko katika madhehebu ya Zaidiyya.

2) Mashia waliokuja baada ya Masahaba ndio walioanza kuleta bidaa mbovu katika dini na kila zama zikenda mbele ikawa mambo mapya yanatungwa hadi kufikia kwenye bidaa ya itikadi ya kupotoshwa Qur-ani, kujipiga kwa minyororo, kuomba msaada kwa Husain naye ameshakufa n.k. Na hapo ndio ukaanza utunzi wa riwaya nyingi ili kutaka kuupa nguvu msimamo wao. Al-Bukhari na wengine wamepokea riwaya kwa Mashia hawa na wale. Na hapa ndipo walipoteleza na hatimae vitabu vya Kisunni vikawa Hadithi zake nyingi za kutunga zimetokana na Mashia. Kitabu kama *Al-Mu'ujamu Al-Kabir* cha Al-Tabarani j. 3, kimejaa riwaya za utunzi wa Shia, halkadhalika *Al-Mustadrak* cha Al-Hakim, na *Taarikh Dimashq* cha Ibn Asaakir ndicho chenye kusikitisha kuliko vyote. Kule Sunni kuwafanyia Shia hao *husnu dhani* ndiko kuliko wachongea wakawamiminia Hadithi za kutunga nyingi; na wengine walikuwa na watoto wa kambu wa Kishia wakawa wanawatungia Hadithi na kuwatilia katika vitabu vyao. Yote haya yameelezwa na wajuzi wakuu wa elimu ya Hadithi.

3) Hao Maulamaa wa Hadithi aliowataja Sheikh X ambao wamesimulia riwaya kutoka kwa Mashia, wameeleza kwa uwazi kwamba ikiwa riwaya imesimuliwa na mtu wa bidaa (na Shia – kama unavyojua – kwa mtazamo wao ni mtu wa bidaa) basi riwaya ambayo inaunga mkono itikadi yake hawaikubali. Na hili limeelezwa katika vitabu vya elimu ya Hadithi, rejea kitabu mama chochote kile cha elimu hio utayakuta hayo. Hata Ibn Kathir kayakariri maneno haya katika sehemu kama mbili (ninavyokumbuka) za tafsiri yake, pia Al-Dhahabi katika *Al-Mizan* na Ibn Hajar katika *Lisanu Al-Mizan* wameyaeleza hayo.

4) Hata wao Shia hawazikubali riwaya za Madhehebu nyengine ila zikubaliane na riwaya zao na wala Shia hawana sababu ya kielimu kwa kufanya kwao hivyo, kwa hivyo nao wasione ubaya watu wengine wanapozikataa riwaya zao nao wana sababu ya msingi kwa kufanya kwao hivyo, nayo ni kwa sababu ya tabia yao ya kukithiri kutunga Hadithi.

5) Katika makala zangu na vitabu vyangu, sikubainisha kwamba hao ni wapokezi Mashia tu, bali nimebainisha pia kwamba:

a) Ni wapokezi dhaifu.

b) Hadithi hizo zinagongana na akili; zinagongana na Hadithi nyengine sahihi; zinagongana na Qur-an. Huu ni mukhtasari wa jawabu ya makala na. 6 ya Sheikh X.

Kisha Sheikh X akaandika makala na. 7. Lakini – kwa bahati mbaya – inakariri suala lile lile la Shura ambalo tumeshalizungumzia humu; na kwa hoja zile zile: hakuna jipya. Nayo pia si maudhui ya mjadala huu: maudhui ya mjadala huu ni "Je kuna amri ya Allah na Mtume wake kuwa Ali ndiye khalifa baada ya Mtume (s.a.w.)". Hata hivyo, Sheikh X alipoleta sula la shura nilimjibu kwa sababu ni suala lililokaribiana na maudhui yetu. Kwa hivyo, jawabu ya makala yake ya saba tumeshaizungumzia humu, hatuna haja ya kukariri.

MUKHTASARI

Kwa kweli sina budi kusema kwamba mjadala huu ni mjadala wa kustaajabisha! Mtu mwenye kutafakari vizuri, natarajia amekuwa akijiuliza na kustaajabu sana! Mimi maudhui nilioijadili katika makala zangu za asili ambazo kwa sasa ndio sura ya kwanza, ya pili na ya tatu ya kitabu hiki, ni maudhui "Je Allah na Mtume wake wamesema kuwa Ali ndiye khalifa baada ya Mtume (s.a.w.)"? Sheikh X akajimwaga uwanjani kunijibu makala zangu hizo, lakini ukitazama katika jawabu zake huoni wapi katoa Aya au Hadithi inayosema kuwa Ali ni khalifa baada ya Mtume (s.a.w.). Iliokaribu zaidi na maana hio ni Hadithi isemayo: "Yule ambaye mimi ni *Mawla* wake, basi na Ali ni *Mawla* wake". Nayo – kama ulivyoona – ni Hadithi ambayo haina maana ya ukhalifa kamwe. Ama *Hadithi Al-Thaqalain* ni kinyume kabisa na itikadi ya Kishia hata kama Hadithi hio ilikuwa sahihi, kwani Hadithi hio inatwambia kwamba Mtume (s.a.w.) katuachia Qur-an na Ahlu Al-Bait, kisha ikawabainisha Ahlu Al-Bait kuwa ni: Kizazi cha Ali, kizazi cha Aqil, kizazi cha Abbas, kizazi cha Ja'afar na wake wa Mtume (s.a.w.). Kwa hivyo, ikiwa maana ya Hadithi hio ni kuwa Ahlu Al-Bait wawe ndio watawala wetu, basi hawa wote ndio watawala wetu: si kizazi cha Ali peke yake, bali na wake wa Mtume (s.a.w.) pia nao wangeweza kuwa watawala!

HATIMA

Hadi hapa tutakuwa tumetia nanga katika msafara wetu huu wa mjadala. Natarajia kwamba msomaji – japokuwa mjadala huu haukukamatana 100% na maudhui ya asili ya kitabu hiki, lakini – atakuwa amefaidika kiasi fulani kwa majibizano haya, kama ambavyo atakuwa amefaidika kwa kitabu chenyewe. Tunamuomba Allah (S.W.) atupokelee kazi yetu hii na aijaalie kuwa *Khalisan Li-Wajhihi Al-karim* na iwe hoja yangu na ya Waislamu duniani na akhera na kwayo awanufaishe Waislamu, na awaunganishe Waislamu katika itikadi ya haki alioiridhia, hakika Yeye Ndiye Mwenye kusikia kila kitu, Aliye karibu na ni Mwenye kupokea dua. Na rehema na Taadhima ziwe juu ya Bwana wetu na Mtume wetu

Muhammad (s.a.w.) pamoja na Masahaba wake watakatifu, na Mitume waliotangulia na Masahaba wao wote na wate wale waliowafuata katika wema hadi siku ya malipo. *Aamin!*

Juma Muhammad Rashid Al-Mazrui.

VITABU VYENGINE VYA MUANDISHI

1) *Hoja Zenye Nguvu Juu Ya Kutoonekana Mwenyezi Mungu Kwa Macho.*
2) *Kisimamo Katika Sala.* (Jawabu kwa waliosema kuwa wasionyanyua mikono wakati wa kusali wanasali kama mipopoo).
3) *Hali Sahihi Ya Kimaumbile.* (Kubainisha uharamu wa maingiliano ya kindoa kwa njia isio ya kawaida).
4) *Mezani Ya Haki.* (Kinatoa ufafanuzi juu ya *Hadithi Thaqalain* na juu ya Ahlu Al-Bait).
5) *Ushahidi Uliowekwa Wazi.* (Kinazungumzia kuhusu suala la miandamo ya mwezi, na je muandamo mmoja unatosheleza duniani kote au kila eneo fulani na muandamo wake).
6) *Jawabu Yetu.* (Kinatoa jawabu kwa wale waliotoa kitabu chao ili kukijibu kitabu changu cha mwezi *Ushahidi Uliowekwa Wazi).*
7) *Ukhalifa.* (Juzuu ya 1 na ya 2. Nacho ndicho kitabu hiki kilichomo mikononi mwako. Hii ni juzuu ya 1, itafutatiwa na ya 2 *in shaa Allah*).
8) *Hukumu Za Sala ya Safari.* (Hakijachapishwa).
9) *Fimbo Ya Musa* **(عصا موسى).** (Juzuu nne. Jawabu kwa Kasim Mafuta wa Tanga kuhusu itikadi ya kumuona Allah na itikadi ya Mungu mwenye kiwiliwili na nyenginezo. Imetoka ya kwanza na itatoka ya nne karibu *in shaa Allah*).
10) *Sherehe Na Maelezo Ya Tafsiri Ya Sheikh Abdullah Salih Al-Farisi.* (Iko Mwanzoni).
11) *Al-Khawarij Reality Or Legend.* (Juzuu tisa kwa lugha ya kiingereza, nacho ni tafsiri ya kitabu chetu *Khawarij Baina Ya Ukweli Na Visa Vya Kutunga*. Hadi sasa kimetoka juzuu ya kwanza na yapili).
12) *Khawarij Baina Ya Ukweli Na Visa Vya Kutunga.* (Juzuu nne, kinahusu suala la wanaoitwa Khawarij, na historia yao na riwaya zilizopokewa juu ya suala hili. Hadi sasa imechapishwa juzuu ya kwanza).
13) *Wele Wake Kila Mwenye Kukadhibisha Ukweli.* Jawabu kwa Kasim Mafuta kuhusu kitabu chake *Ole Wake Kila Mzushi Mwenye Dhambi.*